

**UHAKIKI LINGANISHI WA FANI KATIKA TAFSIRI MINTARAFU YA  
MKAGUZI MKUU WA SERIKALI (MWAKASAKA, 1979) NA MKAGUZI WA  
SERIKALI (MADUMULLA, 1999)**

**NA**

**SOPHIA JEPTOO SEREM**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI  
YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA KISWAHILI  
IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**CHUO KIKUU CHA MOI**

**NOVEMBA, 2018**

## **IKIRARI**

### **Ikirari ya Mzamifu**

Tasnifu hii ni utafiti wangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu chochote ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada yoyote. Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kutoleshwa nakala bila idhini na ridhaa yangu au Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi.....Tarehe.....

**Sophia Jeptoo Serem**

(SASS/DPHIL/KIS/07/14)

### **Ikirari ya Wasimamizi**

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliochaguliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.

Sahihi.....Tarehe.....

**Dkt. Mosol Kandagor**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

**ELDORET-KENYA.**

Sahihi.....Tarehe.....

**Dkt. S. M. Obuchi**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

**ELDORET-KENYA**

**TABARUKU**

Tasnifu hii nawatabarukia:

Wazazi wangu Zeinabu Serem na Boaz Serem (Marehemu),

Mmenilea na kunikuza vyema,

Kama si nyinyi nisingefikia kiwango hiki,

Watoto wangu, Jamal, Husna, Leyla na Salim

Mmekuwa wanafunzi na walimu wangu maishani mwangu,

Mmevumilia kutokuwa nami nilipobukua vitabu,

Baraka na neema zake Mola ziwe nanyi siku zote maishani mwenu.

## SHUKURANI

Uandishi wa tasnifu ni kazi ngumu na ina changamoto kabambe. Hivyo, sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwa watu kadha wa kadha ambao walichangia kwa njia moja au nyingine katika kufaulisha tasnifu hii. Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa neema, aliyenijalia afya nzuri, nguvu na uwezo wa kutekeleza tasnifu hii. Kama si yeye yangukuwa vinginevyo. Amina!

Nina furaha kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu wa kiakademia: Dkt. Mosol Kandagor, ambaye pia ni mkuu wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika na Dkt. Obuchi Samuel kwa kunishauri, kunielekeza na kuniongoza vilivyo bila kuchoka nyakati zote nilipokuwa nikiandika kazi hii. Naomba mbarikiwe sana.

Sitawasahau wahadhiri wangu wote katika kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii: Prof. Peter Simatei, Fr. Prof. Kiruki Kahiga, Prof. Nathan Ogechi, Prof. Naomi Shitemi (marehemu), Dkt. Allan Opijah, na Bw. John Munyua kwa kuniongoza vyema masomoni. Pia Prof. Zaja Omboga (Chuo Kikuu cha Nairobi) na Dkt. Kipkosgei Sawe (Chuo Kikuu cha Kabianga). Mchango wenu katika kunishauri na kunikuza kitaaluma umeniwezesha kuibuka na tasnifu hii, nami kuitwa msomi. Kwenu nyote nasema asanteni sana.

Shukrani za kipekee ni kwa Bw. Isaac Chepkwony kwa kunitia moyo kila wakati, kunishauri na kwa fadhila zake tele. Ninakuombea nehema zake Mola. Nawashukuru pia wazamifu wenzangu tulioshuriana nao kitaaluma: Dkt. Tecla Muge, Dkt. Sarah Okyere, Bw. Wanyonyi Joseph, Bw. Abuga, Bw. Magugu na hasa Dkt. Ramadhan Kadallah kwa kunipa makala na vitabu vilivyoniauni na kuniongoza vilivyo katika tasnifu hii. Aidha, jamaa na marafiki walionihimiza kila mara, Mungu awakumbuke kwa sababu mlikuwa wa msaada mkubwa kwangu nilipowahitaji zaidi.

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kutambua tofauti za kitafsiri katika tamthilia zilizotafsiriwa za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (MMS) (Mwakasaka, 1979) na *Mkaguzi wa Serikali*, (MS) (Madumulla, 1999). Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni kuhakiki kiulinganishi mbinu za lugha katika MMS na MS kuchambua kiulinganishi uwasilishaji wa ujumbe katika MMS na MS, kuchanganua kiulinganishi uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika MMS na MS. Upeo wa utafiti huu ulijikita katika MMS na MS. utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uamilifu katika tafsiri mtazamo wa kuhakiki matini uliopendekezwa na Reiss (1977). Mihimili mikuu ya mtazamo huu ni: utambuzi wa kuhakikisha kuwa, kuna utoshelevu wa kimaana, kisarufi na kimtindo katika lugha lengwa kwa minajili ya kuuwasilisha ujumbe kwa wapokeaji wake, Kaida za matumizi ya lugha na uelewa ya kwamba kwa ajili ya mawasiliano maana ya neno hurejelewa kwa kuhusishwa na maneno mengine yanayohusiana na mada au muktadha wa diskosi unayozungumziwa, na kwamba matini pokezi inatarajiwa kudhihirisha mguso sawa na ule unaojitokeza katika matini asilia. Sampuli ya kimaksudi ilitumika katika uteuzi wa *Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mkakuzi wa Serikali* kwa sababu ni tamthilia zilizotafsiriwa na zinalenga matini asilia moja. Katika utafiti huu tulichunguza maonyesho yote yanayopatikana katika matini pokezi zilizoteuliwa. Ukusanyaji wa data ya tasnifu hii ulifanywa kwa kuzisoma kihakikifu matini zilizoteuliwa, kisha kuchanganua kiulinganishi mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na usawiri wa wahusika mintarafu ya malengo ya utafiti na kwa kuongozwa na nadharia ya Uamilifu katika Tafsiri, Kitengo cha kuhakiki Matini kilichopendekezwa na Reiss. Uwasilishaji wa data ulifanywa kiufafanuzi na matokeo ya uchunguzi huu yatachangia marejeleo yanayohusu tafsiri linganishi. Ildhihirika kuwa, mbinu za lugha, ujumbe au taarifa zilizowasilishwa na tabia za wahusika ni sifa bainifu zisizoweza kupuuzwa katika tafsiri linganishi. Aidha ilibainika kwamba, kuna tofauti katika matumizi ya mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uchanganuzi wa wahusika katika MMS na MS. Mtafiti anapendekeza kuwa, watafiti wa baadaye katika nyanja ya tafsiri linganishi wanaweza kushughulikia vitabu vingine tofauti na vilivyoshughulikiwa katika utafiti huu vilivyotafsiriwa na vinalenga matini asilia moja, huenda wakaibuka na matokeo tofauti. Hivyo, watafsiri wanaweza kupata kichocheo cha kutafsiri tena kazi za fasihi ambazo tayari zilishatafsiriwa. Washikadau katika uundaji wa silabasi ya Kiswahili katika vyuo vikuu wanaweza kutilia maanani kipengele cha Nadharia ya Uhakiki wa Matini katika kozi za tafsiri ili kuwawezesha wanafunzi kuwasilisha kazi za tafsiri zinazofaa zaidi. Isitoshe, utafiti huu utachangia kuibuka kwa tafiti za kuhakiki kiulinganishi vitabu vya fasihi vilivyotafsiriwa na watafsiri tofauti. Zaidi, utafiti huu utawafaa wanafunzi na wataalamu wa tafsiri linganishi.

## ABSTRACT

This research analysed comparatively the stylistic devices, the language used in presentation of themes and characters in the two Kiswahili translations: *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (MMS) by Mwakasaka, (1979) and *Mkaguzi wa Serikali* (MS) by Madumulla, (1999). The objectives of this study were: to analyze comparatively the stylistic devices used in the *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* and *Mkaguzi wa Serikali*, to comparatively critique the language used in the presentation of themes in the *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* and *Mkaguzi wa Serikali* and to compare and contrast the choice of vocabulary in the characterization in the two Kiswahili translation: *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* and *Mkaguzi wa Serikali*. The scope of the study was limited to the two Kiswahili translated texts: *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* and *Mkaguzi wa Serikali*. The research was guided by Functional Theory of translation, Text Type Approach by Reiss (1977). The key tenets of the Approach by Reiss (1977) state that any translation work: should comply with the target linguistic system, ought to be creative and aesthetically communicative, and should fit the context of the message and aspire to occupy a position in the target literature as any other original works of art. Purposive sampling was used in the selection of the two Kiswahili translations used in this research: *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* and *Mkaguzi wa Serikali*. When collecting data, the researcher read the selected texts and analyzed comparatively the stylistic devices, themes and characterization. Analytical research design was applied in this study whereby the researcher collected the data from the two texts and did a theory guided comparative analysis. Critical discourse approach was applied in undertaking comparative analysis, interpretation and explanation. Presentation of data was done through explanation of the findings basing on the research objectives and functional theory of translations; Text Type Approach by Reiss. From the study, the researcher found out significant differences in the stylistic devices, language used in the presentation of themes and characters. The researcher recommends that future researchers in the field of comparative literature can research on two or more translated texts with same original source and may come up with different results. Hence translators can be motivated to translate books which have already been translated. Syllabus designers can include different models of Discourse Analysis theory in Translation courses so as to assist students to present translations that are more accurate. The study will contribute to other comparative research texts translated by different translators. Further, this study will benefit both students and scholars of translation because it will give an highlight on the key elements of translation.

## YALIYOMO

IKIRARI .....	ii
SHUKURANI .....	iv
IKISIRI .....	v
ABSTRACT .....	vi
YALIYOMO .....	vii
ORODHA YA MAJEDWALI .....	xi
MAELEZO YA AKRONIMU .....	xii
MAELEZO YA ISTILAHU .....	xiii
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
<b>MISINGI YA UTAFITI .....</b>	<b>1</b>
1.0 Utangulizi .....	1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti .....	1
1.2 Suala la Utafiti .....	13
1.3 Malengo ya Utafiti .....	14
1.4 Nadharia Tete .....	14
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti .....	15
1.6 Umuhimu wa Utafiti .....	15
1.7 Mbinu za Utafiti .....	17
1.7.1 Sampuli na Usampulishaji .....	17
1.7.2 Njia za Kukusanya Data .....	18
1.7.3 Uchanganuzi wa Data .....	19
1.8 Hitimisho .....	21
SURA YA PILI .....	22
MAPITIO YA MAANDISHI NA MSINGI WA KINADHARI .....	22
2.0 Utangulizi .....	22
2.1 Dhana ya Tafsiri .....	22
2.2 Historia Fupi ya Tafsiri .....	27
2.3 Mbinu za Lugha Katika Tafsiri .....	30
2.4 Uwasilishaji wa Ujumbe katika Tafsiri .....	33
2.5 Usawiri wa Wahusika Katika Tafsiri .....	37
2.6 Misingi ya Kinadharia .....	44
2.7 Hitimisho .....	48
<b>SURA YA TATU .....</b>	<b>50</b>

<b>UHAKIKI LINGANISHI WA MBINU ZA LUGHA KATIKA MKAGUZI MKUU WA SERIKALI NA MKAGUZI WA SERIKALI.....</b>	<b>50</b>
3.0 Utangulizi.....	50
3.1 Chuku.....	50
3.2 Uzungumzi Nafsia .....	60
3.3 Misemo .....	64
3.4 Kinaya.....	66
3.5 Mbinu Rejeshi.....	68
3.6 Kejeli.....	73
3.7 Taswira.....	77
3.8 Matumizi ya Barua.....	78
3.9 Ukweli kinzani .....	84
3.10 Hadithi Ndani ya Hadithi .....	86
3.11 Tashihisi.....	88
3.12 Matumizi ya Ndoto .....	89
3.13 Hitimisho.....	91
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>93</b>
<b>UWASILISHAJI KIULINGANISHI WA UJUMBE KATIKA MKAGUZI MKUU WA SERIKALI NA MKAGUZI WA SERIKALI.....</b>	<b>93</b>
4.0 Utangulizi .....	93
4.1 Dhuluma.....	93
4.2 Matumizi Mabaya ya Mamlaka .....	96
4.3 Ufisadi.....	99
4.4 Kutowajibika.....	102
4.5 Unafiki .....	106
4.6 Matumizi ya Dawa za Kulevya.....	110
4.7 Hofu .....	113
4.8 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii .....	115
4.9 Hitimisho.....	122
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>123</b>
<b>UTEUZI WA MSAMIATI KATIKA USAWIRI WA WAHUSIKA KATIKA MKAGUZI MKUU WA SERIKALI NA MKAGUZI WA SERIKALI .....</b>	<b>123</b>
5.0. Utangulizi.....	123
5.1 Majina ya Wahusika katika Tamthilia za MMS na MS .....	123



5.2 Upangaji wa Majina ya Wahusika .....	125
5.2.1 Tofauti ya Idadi ya Wahusika katika MS na MMS .....	126
5.2.2 Nafasi ya Wahusika .....	126
5.3. Sifa na Tabia za Wahusika.....	127
5.3.1 Mkuu wa Wilaya (Meya) .....	127
5.3.1.1 Katili .....	128
5.3.1.2 Nafiki .....	132
5.3.1.3 Fiisadi.....	136
5.3.1.4 Mwenye Dharau.....	138
5.3.1.5 Mwenye Kuchanganyikiwa .....	140
5.3.2 Ghlestakovu/Hilestakov .....	141
5.3.2.1 Mpenda Anasa .....	141
5.3.2.2 Msomi .....	144
5.3.2.3 Asherati .....	145
5.3.2.4 Msaliti .....	148
5.3.2.5 Mtovu wa Nidhamu .....	150
5.3.2.6 Asiyewajibika .....	151
5.3.2.7 Mwenye Madharau .....	152
5.3.4 Bwana Hakim/Jaji.....	157
5.3.4.1 Asiyewajibika .....	158
5.3.4.2 Fisadi.....	160
5.3.4.3 Asherati .....	161
5.3.4.4 Mratibu wa Elimu/Mkaguzi wa Mashule .....	163
5.3.4.5 Asiyewajibika .....	163
5.3.4.6 Anna/Ann .....	165
5.3.4.7 Asherati.....	166
5.3.4.8 Mbishi .....	168
5.3.5 Maria/Marya .....	170
5.3.5.1 Mpenda Urembo .....	170
5.4 Hitimisho.....	172
<b>SURA YA SITA.....</b>	<b>174</b>
<b>HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>174</b>
6.0 Utangulizi.....	174
6.1 Muhtasari wa Tasnifu .....	174

6.2 Matokeo ya Utafiti .....	175
6.2.1 Mbinu za Lugha .....	176
6.2.2 Uwasilishaji wa Ujumbe .....	176
6.2.3 Uteuzi wa Msamiati katika Usawiri wa Wahusika .....	177
6.3 Mchango wa Utafiti .....	178
6.4 Mapendekezo ya Utafiti .....	179
MAREJELEO .....	181
KIAMBATISHO: (DATA) .....	186

**ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali 5.1: Ulinganishaji wa majina katika Tafiri za: MMS na MS .....	125
Jedwali 5.3.5: Tafiri za Majina kulingana na Nafasi za Wahusika .....	126

## MAELEZO YA AKRONIMU

Akronimu tulizotumia katika tasnifu hii ni zifuatazo:

HA	Hadhira Asilia
HL	Hadhira Lengwa
LC	Lugha Chanzi
LP	Lugha Pokezi
MA	Makala Asilia
MA	Matini Asilia
MC	Matini Chanzi
ML	Matini Lengwa
MMS	Mkaguzi Mkuu wa Serikali
MP	Makala Pokezi
MP1	Makala Pokezi 1
MP2	Makala Pokezi 11
MS	Mkaguzi wa Serikali
MT	Matini Tafsiri
TA	Tamthilia Asilia
TC	Tamthilia Chanzi
TT	Tamthilia Tafsiri

**MAELEZO YA ISTILAHU**

Dhamira	Lengo kuu la mwandishi katika kazi ya fasihi
Fani	Jumla ya mbinu za lugha, ujumbe na usawiri wa wahusika
Tafsiri huru	Hali ya mtafsiri kuteua msamiati kwa minajili ya kurithisha hadhira lengwa
Ubunifu	Hali ya msanii kuibuka na wazo au jambo fulani katika fasihi
Uhawilishaji	Uhamishaji wa maana ya ujumbe katika tafsiri.
Ujumbe	Maswala yoyote muhimu katika kazi ya fasihi

## SURA YA KWANZA

### MISINGI YA UTAFITI

#### 1.0 Utangulizi

Sura hii inahusu usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti, nadharia tete, upeo na mbinu za utafiti. Aidha sehemu hii inafafanua dhana za uhakiki na tafsiri ambazo ndizo vipengele muhimu katika tasnifu hii. Sehemu hii imeanza kwa kushughulikia usuli wa suala la utafiti.

#### 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Katika utafiti huu, nimehakiki kiulinganishi fani katika tafsiri mintarafu ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Mwakasaka, 1979) na *Mkaguzi wa Serikali* (Madumulla, 1999). Nimechunguza tofauti za kitafsiri katika uhawilishaji wa ujumbe katika tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (MMS) (Mwakasaka 1979) ambacho ni tafsiri ya tamthilia ya Kiingereza ya *Government Inspector* (kilichotafsiriwa kutoka tamthilia ya Kirusi *The Revizor* (Gogol 1836) na kulinganisha na tamthilia ya *Mkaguzi wa Serikali* (MS) (Madumulla, 1999) kilichotafsiriwa kutoka tamthilia ya *The Revizor* (Gogol, 1836) ambayo tafsiri yake ya Kiingereza ni *Government Inspector*.

Fani katika utafiti huu, ilijumuisha mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika tafsiri za MMS na MS. Kabla ya kuhakiki kiulinganishi fani katika tasnifu hii, ilikuwa muhimu kuelezea dhana za uhakiki na tafsiri. Kulingana na Njogu na Chimera (1999) kitenzi “kuhakiki” kina maana ya kupata hakika au ukweli wa jambo. Wataalamu hao wanaeleza kuwa katika kuhakiki kazi za fasihi, wahakiki huchunguza vipengele kadhaa ambavyo ni pamoja na dhamira, matumizi ya lugha, usawiri wa wahusika, maudhui na kufanikiwa au

kutofanikiwa kwa msanii katika kuwasilisha malengo yake. Yaani uhakiki huvyanza masuala yote ya uandishi katika matini za fasihi.

Watafsiri wengi wametafsiri vitabu mbalimbali kutoka lugha moja hadi nyingine lakini kazi zinazohusu ulinganishi wa matini za fasihi zilizotafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili ni chache. Tafsiri linganishi basi ni uwanja mpya ambao haujazamiwa sana na katika mkabala huo, utafiti huu ni wa kipekee kwa kuwa unahusu uhakiki linganishi wa fani katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (MMS) na *Mkaguzi wa Serikali* (MS).

Katika tasnifu hii hatukulinganisha tafsiri pokezi za MMS na MS na tafsiri chanzi yoyote kwani tulichukulia Tafsiri Pokezi hizi mbili kama vitabu vinavyojitegemea kwa kuwa aghalabu kazi ya tafsiri ni kazi ya kibunifu. Kwa mfano katika tamthilia ya MMS, kwenye utangulizi, Mwakasaka (1979: iii) anaeleza kuwa:

“Tafsiri hii inafuatia sana tafsiri ya Kiingereza (*The Government Inspector*) ya D.J. Campbell. Mabadiliko kidogo sana yamefanywa: nimekata maelezo ya jukwaani kila nilipoona kuwa sio ya lazima. Nimemwita Meya, Mkuu wa Wilaya ambaye kwa kweli huko Urusi alikuwa mkuu wa usalama wa mji ili mchezo ueleweke na uwe na uzito zaidi. Nimeyapa majina ya Kirusi matamshi ya Kiswahili na nimetumia vitu vinavyopatikana na kutumika huku kwetu badala ya vile vya Kirusi ambavyo hatunavyo na ungefanya mchezo usieleweke vizuri. Kwa mfao nimetumia shilingi badala ya “rubo” na tena bila kujali tofauti ya thamani zake”.

Kwenye ukumbi wa utangulizi katika tamthilia ya MS, Rifat Pateev katika Madumulla (1999: iv) anaeleza kwamba;

“Tafsiri ya kwanza ya *Mkaguzi wa Serikali* ilifanywa na Bw. Christian Mwakasaka ...1979. Hata hivyo mtafsiri alifanya kazi inayostahili sifa. Tafsiri hii ni ya pili na imefanywa na Dr. Joshua Madumulla. Tafsiri hii imefanywa kwa kuzingatia tamthilia ya Kirusi jinsi ilivyoandikwa na Gogol ikiwa na matendo matano. Ni matumaini yetu kuwa tafsiri hizi mbili zinautajirisha uga wa tafsiri linganishi pia.”

Ingawa Rifat (katika Madumulla, 1999) anaeleza kwamba Mwakasaka anafaa kupewa sifa katika kazi yake ya kutafsiri tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* lakini

haijulikani ni kwa nini Madumulla aliamua kukitafsiri kitabu ambacho tayari kilikuwa kimetafsiriwa. Katika utafiti huu, tulidahili kuwa, huenda Madumulla alitaka kurekebisha makosa ya kitafsiri aliyoyaona katika MMS. Aidha, kuna uwezekano kwamba katika tafsiri yake, Madumulla alishawishiwa kwa kiasi kikubwa na kazi ya Mwakasaka. Yaani, Madumulla aliisoma kazi ya Mwakasaka kabla ya kufanya tafsiri yake ya MS kwa kuwa ametafsiri tamthilia ya MS miaka ishirini baada ya kutafsiriwa tamthilia ya MMS.

Ninahoji kuwa MMS na MS zilitafsiriwa kutoka matini chanzi moja, *The Revizor* (Gogol 1836), ndio maana hakuna tofauti kubwa ya dhamira, maudhui na wahusika katika tafsiri hizo mbili. Hata hivyo, kuna ushahidi kwamba ipo tofauti katika uhawilishaji wa ujumbe baina ya tamthilia za MMS na MS ambao ulisababisha kuibuka kwa utafiti huu unaochangia katika taaluma ya fasihi linganishi.

Coombes (1969) anadahili kwamba uhakiki unahusu kusaili, kutathmini, kuweka katika mpangilio sawa na hata kulinganisha kazi moja na nyingine. Aidha, mtaalamuu huyu anadai kuwa mhakiki bora hutupa maoni yake kamili na yaliyo wazi kuhusu falsafa ya mtunzi wa tamthilia, shairi au tungo lolote ili kutuwezesha kufurahia kazi ile pamoja na kuelewa tajriba iliyomo katika utunzi. Jambo muhimu analosisitiza Coombes ni kwamba uhakiki wa kifasihi hujikita katika hisia za wahakiki. Kwa hivyo tulipaswa kuihakiki kazi yoyote ile ya sanaa kwa misingi ya athari inayotoka kwa hisia zetu halisi. Yaani, uhakiki ni somo linalohusika na kueleza, kuainisha, kutathmini na kupima kazi za fasihi lakini sio kuitafutia makosa. Kwa hivyo, kuhakiki kazi za fasihi ni kitendo cha kitaaluma kuhusu jinsi maoni ya msomaji yanavyofungamana na matini husika.



Linalodhihirika kutokana na maelezo ya wataalamu tuliwarejelea hapo juu ni kwamba uhakiki ni tendo linalolenga kueleza na kuchunguza kwa makini kazi ya fasihi. Kazi ya uhakiki wa fasihi inahusu kutathmini na kueleza, kuainisha na kutoa maoni kuhusiana na kazi ya mtunzi. Kwa hivyo, mchakato wa kuhakiki kazi za fasihi husaidia wasomaji wa fasihi kuelewa na kubaini ujumbe muhimu wa kazi husika. Mchakato wa tafsiri ni taaluma muhimu sana katika maisha ya kila siku ya mwanadamu na ni jambo ambalo haliwezi kuepukika kwa kuwa maendeleo ya sayansi na teknolojia yamesababisha kuwepo kwa utandawazi. Hivyo imekuwa rahisi na upesi mno kwa wanadamu kutoka maeneo mbalimbali ya ulimwengu kutangamana katika shughuli za kila siku. Katika harakati za kutangamana, shughuli za tafsiri huwa jambo muhimu kwa vile hufanikisha mawasiliano kati ya watu wa jamii mbalimbali.

Bistin (2006) anadai kuwa, karne ya ishirini ndiyo Karne ya tafsiri, yaani karne yenye matumizi mengi ya kazi za tafsiri kutokana na mabadiliko na maendeleo katika nyanja tofautitofauti maishani. Kabla ya kutafsiri matini yoyote ile ni sharti kuwepo na Makala Asilia (MA) ambayo baada ya kutafsiriwa tulipata Makala Pokezi (MP) ama Matini Tafsiri (MT). Kwa hivyo katika mchakato wa tafsiri ni lazima maandishi fulani ambayo yanatarajiwa kutafsiriwa yawepo. Fasihi andishi ilianza miaka ya 1500 –1662 baada ya Masiah (Abdullaziz, 1979, Knappert, 1979, Wamitila 2001, 2002, Massamba, 2002).

Kuna kazi nyingi mno za fasihi andishi za Kiswahili hasa zilizotafsiriwa kutoka lugha na tamaduni nyingi za ulimwengu. Hii ni kwa sababu Kiswahili kilitagusana na lugha na tamaduni nyingi wakati wageni kutoka nchi mbalimbali walizuru nchi za Afrika Mashariki katika shughuli za biashara na za kidini. Tafsiri za fasihi andishi za Kiswahili zimechangia katika maendeleo ya kijamii, kitamaduni na kiuchumi hasa katika nchi za Afrika Mashariki. Mtafsiri wa matini yoyote anapaswa kuwa na ufahamu na umilisi wa

lugha zote zinazohusika, yaani lugha chanzi (LC) na lugha pokezi (LP). Tafsiri ni mchakato wa kubadilisha ishara au viwakilishi vingine na ni utoaji wa mawazo na fikra kutoka lugha moja hadi nyingine, yaani lugha chanzi (LC) hadi lugha pokezi (LP).

Tafsiri hutegemea kwa kiasi kikubwa muktadha wa jamii husika kwa kuwa jamii mbalimbali hutofautiana za kiutamaduni na kimazingira kwa kutegemea mapisi ya kila mojawapo. Kwa hivyo ni wazi kuwa katika shughuli ya tafsiri, kipengele cha lugha hakiwezi kuepukika na pia ubadilishaji wa mawazo, fikra na ujumbe. Scholes (1972), Shitemi (1990) na Omboga (1986) wanadahili kuwa ufahamu wa utamaduni unaozungumziwa na msemaji au unaoandikiwa na mwandishi, na utamaduni wa wasikilizaji na wasomaji ni muhimu kwa tafsiri inayotekelezwa. Wataalam hao pia wanadai kuwa mtafsiri au mkalimani atafaulu katika kutekeleza kazi yake iwapo anaelewa utamaduni wa lugha asilia kwani bila kuelewa hatapokea maana inayowasilishwa na msemaji au mwandishi asilia. Licha ya kuelewa utamaduni wa lugha asilia, ni sharti mtafsiri aelewe utamaduni wa hadhira yake, hali hii itamsaidia anaposhughulikia ujumbe na dhamira katika mchakato wa tafsiri. Swali linaloibuka hapa ni kuwa, kwa nini kazi ya tafsiri itekelezwe? Tafsiri hutekelezwa kwa madhumuni ifuatayo:

- a) Kupanua usomaji ili kuwezesha wasomaji wa lugha mbalimbali kuelewa matini ya lugha chanzi. Kwa mfano *So Long a Letter* (Ba, 1979) ni kitabu kilichotafsiriwa katika Kiswahili kama *Barua Ndefu Kama Hii* (Maganga, 1994). Hivyo basi wasomaji wa Kiswahili waliweza kuilewa barabara kazi ambayo ilikuwa imeandikwa kwa Kiingereza.
- b) Kufasiri upya yaliyo katika kazi chanzi. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Masaibu ya Ndugu Jeru* (Yahya, 1974), mtafsiri ametumia mandhari ya Kiislamu ilhali

katika matini asilia, *The Trials of Brother Jero* (Soyinka, 1964), mandhari yanayoangaziwa ni ya Kikristo. Huenda katika *Masaibu ya Ndugu Jero*, mtafsiri alitaka kuridhisha hadhira lengwa, kwa kuwa aliiandikia mazingira ya pwani ambapo asilimia kubwa ya watu katika jamii hiyo ni waislamu.

- c) Kubadilisha mtindo katika lugha lengwa. Kwa mfano, kuna kazi ambazo hutafsiriwa kwa kumega, yaani kwa kuwacha nje hadithi nyingine za matini chanzi. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Shetani Msalabani* ambayo ni tafsiri ya *The Devil on the Cross* Thiong'o, (1980), mwandishi alipuuzua maudhui ya umasikini na ukabila. Pia mwandishi wa *Nchi bila Mgurumo* ambayo ni tafsiri ya *The Land Without Thunder* (Ogot, 1966) alipuuzilia mabli maudhui mengine.

Lengo kuu la mtafsiri ni kuzalisha matokeo yanayofanana na yaliyowasilishwa na mwandishi wa matini asilia kwa msomaji katika lugha lengwa. Kazi yoyote ya tafsiri huhitaji ujuzi wa kiisimu pamoja na ubunifu wa mtafsiri. Picken (1993) anaeleza kuwa rasilimali muhimu kwa mtafsiri ni tajriba yake katika maisha. Hii ni kwa sababu tajriba humsaidia mtafsiri katika kuamua ni mbinu gani atakayotumia katika tukio maalum.

Kutokana na maoni ya wataalam mbalimbali, ni bayana kuwa katika kazi ya tafsiri, kuna maswala kadhaa ya kuzingatiwa kama vile, masuala ya kiutamaduni, kimazingira, tajriba ya mtu binafsi katika maisha na matumizi na ubunifu wa lugha. Bila shaka masuala hayo ndiyo yanayochangia kuwepo kwa watafsiri wengi wa matini asilia moja. Tafsiri ina historia ndefu kwa kuwa maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisayansi tuliyoyafurahia leo duniani yalitokana na juhudi za watu wa kale na yametufikia kwa njia ya tafsiri (Mwansoko, 1996).

Mwansoko (1996) pia anadahili kuwa inakisiwa kwamba, mwaka wa 3000 (KK), Elephantine, Mfalme wa Misri aliona maandishi ya lugha mbili tofauti ambayo yalikuwa yakizungumzia ujumbe wa makala moja. Mfalme huyo alitambua kwamba maandishi hayo yalikuwa tafsiri za makala moja na kufikia mwaka wa 3000 (KK), makala zilizotafsiriwa zilitumika barani Uropa kueneza tamaduni, maarifa na teknolojia miongoni mwa mataifa ya Ulaya. Uyunani kwa mfano iliathiri Dola ya Warumi kimaisha kutokana na tafsiri na pia kupitia kwa tafsiri, Warumi nao waliathiri tamaduni zingine za Ulaya.

Abdulaziz, 1979 na Mulokozi 1995 wanadahili kwamba maendeleo ya kisayansi na kiviwanda katika karne ya kumi na saba na kumi na nane yalisababisha kuwepo kwa haja ya kazi za tafsiri. Kwa mfano, ni bayana kuwa bidhaa zilizouzwa katika nchi mbalimbali zilihitaji maelezo kwa lugha mbalimbali. Hivyo basi mchakato wa tafsiri ukawa ni muhimu ili kuwezesha bidhaa hizo kuuzika katika jamii husika. Aidha, taaluma ya tafsiri iliwezesha Wajerumani na Waingereza kutafsiri Biblia kutoka lugha ya Kigiriki.

Wataalamu hawa pia wanadai kwamba Martin Luther alitafsiri Biblia ya Kigiriki kwa lugha ya Kijerumani (1522 BK). Aidha, mfalme James wa Uingereza aliidhinisha tafsiri ya Biblia kutoka lugha ya Kigiriki hadi ya Kiingereza (1611 BK). Kwa mujibu wa Abdulaziz, 1979, Mulokozi 1995, Mutiso 1996, Wamitila 2001, 2002, na Massamba, 2002, vitabu vingi vya fasihi ya Kiswahili ni tafsiri kutoka lugha na tamaduni anuwai. Hii ni kwa kuwa kumekuwepo na mwingiliano wa fasihi ya Kiswahili na tamaduni nyingi za nchi mbalimbali. Fasihi andishi ilianzishwa takriban kati ya mwaka wa 1500-1662 BK au 937 -1062. Vitabu vya fasihi ya Kiswahili

vilivyotafsiriwa kutoka lugha nyinginezo vimechangia mno historia na maendeleo ya Kiswahili.

Tunahoji kwamba kuna wataalam wa fasihi wanaoienzi fasihi ya Kiswahili na kwa upande mwingine kuna wale wanaoikashifu. Kwa mfano kuna tafiti ambazo zinahusu upungufu uliomo katika kazi za Kiswahili zilizotafsiriwa, yaani tafiti ambazo hukashifu vitabu vya Kiswahili vilivyotafsiriwa. Kwa mfano, Mwansoko (1996) na wataalam wengine walitafitia makosa yanayopatikana katika vitabu vya Kiswahili vilivyotafsiriwa kwa kujikita katika makosa ya kiisimu, kijamii na kitamaduni.

Tafsiri za fasihi pia huonekana kama njia ya kuwezesha fasihi za kigeni kukubalika katika lugha pokezi, kiisimu, kijamii na kitamaduni, (Neubert na Shreeve 1992). Aghalabu mchango wa fasihi za kigeni katika lugha pokezi kupitia mchakato wa tafsiri iliweza kuwa wa manufaa kwa lugha na fasihi. Ni bayana kuwa kazi za tafsiri kama vile kazi ya Nyerere: *Mabepari wa Venisi* ambayo ni tafsiri ya *The Merchant of Venice*, *Barua Ndefu kama Hii* ambayo ni tafsiri ya *So Long a Letter* (Ba 1994) na *Utenzi wa Kalevala* ambayo ni tafsiri ya *The Kalevala* (Knappert, 1992) ziliibua tamaduni mpya katika jamii za lugha lengwa.

Omboga (2006) anadai kwamba, kuna kazi zingine za tafsiri ambazo zilitekelezwa kiholela. Kwa mfano, mtaalamuu huyu anakashifu tamthilia ya *Usaliti Mjini iliyotafsiriwa kutoka tamthilia ya Kiingereza ya Betrayal in the City* (Kisia na Wasyatsa 1994). Omboga anadai kwamba watafsiri hao walipuuza kabisa matini asilia na kuibuka na kazi tofauti mno. Hivyo, Omboga anadai kwamba hiyo ni kazi mbaya kwa kuwa siyo tafsiri ya matini chanzi lakini inazua tu suitafahamu.

Mwansoko (1996) anasema kwamba, katika karne ya 19, wamishenari walitafsiri vitabu vingi vya Kikristo ikiwemo Biblia kwa Kiswahili na kwa baadhi ya lugha za makabila makubwa ya Tanzania. Mtaalamu huyu anaeleza kuwa wakati wa ukoloni baadhi ya vitabu vilivyotafsiriwa ni pamoja na: *Hekaya za Abunwasi na Hadithi Nyingine, Alfu Lela Ulela, Siku Elfu na Moja na Hadithi za Esopo*. Munday (2001) anadai kuwa, katika miaka ya 1970 na 1980 kuliibuka mabadiliko katika mchakato wa tafsiri kule Ujerumani. Kwamba kuliibuka mabadiliko kutoka tafsiri sisisi au ya neno kwa neno na kukaibuka aina ya tafsiri ya kuzingatia uamilifu na umuhimu wa mawasiliano katika tafsiri.

Baada ya uhuru katika nchi za Afrika Mashariki, wazalendo walifanya juhudi za kuvitafsiri vitabu mbalimbali katika Kiswahili. Kwa mfano, Mwalimu Julius Nyerere aliitafsiri *The Merchant of Venice* na kuiita *Mabepari wa Venisi*. Pia Nyerere aliitafsiri *Julius Caecar* ikawa *Juliasi Kaizari*. Naye Paul Sozigwa alitafsiri kitabu cha *Song of Lawino* na kukiita *Wimbo wa Lawino*.

Wakati uvumbuzi wa mashine ya kupiga chapa ulipotekelezwa na Gutenberg (1456), Biblia ilitafsiriwa katika lugha 33 za ulimwengu (Mertzer 1992). Mtaalamu huyu anadai kuwa kulingana na watafiti mbalimbali, idadi ya lugha ulimwenguni ni 6,170. Mertzer (1992) anasema kuwa mnamo mwaka wa 600 kabla ya Kristo Biblia ilikuwa imetafsiriwa katika lugha nane za ulimwengu. Aidha, katika karne ya kumi na tisa, Biblia ilitafsiriwa katika lugha zaidi ya 40 za ulimwengu.

Isitoshe, Mwansoko (1996) anadai kwamba katikati ya karne ya 20, Biblia ilikuwa imetafsiriwa katika takriban lugha mia tano na kufikia mwaka wa 1991, Biblia ilikuwa imetafsiriwa katika lugha na lahaja 1,946. Kufikia sasa inakisiwa kuwa asilimia themanini ya watu wana angalau nakala moja ya Biblia iliyotafsiriwa katika

lugha yao ya mama. Hivyo basi ni dhahiri kwamba Biblia ndio matini ambayo imetafsiriwa katika lugha nyingi za ulimwengu kuliko kazi nyingine yoyote ya fasihi.

Olgierda na Achenbach (2004) wanadai kuwa, Biblia ya kwanza haikuwa imeandikwa katika Kiingereza wala Kiswahili. Watalamu hao wanasema kuwa, Agano la Kale la Biblia liliandikwa katika Kiebrania na Agano Jipya likaandikwa kwa Kiyunani. Hivyo basi, wakalimani walikuwa wanatumika ili kuwasilisha ujumbe wa mahubiri kutoka lugha ya Kiibrania au Kiyunani hadi lugha zingine kama vile lugha ya Kiingereza, Kifaransa na Kijerumani. Olgierda na Achenbach (2004) pia wanadai kuwa maendeleo ya ukalimani yaliambatana na yale ya tafsiri. Aidha, wataalam hao wanadahili kuwa, mnamo mwaka wa 1480, makanisa ya kiprotestanti yaliendelea kusesitiza maendelezi ya tafsiri ya Biblia katika lugha nyinginezo.

Kufikia karne ya kumi na tisa, wamishenari waliotoka Ulaya walizuru Afrika Mashariki ili kueneza dini ya Kikristo na walianza kujifunza lugha ya Kiswahili ili waweze kuwasiliana na wenyeji wa pwani. Dkt Krapf ndiye mmishenari wa kwanza aliyeanzisha kazi ya umishenari mnamo Agosti (1846). Dkt. Krapf aliweza kujifunza lugha ya Kiswahili kwa sababu alipata Waafrika walioshirikiana naye. Waafrika hao, kama anavyodahili (Mbaabu 1991, 1985), walimsaidia Krapf katika kufanya ukalimani na tafsiri. Krapf alitafsiri Biblia ya Kiingereza hadi Kiswahili, akaandika kamusi ya kwanza ya Kiswahili na kisha akaandika kitabu cha sarufi ya Kiswahili.

Biblia imetafsiriwa katika lugha mbalimbali za ulimwengu, yaani watafsiri wengi wametafsiri matini hiyo moja. Licha ya kuwa Biblia imetafsiriwa katika lugha mbalimbali, pia kuna suala la suitafahamu kwa kuwa katika lugha moja mahususi pia kuna uwezekano wa kuwa na fasiri mbalimbali za matini chanzi moja. Kwa mfano, Biblia ya Kiingereza imefasiriwa na watafsiri mbalimbali na katika tafsiri za

Kiingereza kuna; *Revised Standard Bible, The Holy Bible, Good News Bible, The Gideons Bible* na *King James Bible*.

Fasiri mbalimbali za Biblia zimeibuka kwa kuwa katika mchakato wa tafsiri, kila mtafsiri ana namna yake ya kuteua msamiati na huathiriwa na mazingira ya kulelewa, masuala ya kiutamaduni na tajriba ya mtu binafsi katika maisha. Aidha, kuna vitabu vya fasihi ambavyo vimetafsiriwa na wasanii tofauti tofauti. Kwa mfano, Farahzad (2009) alihakiki kazi zilizotafsiriwa na wataalamu wawili waliotafsiri kwa Kiingereza tamthilia Kiamarekani inayoitwa *Gone with the Wind*. Mtaalamu huyu alichunguza kiulinganishi tofauti katika ujumbe, dhamira na usawiri wa wahusika. Kwa kuwa kila mtu ana namna yake ya kusoma na kufasiri kazi ya fasihi, tulipata makala anuwai za matini asilia. Kwa mfano, Bahrami (2001) na Safavian (2009) walitafsiri tamthilia ya *Things Fall Apart (1958)* katika lugha ya Kiajemi.

Katika utafiti huu, tulihakiki kiulinganishi tamthilia zilizotafsiriwa ambazo ni MMS, (Mwakasaka, 1979) na MS (Madumulla, 1999). Mwakasaka na Madumulla ni watafsiri kutoka Tanzania. Huenda ikawa Madumulla (1999) alipotekeleza tafsiri yake alikuwa na lengo la kurekebisha makosa ya kitafsiri aliyoyabaini katika kazi ya Mwakasaka (1979). Hata hivyo, swali linaloibuka ni je, tafsiri za Mwakasaka na Madumulla zinatofautiana kwa nini? Tulidahili kuwa inaelekea tafsiri za watafsiri hao zinatofautiana katika uhawilishaji kwa kuwa wameathiriwa na masuala ya kiutamaduni, tajriba na taaluma zao mbalimbali.

Katika utafiti huu nilinua kubainisha iwapo kuna tofauti katika uhawilishaji wa ujumbe katika tafsiri za MMS na MS. Kwa hivyo, tasnifu hii inachunguza kiulinganishi jinsi vipengele vya fani; (mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na usawiri wa wahusika) vimejitokeza katika tafsiri za Kiswahili za MMS, na MS.



Tulihakiki tamthilia hizo na kubainisha tofauti za kitafsiri baina ya MMS na MS. Kwa mujibu wa uchunguzi wetu, hatujakutana na utafiti mwingine ambao umeshughulikia uhakiki linganishi wa vitabu viwili vya Kiswahili vilivyotafsiriwa kutoka katika matini asilia moja.

Katika kuchunguza tofauti hizo, tulijikita katika matini pokezi mbili: MMS na MS pasipo kuzingatia matini chanzi yoyote, yaani, ingawa MMS na MS ni tafsiri za matini chanzi ya Kirusi (*The Revizor*) iliyotafsiriwa katika Kiingereza kama *The Government Inspector*, katika utafiti huu tulihakiki kilinganishi vitabu hivyo pasi na kuvilinganisha na matini chanzi yoyote. Hivyo, tulichunguza kiulinganishi tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali* kama vitabu vya fasihi vilivyotafsiriwa na vinavyojitegemea. Katika tamthilia tafsiri za MMS na MS, maudhui makuu yanayojitokeza ni; uongozi mbaya uliojawa na dhuluma, ufisadi na unafiki.

Mtafsiri kwa kweli kabla hajaitwa mtafsiri ni msomaji, na kama msomaji ana misimamo yake na anaweza kushawishika kwa namna yake. Mwakasaka na Madumulla ni wasomaji na kabla ya kutafsiri walifasiri matini chanzi kulingana na tajriba yao katika maisha. Tulihoji kuwa, huenda Madumulla (1999) alishawishiwa na tafsiri ya MMS, Mwakasaka (1979). Kutokana na maoni ya Munday (2001), kazi ya kifasihi ni kazi ya kibunifu, kwa hivyo watafsiri wanapoingiza kazi waliyofasiri katika tafsiri, hushurutishwa kuwajibika na mambo yafuatayo:

1. Kumwajibikia mwandishi wa matini chanzi kwa kuwa waaminifu.
2. Kuwajibikia hadhira inayolengwa katika tafsiri.
3. Kuwajibikia lugha ya matini lengwa; ijitosheleze kiisimu, kimatumizi na kiuamali.

Mambo hayo matatu tuliyoyataja yanaweza kuathiri ufasiri wa mtafsiri kwa kujua au kutojua. Aidha, Munday (2001), anadahili kwamba, jambo muhimu katika tafsiri ni kuhamisha ujumbe wa matini asilia hadi matini lengwa kama alivyoandika mwandishi wa matini asilia. Watafsiri, katika mchakato wa tafsiri, wana uhuru wa kuteua msamiati wanavyotaka ili kuridhisha hadhira lengwa. Mtafsiri anapoteua msamiati, huongozwa na mazingira anayotafsiria, tajriba ya maisha katika jamii na utamaduni wa jamii husika. Ndiposa katika utafiti huu tulibainisha tofauti iliyopo baina ya uwasilishaji wa ujumbe katika MMS na MS.

Maoni hayo kuwa kuna uwezekano wa watafsiri wawili au zaidi waliotafsiri matini chanzi moja kutofautiana katika uwasilishaji wa ujumbe ndiyo yaliyoibua suala la utafiti tulilolishughulikia katika sehemu ifuatayo.

## **1.2 Suala la Utafiti**

Kuna tafsiri nyingi katika fasihi ya Kiswahili zilizotekelezwa na mtafsiri mmoja na zinatokana na matini chanzi moja. Hata hivyo, kuna uwezekano wa kuwa na watafsiri wawili au zaidi ambao wamekitafsiri kitabu kimoja au matini chanzi moja. Katika utafiti huu, tulihakiki kiulinganishi matini pokezi mbili: *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*, (Mwakasaka, 1979) na *Mkaguzi wa Serikali* (Madumulla, 1999). Tulichukulia matini pokezi hizo kama tamthilia zilizotafsiriwa na zinajitegemea kwa sababu kazi y tafsiri ni kazi ya kiubunifu.

Mwakasaka na Madumulla walitafsiri katika mazingira na wakati tofauti. Kwa hivyo, kuna ushahidi kuwa namna watafsiri hao walivyohawilisha ujumbe wa matini pokezi ulitofautiana. Kimsingi, namna mtafsiri anavyoelewa na kufasiri ujumbe huathiri jinsi atakavyowasilisha mawazo ya msanii wa matini asilia kwa wasomaji. Maoni hayo

kuwa watafsiri wanaweza kufasiri kazi ya fasihi katika mitazamo mbalimbali kwa kutegemea kuelewa kwao kwa ujumbe husika ndiyo kichocheo cha utafiti huu.

Katika hali hiyo basi, suala muhimu lililoibuka na lilihitaji kujibiwa kupitia utafiti huu lilikuwa: Je, kuna tofauti gani katika uhawilishaji wa: mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika baina ya tafsiri za MMS na MS? Ili kushughulikia suala hilo, katika utafiti huu tuliongozwa na malengo ya utafiti yanayojitokeza katika sehemu ifuatayo.

### **1.3 Malengo ya Utafiti**

Katika utafiti huu, tulinuia kutimiza malengo yafuatayo;

- a) Kuhakiki kiulinganishi mbinu za lugha katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*.
- b) Kuchambua kiulinganishi uwasilishaji wa ujumbe katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*.
- c) Kuchunguza kiulinganishi uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*.

### **1.4 Nadharia Tete**

Katika utafiti huu tuliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

- a) Mbinu za lugha zilizotumiwa na watafsiri wa MMS na MS zinafanana.
- b) Kuna tofauti kubwa katika uwasilishaji wa ujumbe katika MMS na MS.
- c) Uteuzi wa msamiati wa usawiri wa wahusika ulitekelezwa kwa namna inayofanana katika tamthilia za MMS na MS.

### **1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Katika utafiti huu, tulijikita katika upeo na mipaka mahsusi. Yaani, tulihakiki kiulinganishi, tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Mwakasaka, 1979) na *Mkaguzi wa Serikali* (Madumulla, 1999). Tulijikita katika ulinganishaji wa vipengele vya fani ambavyo ni mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe pamoja na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika tamthilia MMS na MS. Nadharia ya Uamilifu katika Tafsiri (kitengo cha kuhakiki matini) iliongoza utafiti huu na maelezo kuhusu nadharia hiyo yamefafanuliwa kwa kina katika sura ya pili.

Katika tasnifu hii, tulinuia kuchunguza iwapo mbinu za lugha kama vile chuku, tashbihi, jazanda, uzungumzi nafsia, matumizi ya ndoto, misemo na nahau zinatofautiana katika MMS na MS. Kwa mujibu wa utafiti huu, ujumbe ni jumla ya masuala makuu yanayoshughulikiwa katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*. Kwa misingi hiyo, utafiti huu ulichunguza tofauti iliyopo katika uhawilishaji wa ujumbe katika MMS na MS. Ujumbe ulioshughulikiwa ni; ufasidi, dhuluma, unafiki, matumizi mabaya ya mamlaka, usaliti na kutowajibika.

Katika mchakato wa tafsiri, mtafsiri hana budi kufahamu shughuli za wahusika katika fasihi ili aweze kuelewa barabara falsafa na msimamo wa msanii wa matini chanzi. Kwa hivyo, nimechunguza kiulinganishi usawiri wa wahusika katika MMS na MS. Wahusika walioshughulikiwa ni kama vile; Mkaguzi Mkuu wa Serikali (Meya), Ghlestakov/Hilestakov, Anna/Ann na Maria/Marya. Sehemu ifuatayo inaangazia umuhimu wa utafiti huu.

### **1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Wataalamu wengi wamejihusisha na suala la tafsiri kwa mikabala tofauti kama tulivyobainisha katika usuli wa suala la utafiti (sehemu ya 1.1). Kwa mfano, baadhi ya

watalamu wametafsiri tamthilia, riwaya, ushairi, vitabu vitakatifu kama vile Biblia na Koran, katiba na makala nyinginezo. Hata hivyo, kuna masuala mengine ambayo hayajashughulikiwa kama vile kwa nini matini moja itafsiriwe na watafsiri tofauti na kuibuka na kazi tofauti?

Katika harakati ya kulijibu swali linalojitokeza, tumeamua kutekeleza uhakiki linganishi wa uhawilishaji wa ujumbe katika MMS na MS. Yaani, nimelenga kutambua iwapo uwasilishaji wa ujumbe katika MP hizo mbili (MMS na MS) zinafanana au zinatofautiana. Watafiti wengi wa hapo awali waliochunguza tafsiri walijikita katika maeneo tofauti tofauti na walikuwa na malengo mbalimbali. Kulingana na uchunguzi wetu, hakuna tafiti zilizofanywa kuhusu uhakiki linganishi wa makala pokezi mbili za Kiswahili zinazolenga makala asilia moja kama ilivyo madhumuni ya utafiti huu. Hivyo, uchunguzi huu utakuwa ni mchango muhimu katika nyanja ya taaluma ya tafsiri.

Matokeo ya utafiti huu yatawafaidi wataalamu wenye hamu ya kujua kuhusu uhakiki wa kazi za tafsiri. Yaani, matokeo hayo yatawatia ilhamu wasomi wengine almuradi wajitose katika tafiti zaidi hususan, kutafsiri vitabu vingine vya fasihi ya Kiswahili ambavyo tayari vilishatafsiriwa. Nimeteua mada hii kwa kuwa itachangia kuibuka kwa tafiti mbalimbali zinazohusiana na tafsiri. Kwa mfano, kutokana na utafiti huu, watafsiri wanaweza kupata kichocheo cha kutafsiri tena kazi za fasihi ambazo tayari zilishatafsiriwa. Aghalabu, watafsiri wengi huwa hawashughuliki kutafsiri kazi za fasihi ambazo tayari zimeshatafsiriwa na watafsiri wengine. Isitoshe, mada hii itachangia kuibuka kwa tafiti mbalimbali za kuhakiki kiulinganishi vitabu vya fasihi (tofauti na za utafiti huu) ambavyo vimetafsiriwa na watafsiri tofauti na vinalenga matini chanzi moja.

Utafiti huu pia, utawafaidi wanafunzi wa taaluma ya tafsiri kwa kuwa matokeo yake yamefafanua baadhi ya vipengele muhimu vinavyofaa kuzingatiwa katika utekelezaji wa tafsiri ambavyo ni: mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na usawiri wa wahusika. Aidha, utafiti huu umebainisha uamilifu wa mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na usawiri wa wahusika katika tafsiri na namna vinavyochangia katika utimiaji wa tafsiri kwa kuzingatia tamthilia za MMS na MS. Mbinu za utafiti huu zimeelezwa katika sehemu ifuatayo ya 1.7.

### **1.7 Mbinu za Utafiti**

Sehemu hii ilidhihirisha mbinu za utafiti zilizotumiwa ili kufanikisha utafiti huu. Vipengele vilivyochunguzwa katika sehemu hii ni kama vile; sampuli na usampulishaji, njia za kukusanya data na uchanganuzi wa data. Kwa hivyo, tulifafanua vipengele hivyo tulivyovitaja na tulianza na Sampuli na Usampulishaji ifuatavyo.

#### **1.7.1 Sampuli na Usampulishaji**

Sampuli iliyoteuliwa katika tasnifu hii ni ya kimakusudi na usampulishaji unaofanywa kwa jinsi hii huhusisha uteuzi wa sehemu fulani kama eneo la utafiti au watu fulani kama watafitiwa. Kwa mujibu wa Thanulingom (2000), watu hao au sehemu hiyo huteuliwa kwa kuzingatia sababu maalum. Kwa hivyo, katika utafiti huu tuliteua kimakusudi tamthilia za Mkaguzi Mkuu Serikali (Mwakasaka, 1979) na Mkaguzi wa Serikali (Madumulla, 1999) kwa sababu ni tamthilia zilizotafsiriwa na watafsiri wawili tofauti ilhali zinalenga matini asilia moja. Tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Mwakasaka 1979) ni tafsiri ya tamthilia ya Kiingereza ya *Government Inspector* (iliyotafsiriwa kutoka tamthilia ya *The Revizor* (Gogol 1836) na kulinganisha na tamthilia ya *Mkaguzi wa Serikali* (Madumulla, 1999) iliyotafsiriwa

kutoka tamthilia ya *The Revizor* (Gogol, 1836) ambayo tafsiri yake ya Kiingereza ni *Government Inspector*.

Nimekusanya data kutokana na sampuli ya maonyesho yote na sura zote zinazopatikana katika tamthilia za MMS na MS. Kwa mfano, katika MMS kuna maonyesho matatu na katika kila onyesho kuna sehemu mbalimbali. Kwa upande mwingine, mtafsiri wa MS aligawa tamthilia katika matendo mbalimbali na katika kila tendo, kuna maonyesho tofauti. Kutokana na maonyesho na matendo hayo kutoka MMS na MS, mtafiti alichunguza kiulinganishi mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika ili kufanya uchanganuzi na kufikia mahitimisho yanayotegemewa.

Tamthilia za MMS na MS ndizo malighafi ya data katika utafiti huu. Kwa hivyo, mtafiti alizisoma tamthilia hizo kwa makini huku akichunguza na kuvinakili vipengele mbalimbali vilivyokuwa muhimu pia katika ufafanuzi wa matokeo ya utafiti. Vipengele vilivyoshughulikiwa ni, mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika. Njia za kukusanya data zimeshughulikiwa katika sehemu ifuatayo.

### **1.7.2 Njia za Kukusanya Data**

Katika kukusanya data ya utafiti huu, nilizinunua tamthilia za MMS na MS kutoka madukani. Nilizisoma kwa makini tamthilia hizo huku nikichunguza kiulinganishi vipengele vya uchanganuzi ambavyo ni mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika. Baada ya kusoma tamthilia za MMS na MS, mtafiti alivinakili vipengele vya uchanganuzi kutoka kwa kila kitabu. Kimsingi, ukusanyaji wa data ulitekelezwa kwa njia zifuatazo:

Kwanza, mtafiti alinakili kiulinganishi mbinu za lugha kama vile tashbihi, chuku, jazanda, misemo, matumizi ya sauti, barua na ndoto. Pili, mtafiti alinakili kiulinganishi ujumbe unaojitokeza katika MMS (1979) na MS (1999) kama vile dhuluma, matumizi mabaya ya mamlaka, ufisadi, usaliti, nafasi ya mwanamke na unafiki. Kuhusiana na wahusika, mtafiti alinakili kiulinganishi majina ya wahusika na sifa zao. Wahusika walioshughulikiwa ni kama vile Mkuu wa Wilaya (Meya), Abdulin/Abdulini, Marya/Marya, Ann/Anna, Jaji/Mkaguzi wa Mahakama na Bw. Huruma/Mkaguzi wa Misaada na Mratibu wa Elimu/Mkaguzi wa Elimu. Baada ya kukusanya data iliyohitajika, mtafiti alichanganua data hiyo kwa misingi ya malengo na nadharia ya utafiti huu. Namna uchanganuzi huo ulivyotekelezwa inaelezewa katika sehemu inayofuata.

### **1.7.3 Uchanganuzi wa Data**

Hatua nyingine muhimu baada ya kukusanya data, ni uchanganuzi wa data hiyo kwa kuwa hatua hii ya uchanganuzi wa data humwezesha mtafiti kupata matokeo ya utafiti. Katika utafiti huu, data zilizokusanywa ziliwekwa pamoja, kisha kugawanywa kulingana na kategoria za uchanganuzi, yaani mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiti katika usawiri wa wahusika. Kwa mfano, kuhusiana na mbinu za lugha, mtafiti alichunguza kiulinganishi jinsi watafsiri wa MMS na MS walivyohawilisha mbinu za lugha katika kazi zao.

Baada ya kuchunguza uhawilishaji wa mbinu za lugha, mtafiti alizidondoa tofauti zozote za matumizi ya mbinu za lugha zinavyojitokeza katika tamthilia za MMS na MS. Halafu mbinu hizo za lugha zikachanganuliwa kwa misingi ya lengo la kwanza la utafiti huu ambalo ni kuchunguza kiulinganishi mbinu za lugha katika MMS na MS. Mifano ya mbinu za lugha tulizozichunguza katika tasnifu hii ni kama vile



chuku, matumizi ya sauti, uzungumzi nafsia, matumizi ya barua, jazanda, tashbihi na misemo.

Mtafiti pia alichunguza kiulinganishi tofauti zinazojitokeza katika uwasilishaji wa ujumbe katika tafsiri za MMS na MS. Mtafiti alichanganua kipengele hiki kwa misingi ya lengo la pili la utafiti huu ambalo ni kuchambua kiulinganishi uwasilishaji wa ujumbe katika MMS na MS. Ujumbe ulioshughulikiwa ni kama vile ufisadi, matumizi mabaya ya mamlaka, dhuluma, kutowajibika, uasherati na nafasi ya mwanamke katika jamii.

Kuhusiana na wahusika, mtafiti alichunguza kiulinganishi uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika MMS na MS. Yaani, mtafiti alichunguza kiulinganishi tabia za wahusika wa MMS kwa misingi ya lengo la tatu la utafiti huu ambalo ni kuhakiki kiulinganishi uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika MMS na MS. Mifano ya wahusika walioshughulikiwa ni kama vile, Mkuu wa Wilaya (Meya), Ghlestakov/Hilestakov, Mkguzi wa Elimu/ Anne/Ann, Marya/Maria.

Katika uchanganuzi wa tasnifu hii mtafiti aliongozwa na nadharia ya uamilifu katika tafsiri, mtazamo wa kuhakiki matini kwa sababu mihimili mikuu mitatu ya nadharia hii inaoana na malengo ya utafiti huu. Maelezo kuhusu mihimili hiyo yamebainishwa kwa kina katika sura ya pili. Kwa hivyo, data tuliyowasilisha katika tasnifu hii ni, mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na usawiri wa wahusika ulivyojitokeza katika MMS (Mwakasaka, 1979) na MS (Madumulla, 1999).

Katika tasnifu hii, Makala pokezi 1 ni *Mkguzi Mkuu wa Serikali* (MMS) (Mwakasaka, 1979) na makala pokezi 2 ni *Mkguzi wa Serikali* (MS) (Madumulla, 1999). Aidha, maandishi yote ambayo ndiyo data ya tasnifu hii yamewasilishwa kwa

kuwekwa katikati ya kurasa na pia kupigiwa mistari. Maandishi yanayotaja mada za vitabu, yamewasilishwa kwa herufi za mlazo. Maelezo mengine yote yameandikwa kwa herufi za kawaida.

### **1.8 Hitimisho**

Sura hii imefafanua masuala muhimu na ya kimsingi katika mchakato wa utafiti wa kiakademia ambayo ni, usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti, nadharia tete, upeo na mipaka ya utafiti na mbinu za utafiti. Isitoshe, katika usuli wa utafiti, imedhihirika kwamba tamthilia za MMS na MS ni tafsiri ya matini chanzi ya tamthilia ya Kirusi ya *The Revizor* (Gogol, 1836). Utafiti huu ni wa kipekee kwa kuwa haujahakiki tafsiri hizi (MMS na MS) na kulinganisha na matini chanzi mahsusi bali umechukulia kazi hizo zilizotafsiriwa kama matini zinazojitegemea.

Katika kuchunguza mbinu za utafiti, imebainika kwamba makala pokezi mbili: *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali* ndizo zilikuwa malighafi ya data katika utafiti huu. Aidha, maelezo kuhusu uchanganuzi na uwasilishaji wa data katika sehemu hii yamebainika barabara. Katika sura ya pili ifuatayo, tumeeleza kuhusu tahakiki ya maandishi na msingi wa kinadharia wa utafiti huu.

## SURA YA PILI

### MAPITIO YA MAANDISHI NA MSINGI WA KINADHARI

#### 2.0 Utangulizi

Katika sura hii tumehakiki baadhi ya tafiti ambazo zinahusiana na utafiti huu. Tuliangazia maandishi yanayohusu kazi za tafsiri linganishi katika fasihi na tulijikita katika malengo ya utafiti huu. Malengo hayo ni kuhakiki kiulinganishi mbinu za lugha katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*, kuchambua kiulinganishi uwasilishaji wa ujumbe katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali* na kuchunguza kiulinganishi uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*. Tumeelezea dhana ya tafsiri katika sahemu inayofuata ya 2.1.

#### 2.1 Dhana ya Tafsiri

Sehemu hii inaangaza dhana ya tafsiri kwa mujibu wa wasomi mbalimbali. Kwa mfano, Jilala (2014) anaeleza kuwa tafsiri ni dhana telezi na haiwezi kufasiliwa kwa namna moja tu na wataalamu tofauti. Hii ina maana kwamba fasili ya tafsiri ni pana sana na haiwezi kufasiliwa kwa namna moja tu. kila mtaalamuu ameeleza dhana ya tafsiri kwa mujibu wa uelewa na mtazamo wake. Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI, 2004), kutafsiri ni kuhamisha maana ya maneno kutoka lugha chanzi kwenda lugha pokezi.

Kihore (2005) anaeleza kwamba tafsiri ni jaribio la kuwasilisha ujumbe ulioandikwa katika lugha moja kwa lugha nyingine tofauti. Mtaalamuu huyu anasisitiza kwamba katika mchakato wa tafsiri, ni vizuri ujumbe kubakia ulivyo katika matini chanzi bila kubadilika. Mwansoko na wenzake (2006) wanasema kwamba tafsiri ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine.

Wanajadili kuwa katika mchakato wa tafsiri, uhawilishaji wa ujumbe unahusishwa na maandishi na wala sio mazungumzo. Mwansoko (1996) amebainisha mambo makuu mawili ambayo ni muhimu kuzingatiwa katika kufanya tafsiri ya aina yoyote. Mwanzo, mawazo yanayoshughulikiwa na mtafsiri ni sharti yawe katika maandishi. Pili, mawazo au ujumbe kati ya lugha chanzi na lugha pokezi sharti yalingane. Katika kujadili hilo, mtaalamuu huyu anadai kuwa hakuna tafsiri iliyo sawa kabisa na matini chanzi. Aidha, Mwansoko anadai kuwa kazi kubwa ya mtafsiri ni kujaribu kuleta ulinganifu mzuri kati ya matini chanzi na ile ya matini lengwa.

Weisstein (1973), anasema kuwa, fasihi linganishi ni tawi la historia ya fasihi na taaluma inayohusu mahusiano, mapatano, makutano na maelewano ya kimataifa ya kazi zizotafsiriwa za waandishi wanaotoka katika nchi mbalimbali. Kwa mujibu wa Bassnett (1993) dhana ya fasihi linganishi imezua suitafahamu kwa kuwa, wahakiki wengi wameibuka na maoni tofautitofauti kuhusu dhana hii. Mtaalamuu huyu anadai kuwa fasihi linganishi ni taaluma inayohusu matini za tamaduni mbalimbali.

Bassnett (1993) anadai kuwa, fasihi linganishi iliibuka katika karne ya 19 kule Ujerumani. anasema kuwa, katika mwaka wa 1897, fasihi linganishi ilitambuliwa kama taaluma. Anaeleza kwamba, fasihi linganishi ni muhimu kwa kuwa, huondoa mipaka iliyopo katika fasihi mbalimbali za ulimwengu. Kwa mfano India ni nchi katika ulimwengu wa tatu na ina lugha nyingi sana na watu na tamaduni mbalimbali. Hivyo, wahakiki wa fasihi linganishi wanaweza kuondoa mipaka ya lugha na tamaduni hizo.

Ligembe (1995) alilinganisha matumizi ya sitiari katika tamthiliya ya *Nguzo Mama* (1982) iliyoandikwa na Penina Mhando. Katika utafiti wake, Ligembe (1995) alilenga

kulinganisha matumizi ya sitiari ili kubaini ni sitiari ipi yenye mda fao mkubwa zaidi ikilinganisha na sitiari nyingine. Mtaalamu huyu alijikita katika kipengele kimoja cha tamathali za semi kinavyotumiwa na msanii mmoja. Mwansoko (1996) anaieleza lugha kama kipengele na kielelezo muhimu cha utamaduni wa jamii. Anaendelea kueleza kuwa, msamiati wa lugha kwa kiwango kikubwa hujenga maana za maneno kutokana na utamaduni wa jamii inamozungumzwa. Hivyo, maana za maneno ni kiungo au daraja madhubuti kati ya utamaduni na lugha na ndicho kitovu cha tafsiri.

Wellek na Warren (1996) wanadai kwamba fasihi linganishi ni mbinu itumiwayo na wahakiki wengi wa fasihi kwa kujadili njia maalum ya usomaji wa sanaa mbalimbali ulimwenguni. Ulinganishaji unaweza kuwa wa fasihi ya Kiafrika na Kizungu au fasihi ya Kizungu dhidi ya Kihindi nk. Mosha (2002) alilinganisha sitiari katika tanzu mbili, yaani ngano na ushairi.

Ramadhani (2005) alilinganisha matumizi ya sitiari katika tamthilia ya *Ng'wanamalundi* (1988) na tamthilia ya *Mashetani* (Hussein, 1971). Saleem (2013) alilinganisha ujumbe na fani katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Kivuli Kinaishi* (1980). Saleem aliibuka na maoni kuwa waandishi wa tamthilia za *Mashetani* (1971) na *Kivuli Kinaishi* wanatofautiana katika utamaduni, uzoefu na jiografia ya maeneo yao.

Wamitila (2003) anaieleza fasihi linganishi kuwa ni mbinu ya kuchunguza, kuchambua na kuelezea sifa zinazotofautiana zilizomo katika matini zaidi ya moja za kifasihi. Van Tieghem (1931) katika Wellek (1988) anaifasili fasihi linganishi kuwa ni somo linalojishughulisha na uhusiano wa vitu viwili ambavyo vinaweza kuwa kazi ya mtu binafsi, kundi la waandishi na binadamu au fasihi kwa jumla. Wellek (1988) anaiona fasihi linganishi kuwa ni taaluma ya fasihi nje ya mipaka ya kitaifa, ni

kujifunza uhusiano uliopo baina ya fasihi na eneo jingine la maarifa, mfano sanaa, falsafa, historia ya sanaa za jamii sayansi na dini.

Kutokana na fasili hizo za wataalam wa fasihi linganishi katika kuelezea dhana hiyo, hawajatofautiana na ninakubaliana nao kwamba fasihi linganishi ni taaluma inayoshughulika na ama kufanana au kutofautiana katika kazi mbalimbali za fasihi. Kazi hizo zinaweza kuwa za lugha mbalimbali kama vile fasihi ya Kiswahili, Kijerumani, Kichina, Kiingereza na nyinginezo. Jilala (2014) anadai kuwa mwandishi wa kazi za fasihi huhamisha ujuzi, kaida, uzoefu na uelewa wake wa utamaduni wa jamii yake. Kwa hivyo mwandishi huteua maneno na mbinu za kisanii zinazoangazia uhalisia wa jamii yake na mazingira yanayomzunguka katika jamii iliyomzaa na kumlea.

Mtaalamu huyu (Jilala, 2014) ameangazia mambo kadhaa ambayo mtafsiri hupasa kuzingatia anapofanya kazi ya tafsiri, nayo ni weledi wa mtafiri, ujuzi wa lugha chanzi na lugha lengwa na uaminifu wa mfasiri. Jilala (2014), anaeleza kwamba ni dhahiri kuwa, kufanya tafsiri ni kuhusisha tamaduni mbili zinazofanyiwa kazi: na kutafsiri siyo tu kushughulikia lugha bali ni pamoja na kushughulikia utamaduni wa lugha hizo. Hili ni kutokana na ukweli kwamba, maana ya maneno hujikita katika uelewa wa utamaduni wa jamii husika.

Jilala (2014) anaendelea kueleza kuwa, tafsiri ni taaluma ambayo haiwezi kutengana na fasihi linganishi, yaani, ni taaluma muhimu sana katika kuchunguza, kuchambua, kuhakiki na kutasiri fasihi za duniani. Mtaalamu huyu anadai kwamba katika ulimwengu wa utandawazi, tafsiri inatumika kama nyenzo ya mawasiliano na utambuzi wa fasihi ili kuweza kuelewa fasihi ya ulimwengu. Anaeleza kwamba, mtu hawezi kulinganisha vitu viwili ambavyo havitambui na haelewi maarifa na misingi

yake. Hivyo, tafsiri huweka bayana na kutusaidia kuweza kujua kile kinachowasilishwa na fasihi ya jamii nyingine.

Tafsiri ni taaluma muhimu sana katika kuelewa fasihi linganishi ya ulimwengu, ni kama daraja linalounganisha jamii za lugha na tamaduni tofauti. Jilala (2014) anaendelea kudahili kuwa lugha imefungamana na utamaduni wa jamii lugha husika. Mtaalamu huyu anasema lugha ni sehemu ya ndani ya ombwe pana la utamaduni na hutumika kama nyenzo ya mawasiliano baina ya watu wenye utamaduni mmoja. Anadai kwamba watu wa lugha moja ni misingi ya jamii ya watu ambao hutumia huwasilisha uzoefu, utamaduni, imani, mielekeo na mitazamo yao katika jamii mahsusi.

Fadhil (2014) alilinganisha dhima ya mtindo katika tamthilia za kihistoria za *Morani* (1993) na *Kinjekitile* (1969). Mkuwili (2015) alilinganisha ujumbe na fani katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wana malundi* (1988) na *Kivuli Kinaishi* (1980). Mningo (2015) alilinganisha tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na *Fumo Liyongo* (2009). Ulinganishaji huu ulihusisha kazi za Emmanuel Mbogo katika vipindi tofauti. Ni bayana kuwa kazi nyingi tulizoziangazia, ni tafiti ambazo zililenga kulinganisha kazi za mtunzi mmoja na mtunzi mwingine, utanzu mmoja na utanzu mwingine ama kujikita tu katika kazi za mtunzi mmoja.

Kazi hizo za fasihi linganishi tulizoziangazia zilitusaidia na kutupatia mwelekeo ingawa zinatofautiana na utafiti wetu kwa kuwa utafiti huu unashughulikia uhakiki linganishi wa tamthilia za MMS (1979) na MS (1999). Katika tasnifu hii, mtafiti alinuia kutambua kiulinganishi iwapo kuna tofauti katika tafsiri hizo. Katika sehemu inayofuata ya 2.2, tumeshughulikia historia fupi ya tafsiri.

## 2.2 Historia Fupi ya Tafsiri

Olgierda na Achenbach (2004), wanadahili kuwa tafsiri ilisababishwa na lengo la kutimiza mawasiliano baina ya wasemaji wa lugha tofauti. Wanaendelea kudai kuwa ukalimani ulianza kuwepo mnamo miaka ya 3000 KYM (kabla ya Masiya) na kwamba maendeleo ya ukalimani yaliambatana na yale ya tafsiri. Wataalam hao wanahoji kuwa Wamisri kwa kipindi hicho walikuwa wakilitumia neno "hieroglyphic" lililomaanisha ukalimani. Kuwepo kwa neno hili katika enzi hizo inamaanisha kuwa shughuli za ukalimani zilikuwepo miaka hiyo ya 3000 KYM.

Wataalam hao (Olgierda na Achenbach), wanadahili kuwa, Agano la Kale la Biblia liliandikwa katika Kiebrania na Agano Jipya likaandikwa kwa Kiyunani. Hivyo, wakalimani walikuwa wanatumika ili kuwasilisha ujumbe wa mahubiri kutoka lugha ya Kiebrania au Kiyunani hadi lugha zingine kama vile Kiingereza. Kwa mujibu wa wataalamu hao: (Jean 1995, Gaiba 1998, Wilss, 1999 na Iser, 2000), mchakato wa tafsiri ulianza kuibuka kwa sababu ya kuwepo kwa lugha nyingi na kuwepo kwa wasemaji wa lugha mbalimbali wasioelewana.

Mnamo mwaka wa 1480, makanisa ya kiprotestanti yaliendelea kusesitiza maendelezi ya tafsiri ya Biblia katika lugha nyinginezo na hii iliwezesha Ukristo kuzidi kuenea katika sehemu mbalimbali. Mbaabu (1985) anaelezea kuwa, kutokana na chimbuko la ukalimani, wamishonari walichangia pakubwa katika ukuzaji wa Kiswahili. Mtaalamu huyu anadahili kwamba, lugha ambayo imekuzwa zaidi kupitia maandishi huwa rahisi kuifanyia ukalimani kuliko lugha ambayo haijashughulikiwa kabisa kimaandishi. Isitoshe, kushiriki kwa wamishonari hao katika tafsiri ya Biblia ya Kiswahili kumewasaidia wakalimani wanaofanya ukalimani wa mahubiri kutoka Kiingereza hadi Kiswahili.



Bressler (2007), anadahili kuwa historia ya fasihi ya wakati wa ukoloni ilianza mnamo mwanzo wa karne ya ishirini. Baada ya bara Hindu kujinyakulia uhuru, vyama mbalimbali vilianzishwa katika bara zingine kama vile Afrika, Amerika Kusini na Australia ili kushughulikia maswala ya ukombozi. Bressler anahoji kwamba watafsiri wengine walianza kutafsiri vitabu mbalimbali kuhusu athari za kuja ya wakoloni. Katika karne ya kumi na saba kukawa na tafsiri za kazi nyingi, ambapo kazi za fasihi ya Kifaransa zilitafsiriwa katika Kiingereza.

Tawi la isimu limeshughulikiwa na watafiti kama vile Harries (1952), Van Dijk (1983), Brown na Yule (1983). Wataalam hao walihusisha tafsiri na taaluma za Isimu, anthropolojia na saikolojia kwa sababu uchambuzi wa diskosi ni kipengele muhimu katika mchakato wa tafsiri. Katika karne ya 19 na 20, kuliibuka nadharia nyingi ambazo ziliathiri nadharia za tafsiri. Nadharia hizo ni kama vile; nadharia ya Mawasiliano, nadharia ya Umuundo na nadharia ya Isimu. Wataalamu hao wanaendelea kuhoji kuwa katika harakati ya kutafsiri Biblia, Jumuiya ya Biblia ya Kenya na ya Tanzania zilikumbwa na matatizo kadhaa. Kwa mfano, watafsiri walikabiliwa na shida ya kutafsiri majina zaidi ya 3,500 ya watu na mahali na iliwalazimu kubuni majina mengine ili kuondoa tatizo hilo. Aidha, watafsiri hao walitohoa baadhi ya majina hayo kama vile "Yehova" na "Yesu".

Mbaabu (1991) anadahili kwamba, kufikia karne ya kumi na tisa wamishonari waliotoka Ulaya walizuru Afrika Mashariki ili kueneza dini ya Kikristo na walianza kujifunza matumizi ya Kiswahili ili waweze kuwasiliana na wenyeji. Ludwing Krapf ndiye mmishenari wa kwanza aliyeanzisha kazi ya umishenari mnamo Agosti 1844. Krapf aliweza kujifunza lugha ya Kiswahili kwa sababu alipata Waafrika walioshirikiana naye na walimsaidia Krapf katika kufanya ukalimani na tafsiri.

Kane (1980) na Mbaabu (1991) wanahoji kuwa Krapf alitafsiri Biblia ya Kiingereza hadi Kiswahili, akaandika kamusi ya kwanza ya Kiswahili na kisha akaandika kitabu cha sarufi ya Kiswahili. Juhudi zake zilikuwa muhimu sana katika shughuli za ukalimani baina ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Pia wataalam hao wanadai kuwa Katika mwaka wa 1864, Askofu Edward Steer na Tozer walifika Unguja. Kulingana na Steer, Kiswahili, kama lugha nyingine za wenyeji, ilikuwa chombo muhimu mno katika uenezaji wa dini ya Kikristo.

Steer na Tozer walipowasili pwani ya Afrika Mashariki, ukalimani uliohusisha lugha ya Kiingereza na Kiswahili uliendelezwa. Steer aliandika baadhi ya vitabu maarufu vya Kiswahili ambavyo baadaye vimetafsiriwa hadi Kiingereza. Kwa mfano, *Swahili Tales* (1869) na *A Handbook of the Swahili Language as Spoken at Zanzibar* (1870) vilichapishwa kule London na vilichangia pakubwa katika kukuza watafsiri wa Kiswahili na Kiingereza. Wamishonari pia waliweza kuchangia usambazaji wa Kiswahili hadi maeneo mengine kupitia juhudi zao za kueneza ujumbe wa Biblia.

Tulihoji kuwa, fasihi nzuri ulimwenguni kwa wakati huu husambazwa dunia nzima kupitia tafsiri, kwa kuwa kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia imekuwa rahisi kwa watu kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu kutangamana. Hivyo, watu wanaweza kusoma na kuelewa tamaduni tofauti tofauti kutokana na kazi za fasihi zilizotafsiriwa. Kwa mujibu wa Bastin na Band (2006), taaluma ya tafsiri haijatafitiwa sana na haiwezi ikalinganishwa na aina yoyote ya tafiti katika fasihi, hivyo, bado kuna mapengo yanayofaa kuzibwa katika taaluma ya tafsiri. Utafiti huu basi ni muhimu kwa kuwa tulihakiki kiulinganishi vipengele muhimu katika MMS na MS.

Katika sehemu ifuatayo tumeangazia tafiti mbalimbali zinazohusiana na utafiti huu kwa kujikita hasa katika malengo ya utafiti ambayo ni; kuhakiki kiulinganishi mbinu

za lugha katika MMS na MS, kuchambua kiulinganishi uwasilishaji wa ujumbe katika MMS na MS na kuchunguza kiulinganishi uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika MMS na MS. Hivyo katika sehemu inayofuata ya 2.3 tumeanza kwa kuangazia tafiti mbalimbali zinazohusiana na mbinu za lugha katika tafsiri.

### **2.3 Mbinu za Lugha Katika Tafsiri**

Riwaya ya *Things Fall Apart* iliyoandikwa na Achebe (1958) ilitafsiriwa kwa lugha ya Kiajemi na watafsiri wawili: Bahrami (2001) na Safavian (2009). Mandana (2012) alihakiki kiulinganishi tamthilia za Bahrami (2001) na Safavian (2009) akilinganisha na matini chanzi. Mandana (2012) alichunguza kiulinganishi usawiri wa wahusika, uwasilishaji wa maudhui, ploti na dhamira katika tamthilia za Bahrami (2001) na Safavian (2009) na aliibuka na madai kuwa ingawa kazi hizi mbili zilifanana kwa upande wa usawiri wa wahusika, lakini kazi ya Bahrami ilikuwa mwafaka zaidi kuliko ya Safavian.

Kazi ya Mandana (2012) ilituongoza kwa kuwa pia alihakiki kiulinganishi vipengele katika tamthilia zilizotafsiriwa za *Things Fall Apart*. Mandana (2012) alihakiki kiulinganishi tamthilia zilizotafsiriwa katika Kiajemi nazo ni: *HamechizForomipashad (Things Fall Apart)*, (Barahmi, 2001) na *HamechizForoMirizad (Things Fall Apart)* (Safavian, 2009). Kwa upande mwingine, utafiti wetu ulihakiki kiulinganishi tamthilia zilizotafsiriwa katika Kiswahili za: *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* kilichotafsiriwa (Mwakasaka, 1979) na *Mkaguzi wa Serikali* kilichotafsiriwa (Madumulla, 1999). Isitoshe, Mandana (2009) alichunguza matumizi ya lugha ilhali katika utafiti huu tulihakiki kiulinganishi mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika.

Kwa mujibu wa Jacobson (1959), mfumo wa sarufi wa lugha huweza kuathiri uhawilishaji wa ujumbe katika tafsiri kwa sababu lugha ni kipengele muhimu sana katika mchakato wa tafsiri. Cartford (1989) anadahili kuwa aghalabu tafsiri mbovu hutokea kwa sababu ya mtafsiri kutofahamu vyema sarufi ya lugha husika. Maoni ya wataalam hao yalitufaa kwa sababu tulishughulikia pia ulinganishaji wa matumizi ya mbinu za lugha katika tamthilia za MMS na MS.

Halliday (1970) anadai kwamba mtafsiri huhitaji maarifa ili aweze kutambua matumizi ya mbinu za lugha katika kazi ya tafsiri. Mawazo haya ya Halliday yanatilia mkazo umuhimu wa kufahamu mbinu mbalimbali za lugha ili kuweza kutekeleza kazi ya tafsiri kwa njia mwafaka. Maoni ya mtaalamu huyo yanatupa mwelekeo katika tasnifu hii kwa kuwa mojawapo ya vipengele tulivyochunguza katika tasnifu hii ni mbinu za lugha. Aidha, vitabu mbalimbali vya fasihi vimetafsiriwa kutoka lugha moja hadi nyingine. Kwa mfano, tamthilia ya *Betrayal in the City* (Imbuga, 1976), ilitafsiriwa katika Kiswahili na Kisia na Wasyatsa, (1994) na ikaitwa *Usaliti Mjini*. Aidha, tamthilia ya Kiingereza inayoitwa *The Trials of Brother Jero* iliandikwa na Soyinka (1964), ilitafsiriwa na Yahya (1974) na alikiita *Masaibu ya Ndugu Jero*.

Bibilia ilitafsiriwa kutoka lugha ya Kilatini hadi Kiingereza, Kiswahili na lugha nyinginezo za ulimwengu. Al-Barwani (2001) pia alitafsiri Koran takatifu kutoka lugha ya Kiarabu hadi lugha ya Kiswahili na lugha nyingine nyingi za ulimwengu. Suala muhimu linaloibuka katika matukio hayo ni: Je, kwa nini kuwepo na matini pokezi anuwai kutoka kwa matini asilia moja? Brotoz (2004) alihakiki kiulinganishi mbinu za lugha katika tafsiri za tamthilia ya *The Catcher in The Rye* iliyoandikwa na Salinger (1951). Tafsiri hizo ni nne kwa jumla: mbili za Kislovaki zilizotafsiriwa na Saje (1966) na Jokic (1990), moja ya Serbia-Krotia iliyotafsiriwa na Andric (1987) na

nyinginea ya Kiitaliano iliyotafsiriwa na Motti (1961). Mbinu za lugha alizozichunguza Brotoz katika tamthilia tafsiri hizo nne ni pamoja na; jazanda, methali, tashbihi na chuku. Aliibuka na madai kwamba, kati ya hao watafsiri wanne waliotafsiri tamthilia ya *The Catcher in The Rye*,

Andric (1987) alitumia lugha ya Kiserbia-Krotia katika tafsiri yake, na aliyezingatia kwa kiwango kikubwa fani za lugha kama ilivyo katika matini asilia. Mtaalamu huyu alihitimisha kwamba mtafsiri wa tamthilia kama alivyo mshairi ana jukumu la kuhawilisha mbinu za lugha kama zilivyowasilishwa katika matini asilia.

Kazi ya Brotoz (2004) ilituongoza katika utafiti huu kwa sababu tulishughulikia uhakiki linganishi wa mbinu za lugha katika kazi za fasihi zilizotafsiriwa na watafsiri wawili huku wakilenga makala asilia moja. Tofauti kati ya tasnifu hii na utafiti wa Brotoz (2004) ni kuwa Brotoz alihakiki kiulinganishi mbinu za lugha katika tafsiri nne za tamthilia ya *The Catcher in The Rye* iliyoandikwa na Salinger (1951). Katika utafiti wetu, tulichunguza kiulinganishi mbinu za lugha katika tafsiri mbili za Kiswahili za MMS na MS.

Mtaalamu huyu pia, alichunguza tofauti zinazojitokeza katika uhawilishaji wa mbinu za lugha katika tafsiri hizo zikilinganishwa na matini asilia ilhali katika tasnifu hii, tulichunguza kiulinganishi mbinu za lugha katika MMS na MS pasi na kulinganisha na matini chanzi yoyote. Aidha, tulichunguza kiulinganishi tofauti katika uhawilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*. Sehemu ifuatayo imehakiki tafiti zilizoshughulikiwa na zinazohusu uwasilishaji wa ujumbe katika kazi ya tafsiri.

## 2.4 Uwasilishaji wa Ujumbe katika Tafsiri

Syke (1962), anaeleza kuwa ili mtafsiri aweze kutekeleza kazi yake kwa njia mwafaka, anahitaji kuelewa maana mbalimbali za msamiati. Pia anadahili kwamba, mtafsiri anafaa kufahamu kuwa maneno katika lugha tofauti huenda yakawa na visawe halisi au visivyo halisi. Aidha, Syke ana maoni kwamba, iwapo mtafsiri anataka kuibuka na kazi nzuri, hana budi kuelewa mtindo wa lugha aliotumia mwandishi wa matini asilia. Sifa hizi anazozitungumzia Syke ndizo zinazochangia katika umuhimu wa kuelewa uamilifu wa lugha.

Shitemi (1997) anatilia mkazo kipengele hicho cha uaminifu wa tafsiri katika utafiti wake, kwa hivyo, mtafsiri ana jukumu la kuhakikisha kuwa kazi yake ni ya kuaminika. Maoni hayo yalitufaa hususan tulipohakiki kiulinganishi kazi zilizotafsiriwa katika utafiti huu. Kwa mujibu wa Catford (1965), mfumo wa sarufi na maneno ndivyo vipengele muhimu katika lugha yoyote ile. Hivyo, mtafsiri asipoelewa vipengele hivi vya lugha, basi huweza kupotosha ujumbe wa msanii wa matini asilia.

Katika tasnifu hii, tulichunguza kiulinganishi matumizi ya lugha katika uwasilishaji wa ujumbe katika tamthilia zilizotafsiriwa za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*. Maoni ya mtaalamu Catford (1965) yalitupa mwanga katika utafiti wetu kwa kuwa tulihakiki kiulinganishi mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika tamthilia mbili zilizotafsiriwa za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*.

Kulingana na Newmark (1982), lengo kuu la mtafsiri ni kuzalisha matokeo yanayofanana na yaliyowasilishwa na mwandishi wa matini asilia kwa wasomaji. Mtaalamu huyu anarejelea hali hii kama kanuni linganifu na anadahili kuwa, kazi yoyote ya tafsiri huhitaji ujuzi wa kiisimu pamoja na ubunifu wa mtafsiri. Utafiti wa

Newmark pia umechangia uchunguzi wa tasnifu hii kwa kuwa mtalaam huyu aligundua kuwa kiwango cha elimu hakikuwa kibainishi katika tafsiri na kwamba mtafsiri anaweza kufanya tafsiri kwa namna inayoweza kupitisha ujumbe. Alihitimisha kuwa, tajriba ya mtafsiri katika lugha zote mbili ni muhimu hata kuliko elimu. Utafiti huu uliongozwa na mawazo hayo kwa vile, katika tasnifu hii tulichunguza kiulinganishi matumizi ya lugha katika uwasilishaji wa ujumbe na usawiri wa wahusika katika kazi zilizotafsiriwa za MMS na MS.

Picken (1983) anaeleza kuwa rasilimali muhimu kwa mtafsiri ni tajriba yake. Hii ni kwa sababu tajriba humsaidia mtafsiri katika kuamua ni mbinu gani itakayotumiwa katika mchakato wa tafsiri. Maoni hayo yalituongoza kwa kuwa katika utafiti huu hatukuwa na budi kuchunguza iwapo tajriba ya watafsiri iliathiri utendaji wao. Crystal (1987) anajadili kuwa, tafsiri inayofanywa ni lazima iwe sahihi kihistoria na iwe ya kuaminika. Anadai kuwa, tafsiri ni lazima ikubalike kwa watu wanaolengwa.

Newmark (1988) alitafitia umilisi wa mtafsiri katika lugha asilia na lugha lengwa. Kutokana na utafiti wake, mtafsiri hawezi kutafsiri iwapo hajaizoea lugha lengwa. Utafiti wa Newmark ulikuwa ukichunguza tafsiri tofauti na uchunguzi huu, lakini ulituongoza katika utafiti huu. Kinyume na ulivyokuwa utafiti wa Newmark (1988), katika utafiti huu tulichunguza kiulinganishi tofauti katika matumizi ya lugha katika MMS na MS.

Cartford (1989) anadahili kuwa, mara nyingi tafsiri mbovu hutokea kwa sababu ya mtafsiri kutofahamu vyema sarufi za lugha za matini chanzi na matini pokezi. Mawazo haya ya Cartford yanachamgia katika utafiti huu kwa kuwa yanaonyesha kwamba, ni muhimu kwa mtafsiri kuelewa sarufi ya lugha ya matini chanzi na matini pokezi ili aweze kutekeleza kazi yake ifaavyo. Vilevile anasema kuwa, kujifunza

sarufi katika ombwe tupu huenda kukamvunja mtafsiri moyo na hivyo basi anayejifunza anafaa kuelewa matini sahili kabla ya matini changamano inayohitaji kamusi kueleweka. Hii ina maana kuwa, kuna mambo mengi ambayo yanaathiri sarufi ya lugha na hivyo basi si jambo ambalo linajisimamia kivyake bila kuhusisha mambo hayo.

Newmark (1991) anaelezea kwamba, hapo awali tafsiri ilichukuliwa kama harakati isiyowezekana na isiyotimiza lengo la kuwaunganisha wanawingilugha wasiokuwa na lugha shirikishi. Anadai kuwa kwa sasa tafsiri imekubalika kama njia mojawapo ya kufanikisha mawasiliano duniani kote. Utafiti wake ulichunguza iwapo vipengele muhimu katika matini hutafsiriwa na iwapo tafsiri yenyewe ni ya kiwango cha juu. Utafiti huu wa Newmark ulituongoza kwa kuwa, katika utafiti huu, tulichunguza kiulinganishi uwasilishaji wa vipengele muhimu katika mchakato wa tafsiri.

Baker (1992) katika utafiti wake anadahili kuwa, katika hali ya kuripoti matukio, kila mtu (kutegemea lugha mahsusi) hufanya uchaguzi wa kipekee kutoka kwa idadi kubwa ya maneno kwa mujibu wa fikra za kipekee kuhusu wakati, idadi, jinsia, umbo na kadhalika. Kwa hivyo, kusababisha kuwepo na umuhimu wa kuelewa namna LA na LP zinavyochukulia mambo ili kuweza kuyashughulikia ipasavyo.

Baker (1992) anaendelea kusema kuwa, lugha huweza kuwasilisha ujumbe wowote ambao wazungumzaji wa lugha hiyo wangependa kuwasilisha. Hata hivyo, mfumo wa sarufi wa lugha husika utaamua namna mambo fulani kama vile wakati na tukio na jinsi yatakavyoshughulikiwa kwa ukamilifu. Yaani, tulichunguza namna vipengele mbalimbali vya sarufi vinavyoweza kutafsiriwa na hali kama hii huathiri maamuzi katika tafsiri.



Santiago (2011) alihakiki kiulinganishi tafsiri za Kiajentina za shairi la Kifaransa lililoitwa *Les Fleurs du ma* ambalo msanii wake ni Bandelaire (1857). Tafsiri hizo ni kazi za Lamarque (1948) na Cristofalo (2006). Santiago (2011) aliibuka na maoni kuwa Lamarque (1948) katika kutafsiri sentensi, alizibadillisha kabisa na kuibuka na maana tofauti. Hatimaye tafsiri ya Lamarque ikawa karibu kinyume kabisa na makala asilia. Kwa mujibu wa Santiago (2011), kazi ya tafsiri ya Cristofalo (2006) inaeleweka moja kwa moja, yaani kila ubeti umepangwa na kuoana na matini chanzi. Aidha, msamiati uliotumiwa ni karibu sawa na wa makala asilia kwa kiwango kikubwa. Isitoshe, Santiago (2011) aliibuka pia na madai kwamba kazi ya tafsiri sio tu uhamishaji wa ujumbe kutoka makala asilia hadi makala pokezi bali pia ni kazi ya uhakiki na ubunifu wa anayetafsiri.

Kazi ya Santiago (2011) ilioana na utafiti wetu kwa kuwa, tulihakiki pia kiulinganishi kazi za fasihi zilizotafsiriwa na wasomi tofauti. Tofauti kati ya utafiti wetu na wa Santiago (2011) ni kuwa, kazi yetu inahusu tafsiri za Kiswahili za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali* ilhali Santiago alihakiki tafsiri za Kiajentina za Shairi la Kifaransa liitwalo *Les Fleurse du Mal*, lililoandikwa na Bandelaire, (1857).

Christensen (2011) alitafsiri tamthilia ya Kiingereza iitwayo *Cara Gayne* iliyoandikwa na O'Neill (1963) katika Kidanishi. Ujumbe wa tamthilia ya *Cara Gayne* unahusu mwanamke wa Kizungu aliyeenda Marekani kwa kumtoroka mumewe aliyekuwa asherati. Mwanamke huyu katika harakati ya kumtoroka mumewe alikumbana na matatizo chungu nzima lakini hatimaye alimpata mme aliyempenda na kumthamini.

Mtafsiri wa tamthilia ya *Cara Gay* alitarajia kuwa wasomaji wangeweza kuelewa barabara jinsi Wamarekani na Wadanishi walivyoishi baina ya miaka ya 1950 na

1960. Utafiti huo wa Kidanishi ulituongoza katika kazi yetu kwa vile pia ulishughulikia lugha kama mojawapo ya changamoto za tafsiri ilhali katika utafiti huu tulichunguza kiulinganishi mbinu za lugha katika MMS na MS. Isitoshe, Christensen (2011) katika kazi yake alitumia nadharia ya vipengele vinne vya uhakiki wa tafsiri (T.Y) iliyoasisiwa na Anne Schjoldager ilhali katika tasnifu hii tulitumia nadharia ya uamilifu katika tafsiri mtazamo wa kuhakiki matini iliyopendekezwa na Reiss (1977, 1989). Katika sehemu ifuatayo tumeshughulikia maandishi ya wataalamu wengine waliojadili usawiri wa wahusika katika tafsiri.

## **2.5 Usawiri wa Wahusika Katika Tafsiri**

Kwa mujibu wa Oettinger (1960), tafsiri ni mchakato wa kubadilisha ishara au viwakilishi vingine vya lugha katika matini. Yaani, ili kuwepo na ufanisi wa mawasiliano katika mchakato wa tafsiri, kipengele cha lugha hakiwezi kuepukika. Pia jambo la msingi katika tafsiri ni ubadilishaji wa mawazo, fikra, maudhui na wahusika kutoka lugha moja hadi nyingine. Maoni ya mtaalamu huyu ni ya muhimu katika kazi hii kwa kuwa tulishughulikia pia uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Mwakasaka, 1979) na *Mkaguzi wa Serikali* (Madumulla, 1999).

Winter (1962) ana maoni kuwa, kiwango cha chini zaidi na cha msingi katika tafsiri hakiwezi kutekelezwa pasipo kupata shida. Kila mara mtafsiri hataweza kusawazisha ujumbe katika lugha A na usemi ulio sawa kabisa katika lugha B kwa sababu kile kinachoweza kusemwa na sifa ya lugha A si sawa na jinsi inavyoweza kusemwa katika lugha B. Maoni haya ya Winter (1962) yanaonyesha upekee wa uamilifu wa kila lugha katika utekelezaji wa tafsiri. Maelezo yake kuhusu upekee wa lugha na

namna unavyoathiri tafsiri ni muhimu kutiliwa maanani katika ulinganishi wa kazi katika utafiti huu.

Cartford (1965) anadahili kuwa, ni kupitia viwango vya sarufi na kiwango cha neno ambacho mtafsiri anaweza kutekeleza tafsiri yake. Kwa hivyo, Cartford (1965) akatumia kauli ya ‘mawazo yanayolingana’ na siyo mawazo yaliyo sawa. Hii ni kwa sababu tofauti za kiisimu, kiutamaduni, kuhistoria na kimazingira kati ya lugha mbalimbali hufanya iwe vigumu kutafsiri mawazo ya lugha moja katika lugha nyingine bila kupoteza, kupotosha au kubadili maana hata kama ni kwa kiwango kidogo.

Cartford (1989) akizungumza kuhusu umuhimu wa mtafsiri kuelewa LA na LP, anasema kuwa kilicho muhimu ni mtafsiri kujua vipengele vya lugha ambavyo vimewakilishwa katika matini ya tafsiri na anavyoweza kutafsiri kwa kupitia uteuzi mwafaka wa maneno, mfuatano wa maneno na uakifishaji. Cartford katika Catriona (1989) anaongezea kuwa, mtafsiri anafaa awe na uwezo wa kutambua kuwa, maneno na sifa za maneno hayo hutofautiana katika lugha husika. Pia Cartford anadai kuwa, mtafsiri inafaa awe na ufahamu kuwa maneno katika lugha tofauti tofauti huenda yakawa na visawe au yasiwe navyo. Isitoshe, awe na uelewe wa muundo wa sarufi ya lugha asilia na lugha pokezi ili kuweza kutambua maana iliyokusudiwa na athari ya muundo huo.

Scholes (1972) anadahili kuwa, utamaduni wa matini chanzi huathiri matini lengwa. Na utamaduni wa mzungumzaji pia huathiri ukalimani. Kwa sababu mtafsiri hawezi kufahamu barabara ujumbe unaowasilishwa na msemaji au mwandishi wa matini chanzi iwapo hajaelewa utamaduni wa lugha hiyo. Utafiti wa Scholes unatupa mwangaza katika utafiti wetu kwa kuwa tulinuia kulinganisha uhawilishaji wa ujumbe

katika tamthilia zilizotafsiriwa za MMS na MS. Kwa mfano, iwapo mtafsiri haelewi tamaduni za lugha ya matini chanzi, huenda akawapa wahusika sifa potovu na basi ujumbe wa msanii wa matini chanzi huweza kupotoka.

Picken (1983) aligundua kuwa, aghalabu lugha zote zina maneno ambayo huwa ni vigumu kupata visawe vyao mahususi katika lugha au utamaduni lengwa ndiposa mara nyingi maana kupotoshwa maneno hayo yanapotafsiriwa. Sifa hizi zilizopendekezwa na Picken kuhusu watafsiri zinafaa katika uteuzi wa watafsiri bora watakaofaulu kupitisha ujumbe. Mtaalamu huyu alidokeza kuwa, maneno kama haya hutafsiriwa kwa matumizi ya zaidi ya neno moja ili maana isipotoshwe katika lugha lengwa. Mawazo hayo ni muhimu katika kazi yetu kwa vile tulichunguza jinsi watafsiri wawili walivyotafsiri kazi zao.

Picken (1983) anaongezea kwamba, ufafanuzi katika tafsiri hujaza mapengo yaliyopo baina ya lugha lengwa na lugha asilia. Maneno mengi mara nyingi huathiriwa na mazingira ya kimatumizi na utamaduni wa wanaotumia lugha husika. Anapendekeza kwamba, inafaa matini nzima isomwe kabla ya kufanyiwa tafsiri. Aidha, mtaalamu huyu ametoa fasili ya sifa muhimu za watafsiri wa matini. Kwa mfano, amedai kwamba mtafsiri ni lazima awe na uwezo wa kuteua maneno yanayofaa kimatumizi katika matini rasmi na isiyo rasmi. Aidha, aweze kuchagua mpangilio mwafaka wa maneno na jinsi ya kuakifisha maneno hayo kwa njia inayofaa.

Watafsiri na wakalimani kwa mfano, wataweza kuwakilisha ujumbe kwa urahisi zaidi iwapo wana uwezo wa kuchagua maneno yafaayo ya kutumiwa katika muktadha maalum. Aidha, watafsiri na wakalimani watatimiza mawasiliano kwa kuchagua mpangilio ufao wa maneno katika sentensi za lugha lengwa, na kuteua namna ya kutumia viziada lugha na arudhi za kifonolojia kama vile shadda, kiimbo na

kadhalika. Kwa mfano, katika tasnifu hii watafsiri walitumia maneno mengi katika kupitisha ujumbe. Katika MMS mtafsiri alitumia sura ishirini na tano kama ilivyo katika makala asilia lakini kurasa ni nyingi zaidi. Katika makala asilia ya *Government Inspector*, msanii alitumia kurasa mia moja hamsini na moja (151) ilhali katika tamthilia ya MMS kuna kurasa mia moja tisini na nne (194).

Newmark (1991) anadai kuwa mtafsiri ni sharti afasiri yale yaliyoandikwa na mwandishi asilia ndiposa tafsiri ifanikishe mawasiliano. Utafiti huu umefaidika kutokana na mawazo haya katika kuchunguza mielekeo ya kazi zilizotafsiriwa. Newmark (1991) ameyataja baadhi ya mambo muhimu ambayo mtafsiri mweledi anastahili kudhihirisha, nayo ni:

- (i) Wepesi wa kuelewa.
- (ii) Ufahamu wa lugha na tamaduni mbalimbali.
- (iii) Maarifa ya awali kuhusu mada.

Baadhi ya sifa zilizotajwa na Newmark (1991) zilinufaisha uchunguzi huu kuhusiana na ufahamu wa lugha ambao wanaotafsiri wanafaa kuwa nao ili wafanye kazi ya tafsiri kwa njia inayostahili. Inadhihirika kuwa watafsiri ni sharti wawe na ujuzi wa lugha asilia na lugha lengwa. Zguta (1971) katika Baker (1992) anaeleza kuwa kila neno (msamiati) una kitu ambacho ni cha nafsi ambacho kinafanya neno hilo kutofautiana na maneno mengine, hivyo, ni maana ya msamiati huo ambao ni dhihirisho kuu ya neno hilo.

Venuti (1992) aligundua kuwa, matini lengwa haiwi aminifu na huru kwa kiwango fulani. Mtaalamu huyu alionyesha kuwa wakati mwingine matini lengwa hutofautiana kabisa na matini asilia kwa sababu utafsiri huathiriwa na hali mbalimbali kama vile masuala ya kiutamaduni, kimazingira na tajriba ya mtu binafsi katika maisha.

Kutokana na utafiti wake, Venuti (1992) anaeleza kwamba, mtafsiri mashuhuri anastahili kutoa tafsiri ya maana na sio umbo. Mtaalamu huyu anadai kuwa, tafsiri ya kazi yoyote hufanikiwa ikiwa itaweza kusomeka kwa wepesi. Matini zilizotafsiriwa vizuri hubeba ujumbe asilia na huonyesha dhahiri mawazo na maana ya mwandishi wa matini asilia. Maoni hayo ya Venuti yanatuongoza katika tasnifu hii kwa kuwa, tulilinganisha matini pokezi za MMS na MS.

Newmark (1988), Wills (1992) na Mwansoko (1996) wanahoji kuwa, dhana ya uhawilishi katika tafsiri huhusu hali ya kuleta athari sawa katika kazi iliyotafsiriwa kama ilivyo katika makala asilia. Yaani, msomaji wa makala pokezi apate athari sawa na ilivyokusudiwa na mwandishi wa makala asilia. Jambo hili laweza kukumbwa na changamoto hasa ikiwa kuna tofauti kubwa kati ya makala asilia na makala pokezi kwa uhawilishi wa matini chanzi hutofautiana au hufanana kwa kutegemea mbinu iliyotumika katika tafsiri na hadhira lengwa.

Nord (1997) alichunguza dhima za mtafsiri katika mawasiliano na alieleza kuwa, mtafsiri yeyote ana jukumu kuu la kupitisha maana asilia katika lugha lengwa. Nord anahoji kuwa, katika tafsiri, matini asilia inaweza kutafsiriwa kwa muda mrefu kwa vipindi tofauti tofauti. Watafsiri aghalabu wanaweza kutumia muda mrefu na kurejelea kamusi ili kufanya tafsiri ifaayo zaidi kinyume na ukalimani ambapo mkalimani hana wakati wa kurejelea kamusi kwani ukalimani hufanywa wakati huo huo msemaji anapozungumza.

Pili, katika kazi ya tafsiri, matini inayotafsiriwa inaweza kufanyiwa mabadiliko ili kustawisha uwasilishaji wa ujumbe na hata kuna uwezekano wa kuwa na matokeo tofauti za tafsiri ya matini moja. Aidha, tafsiri huandikwa na matini inayojitokeza huweza kuchukua muda mrefu kama hajjafikia hadhira yake. Tofauti hizi

zilizoshugulikiwa na Nord (1997) zitafaidi utafiti huu kwa kubainisha tafsiri na ukalimani.

Nord (1997) alichunguza iwapo kuna tofauti baina ya tafsiri na ukalimani. Uchunguzi wake ulibaini kuwa, malengo ya ukalimani na tafsiri huwa sawa. Malengo yenyewe ni yale ya kuhakikisha kuwa kuna mawasiliano madhubuti. Madai ya Nord ni muhimu katika tasnifu hii kwa kuwa yaliwezesha uchunguzi huu kutambua umuhimu wa kuipa kipaumbele kipengele cha kufanikisha mawasiliano katika tafsiri. Mtaalamu huyu alichunguza matumizi ya viziada lugha na jinsi vinavyotafsiriwa na wanaoifanyia ukalimani matini. Mtaalamu huyu aligundua kuwa watu wanaomsikiliza mkalimani mara nyingi hutegemea sauti pamoja na viziada lugha vinavyotumiwa na mkalimani ili kuupokea ujumbe unaowasilishwa. Nord (1997) anadai kuwa, kutofautiana kwa viziada lugha vya lugha asilia na vya lugha lengwa kunaweza kusababisha hitilafu za kimawasiliano.

Shitemi (1990), anatilia mkazo umuhimu wa tafsiri katika kuunganisha tamaduni mbalimbali na wanadai kwamba mtafsiri ni sharti aelewe utamaduni wa jamii ya lugha chanzi pamoja na utamaduni wa lugha pokezi ili aweze kufanikiwa katika kazi ya tafsiri. Maoni haya ya Shitemi yalituongoza kwa kuwa tulihakiki tafsiri mbili za matini chanzi moja ingawa hatukushughulikia suala la utamaduni, lakini utafiti wetu ulichunguza matini mbili zilizotafsiriwa kutokana na matini chanzi moja

Shitemi (1997) anadai kuwa, haiwezekani tafsiri kufanywa katika ombwe tupu kwa sababu, katika kutimiza mawasiliano, mtafsiri atazingatia kwa makini uhusiano uliopo baina ya virejelezi, virejelewa na muwala unaovipatia umaalum wa kimaana. Maelezo haya yanabainisha wazi kuwa tafsiri haifanyiki kiholela, yaani mtafsiri anapaswa kuzingatia kanuni na vigezo maalum ili kuwepo na mawasiliano maalum. Shitemi

(1997) alichunguza uaminifu katika tafsiri za kazi za kishairi na anadai kuwa, "baadhi ya wahakiki wa tafsiri wanakieleza kitendo cha kutafsiri kama kisichotimilika na kumwona mtafsiri akiwa msaliti wa mtunzi asilia na makala yanayotafsiriwa". Ingawa utafiti wa Shitemi ulikuwa unahusu mashairi, matokeo ya utafiti wake ni muhimu katika utafiti huu.

Mojawapo ya kipengele nilichokianguzia kwenye utafiti huu ni kile alichokitaja Shitemi (1997) kama "usaliti wa mtunzi." Hii ni kwa sababu katika tasnifu hii tutachanganua kiulinganishi makala mbili zilizotafsiriwa na zinalenga makala moja asilia. Hivyo basi, msanii ambaye atakuwa hajaelezea au kupitisha mawazo yake kama yalivyo katika makala asilia basi atakuwa amemsaliti mtunzi wa makala asilia.

Shitemi (2004) anadai kuwa, kuna hatua mbalimbali za kufuatwa katika kusoma na kuandaa tafsiri mojawapo ikiwemo ile ya kutalii upekee wa kiisimu baina ya LA na LP na kuibuka na namna ya kufidia tofauti zilizopo. Maelezo haya ya Shitemi (2004) yanachangia katika utafiti wetu kwa kudhihirisha kuwa kuna umuhimu wa kutalii vipengele vya kiisimu katika LP na LA ili kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi kuhusu namna ya kutekeleza tafsiri. Tofauti ni kuwa, tasnifu hii inajishughulisha na uhakiki linganishi wa mbinu za lugha, matumizi ya lugha katika uwasilishaji wa taarifa mbalimbali na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika vitabu vilivyoteuliwa.

Makala katika Taifa leo ya tarehe (20 Juni, 2005) inaelezea matokeo ya uchunguzi kuhusu tafsiri za kazi za sanaa za kigeni katika Kiswahili. Mwandishi wake anafafanua tafsiri kama fani ambazo zinahitaji ujuzi wa lugha mbili zinazohusika. Mwandishi huyo wa Taifa leo ya tarehe 20, Juni (2005) anadadisi kwamba, ili mtafsiri aweze kuwakilisha matini ya lugha asilia hadi lugha lengwa ipasavyo, ni sharti aelewe



utamaduni wa lugha asilia na wa lugha lengwa barabara. Madai hayo katika Taifa leo ya tarehe (20, Juni 2005) yanatupa mwanga kuhusiana na uchunguzi wa uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika tasnifu hii kwa vile watafsiri wanafanikiwa kuwasilisha ujumbe iwapo wanazimudu utamaduni wa lugha asilia na lugha lengwa.

Farazad na wenzake (2009) walihakiki kazi zilizotafsiriwa na watafsiri wawili waliotafsiri tamthilia ya Kiamarekani inayoitwa Marekani inayoitwa *Gone With the Wind*. Wataalam hao walichunguza kiulinganishi tofauti katika uwasilishaji wa maudhui, dhamira na usawiri wa wahusika na waliibuka na maoni kuwa tafsiri hizo mbili zilitofautiana hasa katika usawiri wa wahusika na uwasilishaji wa maudhui. Kazi ya wataalamu hao ilituongoza kwa vile utafiti huu pia ulishughulikia uhakiki linganishi wa tamthilia za Kiswahili za MMS na MS.

Tofauti kati ya kazi hiyo na utafiti wetu ni kwamba wao walishughulikia uhakiki lilinganishi wa tamthilia zilizotafsiriwa na zilizolenga matini asilia moja ambayo ni *Gone With the Wind* ilhali utafiti huu ulichunguza kiulinganishi tofauti za kitafsiri katika tamthilia za Kiswahili za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*. Nadharia ya Uamilifu katika Tafsiri Mtazamo wa Kuhakiki Matini iliongoza utafii huu na imeangaziwa kwa kina katika sehemu ifuatayo.

## **2.6 Misingi ya Kinadharia**

Nadharia ya Uamilifu katika Tafsiri iliasisiwa na Nida (1964) na inahusu mbinu anuwai za kukabili makala katika tafsiri. Kuna mitazamo mbalimbali ya Nadharia ya Uamilifu katika Tafsiri nazo ni: Nadharia ya Uamilifu katika Tafsiri, Mtazamo wa Kuhakiki Matini (Text Type Approach), Nadharia ya Uamilifu katika Tafsiri:

Mtazamo wa Utenda Kazi na Nadharia ya Uamilifu katika Tafsiri: Mtazamo wa Skopos.

Nida (1964) anahoji kuwa kulingana na Nadharia ya Uamilifu, tunaposhugulikia jambo lolote katika mchakato wa tafsiri, ni muhimu kuangazia dhima au kazi ya jambo hilo. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uamilifu katika Tafsiri Mtazamo wa Kuhakiki Matini (Text Type Approach) uliopendekezwa na Reiss (1977). Mtaalamu huyu anadai kwamba kimsingi tafsiri ni hali ya kuhamisha vipengele vya isimu kutoka lugha asili hadi lugha pokezi na anatilia mkazo kwenye matini na wala sio neno ama sentensi, yaani anasisitiza hoja kuwa matini huibua mawasiliano katika jamii. Pia anadahili kuwa, Mtazamo wa Kuhakiki Matini (Text Type Approach), unachukulia kazi ya tafsiri kama zisizotekelezwa kiholela bali zinazolenga kutimiza mahitaji fulani katika jamii.

Katika kutimiza malengo ya utafiti huu, mtazamo huu ulikuwa msingi wa kutegemewa kwani hakuna kipengele chochote katika shughuli ya tafsiri ambacho hutekelezwa bila kuwa na uamilifu wake. Vipengele hivyo ni: mbinu za lugha, maudhui na wahusika katika fasihi na vipengele hivi ndivyo tulivyovishughulikia katika utafiti huu. Kulingana na Reiss (1977), tafsiri iliyokamilika ni ile ambayo kusudi katika LP ni sawa ikilinganishwa na ile inayopatikana katika LA. Yaani, tafsiri ifanye kazi ya kuutoa ujumbe kutoka LA na kuwakilisha katika LP.

Mtaalamu huyu pia anadahili kuwa, kila lugha huwa na upekee wake katika ubunifu wa majina. Yaani, lugha hazitoi majina au msamiati tu kwa vitu au dhana zilizopo bali zina mfumo maalum wa kubuni. Hivyo, nadharia hii ni muhimu kwa kuwa tulihakiki MP mbili zilizotafsiriwa kutoka kwa lugha ya Kirusi na Kiingereza. Upekee

huu unaopelekea lugha moja kutofautiana na nyingine ndio pia unaozua swala la uamilifu wa lugha na hasa katika tafsiri.

Kutokana na maelezo haya ya Reiss (2000), tafsiri sio jambo la moja kwa moja kutoka lugha moja hadi nyingine kwa kufuata utaratibu wa uchopezi. Kinyume chake ni kwamba tafsiri ni mchakato unaohitaji kuelewa upekee huo unavyowasilishwa kwa LP. Reiss (2004) anadahili kuwa, tafsiri nzuri ni ile ambayo wazungumzaji wa lugha pokezi wataupokea, kuelewa na kuuhisi ujumbe wa matini chanzi kama vile wazungumzaji wa lugha asilia (LA). Tafsiri inahusu namna LP kama chombo muhimu cha mawasiliano kimefanya kazi na kusawazisha ujumbe kutoka LA.

Msingi wa Nadharia ya Uamilifu ni kwamba, tafsiri inahusu kulenga nia fulani mahsusi ya kimawasiliano ambayo huenda inafanana au kutofautiana na ile waliyonayo wahusika wengine katika makala pokezi. Reiss (1989) anadai kuwa, tafsiri hufanywa kwa njia inayoweza matini kuwa na uamilifu katika mazingira ambamo inatumika na kwa watu wanaotaka kuitumia kwa namna wanavyotaka itumike. Nadharia ya Uamilifu katika tafsiri Mtazamo wa Kuhakiki Matini ina mihimili mikuu mitatu. Mihimili hiyo ilikuwa muhimu katika uchanganuzi wa data ya utafiti huu na nimeelezea ifuatavyo:

- a) Utambuzi kuwa maneno ni malighafi muhimu kwa yeyote anayetaka kutumia lugha fulani katika miktadha tofautitofauti. Mtazamo wa Kuhakiki matini, huhakikisha kuwa kuna utoshelevu wa kimaana, kisarufi na kimtindo katika lugha lengwa kwa minajili ya kuuwasilisha ujumbe kwa wapokeaji wake. Kipengele hiki kilikuwa muhimu katika utafiti wetu kwa sababu kilitusaidia kutambua kiulinganishi jinsi mbinu za lugha zilivyotumiwa katika tafsiri za MMS na MS. Nadharia hii ilituongoza kutambua kiulinganishi namna watafsiri

wa MMS na MS walivyotumia mbinu za lugha kama vile chuku, tashbihi, kinaya na uzungumzi nafsia kwa kuwa lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza kiulinganishi mbinu za lugha katika MMS na MS. Katika tasnifu hii tumelinganisha mbinu za lugha katika MMS na MS pasi na kuzingatia matini chanzi yoyote kwa sababu kila lugha huitalii ulimwengu kwa namna tofauti na lugha nyingine.

- b) Kaida za matumizi ya lugha na welewa ya kwamba maana ya neno hurejelewa kwa kuhusishwa na maneno mengine katika sentensi na kuhusisha na sentensi nyingine katika matini au kwa kuhusisha na matamshi mengine yanayohusiana na mada au muktadha wa diskosi inayohusika. Kwa mtazamo wa nadharia hii, muundo na maneno ya lugha asilia yanaweza kuachwa na maana asilia ikawasilishwa kwa msamiati tofauti wa lugha lengwa ili kuupitisha ujumbe. Hii ina maana kuwa, ujumbe unapewa umuhimu zaidi katika mchakato wa tafsiri kuliko miundo na maumbo. Yaani, mtafsiri anapokosa kutumia lugha sahihi kwenye kazi yake, mawasiliano yanakosa kutimia kama ilivyokusudiwa na msanii wa makala asilia.

Kipengele hiki ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu kilitusaidia katika kutambua kiulinganishi jinsi ujumbe ulivyowasilishwa katika MP1 na MP2. Hii ni kwa sababu lengo la pili la utafiti huu ni kuchambua kiulinganishi uwasilishaji wa ujumbe katika MMS na MS.

- c) Muktadha wa mazingira ni muhimu katika tafsiri, yaani maneno hayana maana moja tu lakini huweza kupata maana zaidi kwa kutegemea mazingira ya kijamii ambamo neno hilo limetumika. Hivyo, matini pokezi inatarajiwa iwe na mguso sawa na inavyodhihirika katika matini asilia.

Kwa mujibu wa utafiti huu, mguso aupatao msomaji wa kazi za fasihi, hutegemea jinsi msanii alivyowabuni na kuwasawiri wahusika wake. Kwa kuwa wahusika hutumika katika kupitisha ujumbe na falsafa ya msanii kupitia maswala makuu (ujumbe). Kipengele hiki ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu kilitusaidia kutambua kiulinganishi jinsi ubunifu na usawiri wa wahusika katika kazi ya fasihi unavyoweza kuathiri mchakato wa tafsiri, kwa sababu, lengo la tatu la utafiti huu ni kuhakiki kiulinganishi usawiri wa wahusika katika tafsiri za MMS na MS. Hata hivyo, katika utafiti huu, tabia na sifa za wahusika wa vitabu vilivyoteuliwa zililinganishwa pasi na kuegemezwa kwenye Matini Chanzi yoyote.

## **2.7 Hitimisho**

Katika sura ya pili, imebainika kwamba wataalamu mbalimbali wameshughulikia mada tofautitofauti kuhusiana na suala la tafsiri kwa ujumla. Kwa mfano, wataalam wengine wameshughulikia vipengele vinavyosababisha kuwepo na ufaafu katika tafsiri na michango inayotokana na tafsiri. Ingawa utafiti huu ni tofauti na uchunguzi wa wataalam hao, yapo maandishi mengi kuhusu tafsiri kwa jumla na tafsiri za kazi za fasihi, hususan mifano ya fasihi za Kiingereza na lugha nyinginezo za kimagharibi. Maelezo hayo na mifano yamefanikisha utafiti huu. Mahitimisho kadha wa kadha yaliyofikiwa na wataalamu walioishughulikia taaluma ya tafsiri yamechangia katika ufanisi wa tasnifu hii.

Sehemu hii pia imejadili nadharia iliyoongoza tasnifu hii ambayo ni Nadharia ya Uamilifu katika Tafsiri Mtazamo wa Kuhakiki Matini (Text Type Approach) iliyopendekezwa na Reiss (1977). Imebainika kuwa, nadharia hyo ilikuwa mwafaka katika tasnifu hii kwa kuwa mihimili mikuu ilioana na malengo ya utafiti. Hata hivyo,

katika utafiti huu, suala la uaminifu katika tafsiri halijazingatiwa kwa sababu kazi ya tafsiri ni kazi ya kiubunifu. Sura zifuatazo za tatu, nne na tano ni sura za uchanganuzi katika tasnifu hii. Sura ya tatu ifuatayo imeshughulikia uchanganuzi wa mbinu za lugha katika tamthilia za MMS na MS.

## SURA YA TATU

### UHAKIKI LINGANISHI WA MBINU ZA LUGHA KATIKA

#### *MKAGUZI MKUU WA SERIKALI NA MKAGUZI WA SERIKALI*

### 3.0 Utangulizi

Sura hii inachanganua kiulinganishi mbinu za lugha katika tafsiri za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Mwakasaka, 1979) na *Mkaguzi wa Serikali* (Madumulla, 1999) katika sehemu zifuatazo za sura hii, nimechanganua kiulinganishi mbinu za lugha zilivyotumiwa kiufundi katika tafsiri za MMS na MS. Baadhi ya mbinu za lugha zilizohakikiwa ni chuku, uzungumzi nafsia, kejeli, matumizi ya barua, kinaya, matumizi ya ndoto, kuchanganya ndimi, misemo na nahau. Katika sehemu ifuatayo ya 3.1, tumechanganua kiulinganishi matumizi ya mbinu ya chuku yanavyojitokeza katika tamthilia za MMS na MS.

### 3.1 Chuku

Kulingana na TUKI (2013), chuku ni mbinu ya kuongeza chumvi kwenye taarifa au ujumbe ili kusababisha kicheko. Mbinu ya chuku ilitumiwa katika visa mbalimbali katika tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (MMS) na *Mkaguzi wa Serikali* (MS) na visa hivyo vimenukuliwa kama mifano tofautitofauti. Mwanzo, tumeangazia mfano 1 ufuatao ambao ni nukuu inayothibitisha matumizi ya chuku kutoka tamthilia za MMS na MS.

#### Mfano 1

**MMS:** Hakimu .... Lakini kama ungeona moja ya makaratasi basi maisha hayangekuwa tena mazuri kama yalivyo. ---Solomon mwenyewe hangejua vipi kutofautisha ukweli na uwongo! (uk 10-11).

**MS:** Jaji:... Mungu amhurumie yule atakayejaribu kuchunguza usahihi wa vitabu na stakabadhi zote zile, kwa sababu atajutia siku aliyozaliwa!-- Hata yule Mfalme Suleiman anayesemekana kuwa alijaliwa hekima tele asingeweza kuchanganua mambo ya hapa (mahakamani). (uk 15)

Mfano 1 unabainisha kwamba, watafsiri wa MMS na MS walifaulu kuhawilisha matumizi ya mbinu ya chuku kutokana na namna ambavyo kumbukumbu zimechanganywa kule mahakamani. Hata hivyo, uteuzi wa maneno uliofanywa na watafsiri hao unatofautiana inavyoonekana katika mfano 1. Kwa mfano, katika MMS, Hakimu anasema kuwa; mtu angeona moja ya makaratasi basi maisha hayangekuwa tena mazuri kama yalivyo...hata Solomon mwenyewe hangejua vipi kutofautisha ukweli na uwongo.

Kwa upande mwingine, katika MS, Jaji anasema; Mungu amhurumie yule atakayejaribu kuchunguza usahihi wa vitabu na stakabadhi zote zile, kwa sababu atajutia siku aliyozaliwa! Hata yule Mfalme Suleiman anayesemekana kuwa alijaliwa hekima tele asingeweza kuchanganua mambo ya hapa. Inaelekea kwamba utungo huu; ‘kujutia siku ya kuzaliwa’ na ‘Mfalme Suleiman kutoweza kung’amua ufidadi ulioendelezwa mahakamani’ unajitokeza katika MS (mfano 1) bali haupo katika MMS.

Katika utafiti huu, tulihoji kuwa kutofautiana kwa watafsiri wa MMS na MS (mfano 1) katika uhawilishaji wa ujumbe kunaashiria ukiushi wa kimtindo ambapo mtafsiri hatumii visawe vya maneno yaliyotumiwa na mwandishi wa matini chanzi. Hali hii ya ukiushi inaonyesha uhuru uteuzi wa msamiati unaoweza kufanywa na watafsiri. Katika tasnifu hii tulichukulia kwamba, uhuru huo wa mtafsiri wa kuteua msamiati katika mchakato wa tafsiri unaweza kuathiriwa na mazingira ya kulelewa ya mtafsiri na tajriba ya mtu binafsi katika maisha. Mfano 2 ufuatao pia unabainisha matumizi ya mbinu ya chuku yalivyojitokeza katika MMS na MS.



## Mfano 2

**MMS:** Mkuu wa wilaya:... Lakini anafundisha kwa mori kiasi cha kuwa huwezi kumwelewa. ...lakini alipomfikia Aleksanda mkuu hungeweza kuamini kabisa, nilidhani kuwa mahali panaungua moto (uk 5).

**MS:** Meya: ... Mwalimu wa somo la historia ni mwerevu sana na hulimudu somo lake lakini mbona hupandwa na jazba kiasi kwamba anapofunza, mtu atadhani kwamba shule inaungua moto? (uk 6-7).

Katika mfano 2, watafsiri wa MMS na MS walitumia mbinu ya chuku kwa kuelezea jinsi mwalimu alivyofunza somo la Historia. Kwa mfano, katika tamthilia ya MMS (mfano 2), Mkuu wa Wilaya anaeleza kwamba: mwalimu anafundisha kwa mori kiasi cha kuwa mtu hawezi kumwelewa, bali katika tamthilia ya MS (mfano 2), Meya anasema kuwa; Mwalimu wa somo la historia ni mwerevu sana na hulimudu somo lake lakini hupandwa na jazba wakati anapofundisha kiasi cha kwamba mtu atadhani kuwa shule inaungua moto.

Ingawa mbinu ya chuku ilitumiwa na watafsiri wa MMS na MS katika mfano 2, watafsiri hao walitofautiana katika uteuzi wa maneno. Kwa mfano, katika MMS (mfano 2), Mkuu wa Wilaya anasema kuwa, mwalimu alifundisha 'kwa mori' bali katika MS (mfano 2), Meya anaeleza kwamba, mwalimu hupandwa na jazba anapofundisha. Tungo zilizopigiwa mistari hazifanani kimaana kwa kuwa, kulingana na TUKI, (2013) neno jazba lina maana ya msisimko wa kihisia ambao husababisha mtu kuchachawa ilhali neno mori lina maana ya hasira nyingi mno.

Katika tasnifu hii, tulihoji pia kwamba, katika mfano 2, kishazi katika MMS: mahali panaungua moto ni tofauti kimaana na kishazi katika MS: shule inaungua moto. Yaani, neno shule haiwezi kuwa ni sinonimi ya neno mahali. Hivyo tulidahili kuwa, mtafsiri huweza kuibuka na matini ambayo ni tofauti kabisa na matini chanzi kwa

kuwa ana uhuru wa kuteua msamiati anavyotaka. Matumizi ya chuku pia yalijitokeza katika mfano 3 ufuatao.

### Mfano 3

**MMS:** Ghlestakovu: Mungu wangu! Aina gani hii ya supu? Sidhani kuna mwingine yeyote duniani anayeweza kumeza supu hii! Shetani tu ndiye ajuaye ni nini lakini si kuku. (Uk 20).

**MS:** Hilestakov: Mungu wangu, mchuzi umeoza kabisa! ... Siamini kama mtu yeyote anayeishi amepata kuonja kitu kibaya kushinda supu hii!. Ni Mungu tu anajua, lakini si nyama. Ni ngumu kabisa! (Uk 31).

Mfano 3, unadhihirisha matumizi ya mbinu ya chuku yalivyojitokeza katika MMS na MS Ghlestakovu/Hilestakov alipoinywa supu hotelini na kulalamika kuwa haikuwa supu nzuri. Kwa mfano, katika MMS, Ghlestakov anasema kwamba: Mungu wangu! Aina gani hii ya supu? Sidhani kuna mwingine yeyote duniani anayeweza kumeza supu hii! Shetani tu ndiye ajuaye ni nini lakini si kuku.

Katika MS, Hilestakov anasema: Mungu wangu, mchuzi umeoza kabisa! Siamini kama mtu yeyote anayeishi amepata kuonja kitu kibaya kushinda supu hii!. Ni Mungu tu anajua, lakini si nyama. Ni ngumu kabisa. Katika MMS, Ghlestakov anasema kuwa, ni shetani tu ndiye anajua aina ya supu aliyopewa naye Hilestakov katika MS anasema kuwa, ni Mungu tu aliyejua nyama hiyo aliyopewa ilikuwa ni nini.

Tulidahili kuwa, Hilestakov alidai kuwa chakula hicho kilikuwa kibaya na alikihusisha na shetani, kwa kuwa katika uhalisia wa maisha, shetani huhusishwa na chochote kibaya. Kwa upande mwingine, Ghlestakov anasema kwamba ni Mungu tu ndiye angeweza kufahamu aina ya nyama aliyopewa, hivyo anamtaja Mungu kana kwamba anahitaji usaidizi wa Mwenyezi Mungu amwauni kutokana na jambo lisilofaa. Aidha, tulidahili kwamba, uhuru wa mtafsiri wa kuteua msamiati katika shughuli za tafsiri, hupelekea watafsiri kuteua msamiati wanavyopenda na kuibuka na

tofauti katika uhawilishaji wa ujumbe. Mfano 4 pia umeangazia matumizi ya chuku katika MMS na MS.

#### Mfano 4

**MMS:** Mkuu wa wilaya:... Nimewalaghai walaghai kwa maelfu. Majangili na majambazi ambao wangeweza kuiba dunia nzima, wote wamenaswa. (uk 76).

**MS:** Meya: Nimewahadaa magwiji wa kuhadaa ambao wangeweza kuwahadaa binadamu wote wakaangamia! (uk 113-114).

Watafsiri wa MMS na MS walitumia mbinu ya chuku inavyobainika katika mfano 4.

Kwa mfano, katika MMS (mfano 4), Mkuu wa Wilaya anasema kuwa: Nimewalaghai walaghai kwa maelfu. Majangili na majambazi ambao wangeweza kuiba dunia nzima,

wote wamenaswa bali katika MS (mfano 4), Meya anasema kuwa: Nimewahadaa magwiji wa kuhadaa ambao wangeweza kuwahadaa binadamu wote wakaangamia.

Tungo zilizopigiwa mistari kutoka (mfano 4) hazifanani kimaana. Kwa mfano, maneno haya: walaghai, majangili na majambazi yametumiwa tu katika MMS bali katika MS, Madumulla ametumia magwiji wa kuhadaa.

Katika MMS (mfano 4), Mkuu wa Wilaya anaeleza kuwa: majangili na walaghai hao wangeweza kuiba dunia nzima ilhali katika MS (mfano 4), Meya anasema kwamba,

magwiji hao wa kuhadaa wangeweza kuwahadaa binadamu wote wakaangamia. Swali linaloibuka ni je, kishazi katika MMS: angeweza kuiba dunia nzima ni sinonimi ya

kishazi katika MS: wangeweza kuwahadaa binadamu wote wakaangamia? Katika utafiti huu, tulidahili kwamba, tofauti ya kimaana katika tungo zilizopigiwa mistari

zimeibuka kwa sababu ya uhuru walionao watafsiri wa kuteua msamiati kulingana na mapenzi yao. Pia, mfano 5 ufuatao unathibitisha matumizi ya chuku yalivyojitokeza

katika tamthilia za MMS na MS.

## Mfano 5

**MMS:** Mkuu wa wilaya: ... Mungu wangu! Nilisahau. Nyuma ya uzio huo kuna lundo la takataka ambazo hata mikokoteni arobaini haiwezi kuziondoa. (Uk 12).

**MS:** Meya: Hapana, ngoja! Mungu wangu! Nilisahau kabisa kuhusu rundo la takataka zilizooza lililopo nyuma ya ule ua. Hata mikokoteni arobaini haitaweza kulimaliza rundo hilo hata kama itafanya kazi hiyo kwa wiki nzima. (Uk 17-18).

Mfano 5 umedhihirisha mbinu ya chuku ilivyojitokeza katika MMS na MS, Mkuu wa Wilaya (Meya) alipozungumzia rundo la takataka linalopatikana nyuma ya uzio. Kwa mfano, katika MMS (mfano 5), Mkuu wa Wilaya anasema kuwa: kuna rundo la takataka ambazo hata mikokoteni arobaini haiwezi kuziondoa ilhali katika MS (mfano 5), Meya anasema kuwa: kuna rundo la takataka ambalo hata mikokoteni arobaini haitaimaliza hata kwa wiki nzima.

Kutokana na tungo zilizopigiwa mistari (mfano 5), mtafsiri wa MS amezungumzia kipindi cha wakati, yaani anaeleza kwamba, kama mikokoteni arobaini ingeshughulikia kazi ya kuondoa uchafu huo hata kwa wiki nzima, haingefaulu. Mtafsiri wa MMS, hakutaja kipindi maalum. Badala yake anaeleza kwamba uchafu umejaa mno katika uzio huo hata mikokoteni arobaini ingetumika kuuondoa haitaweza. Katika tasnifu hii tulihoji pia kwamba, mtafsiri wa MMS hakutaja usemi wa wiki mbili kwa kuwa, kama mtafsiri, ana uhuru wa ama kupuuza, au kuongeza maneno anavyopenda katika mchakato wa tafsiri ili aweze kutosheleza hadhira lengwa. Aidha, mfano 6 ufuatao unadhihirisha matumizi ya chuku katika MMS na MS.

## Mfano 6

**MMS:** Ghlestakovu: Ni chumba duni kabisa. Na kunguni waliomo, sijapata kuona aina yake. (uk 25).

**MS:** Hilestakov: Kina unyevunyevu? Mahali hapa ni pito la uchafu! Na bado hujawaona kunguni-wanaouma kama mbwamwitu. (uk 37).

Mfano 6, ulionukuliwa kutoka tamthilia za MMS na MS unathibitisha matumizi ya mbinu ya chuku. Kwa mfano, katika MMS na MS, Ghlestakovu/Hilestakov alimlalamikia Mkuu wa Wilaya (Meya) kuhusu kunguni waliomo katika chumba alicholala. Kwa mfano, katika MMS, Ghlestakov anasema kuwa, hajapata kuwaona aina ya kunguni waliomo kwenye chumba kile bali katika MS, Hilestakov anamwambia Meya kuwa hajawaona kunguni wanaouma kama mbwa mwitu.

Matumizi ya tashbihi ‘kama mbwa mwitu’ iliyotumiwa katika MS, haijatumika katika MMS. Katika tasnifu hii, tulidahili kuwa, tofauti za kitafsiri zinazobainika katika mfano 6, zimesababishwa na hoja kuwa, aghalabu watafsiri huathiriwa na mazingira ya kulelewa, masuala ya kiutamaduni na hali ya ubunifu ya mtu binafsi. Hivyo, katika harakati ya kutafsiri, mtafsiri ana ule uhuru wa ama kupiku au kudondoa msamiati uliopo kwenye matini chanzi. Matumizi ya mbinu ya chuku pia yamejitokeza katika mfano 7 ufuatao.

### **Mfano 7**

**MMS:** Yosif: Ngoja kidogo, ngoja nipumue. Tumbo wazi hukifanya kila kitu kizito. (uk 32).

**MS:** Osipu: Subiri kidogo nipumue. Whuu! Mzigo mzito huu! Hata mzigo wa nyoya ungekuwa mzito kwa mtu ambaye hajatia kitu tumboni. (uk 47).

Katika mfano 7, watafsiri wa tamthilia za MMS na MS walifaulu katika matumizi ya mbinu ya chuku, Yosif/Osipu anapoutua mzigo analalamika akitumia utani kuwa anahisi njaa sana. Kwa mfano, katika MMS (mfano 7), Yosif anasema kuwa, mtu akihisi na njaa (tumbo wazi), kila kitu huwa ni kizito naye Osipu katika MS (mfano 7), anasema kuwa, mtu akiwa na njaa (hajatia kitu tumboni) hataweza kuubeba hata

mzigo wa nyoya, yaani kila kitu chepesi kabisa huwa kizito. Watafsiri hao wawili walifaulu kuhawilisha mbinu ya chuku lakini uteuzi wa maneno unachangia katika kuibua tofauti ya uwasilishaji wa matumizi ya mbinu ya chuku katika MMS na MS. Neno unyoya haipo katika tamthilia ya MMS badala yake Osipu anasema kuwa, kila kitu huwa kizito. Mfano 8 ufuatao pia ni nukuu kutoka tamthilia za MMS na MS. Mfano huu, unabainisha matumizi ya chuku.

### **Mfano 8**

**MMS:** Ghlestakovu:...Na mnajua niliingia idara kama tufani, kama tufani kabisa! Kila kitu kilitetemeka na kutikisika kama jani! (uk 39).

**MS:** Hilestakov: ...Na mnajua? Nilipoizungukia idara, ungedhani kama kuna tetemeko la nchi kwa jinsi watu wote walivyotetemeka kwa hofu! (uk 55).

Mfano 8 unadhihirisha kuwa mbinu ya chuku ilitumiwa katika tamthilia za MMS na MS, Ghlestakovu/Hilestakov alipoambia hadhira kuwa, watu walimwogopa sana wakati mmoja alipoongoza idara fulani. Ingawa matumizi ya chuku yalijitokeza katika tamthilia za MMS na MS, kuna tofauti ya namna ya uwasilishaji. Kwa mfano, katika MMS Ghlestakovu anasema kuwa, aliingia idarani kama tufani na kusababisha kila kitu kutetemeka kama jani, katika MS, Hilestakov anasema kuwa, alipoizunguka idara mtu angedhani kuna tetemeko la nchi kwa jinsi watu walivyotetemeka kwa hofu.

Kimaana, tungo zilizopigiwa mistari hazifanani kwa kuwa matumizi ya tashbihi, kama tufani na kama jani zinajitokeza tu katika MMS, na hazipo katika MS. Isitoshe, katika MMS Ghlestakov anatumia maelezo ya kijumla kwa kusema kuwa, kila kitu kilitetemeka kinyume na ilivyo katika MS ambapo Hilestakov anasema kuwa, watu wote walitetemeka kwa hofu. Kwa hivyo, maneno: kila kitu (katika MMS) ni tofauti kimaana na maneno watu wote, (katika MS) kwa kuwa, maneno: kila kitu kina maana

ya chochote kama vile nyumba, watu, wanyama nk. Hivyo, katika tasnifu hii tulijadili kuwa, kuna uwezekano kwamba, watafsiri wawili wakitafsiri matini asilia moja wanaweza kuibuka na matini pokezi mbili ambazo ni tofauti kabisa. Katika MMS na MS, matumizi ya chuku yalitumika yanavyoangaziwa katika mfano 9 ufuatao.

### **Mfano 9**

**MMS:** Mkuu wa wilaya: Kuna nini ambacho hawakizungumzii! Kama ungekwenda ukawasikiliza, masikio yako yangevimba. (uk 44).

**MS:** Meya: ..Sema wee, sema wee-Wanawake watasema mpaka masikio yako yang'oke! (uk 61).

Mbinu ya chuku imetumiwa katika tamthilia za MMS na MS (mfano 9), Mkuu wa Wilaya (Meya) alipomlalamikia Yosif/Osipu kuhusu tabia ya wanawake ya kuzungumza sana. Kwa mfano, katika MMS, Mkuu wa Wilaya anamwambia Yosif kuwa: iwapo angesikiza maneno ya wanawake basi masikio yake yangevimba ilhali katika MS, Meya anamwambia Osipu kuwa, akiwasilikiza wanawake watasema hadi masikio yang'oke.

Ingawa watafsiri hao (Mwakasaka na Madumulla), wanadhihirisha matumizi ya chuku, maelezo yao yanatofautiana kwa kuwa katika MMS Mkuu wa wilaya anasema: masikio yatavimba na katika MS, Meya anasema kuwa: masikio yatang'oka. Vishazi vilivyopigiwa mistari havifanani kimaana. Kwa mujibu wa tasnifu hii, kung'oka ni kitenzi kinachomaanisha masikio kuondoka kwa mwili kabisa ilhali kitenzi kuvimba inamaanisha hali ya masikio kufura. Hivyo, tulihoji kuwa, afadhali masikio yakivimba kuliko yaking'oka kabisa. Matumizi ya chuku pia yameangaziwa katika mfano 10 ufuatao.

### Mfano 10

**MMS:** Ghlestakov: Hali ya hewa ni nini kwangu ukilinganisha na hiyo midomo yako ya johari? (uk 59).

**MS:** Hilestakov: Na hiyo midomo yako, bibie, ni ya namna yake; na inavutia kuliko hali yote ya hewa! (uk 86).

Matumizi ya chuku yanajitokeza katika MMS na MS inavyobainika katika mfano 10, Ghlestakovu/Hilestakov anapomsifu Marya/Maria alipokuwa akimtongoza. Kwa mfano, katika MMA (mfano 10), Ghlestakov anauliza swali la balagha: Hali ya hewa ni nini kwangu ukilinganisha na hiyo midomo yako ya johari? Swali hili la balagha linadhihirisha kwamba, kulingana na Ghlestakov, hali ya hewa si chochote, si lolote ikilinganishwa na midomo ya Marya inayovutia kama johari.

Kwa upande mwingine, swali hilo la balagha halipo katika MS (mfano 10), badala yake, Hilestakov alipokuwa akimtongoza Marya, anasema kwamba, midomo ya Marya inavutia kuliko hali ya hewa. Hilestakov anamwambia Marya: Na hiyo midomo yako, bibie, ni ya namna yake; na inavutia kuliko hali yote ya hewa. Hivyo, katika tasnifu hii tulihoji kuwa watafsiri wa MMS na MS (mfano 10) walitofautiana katika kuhawilisha ujumbe huo kwa kuwa, hakuna kanuni yoyote ya kuwashurutisha kutumia tafsiri ya neno kwa neno. Ufuatao ni mfano 11 unaoangazia matumizi ya chuku katika MS.

### Mfano 11

**MS:** Meya: ...Kukunjakunja uso mbele ya watoto darasani huenda ni sawa kwa sababu huenda ni mbinu ya ufundishaji. Lakini je, itakuwa vipi akifanya hivyo kwa mkaguzi? --- (uk 6)

Mfano 11 umedhibitisha kuwa, mtafsiri wa MS, alitumia mbinu ya chuku huku mtafsiri wa MMS hakutumia mbinu hii. Mtafsiri aliyezalisha tamthilia ya MS (mfano 11), anatumia chuku kuhusiana na matumizi ya 'kukunja uso' kama njia ya



kufundisha shuleni kwa vile, kwa kawaida kutabasamu ni mojawapo ya lugha ishara zinazotumika kufundisha lakini sio kukunja uso. Tulihoji kuwa, huenda mtafsiri wa MMS aliona kwamba, matumizi ya mbinu ya chuku katika muktadha huu wa (mfano 11) haufai ama mtafsiri wa MS (mfano 11) aliongeza sehemu hii katika ubunifu wake. Hali hii inaashiria kuwa, ukiushi wa kimtindo unaweza kutokea mtafsiri anapopuuza ama anapoongeza sehemu ya usemi anapohawilisha ujumbe kutoka matini chanzi hadi matini pokezi. Yaani, Inavyojitokeza ni kuwa, utiliaji chumvi uliofanywa katika MS haukufanywa katika MMS. Katika sehemu ya 3.2 ifuatayo, tumeshughulikia mbinu ya uzungumzi nafsia inavyojitokeza katika tamthilia za MMS na MS.

### 3.2 Uzungumzi Nafsia

Kwa mujibu wa utafiti huu, uzungumzi nafsia ni usemi unaotiririka akilini mwa mtu, yaani wakati mtu anapowaza na kuzungumza akiwa pekee. Mifano ifuatayo inaangazia miktadha inayodhihirisha matumizi ya uzungumzi nafsia katika tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*. Tulianza na mfano 12 ufuatao.

#### Mfano 12

**MMS:** Yosif (akijisemeza): Oooou! Nina njaa mno na tumbo langu linanguruma kama ngoma..Nina njaa kiasi cha kuimeza dunia! (uk 15-16).

**MS:** Osipu (akijisemeza): Mungu wangu, ubao umenishika! Jinsi tumbo langu lilivyo tupu na linavyonguruma kwa njaa, utadhani ndani yake kuna kikosi kizima cha wapiga tarumbeta! (uk 22-24).

Mfano 12 umebainisha matumizi ya mbinu ya uzungumzi nafsia katika MMS na MS Yosif/Osipu alipozungumza akiwa peke yake (akidai kuwa ana njaa) hotelini. Kwa mfano, katika MMS (mfano 12), Yosif anasema kwamba, ana njaa sana, hivi kwamba tumbo lake lina nguruma kama ngoma. Yosif ametumia tashbihi kunguruma kama ngoma kinyume na ilivyo katika MS (mfano 12) ambapo hakuna matumizi ya tashbihi. Pia, katika MS (mfano 12), Osipu anasema kuwa: njaa imepelekea tumbo

lake kunguruma hivi kwamba mtu atadhani kuwa ndani yake kuna kikosi kizima cha wapiga tarumbeta.

Tungo zilizopigiwa mistari hazifanani kimaana kwa kuwa kunguruma kama ngoma sio sinonimi ya kikosi kizima cha wapiga tarumbeta. Katika tasnifu hii tulihoji kuwa, tungo hizo zilizopigiwa mistari zinatofautiana kimaana kwa kuwa, watafsiri wangependa kuibuka na kazi yenye mvuto wa kisanaa. Hivyo, kila mtafsiri ana namna yake ya kuteua na kuhawilisha msamiati. Mfano 13 ufuatao pia unaangazia matumizi ya uzungumzi nafsia katika MMS na MS.

### **Mfano 13**

**MMS:** Ghlestakov: Litakuwa janga iwapo hatanipa chochote cha kula... Nasikitika kuwa Joakimu hakutaka nikodishe gari lake... Ningewatembelea wakulima wengi, nikiendesha gari mpaka milangoni kwao; wenyewe wako nyumbani?" (Uk 18-19).

**MS:** Hilestakov: Sijui nitafanyeje iwapo ataendelea kukataa? Sijawahi kubanwa na njaa namna hii katika maisha yangu yote! ...kwani ingekuwa ni fahari iliyoje kuingia kijijini kwangu nikiwa ndani ya gari...Je, familia za kichochole mpo?" (Uk 27-28).

Katika mfano 13, matumizi ya uzungumzi nafsia yanajitokeza katika MMS na MS, Ghlestakov/Hilestakov anapolalamika akiwa pekee kwamba anahisi njaa sana na anajuta kuwa hakuweza kupata gari la kukodi alipotoka kwao. Kwa mfano, katika MMS, (mfano 13), Ghlestakov anaeleza kwamba: litakuwa janga iwapo hatapewa chakula chochote kwa kuwa alihisi njaa sana pia alisikitika kwa kuwa hakuweza kukodisha gari la Joakimu na anasema kuwa iwapo angekodisha gari hilo angewatembelea wakulima wengi, akiendesha gari mpaka milangoni kwao huku akiwauliza ‘wenyewe wako nyumbani?’

Katika MS, Hilestakov anajiuliza atakachofanya ili aithibiti njaa iwapo tajiri atamnyima chakula siku hiyo na pia anajuta kuwa, hakuweza kukodi gari la kusafiri

nalo. Anasema kuwa: kwani ingekuwa ni fahari iliyoje kuingia kijijini kwangu nikiwa ndani ya gari, Je, familia za kichochole mpo?”

Katika tasnifu hii tulihoji kuwa, kishazi; Je, familia za kichochole mpo? kinadokeza hali ya madharau kwani kwa kawaida hata kama mtu ni mchochole sio vizuri kumwambia waziwazi kwamba yeye ni mchochole. Kwa upande mwengine, katika MMS, (mfano 13), utungo; ‘wenyewe wako nyumbani?’ unaashiria utu na heshima. Hivyo, kutokana na utungo kutoka katika MS, (mfano 13): Je, familia za kichochole mpo? na utungo kutoka MS, (mfano 13) ‘wenyewe wako nyumbani?’ inabainika kwamba, uhuru wa mtafsiri katika mchakato wa tafsiri, unaweza kubadilisha ujumbe wa matini chanzi kimaana na kimantiki. Ufuatao ni mfano 14 unaoangazia pia, muktadha wa uzungumzi nafsia unavyojitokeza katika tamthilia za MMS na MS.

#### **Mfano 14**

**MMS:** M/Wilaya... (kwake mwenyewe, akitishia kujipinga ngumi) We nyama! We juha! We hayawani! We pua nene! ...(uk 76).

**MS:** Meya...(anajitishia mwenyewe kwa ngumi) Nilimchukua yule kidudu-mtu, kitita cha takataka, kuwa ni mtu mashuhuri! (uk 114).

Mfano 14 unabainisha matumizi ya uzungumzi nafsia ulivyojitokeza katika MMS na MS, Mkuu wa Wilaya (Meya) alipodhihirisha hasira yake dhidi ya Ghlestakov/Hilestakov na kusema kwamba angelimpata huyo Ghlestakov/Hilestakov angemtusi na hata kumpiga mangumi. Kutokana na mfano 14, watafsiri wa MMS na MS walifaulu kuhawilisha tabia ya mhusika Mkuu wa Wilaya (Meya) kama mtu wa kuwatusi watu wakati ana hasira ingawa wanatofautiana kwa namna walivyohawilisha ujumbe wao.

Katika MMS, Mkuu wa wilaya (akizungumza pekee) anamtusi Ghlestakov kwamba: ‘We nyama! We juha! We hayawani! We pua nene!’ Kwa upande mwengine, katika

MS Meya (akizungumza pekee) anamtusi Hilestakov kuwa yeye ni: kidudu-mtu, kitita cha takataka! Kimaana, utungo: We nyama! We juha! We hayawani! We pua nene! sio sinonimi ya kidudu-mtu, kitita cha takataka. Hivyo, katika tasnifu hii tulidahili kwamba, uhuru wa mtafsiri wa kufasiri na kutafsiri kazi ya fasihi kwa misingi ya mitazamo mbalimbali, hupelekea kuwepo na tofauti katika uhawilishaji wa ujumbe. Mfano 15 pia unaangazia mbinu ya uzungumzi nafsia katika MMS na MS.

### **Mfano 15**

**MMS:** M/Wilaya (akijiwazia) Ni shughuli mbaya sana. ...Watu mashuhuri budi wawe kitu kinachovutia macho, lakini huyu ngedere anaweza kuwa chochote! (uk 42).

**MS:** Meya (kimya kidogo): Ah, hii ni dunia ya vichekesho. Unategemea kumwona mtu wa maana na hadhi yake, kumbe ni kijitu, takataka tu! (uk 59).

Mfano 15 unathibitisha matumizi ya uzungumzi nafsia yanavyojitokeza katika MMS na MS, Mkuu wa Wilaya (Meya) anapowaza kuwa Ghlestakovu/Hilestakov haonekani kama mtu au mgeni aliyetarajiwa. Matarajio ya watu katika wilaya hiyo yalikuwa kumpokea mgeni anayedhihirisha sifa za heshima kutokana na mavazi, mazungumzo na mwenendo wake ndipo aweze kuheshimiwa. Lakini Mkuu wa Wilaya (Meya) anaelezea kuwa Glestakov/Hilestakov hakujibainisha katika kiwango cha hadhi walichotarajia wapokezi wake, hivyo, wenyeji wake hawakumpenda wala kumheshimu Glestakov/Hilestakov.

Katika MMS (mfano 15), Mkuu wa Wilaya anaeleza kuwa, watu mashuhuri inabidi wawe kitu kinachovutia macho, lakini huyu ngedere anaweza kuwa chochote bali katika MS (mfano 15), Meya anasema kuwa, Unategemea kumwona mtu wa maana na hadhi yake, kumbe ni kijitu, takataka tu. Kutokana na tofauti katika tungo zilizopigiwa mstari, tulihoji kuwa, uhuru wa kutafsiri unaweza kusababisha matini

pokezi iwe na ujumbe ambao ni tofauti na alivyokusudia mwandishi wa matini asilia. Sehemu ifuatayo ya 3.3 inashughulikia misemo kama mojawapo ya mbinu za lugha zilizotumiwa na watafsiri wa MMS na MS.

### 3.3 Misemo

Kwa mujibu wa Ndalu na wenzake (2013), msemu ni fungu la maneno litumiwalo na jamii ya watu na huwa na maana iliyo fiche. Watafsiri wa tamthilia za MMS na MS walitumia misemo katika miktadha ya mifano ifuatayo na tulitanguliza na mfano 16 ufuatao.

#### Mfano 16

**MMS:** M/Wilaya...(kwa sauti)... Wazo jema sana hilo. Japo katika safari kuna heri na shari... (Uk 24).

**MS:** Meya....(kwa nguvu) Vema sana. Ninakutakia safari njema. Wanasema atangaye na jua hujua,. (Uk 36).

Katika mfano 16, matumizi ya misemo yanajitokeza katika tafsiri za MMS na MS, Mkuu wa Wilaya (Meya) anapomwambia Ghlestakovu/Hilestakov kuhusu usafiri. Kwa mfano, katika MMS, Mkuu wa Wilaya anatumia msemu kwa kumwambia Ghlestakov kuwa: Japo katika safari kuna heri na shari. Msemu huo uliopigiwa mstari hutumiwa kuwashauri wasafiri kwamba, mtu akiwa safarini huweza kufika salama ama kukumbwa na matatizo yatakayopelekea akose kufanikiwa katika safari yake.

Kwa upande mwingine, katika MS (mfano 16), Meya alimwambia Hilestakov kuwa, Ninakutakia safari njema. Wanasema atangaye na jua hujua. Msemu huo: atangaye na jua hujua, inamaana kuwa, mtu akijitolea kwa bidii kutekeleza jambo fulani, ndipo ataweza kuelewa barabara uzuri na ubaya wa jambo hilo kutokana na matatizo atakayokumbana nayo. Tungo zilizopigiwa mistari ni tofauti kimaana na kimatumizi lakini zilitumiwa na watafsiri wa MMS na MS katika muktadha ulionukuliwa kama

mfano 16. Mfano 17 ufuatao pia unabainisha matumizi ya misemo katika tamthilia za MMS na MS.

### **Mfano 17**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Siyo bahati tu! Yalikuwa malipo ya juhudi na kustahili. M/Elimu (pembeni):Mwamini nguruwe kunusa chakula kinono! (uk 70).

**MS: Meya :** Upuuzi, majaliwa hayana mikono. Upuuzi kabisa. Hiyo ni tuzo muafaka kwa sifa mustahiki. Hilo ndilo jambo lenyewe. Kamishina (pembeni)...Nguruwe mchafu zaidi ndiye huzipata njugu zilizojifukia chini ya udongo. (uk 105).

Katika MMS na MS (mfano 17), Mkuu wa Wilaya (Meya) alitumia misemo alipozungumza na Mkaguzi wa Elimu/Kamishina. Kwa mfano, katika MS, Mkuu wa Wilaya anaeleza kuwa; Upuuzi, majaliwa hayana mikono. Kulingana na uchanganuzi wa tasnifu hii, msemu huu: majaliwa hayana mikono ina maana kuwa, mtu yeyote anaweza kufanikiwa kutokana na mapenzi ya Mungu. Kwa upande mwingine, katika MMS (mfano 17), Meya anasema kuwa, Siyo bahati tu! Yalikuwa malipo ya juhudi na kustahili.

Watafsiri wa MMS na MS wanatofautiana katika uhawilishaji wa ujumbe. Kwa mfano, katika MMS (mfano 17), mtafsiri hajatumia msemu wowote katika muktadha huo. Aidha, katika MMS (mfano 17), Mkurugenzi wa Elimu anasema kuwa, mwamini nguruwe kunusa chakula kinono ilhali katika MS Kamishina anasema kuwa, nguruwe mchafu zaidi ndiye huzipata njugu zilizojifukia chini ya udongo. Kimaana, misemo iliyopigiwa mistari haifanani ilhali ilitumiwa na watafsiri wa MMS na MS katika mfano 17. Ufuatao ni mfano 18 ambao unabainisha mbinu ya matumizi ya barua katika MMS.

### 3.4 Kinaya

Kilonzo na Masaku (2017) wanadahili kwamba, kinaya ni mbinu inayotumiwa na mwandishi kuonyesha kinyume cha matarajio. Katika tamthilia za MMS na MS, kinaya kinajitokeza katika miktadha iliyonukuliwa kama mifano mbalimbali na tulianza kwa kuangazia mfano 18 ufuatao.

#### Mfano 18

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Na wewe Luka Lukichi...Najua hao ni watu waliosoma sana, wamepita katika vyuo mbalimbali, lakini tabia yao ni ya ajabu kabisa. Kuna mmoja ambaye kila wakati anakunja uso wake. (uk 4).

**MS:** Meya: Na wewe Luka Lukich-walimu wako! ...ninajuwa kuwa walimu ni werevu, wasomi na ...lakini naona wanachekesha sana. Kuna yule kwa mfano... yule mwenye pua kubwa-hawezi kusimama mbele ya darasa bila kukunja uso kiajabu ajabu. (Uk 6).

Mfano 18 umebainisha matumizi ya kinaya katika tamthilia za MMS na MS, mwalimu anapofundisha wanafunzi darasani huku amekunja uso wake. Kwa mfano, katika MMS, Mkuu wa Wilaya anasema kuwa: anajua walimu ni watu waliosoma sana na wamepita katika vyuo mbalimbali lakini tabia yao ni ya ajabu sana na kuna mmoja ambaye hukunja uso wake anapofundisha. Kwa upande mwingine, katika tamthilia ya MS, Meya anasema kuwa: anajua walimu ni watu werevu na tena wasomi lakini wanachekesha sana na kuna mwenye pua kubwa ambaye hawezi kusimama darasani bila kukunja uso kiajabuajabu.

Maneno yanayojitokeza katika tamthilia ya MS (mfano 18): mwalimu mwenye pua kubwa hayapo katika tamthilia ya MMS (mfano 18). Aidha, tungo zilizopigiwa mistari hazifanani kimaana, hivyo, tulihoji kuwa, uhuru wa mtafsiri huweza kupelekea kuibuka kwa tofauti katika uhawilishaji wa ujumbe baina ya matini chanzi na matini asilia. Mfano 19, unaangazia pia matumizi ya kinaya katika MMS na MS.

### Mfano 19

**MMS:** Ghlestakovu: Umeweka tu maji machafu katika bakuli. Hakuna ladha; inanuka uvundo. Sitakunywa supu hii... (akikinga supu isichukuliwe): Iache, iache hayawani! ..(anaendelea kunywa) (Uk 20).

**MS:** Hilestakov: Walichofanya ni kutia tu maji ya moto katika sufuria chafu!..Inanuka shombo la vyombo vichafu! Siwezi kula supu hii.. (Akikizuia chakula kwa mikono yake). Acha, acha mjinga we! (anainywa supu kidogo), (uk 31).

Mfano 19 unadhihirisha matumizi ya kinaya katika MMS na MS, Ghlestakovu/Hilestakov alipoinywa supu hotelini huku akidai kwamba supu hiyo hainyweki na kumkataza mhudumu wa hoteli asichukue hiyo supu. Tulihoji kuwa iwapo supu hiyo kwa kweli ilikuwa haifai, kwa nini basi Ghlestakovu/Hilestakov aliendelea kuinywa? Katika MMS (mfano 19), Ghlestakov alipoinywa supu anasema kuwa: ni maji machafu yaliyowekwa kwenye bakuli na inanuka uvundo. Bali katika MS (mfano 19), Hilestakov alipoinywa supu hiyo alilalamika na kusema kuwa: supu iliyoletwa sio supu ni maji ya moto ambayo yalimwagwa kwenye sufuria chafu na inanuka shombo la vyombo vichafu.

Maswali yanayoibuka ni je, maneno katika MMS, (mfano 19): maji machafu kwenye bakuli ni sinonimi ya ya maneno katika MS (mfano 19): maji ya moto kwenye sufuria chafu? Na je, kusema inanuka uvundo ni sawa kimaana na kusema: inanuka shombo la vyombo vichafu? Ufuatao ni mfano 20 unaoangazia pia matumizi ya kinaya katika MMS na MS.

### Mfano 20

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ..Ungeona jinsi mambo yanavyotekelezwa humu! Kila kitu kiko katika hali safi. (uk 26).

**MS:** Meya (pembeni): nitazame mimi kwa mfano ninaweza kukesha usiku kucha kwa kuitumikia nchi yangu kwa hali na mali. (uk 37).



Katika tamthilia za MMS na MS (mfano 20), matumizi ya kinaya yanajitokeza Mkuu wa Wilaya (Meya) alipomwambia Ghlestakov/Hilestakov kwamba katika wilaya yake, kila kitu kilikuwa shwari. Maelezo hayo ya Mkuu wa Wilaya (Meya) kwamba kila kitu katika wilaya yake kilikuwa shwari ni kinaya kwa kuwa kama wasomaji tulielewa kwamba shughuli za idara mbalimbali za serikali katika wilaya hiyo zilienda mrama kwa sababu viongozi hawakuwajibikia kazi zao.

Katika MMS (mfano 20), matumizi ya kinaya yanajitokeza, Mkuu wa Wilaya alipomwambia Ghlestakov kwamba, Ungeona jinsi mambo yanavyotekelezwa humu! Kila kitu kiko katika hali safi. Aidha, matumizi ya kinaya katika tamthilia ya MS (mfano 20), yanajitokeza, Meya alipomwambia Hilestakov kuwa, nitazame mimi kwa mfano ninaweza kukesha usiku kucha kwa kuitumikia nchi yangu kwa hali na mali.

Tulihoji pia kuwa ingawa watafsiri wa MMS na MS (mfano 20) walitumia kinaya lakini walibainisha tofauti za kisarufi katika uhawilishaji wa ujumbe. Kwa mfano katika MMS (mfano 20) Mkuu wa Wilaya anasema kuwa: Ungeona jinsi mambo yanavyotekelezwa humu bali katika MS, Meya anajisifu (umoja) kwa kusema kwamba, Mimi hukesha usiku kucha katika harakati ya kuitumikia nchi yake. Isitoshe, watafsiri wa tamthilia za MMS na MS pia walitumia mbinu rejeshi inavyojitokeza katika sehemu ya 3.5.

### **3.5 Mbinu Rejeshi**

Kulingana na TUKI (2013), mbinu rejeshi hutokea msanii anaporejelea mambo yaliyotukia hapo awali lakini wakati wa kutukia kwake hayakutajwa bali yanazungumziwa baadaye. Watafsiri wa MMS na MS, wametumia mbinu rejeshi kama inavyobainika katika miktadha iliyonukuliwa kama mifano mbalimbali na tulianza na mfano 21 ufuatao.

## Mfano 21

**MMS:** M/Elimu: ...Nilimzungumzia kuhusu jambo hili mara moja, ule wakati ambapo mwana wa mfalme alitutembelea. Huyu bwana alikunja uso sijapata kuona! Nilisutwa kwa kuwaacha vijana wafunzwe tabia ya kinyama na kishetani. (uk 4-5).

**MS:** M/Mashule: ..Nimemwonya mara kadha lakini hasikii. Siku moja Liwali alipoitembelea shule mwalimu huyo alikunja uso kiasi cha kutisha hata huyo mgeni rasmi akanishtaki kuwa tumemwajiri mwalimu mwenye fikra huria kufundisha watoto wetu. (uk 6).

Watafsiri wa *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali* walitumia mbinu rejeshi kama inavyobainika katika mfano 21, mwalimu alipowafundisha wanafunzi darasani huku akikunja uso wake. Kwa mfano, katika MMS (mfano 21), Mkuu wa Wilaya anasema kuwa: anajua walimu ni watu waliosoma sana na wamepita katika vyuo mbalimbali lakini tabia yao ni ya ajabu sana na kuna mmoja ambaye hukunja uso wake anapofundisha ilhali Meya katika MS, anasema kuwa: anajua walimu ni watu werevu na tena wasomi lakini wanachekesha sana na kuna mwenye pua kubwa ambaye hawezi kusimama darasani bila kukunja uso kiajabuajabu.

Ingawa katika tamthilia za MMS na MS, watafsiri walitumia mbinu rejeshi lakini uhawilishaji wa ujumbe ulitofautiana. Kwa mfano katika MMS, Mkuu wa Elimu anasema: Nilimzungumzia kuhusu jambo hili mara moja bali katika MS, Mkurugenzi wa Elimu anasema: Nimemwonya mara kadhaa lakini hasikii. Utungo kumzungumzia mara moja sio sinonimi ya kumwonya mara kadhaa. Aidha, katika MMS, mtafsiri alibuni utungo huu: mwalimu mwenye pua kubwa ambao haupo katika MS. Ufuatao ni mfano 22 ambao pia unaangazia matumizi ya mbinu rejeshi yalivyotumiwa katika tamthilia za MMS na MS.

**Mfano 22**

**MMS:** Yosif: Oooou! Nina njaa mno na tumbo langu linanguruma kama ngoma. Na haielekei kuwa tutafika nyumbani kama mambo ndiyo hivi. Ni miezi miwili tangu tuondoke Pitasbag. (uk 15-16).

**MS:** Osipu: Mungu wangu, ubao umenishika! Jinsi tumbo langu lilivyo tupu na linavyonguruma kwa njaa, utadhani ndani yake kuna kikosi kizima cha wapiga tarumbeta! ...Huu ni karibu mwezi wa pili tangu tulipoondoka Petersburg. (uk 22-23).

Mbinu rejeshi ilitumiwa na watafsiri wa MMS na MS katika mfano 22, Yosif/Osipu na akiwa hotelini anajizungumzia kwamba anahisi njaa sana. Kwa mfano, katika tamthilia ya MMS (mfano 22), Yosif anaeleza kwamba, Nina njaa sana, hivi kwamba tumbo langu linanguruma kama ngoma bali katika MS (mfano 22), Osipu anasema kuwa, njaa imepelekea tumbo lake kunguruma hivi kwamba mtu atadhani kuwa ndani ya hiyo tumbo kuna kikosi kizima cha wapiga tarumbeta. Tulihoji kuwa katika MMS (mfano 22), mtafsiri ametumia tashbihi kunguruma kama ngoma ilhali katika MS, matumizi hayo ya tashbihi hayapo.

Kimaana, tungo zilizopigiwa mistari (mfano 22) hazifanani, hivyo tulihoji kuwa, watafsiri hao (Mwakasaka na Madumulla) walifasiri na kutafsiri matini asilia kwa namna tofauti kwa kuwa kila mmoja wao aliteua msamiati kulingana na tajriba yake katika maisha. Mbinu rejeshi pia imejitokeza katika mfano 23 ufuatao

**Mfano 23**

**MMS:** Ghlestakovu:...Na mnajua niliingia idara kama tufani, kama tufani kabisa! Kila kitu kilitetemeka na kutikisika kama jani! (Uk 39).

**MS:** Hilestakov: ..Na mnajua? Nilipoizungukia idara, ungedhani kama kuna tetemeko la nchi kwa jinsi watu wote walivyotetemeka kwa hofu! (uk 55).

Mfano 23 unathibitisha matumizi ya mbinu rejeshi katika MMS na MS, Ghlestakovu/Hilestakov alipojidai kuwa kwa wakati mmoja alikuwa kiongozi wa idara fulani na watu walimwogopa sana. Kwa mfano, katika MMS (mfano 23),

Ghlestakovu anaeleza kuwa, aliingia idarani kama tufani na kusababisha kila kitu kutetemeka kama jani, ilhali katika MS (mfano 23), Hilestakov anasema kuwa: alipoizunguka idara mtu angedhani kuna tetemeko la ardhi kwa jinsi watu walivyotetemeka kwa hofu.

Tulidahili kuwa katika MMS (mfano 23), mtafsiri alitumia tashbihi, kama tufani na kama jani lakini mtafsiri wa MS katika mfano 23 hakutumia tashbihi. Isitoshe, katika MMS Ghlestakov anatumia maelezo ya kijumla kwa kusema kuwa, kila kitu kilitetemeka kinyume na ilivyo katika MS ambapo Hilestakov anasema kuwa, watu wote walitetemeka kwa hofu. Kila kitu kilitetemeka na watu wote walitetemeka kwa hofu ni maelezo tofauti kimaana na kimantiki. Hivyo katika utafiti huu, tulihoji kuwa watafsiri wawili au zaidi wakitafsiri matini asilia moja huweza kuibuka na makala pokezi mbili ambazo zina ujumbe tofauti. Mfano 24 ufuatao, pia ni muktadha ambao unaangazia matumizi ya mbinu rejeshi katika tamthilia za MMS na MS.

#### **Mfano 24**

**MMS:** Ghlestakov: Rafiki mpendwa Ryapitikini ...Unakumbuka tulipokuwa sote tumefilisika na mwoka mikate akanitupa nje kwa kujaribu kumkopa katika jina la Mfalme wa Uingereza? (uk 73).

**MS:** Hilestakov: “Mpendwa Tryapichkin, ...Kumbuka siku ambazo tulikuwa tumebanwa tuliishi kwa akili zetu na siku ambayo yule mwandalizi wa tamutamu alitutupa nje kwa sababu nilimwambia “atupatie zile sambusa kwa bili ya Mfalme wa Uingereza”! (uk 109).

Katika mfano 24, matumizi ya mbinu rejeshi yanajitokeza katika tamthilia za MMS na MS Ghlestakovu/Hilestakov alipomwandikia rafikiye barua akisimulia kisa kilichowakumba hapo awali. Kwa mfano, katika MMS, Ghlestakovu anamwambia Ryapitikini: akumbuke walipofilisika kisha mwoka mikate akawatupa nje kwa kuwa walijaribu kumkopa katika jina la Mfalme wa Uingereza bali katika MS, Hilestakov anamwambia Tryapichkin kuwa: akumbuke siku ambazo walikuwa wamebanwa na

yule mwandalizi wa tamutamu ambaye aliwatupa nje kwa vile walimwambia awape sambusa kwa bili ya Mfalme wa Uingereza.

Tulihoji kuwa, maneno aliyoyatumia mtafsiri wa MMS: mwoka mkate hayafanani kimaana na maneno aliyoyatumia mtafsiri wa MS: mwandalizi wa tamutamu (katika MS). Kwa mujibu wa tasnifu hii, mwoka mkate ni mtu ambaye hutengeneza mikate ilhali mwandalizi wa tamutamu huandaa peremende. Aidha, katika MMS (mfano wa 24) Ghlestakov anasema kuwa, mwoka mikate aliwatupa nje kwa kuwa walijaribu kumkopa katika jina la Mfalme wa Uingereza. Katika MS (mfano wa 24), Hilestakov anasema kuwa, mwandalizi wa tamutamu alitutupa nje kwa sababu nilimwambia atupatie zile sambusa kwa bili ya Mfalme wa Uingereza.

Kulingana na tasnifu, hii mkate na sambusa ni aina tofauti ya vyakula. Hivyo, katika tasnifu hii tulihoji kwamba, tofauti katika tungo hizo zilizopigiwa mistari imesababishwa na uhuru wa mtafsiri wa kuteua msamiati na kuwasilisha ujumbe wa msanii wa matini asilia kwa namna anayopenda. Mbinu rejeshi pia imetumika katika mfano 25 unaofuata.

### **Mfano 25**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Hapana, hapana ...Nimepata matatizo hapo awali, lakini nimepita katika yote, (uk 10).

**MS:** Meya: Potelea mbali na heshima. ...Tumewahi kuwa katika matatizo makubwa sana wakati mmoja hapo nyuma na wakati wote nilifaulu kuwatoeni salama. (uk 14).

Katika mfano 25, Mkuu wa Wilaya (Meya) katika tamthilia za MMS na MS anazungumzia matatizo aliyokumbana nayo hapo awali. Kwa mfano, katika MMS, Mkuu wa Wilaya anasema kuwa, alipata matatizo hapo awali lakini amepita katika yote ilhali katika MS, Meya anasema kwamba, wamewahi kuwa katika matatizo

makubwa sana wakati mmoja hapo nyuma na wakati huo wote walifaulu kuwatoa salama.

Sentensi zilizopigiwa mistari hazifanani kisarufi, kimaana na kiidadi, hivyo suala linaloibuka ni je, kwa nini tofauti hizo zikatokea? Katika tasnifu hii, tulihoji kwamba, watafsiri wa MMS na MS waliteua msamiati kwa namna tofauti kwa kuwa katika mchakato wa tafsiri, mtafsiri huathiriwa na masuala ya kiutamaduni, tajriba ya mtu binafsi na mazingira ya kulelewa. Uteuzi tofauti wa msamiati ulipelekea kuibuka kwa uwasilishaji tofauti ulivyobainika katika mfano 25. Tofauti hiyo inaweza kupelekea msomaji kujiuliza, je watafsiri hao walitafsiri matini chanzi moja? Ifuatayo ni matumizi ya kejeli yalivyotumika katika mifano mbalimbali katika tamthilia za MMS na MS.

### **3.6 Kejeli**

Kwa mujibu wa Murasi (2013), kejeli ni hali ya kusema na mtu kwa kukebehi au kumwambia mtu maneno ya kuudhi kwa masihara ama kwa mzaha. Aghalabu, kejeli pia hutumiwa kama hali ya kumtania mtu. Katika sehemu ifuatayo tuliangazia miktadha mbalimbali ambapo mbinu ya kejeli ilitumika katika MMS na MS. Mwanzo, tuliangazia mfano wa 26.

#### **Mfano 26**

**MMS:**Yosif: Ni jenerali, kwa kweli, ndani na nje na kutoka nyuma hadi Mbele, (uk 33).

**MS:** Osipu: O, ni Jenerali kwa namna nyingine, (Uk 47).

Katika mfano 26, Yosif/Osipu alitumia mbinu ya kejeli katika MMS na MS alipomjibu Mishka kuhusu hoja ya iwapo Ghlestakov/Hilestakov ni jenerali. Kutokana na mfano 26, watafsiri wa MMS na MS, waliibuka na namna tofauti ya uwasilishaji wa kejeli. Kwa mfano, katika MMS, Mishka anaposisitiza kuwa mgeni

anayekuja ni jenerali, Yosif alimjibu kuwa ni jenerali ndani na nje na kutoka nyuma hadi mbele. Katika MS, Mishka alipomwuliza Osipu iwapo mkubwa wake ni jenerali, Osipu alimjibu kuwa ni jenerali kwa namna nyingine.

Idadi ya maneno katika tungo zilizopigiwa mistari ni tofauti na pia tungo hizo hazifanani kimaana. Ndiposa katika tasnifu hii tulidahili kwamba tungo zilizopigiwa mistari ni tofauti kimaana na kiidadi kwa sababu katika mchakato wa tafsiri hakuna kanuni yoyote ya kumwongoza mtafsiri anapoteua msamiati. Yaani, kanuni ya kutambua kuwa tungo katika MMS: ni jenerali ndani na nje na kutoka nyuma hadi mbele ni bora zaidi kuliko tungo katika MS: ni jenerali kwa namna nyingine. Mbinu ya kejeli pia imetumika katika mfano 27 ufuatao.

### **Mfano 27**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ... Si muda mrefu nitamwoza binti yangu lakini si kwa kabaila mdogo yeyote. Tayarisheni sawasawa hongera, mnaskia? (uk 67).

**MS:** Meya (kwa wenye maduka): ...Lakini chungeni sana kuanzia sasa! Binti yangu haolewi na mshamba kumbukeni hilo-hakikisheni kuwa hongera zenu ni zile zinazostahili-mnaelewa? (uk 101).

Mfano 27 unadhihirisha matumizi ya kejeli katika MMS na MS Mkuu wa Wilaya (Meya) alipowajulisha wafanyabiashara kuhusu uchumba wa bintiye. Kwa mfano, katika MMS, Mkuu wa Wilaya anasema kuwa, si muda mrefu nitamwoza binti yangu lakini si kwa kabaila mdogo yeyote na hivyo watayarishe sawasawa hongera zao bali katika MS, Meya anawaeleza wafanyibiashara kuwa, binti yake haolewi na mshamba na wahakikishe kuwa hongera zao ni zile zinazostahili.

Ingawa maneno: Kabaila mdogo na mshamba yametumiwa kwa kejeli katika mfano wa 27, kimaana maneno hayo mawili ni tofauti mno. Ndiposa katika tasnifu hii tulihoji kwamba, kuna uwezekano wa mmoja wa hao watafsiri wawili: Mwakasaka

na Madumulla ambaye hakuwa mwaminifu kwa matini asilia. Tofauti hii ya uwasilishaji imetokana na uhuru alionao mtafsiri katika kazi yake ya kutafsiri ambao unasababisha watafsiri kuibuka na msamiati tofauti katika harakati za kutafsiri. Mfano ufuatao wa 28 pia unadhihirisha matumizi ya kejeli katika MMS na MS.

### **Mfano 28**

**MMS:** Bw Posta: Si hiki wala kile. Ibilisi tu ndiye ajua yeye ni nani! (Uk 72).

**MS:** Mkuu wa Posta: Si chochote, si lolote! Sijui tumwiteje? (Uk 108).

Katika mfano 28, kuna matumizi ya kejeli katika tamthilia za MMS na MS Bw Posta/Mkuu wa Posta alipowajua wenzake kwamba waliyemdhania kuwa mgeni (*Mkaguzi wa Serikali*) kumbe siye. Mwanzoni, Mkuu wa Wilaya (Meya) hakuamini aliyoambiwa ndipo ikamlazimu Bw. Posta/Mkuu wa posta kuisitiza kwa kejeli. Kwa mfano, katika MMS, Bw Posta anasema kwamba, huyo mgeni hakuwa hiki au kile bali ni ibilisi tu ndiye ajuaye alikua nani ilhali katika MS, Mkuu wa Posta anasema kuwa: mgeni huyo si chochote wala lolote bali hajui wamwiteje.

Tulidahili kuwa, mchakato wa tafsiri unaweza kupelekea kubadilishwa au kupotoshwa kwa ujumbe wa matini asilia. kwa mfano, katika tamthilia ya MMS (mfano 28), Bw Posta anamtaja ibilisi, hivyo inaelekea kwamba katika tajriba ya maisha ya mtafsiri (Mwakasaka), chochote kibaya kinahusishwa na ibilisi. Kwa upande mwingine, mtafsiri wa MS (Madumulla) hajataja neno ibilisi katika MS (mfano 28), badala yake anasema kwamba, hata hajui amwite vipi. Ufuatao ni mfano 29 ambao pia unaangazia matumizi ya kejeli katika MMS na MS.

### **Mfano 29**

**MMS:** Bw Huruma (pembeni): Jinsi anavyoogopa! Mtu duni huyu! hakika yeye ni ibilisi aliyepewa ulimi mtamu na Mungu. (uk 35).



**MS:** Kamishina (pembeni): Msikilize anavyojijenga! Kipawa hicho ama anacho! (uk 50).

Mfano 29 ulionukuliwa kutoka tamthilia za MMS na MS, umetokana na kisa ambacho Mkuu wa Wilaya (Meya) alijisifu kwake Ghlestakovu/Hilestakov lakini akakejeliwa na Bw. Huruma/Kamishena wa Msaada. Kwa mfano, katika MMS, Bw. Huruma anasema kuwa, Mkuu wa Wilaya ni Mtu duni huyu! hakika yeye ni ibilisi aliyepewa ulimi mtamu na Mungu ilhali katika MS Kamishena wa Msaada anasema hivi kumhusu Meya: hakika anajijenga na kipawa hicho ama anacho.

Tungo zilizopigiwa mstari zinadhihirisha tofauti katika uhawilishaji wa ujumbe baina ya tamthilia tafsiri za MMS na MS (mfano 29). Swali linaloibuka ni kuwa, kwa nini kuwepo na tofauti katika uteuzi wa maneno katika MMS na MS (mfano 29)? Tulihoji kuwa, katika MMS, Mwakasaka anatambua kuwepo kwa Mungu na ibilisi maishani ilhali Madumulla hajataja Mungu wala ibilisi. Mfano 30 ufuatao pia unabainisha matumizi ya kejeli katika MMS na MS.

### **Mfano 30**

**MMS:** Bw Huruma: ...Mchukue Mratibu wa Elimu hapa ...Sijui ni kwa nini wakubwa wamemwajiri mtu kama huyo! Ni mwovu zaidi kuliko mwasi. (uk 49).

**MS:** Kamishina: Na yule Mkaguzi wa Shule ... Jinsi alivyopewa kazi ile ni miujiza kabisa! Tazama hayuko tofauti na nyapara na ile shule yake ni chemchemi ya mapinduzi, (uk 71).

Mfano 30, unadhihirisha matumizi ya kejeli katika MMS na MS, Bw. Huruma/Kamishina wa Misaada alipomsaliti Mratibu wa Elimu/Mkaguzi wa shule. Kwa mfano, katika MMS (mfano 30), Bw. Huruma anauliza swali la balagha, Mchukue Mratibu wa Elimu hapa ...Sijui ni kwa nini wakubwa wamemwajiri mtu kama huyo! Ni mwovu zaidi kuliko mwasi. Katika MS (mfano 30), Kamishina wa

Misaada hajatumia swali la balagha lakini anashangaa jinsi Mkaguzi wa Shule alivyopewa kazi hiyo kwani hayuko tofauti na nyapara. Anasema: Na yule mkaguzi wa Shule ...Jinsi alivyopewa kazi ile ni miujiza kabisa! Tazama hayuko tofauti na nyapara na ile shule yake ni chemchemi ya mapinduzi.

Mojawapo ya mihimili mikuu katika Nadharia ya Uamilifu katika Tafsiri, mtazamo wa kuhakiki matini inadai kuwa, mbinu za lugha katika matini pokezi ziwe sawa au kukaribiana na zilivyo katika makala asilia. Hata hivyo, tunahoji kuwa kila mtafsiri huteua msamiati kulingana na tajriba yake katika maisha ndiposa kuna tofauti katika uhawilishaji wa mbinu ya kejeli ilivyotumiwa katika MMS na MS (mfano 30) haifanani. Taswira pia ni mbinu ya lugha iliyotumiwa na watafsiri wa tamthilia za MMS na MS na imeangaziwa katika sehemu ifuatayo ya 3.7.

### 3.7 Taswira

Kwa mujibu wa Mvati na wenzake (2017), taswira ni picha itokeayo katika mawazo ya mtu asomapo au atazamapo hali fulani. Mfano 31 ufuatao unaonyesha matumizi ya taswira yalivyojitokeza katika tamthilia za MMS na MS.

#### Mfano 31

**MMS:** Mkuu wa wilaya: ... Najua kuwa walimu ni watu waliosoma sana, wamepita katika vyuo mbalimbali, lakini tabia yao ni ya ajabu kabisa. Labda hiyo ndiyo hali ya kawaida ya watu waliosoma sijui. Kuna mmoja ambaye kila wakati anakunja uso wake. (Uk 4).

**MS:** Meya: .ninajuwa kuwa walimu ni werevu, wasomi na ...lakini naona wanachekesha sana. Kuna yule kwa mfano... yule mwenye pua kubwa-hawezi kusimama mbele ya darasa bila kukunja uso kiajabu ajabu. Hufanya hivi (anaigiza namna ya kukunja uso). (Uk 6).

Katika mfano 31, mbinu ya taswira ilitumiwa na watafsiri wa MMS na MS, Mkuu wa Wilaya (Meya) alipozungumzia kuhusu mwalimu wa somo la Historia anayekunja uso wakati anapofundisha darasani. Kwa mfano, katika MMS (mfano 31), Mkuu wa

Wilaya anasema kuwa, ingawa walimu ni watu waliosoma sana lakini tabia yao ni ya ajabu kabisa hususan ya kukunja uso kila wakati. kuna mmoja ambaye kila wakati anakunja uso wake. Aidha katika MS (mfano 31), Meya anasema: Ninajua walimu ni watu werevu na wasomi lakini wanachekesha sana hasa yule mwenye pua kubwa anayekunja uso darasani.

Kutokana na maelezo hayo yaliyopigiwa mistari, tulihoji kuwa, mtafsiri wa MMS (mfano 31), alitoa maelezo kwamba mwalimu mmoja hukunja uso akifundisha darasani. Hivyo kuwawezesha wasomaji kupata picha ya mwalimu huyo anayekunja uso anapofundisha. mtafsiri wa MS, (mfano 31), anatoa maelezo ya jinsi mwalimu alivyokunja uso na pia aliigiza sifa hiyo. Isitoshe, katika MS (mfano 31), Meya anaeleza kwamba mwalimu mwenye pua kubwa ndiye hukunja uso darasani bali katika MMS (mfano 31), Mkuu wa Wilaya anasema kuwa kuna mwalimu ambaye hukunja uso anapofundisha lakini hakusema iwapo ana pua kubwa. Sehemu ifuatayo ya 3.8 inaangazia namna watafsiri wa MMS na MS walivyotumia mbinu ya barua.

### **3.8 Matumizi ya Barua**

Kulingana na Ndalu na wenzake (2013), barua ni ujumbe wa maandishi unaopelekewa mtu kwa njia ya posta ama kwa mkono. Aghalabu, barua hutumiwa kuwasilisha habari ambayo ni ya kibinafsi au hata ya siri. Watafsiri wa tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali* walitumia barua kadhaa ili kufanikisha mawasiliano baina ya wahusika. Mifano ifuatayo ni miktadha ambayo ina matumizi ya barua yalivyojitokeza katika MMS na MS na tulianza kwa kuangazia mfano wa 32.

### Mfano 32

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ...Lakini nitawasomea barua ambayo nimeipata sasa hivi kutoka kwa Chimihovu. (Uk 1).

**MS:** Meya: ..Na leo hii asubuhi imefika barua hii kutoka kwa Chimikov. (uk 1).

Mfano 32 ulionukuliwa kutoka katika tamthilia za MMS na MS, unadhihirisha matumizi ya kuna barua, Mkuu wa Wilaya (Meya) alipopokea barua iliyomwarifu kwamba kulikuwa na mpango wa mkaguzi wa serikali kufika kisiri wilayani ili kuikagua idara mbalimbali za serikali. Kwa mfano katika katika MMS (mfano 32), Mkuu wa Wilaya anawaeleza viongozi wenzake kuwa, Lakini nitawasomea barua ambayo nimeipata sasa hivi kutoka kwa Chimihovu.

Katika MS (mfano 32), Meya anawaeleza viongozi wenzake kuwa, Na leo hii asubuhi imefika barua hii kutoka kwa Chimikov. Tulidahili kuwa katika MMS, Mkuu wa Wilaya anawaeleza viongozi wenzake kwamba yuko tayari kuwasomea viongozi barua aliyoipata kutoka kwa Chimihovu. Kwa upande mwengine, katika tamthilia ya MS (mfano 32), Meya hajawaambia viongozi iwapo alikuwa tayari kuwasomea barua badala yake anawajulisha tu kwamba kuna barua ambayo ilikuwa imefika asubuhi hiyo kutoka kwa Chimikov. Mfano 33 ufuatao pia unahusu matumizi ya barua katika tamthilia za MMS na MS.

### Mfano 33

**MMS:** Bw Posta: Hapana. Lakini kuna habari nyingi kuhusu walioko Kostroma na Saratovu. Ni jana tu Luteni mmoja alimwandikia rafiki yake kuhusu mpira katika lugha maridadi sana, fasaha kabisa. (Uk 6).

**MS:** Mkuu wa Posta: Hapana sijaona. Lakini kumekuwa na barua nyingi juu ya maafisa kutoka Saratov na Kostroma. Baadhi ya barua zao ni nzuri sana. ...Na kulikuwa na barua moja kutoka kwa Luteni kwenda

kwa rafiki yake ikieleza juu ya ukumbi wa muziki alikopata kwenda.  
(Uk 9).

Mfano 33, unadhihirisha kwamba matumizi ya barua katika MMS na MS, Bw Posta/Mkuu wa Posta alipoulizwa iwapo amepata habari zozote kutoka Pitasbag. Katika MMS (mfano 33), Bw. Posta anasema kuwa, kuna habari nyingi kuhusu walioko Kostroma na Saratovu na kwamba Luteni mmoja alimwandikia rafikiye kuhusu mpira katika lugha maridadi na fasaha kabisa lakini katika MS (mfano 33), Mkuu wa Posta anasema kuwa, kumekuwa na barua nyingi zinazohusu maafisa kutoka Saratov na Kostroma na pia barua moja kutoka kwa Luteni kwenda kwa rafikiye ikieleza kuhusu ukumbi wa muziki alikopata kwenda.

Tulihoji kuwa, katika tamthilia ya MS (mfano 33), mtafsiri ametoa maelezo kikamilifu na ya kueleweka kuliko maelezo yaliyotolewa na mtafsiri wa MMS (mfano 34). Kwa mfano, katika MMS (mfano 33) Bw. Posta anaeleza kwamba: Luteni mmoja alimwandikia rafikiye kuhusu mpira katika lugha maridadi na fasaha kabisa bali katika MS (mfano 34) Mkuu wa Posta anasema kwamba, kulikuwa na barua moja kutoka kwa Luteni kwenda kwa rafiki yake ikieleza juu ya ukumbi wa muziki alikopata kwenda.

Kutokana na tofauti za kimaana katika tungo zilizopigiwa mistari, maswali yanayoibuka ni je, kwa nini mtafsiri wa MMS anazungumzia suala la mpira ilhali mtafsiri wa MS anazungumzia ukumbi wa muziki? Nani kati ya watafsiri hao aliyekiuka, kudondosha au kubadilisha ujumbe wa matini asilia? Tulihoji kwamba, kwa vyovyote vile, watafsiri hao Mwakasaka na Madumulla hawawezi kukashifiwa kwa misingi ya kutokuwa waaminifu kwa matini asilia kwa kuwa, katika mchakato wa tafsiri, hakuna kanuni zinazomwongoza mtafsiri katika uteuzi wa msamiati.

Hivyo, mtafsiri huongozwa na tajriba yake katika maisha anapoteua msamiati. Katika MMS na MS, matumizi ya barua pia yamejitokeza katika mfano wa 34 ufuatao.

### **Mfano 34**

**MMS:** M/Wilaya (kichinichini kwa Dob): Sikiliza. Nitaandika vikaratasi viwili vya ujumbe ambavyo lazima vipelekwe haraka unavyoweza. Kimoja kwa Zemlyanika huko hospitalini, na kingine kwa mke wangu. (uk 27).

**MS:** Meya (pembeni kwa Dob): Sikiliza, kimbia kama upepo uende nyumbani kwangu kutoa habari juu ya ugeni. (Uk 39).

Mfano 34 unadhibitisha matumizi ya barua katika MMS na MS, Mkuu wa wilaya (Meya) alipomwandikia mke wake (Anna) na Zemlyanika barua kuhusu matayarisho ya kumpokea mgeni aliyetarajiwa (mkaguzi wa serikali). Kwa mfano, katika MS, (mfano 34) Meya aliandika barua moja kwa mkewe (Ann) kuhusu matayarisho ya kumpokea mgeni aliyetarajiwa (mkaguzi wa serikali). Kwa upande mwingine, katika MMS (mfano 34), Mkuu wa Wilaya ameandika barua mbili; moja kwa mkewe na nyingine kwa Zemlyanika.

Katika MMS mfano wa 34, Mkuu wa Wilaya anamwambia Dob kwamba, ataandika vikaratasi viwili vya ujumbe ambavyo lazima vipelekwe haraka iwezekanavyo, kimoja kwa Zemlyanika huko hospitalini, na kingine kwa mke wake (Mkuu wa Wilaya) lakini katika MS, Meya anamwambia Dob kuwa akimbie kama upepo aende nyumbani kwake kutoa habari kuhusu matayarisho ya kuja kwa mgeni. Tungo zilizopigiwa mistari zinadhihirisha tofauti katika uwasilishaji wa ujumbe katika MMS na MS.

Swali linaloibuka ni: kwa nini mtafsiri wa MMS anazungumzia barua moja ilhali mtafsiri wa MS anazungumzia barua mbili? Katika utafiti huu, tulidahili kwamba,

kuna uwezekano kuwa mmoja wa watafsiri hakuwa mwaminifu kwa kazi ya msanii wa matini asilia. Kwa vyovyote vile, uhuru wa mtafsiri hupelekea kuwepo na udondoshaji au kubadilishwa kwa ujumbe wa matini asilia. Ufuatao ni mfano 35 ambao pia unaangazia matumizi ya barua yalivyojitokeza katika MMS na MS.

### **Mfano 35**

**MMS:**Ghlestakovu (kwa Tyapitkini kupitia barua): Rafiki mpendwa Tyapitkini: Lazima nikuandikie kukueleza visa vyangu vipya, (uk 73).

**MS:** Hilestakov (Kwa Tryapichkin kupitia barua): “Mpendwa Tryapichkin, mambo yasiyo ya kawaida yamekuwa yakinitokea” (uk 109).

Mfano 35, unadhihirisha matumizi ya barua katika MMS na MS, Ghlestakovu/Hilestakov alipomwandikia barua rafikiye (Tyapitkini/Tryapichkin) akimjulisha kuhusu hali ilivyokuwa alipokuwa safarini. Kwa mfano, katika MMS (mfano 35), Ghlestakovu akimwandikia barua rafikiye Tyapitkini alianza kwa kusema; Rafiki mpendwa Tyapitkini lazima nikuandikie kukueleza visa vyangu vipya. Kwa upande mwingine, katika MS (mfano 35), Hilestakov alipomwandikia Tryapichkin barua alianza kwa kusema hivi: Mpendwa Tryapichkin, mambo yasiyo ya kawaida yamekuwa yakinitokea.

Kimaana kusema: visa vyangu vipya si sawa na kusema mambo yasiyo ya kawaida. Hivyo, tulihoji kwamba, tofauti hiyo ya uhawilishaji katika mfano 35, umesababishwa na uhuru wa kitafsiri kwa kuwa katika mchakato wa tafsiri, mtafsiri huteuwa msamiati anvyotaka. Watafsiri wa MMS na MS pia walitumia mbinu ya ukweli kinzani ilivyoangaziwa katika sehemu ifuatayo ya 3.9.

### **Mfano 36**

**MMS:** Bw. Posta (akiisoma barua).....! Kwanza kuna huyu Mkuu wa Wilaya: ni mtu mkarimu, wema wake ni kama shoka la mchinja ng’ombe, lakini ni mpumbavu kama punda kihongwe!” (uk 73).

Mfano 36 unathibitisha matumizi ya barua yanavyojitokeza katika tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*, Bw Posta alipowasomea viongozi wenzake barua iliyotoka kwa Glestakov. Katika barua hiyo, Ghlestakov anamtusi Mkuu wa Wilaya na viongozi wengine licha ya kuwa viongozi hao walimpokea kwa moyo mkunjufu. Kwa upande mwingine, katika tamthilia ya MS, hakuzungumzia tukio hilo lililoelezewa kama mfano 36. Hivyo, katika utafiti huu, tulidahili kwamba, uhuru wa kutafsiri humwezesha mtafsiri ama kudondoa au kuongeza vifungu vingine katika makala pokezi tofauti na ilivyokuwa katika makala asilia.

### **Mfano 37**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ...Lakini nitawasomea barua ambayo nimeipata sasa hivi kutoka kwa Chimihovu. (Uk 1).

**MS:** Meya: ...Na leo hii asubuhi imefika barua hii kutoka kwa Chimikov. (Uk 1).

Mfano 37 unatuthibitishia matumizi ya barua katika MMS na MS. Katika MMS, Mkuu wa Wilaya anasema kuwa ataanza kwa kuwasomea barua ambayo ameipata sasa hivi kutoka kwa Chimihovu na katika MS, Meya anasema kuwa asubuhi hiyo ilifika barua kutoka kwa Chimikov. Maneno yaliyopigiwa mistari yanatofautiana kimaana kwa kuwa katika shughuli za tafsiri, kila mtafsiri ana namna yake ya kuteua msamiati. Tunahoji kwamba watafsiri huathiriwa na masuala ya kiutamaduni, kimazingira na tajriba ya mtu binafsi. Kwa hivyo watafsiri wanapotofautiana katika uhawilishaji wa ujumbe, huwa ni kwa sababu mtindo wa uteuzi wa msamiati humtegemea mtu binafsi. Sehemu inayofuata ya 3.10 imeangazia matumizi ya kinaya ilivyojitokeza katika tamthilia za MMS na MS.



### 3.9 Ukweli kinzani

Kwa mujibu wa Kilonzo na Masaku (2013), ukweli kinzani ni mtindo ambao mwandishi hubuni muktadha ambao una ukweli na vilevile ukweli huo una ukinzani, hivyo, mbinu ya ukweli kinzani huwa na maneno yanayopingana bali yametumiwa katika muktadha mmoja. Maneno yanayokinzana au kupingana huwa yanatolewa kwa pamoja ili kuisitiza ujumbe fulani. Katika tamthilia za MMS na MS, watafsiri walitumia mbinu hii ya ukweli kinzani inavyojitokeza katika mifano ifuatayo na tulianza kwa kuangazia mfano 38ufuata.

#### Mfano 38

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Ndiyo ndiyo. Sasa mchukuwe mwalimu wa historia. Ni mtu mwenye uwezo mkubwa sana anayejua somo lake barabara, lakini anafundisha kwa mori kiasi cha kuwa huwezi kumwelewa. (uk 5).

**MS:** Meya: Hiyo ni mbaya! Mbaya sana. Je, na yule mwalimu wa historia? Ni mwerevu sana, mwenye akili mno, ambaye nina hakika analimudu somo lake barabara. Lakini kwa nini hupandwa na jazba? (uk 6-7).

Mfano 38, unadhibitisha kwamba, watafsiri wa MMS (Mwakasaka) na MS (Madumulla) walifaulu kutumia mbinu ya ukweli kinzani. Kwa mfano, katika MMS, Mkuu wa Wilaya anasema kuwa, mwalimu huyo ni mtu mwenye uwezo mkubwa na anayejua somo lake barabara lakini anafundisha kwa mori kiasi kwamba mtu hawezi kumwelewa. Katika MS, Meya anasema kuwa, mwalimu huyo ni mwerevu aliye na akili mno na analimudu somo lake barabara lakini la kushangaza ni kuwa yeye hupandwa na jazba anapofundisha.

Tulihoji kuwa, uhawilishaji wa ujumbe katika MMS na MS (mfano 38) haufanani kwa kuwa, kila mtafsiri aliteua msamiati kulingana na namna alivyofasiri ujumbe wa mwandishi wa matini chanzi. Aidha, uhuru wa mtafsiri unapelekea kuwepo na tofauti katika shughuli za tafsiri hasa iwapo matini chanzi ni moja na watafsiri ni wawili au

zaidi ndiposa mtafsiri wakati mwingine anawez kuibuka na matini pokezi tofauti kabisa na matini kimaudhui na hasa katika matumizi ya lugha. asilia Mfano 39 ufuatao pia ni unaobainisha matumizi ya ukweli kinzani katika MMS na MS.

### **Mfano 39**

**MMS:** Mpishi: Sawa, vipo na tena havipo. (Uk 19).

**MS:** Mhudumu: Kiko, mzee, lakini vilevile hakiko. ( Uk 30).

Mfano 39 unadhihirisha matumizi ya mbinu ya ukweli kinzani katika MMS na MS wakati Ghlestakovu/Hilestakov alimwuliza mpishi/mhudumu iwapo chakula kilikuwa pale hotelini. Kwa mfano, katika MMS (mfano 39), mpishi alimjibu Ghlestakov kuwa, vyakula vipo na tena havipo bali katika MS (mfano 39), mhudumu wa hoteli alimwambia Hilestakov kuwa: kiko mzee, lakini vilevile hakiko. Msomaji yeyote wa mfano wa 40 atataka kujua kwa nini katika MMS, mtafsiri alitumia hali ya wingi (vyakula vipo na tena havipo) ilhali katika MS mtafsiri alitumia hali ya umoja (chakula kiko lakini vilevile hakiko). Tofauti hizi za kitafsiri zimeibuka kwa kuwa, watafsiri wana uhuru wa kuteua msamiati kwa mujibu wa mapenzi yao.

Katika tasnifu hii tulihoji kwamba, ukosefu wa kanuni za kuwaongoza watafsiri huchangia katika tofauti za kitafsiri hivi kwamba kila mtafsiri hufasiri matini chanzi ya fasihi kwa mitazamo tofautitofauti. Hali hii husababisha kuibuka kwa matini pokezi mbili ya matini chanzi moja zinazotofautiana kimaana. Pia matumizi ya ukweli kinzani yanabainika katika MMS na MS kupitia mfano 40 ufuatao.

### **Mfano 40**

**MMS:** Bw Posta: Sauti ililia katika sikio moja: “Usiifungue!” na nyingine ilisema: ifungue! Ifungue!” (uk 72).

**MS:** Mkuu wa Posta :..Ndani ya sikio moja kulikuwa na sauti iliyoninong’oneza usiiguze hiyo lakiri, utajitia matatizoni ukifanya hivyo,” lakini ndani ya sikio jingine sauti nyingine yenye nguvu zaidi

ilinong'ona, "Hebu basi, vunja hiyo lakiri na kuifungua barua!". (uk 108).

Mfano 40, unathibitisha matumizi ya ukweli kinzani katika MMS na MS, Bw. Posta/Mkuu wa Posta alipowaeleza viongozi wenzake ilivyokuwa vigumu kwake kufungua barua. Kwa mfano, katika MMS (mfano 40), Bw. Posta anasema kuwa, Nilishindwa kufanya uamuzi kwa kuwa ndani ya sikio lake alisikia sauti ikisema asiifungue na nyingine ikimwamuru aifungue. Kwa upande mwengine katika MS (mfano 40), Mkuu wa Posta anasema kwamba: katika sikio lake, sauti ilinong'ona ikisema kuwa asiiguze lakiri hiyo na kwamba akifanya hivyo atajikuta matatani. Kisha alisikia sauti katika sikio nyingine ilionong'ona na kumwambia kuwa aivunje hiyo lakiri na kuifungua hiyo barua.

Kutokana na mfano 40, tulihoji kuwa, mtafsiri wa MS (Madumulla) ni mkarimu wa maneno na sentensi kwa vile anatoa maelezo kwa kina bali mtafsiri wa MMS (Mwakasaka) anatoa maelezo kwa mukhtasari. Hivyo, tuliweza kuhitimisha kwamba, katika mfano 40, watafsiri wa MMS na MS huenda walitofautiana katika uhawilishaji wa ujumbe kwa sababu Madumulla aliandika miaka ishirini baada ya Mwakasaka. Miongo miwili ni muda mrefu mno, hivi kwamba hatuwezi kuepuka mabadiliko ya matumizi ya lugha. Hadithi ndani ya hadithi ni mbinu nyingine iliyotumika katika MMS na MS na inashughulikiwa katika sehemu ifuatayo ya 3.10

### **3.10 Hadithi Ndani ya Hadithi**

Hadithi ndani ya hadithi ni mbinu ambayo mwandishi anaweza kuingiza hadithi zingine kwenye kisa kando na hadithi kuu kwa kupitia baadhi ya wahusika (Wamitila, 2003). Mifano ifuatayo inabainisha matumizi ya mbinu ya hadithi ndani ya hadithi ilivyojitokeza katika MMS na MS. tunaanza na mfano ufuatao ulionukuliwa kama mfano 41:

**Mfano 41**

**MMS:** Hakimu: Ndiyo, si muda mrefu kutakuwa na matatizo. Ehee Antoni Antonovichi, nilikuwa njiani kuja kukuonyesha mbwa wangu jike, mgeni, dada kabisa wa yule unayemwelewa. Na umeskia juu ya kesi ya Cheptovichi na Valinski? (Uk 7).

**MS:** Jaji: .. Antoni Antonovich, nilitaka kukupatia zawadi ndogo tangu zamani kidogo, lakini nimekuwa nikisahau. Kijibwa kizuri, ambacho ni mbegu ya lile jibwa kubwa la kwangu. Na kuhusu uwindaje, mimi sasa ni mashuhuri. Je, unajua kwamba Cheptovich amemshtaki Varhovinski? (Uk 10).

katika MMS (mfano 41), Hakimu anamwambia Mkuu wa Wilaya kuwa, Nilikuwa njiani kuja kukuonyesha mbwa wangu jike, mgeni, dada kabisa wa yule unayemwelewa. Na umeskia juu ya kesi ya Cheptovichi na Valinski? Kwa upande mwingine, katika MS, Jaji anamwambia Meya kuwa, nilitaka kukupatia zawadi ndogo tangu zamani kidogo, lakini nimekuwa nikisahau. Kijibwa kizuri, ambacho ni mbegu ya lile jibwa kubwa la kwangu. Na kuhusu uwindaje, mimi sasa ni mashuhuri. Je, unajua kwamba Cheptovich amemshtaki Varhovinski?

Kimaana, tungo zilizopigiwa mistari hazifanani kwa kuwa, katika MMS (mfano 41), Hakimu alimwambia Mkuu wa Wilaya kwamba alikuwa ameenda kumwonyesha tu mbwa wake (Hakimu) bali katika MS, Jaji alimwambia Meya kuwa, alikuwa amempelekea zawadi ambayo ni kijibwa kizuri. Aidha, katika MS, Jaji anamweleza Meya kuhusu uwindaji na anasema; mimi sasa ni mashuhuri. Je, unajua kwamba Cheptovich amemshtaki Varhovinski?

Ingawa katika MMS (mfano 41), Hakimu alimwarifu Mkuu wa Wilaya kuhusu kesi ya Cheptovichi na Valinski lakini hakusema kwamba anawinda katika mashamba yao. Tulihoji kuwa kishazi hiki: Jaji kuwinda katika mashamba ya Cheptovichi na Valinski ni jazanda inayomaanisha kuwa, Jaji ana uhusiano wa kimapenzi na bibi za Cheptovich na Varhovinski kwa kuwa wawili hao wana kesi mahakamani.

## Mfano 42

**MMS** - Mkuu wa Wilaya: ...Jana nili...” Yafuatayo ni mambo ya kifamilia, “Binamu yangu Anna Kirilovna na mumewe wanaishi nasi. Mumewe amenenepa sana na kutwa anapiga zeze,” na kadhalika. (Uk 2).

**MS:** Meya: ...! Dada yangu Anna Krilovna na mumewe Ivan wanakaa pamoja nasi. Ivan Krilovich ameongezeka sana uzito, na haachi kupiga fidla...” Naam, yaliyobaki ni maswala ya kifamilia tu kama mnavyoona. Hapo ndipo mwisho. (Uk 3).

Mfano 42, unathibitisha kuwa, watafsiri wa MMS na MS walifaulu kutumia mbinu ya hadithi ndani ya hadithi, Mkuu wa Wilaya/ Meya alipomwarifu Mratibu wa Elimu kwamba ana wageni kwake. Katika MMS, Mkuu wa Wilaya anadai kuwa binamu wake na mumewe wanaishi nao ambapo mumewe amenenepa na kutwa hupiga zeze. Kwa upande mwingine, katika MS, mwandishi anasema kuwa dada yake na mumewe wanakaa pamoja nao na mumewe ameongezeka sana uzito na haachi kupiga fidla. Mbinu ya tashihisi pia ilihawilishwa na watafsiri wa MMS na MS inavyojitokeza katika sehemu ifuatayo.

### 3.11 Tashihisi

Kulingana na Kilonzo na Masaku (2017), mbinu ya tashihisi ni mtindo ambapo mwandishi wa fasihi hutumia vitu visivyokuwa na uhai na kuvipa sifa na tabia za vitu vilivyo na uhai, aghalabu vitu hivi hutenda vitendo kama anavyotenda mwanadamu. Mbinu hii ya tashihisi imeelezwa ilivyojitokeza katika MMS na MS katika mfano 43 ufuatao.

## Mfano 43

**MMS:** M/Wilaya: ...Lakini wewe... unapoanza kuzungumzia juu ya kuumbwa kwa ulimwengu, unazifanya nywele zangu zisimame. (Uk 4).

**MS:** Meya: Wewe je?...wewe unapoanza kuzungumza juu ya uumbaji wa dunia, unafanya nywele zangu zisisimke! (Uk 6)

Mfano 43, unadhihirisha matumizi ya mbinu ya tashihisi katika MMS na MS, Mkuu wa Wilaya (Meya) na Hakimu/Jaji wanapozungumza kuhusu uumbaji wa ulimwengu. Kwa mfano, katika MMS (mfano 43), mkuu wa wilaya anasema kuwa, hakimu akizungumzia uumbaji wa dunia hupelekea nywele zake zisimame bali katika MS (mfano 43) meya anasema kuwa, jaji anapozungumzia suala la uumbaji wa dunia hupelekea nywele zake zisisimke.

Swali linaloibuka ni je, tungo hizi zilizopigiwa mistari; unazifanya nywele zangu zisimame na unafanya nywele zangu zisisimke zinafanana kimaana? Hivyo, tulidahili kuwa, uhuru wa kutafsiri walio nao watafsiri katika mchakato wa tafsiri, husababisha tofauti wa maneno na uhawilishaji wa ujumbe baina ya matini pokezi mbili za matini chanzi moja. Katika sehemu ifuatayo, tulishughulikia mbinu ya matumizi ya ndoto yalivyojitokeza katika tamthilia za MMS na MS.

### 3.12 Matumizi ya Ndoto

Kwa mujibu wa (TUKI 2013), ndoto ni maono yatokeayo usingizini, pia huitwa njozi. Sehemu ifuatayo inabainisha matumizi ya mbinu ya ndoto kupitia mifano mbalimbali katika MMS na MS na tumeanza na mfano 44 ufuatao.

#### Mfano 44

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ...Usiku mzima uliopita nilikuwa nikiota juu ya panya wawili wakubwa sana. Hakika sijapata kuona madude makubwa kama yale, panya wakubwa sana weusi! Walifika, wakanusanusa na kuondoka wakatoweka. (uk 1).

**MS:** Meya: Jana usiku niliota ndoto juu ya mapanya-buku. Walikuwa ni mapanya-buku wawili weusi wakubwa mno ambao sijapata kuona maishani mwangu. ..Wakainua pua zao kubwa na kunusanusa kwa namna ya kutisha-kisha wakageuka, haooo, wakaenda zao. (uk 1).

Katika mfano 44, watafsiri wa MMS na MS walifaulu kuhawilisha mbinu ya matumizi ya ndoto katika tafsiri zao. Kwa mfano, katika MMS (mfano 44), Mkuu wa Wilaya

alielezea kuwa, Usiku mzima uliopita nilikuwa nikiota juu ya panya wawili wakubwa sana. Hakika sijapata kuona madude makubwa kama yale, panya wakubwa sana weusi! Walifika, wakanusanusa na kuondoka wakatoweka. Katika MS (mfano 44), Meya alieleza kuwa, Jana usiku niliota ndoto juu ya mapanya-buku. Walikuwa ni mapanya-buku wawili weusi wakubwa mno ambao sijapata kuwaona maishani mwangu. .Wakainua pua zao kubwa na kunesanusa kwa namna ya kutisha-kisha wakageuka, haooo, wakaenda zao. Walikuwa ni mapanya-buku wawili weusi wakubwa mno ambao sijapata kuwaona maishani mwangu.

Tungo zilizopigiwa mistari zinadhihirisha tofauti katika uwasilishaji wa ujumbe katika mfano 44. Kutokana na mfano 45, tulidahili kuwa, katika MS (mfano 44), mtafsiri alitoa maelezo kwa kina na kwa uwazi zaidi kumliko mtafsiri wa MMS. Tulihoji kwamba huenda tofauti hiyo ya uhawilishaji iliibuka kwa kuwa tamthilia ya MS ilitafsiriwa miaka ishirini baada ya tamthilia ya MMS kutafsiriwa. Kwa hivyo muda wa miongo miwili huweza kusababisha mabadiliko katika matumizi ya lugha. Mfano 45 ufuatao pia unabainisha matumizi ya ndoto katika MMS na MS.

#### **Mfano 45**

**MMS:** M/Wilaya: Wakati mmoja nililazimika kuwafurahisha watoto fulani na nikawajengea nyumba ya karata, lakini niliporudi kulala nilipatwa na jinamizi. (uk 35).

**MS:** Meya: Wakati mmoja nilitaka kuwafurahisha watoto kwa kuwajengea nyumba kwa kutumia karata. Unajua matokeo yake? Niliota juu ya karata usiku mzima. (uk 50).

Mfano 45 unaonyesha kuwa, kulikuwa na matumizi ya ndoto katika MMS na MS, Mkuu wa Wilaya (Meya) anaposema kuwa, kuna wakati aliota ndoto usiku kuchwa. Kwa mfano, katika MMS (mfano 45), Mkuu wa Wilaya anasema kuwa, Wakati mmoja nililazimika kuwafurahisha watoto fulani na nikawajengea nyumba ya karata, lakini

niliporudi kulala nilipatwa na jinamizi. Lakini, katika MS (mfano 45), Meya anasema kuwa, Wakati mmoja nilitaka kuwafurahisha watoto kwa kuwajengea nyumba kwa kutumia karata. Unajua matokeo yake? Niliota juu ya karata usiku mzima.

Usemi wa Meya katika MMS (mfano 45): nililazimika kuwafurahisha watoto ni tofauti kimaana na usemi wa Meya katika MS (mfano 45): nilitaka kuwafurahisha watoto (MS) havifanani kimaana. Tungo hizi pia: lakini niliporudi kulala nilipatwa na jinamizi, (MMS) Na Niliota juu ya karata usiku mzima, (MS) hazifanani kimaana kwa kuwa, neno jinamizi linavyotumika katika MMS lina maana ya ndoto mbaya huku maana ya ndoto mbaya haijielezwa katika MS. Ndoto inayorejelewa katika MS hatujui kama ni mbaya au nzuri. Hivyo, tulihoji kuwa, kuna uwezekano kwamba kazi zilizotafsiriwa zinaweza kuwa tofauti na matini chanzi kwa kuwa hakuna kanuni za kuwashurutisha watafsiri kutafsiri matini chanzi wakizingatia neno kwa neno. Katika sehemu ifuatayo ya 3.13 tumetoa hitimisho ya sura ya tatu.

### **3.13 Hitimisho**

Katika sura hii tumehakiki kiulinganishi mbinu za lugha zilizotumiwa katika tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*. Imebainika kuwa, kuna mbinu za lugha ambazo zimetumiwa katika MMS na MS kama vile; chuku, tashbihi, matumizi ya: sauti, ndoto na barua, kinaya na misemo. Ingawa watafsiri wa MMS na MS walifaulu kuhawilisha mbinu za lugha tulizozitaja, kulikuwa na tofauti katika namna ya uwasilishaji wa ujumbe.

Katika utafiti huu, tulihoji kuwa, tofauti katika uwasilishaji wa mbinu za lugha zilitokea kwa sababu ya kuwa kila mtafsiri ana namna yake ya ubunifu na uteuzi wa msamiati kulingana na tajriba yake katika maisha. Pia, watafsiri wana uhuru wa kufanya uteuzi wa msamiati wanavyopenda, hivyo kila mtafsiri hutumia msamiati kwa kutegemea



mapenzi yake. Pia, katika sura hii ya tatu, tuligundua kwamba kuna mbinu zingine za lugha ambazo zimetumiwa na mtafsiri mmoja na kupuuzwa na mwengine. Kwa mfano mbinu ya majazi ilitumiwa katika MMS na haikutumiwa katika MS.

Tamthilia ya MS (Madumulla, 1999) iliandikwa miaka ishirini baada ya MMS (Mwakasaka, 1979). Katika tasnifu hii tulidahili kuwa, kuna uwezekano wa kuwepo na tofauti katika matumizi ya mbinu za lugha katika kazi ya tafsiri. Hii ni kwa sababu, tofauti ya miaka ishirini ni muda mrefu sana na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na hata ya matumizi ya lugha huweza kuibuka. Ifuatayo ni sura ya nne ambapo uchanganuzi kiulinganishi wa uwasilishaji wa ujumbe katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (1979) na *Mkaguzi wa Serikali* (1999) umeshughulikiwa.

## SURA YA NNE

### UWASILISHAJI KIULINGANISHI WA UJUMBE KATIKA *MKAGUZI MKUU* *WA SERIKALI NA MKAGUZI WA SERIKALI*

#### 4.0 Utangulizi

Tamthilia ya *Mkaguzi wa Serikali* (MS) ilitafsiriwa na Madumulla, (1999) miaka ishirini baada ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (MMS) kutafsiriwa na Mwakasaka, (1979). Muda wa miaka ishirini ni mrefu mno hivi kwamba, kuna uwezekano wa kuwa na mabadiliko ya siasa, uchumi na hata katika matumizi ya lugha. Ndiposa katika sura hii, tumechanganua kiulinganishi uwasilishaji wa ujumbe mbalimbali katika MMS na MS kulingana na lengo la pili la utafiti huu. Tumechunguza iwapo Mwakasaka na Madumulla walitofautiana katika tafsiri zao walipohawilisha ujumbe mbalimbali kutoka matini chanzi hadi matini pokezi. Ujumbe tuliochunguza katika sehemu hii ni dhuluma, matumizi mabaya ya mamlaka, ufisadi, ujinga, uasherati, kutowajibika, usaliti, unafiki, madawa ya kulevya na nafasi ya wanawake katika jamii. Katika sehemu ifuatayo, tunashughulikia ujumbe wa dhuluma ulivyojitokeza katika MMS na MS.

#### 4.1 Dhuluma

Kulingana na Murasi (2017) dhuluma ni uonevu au hali ya kumnyima mtu haki yake. Ujumbe wa dhuluma unapatikana katika riwaya za MMS na MS kama ulivyoangaziwa katika mifano mbalimbali na tulianza na mfano 46 ufuatao.

#### Mfano 46

**MMS:** Mkuu wa wilaya: Eee Mungu! niepushe na mikono yao wakati huu na nitawasha mshumaa mkubwa kuliko yote uliyopata kuiona! Nitamlazimisha kila mshenzi mfanyabiashara kuchanga kilo hamsini za nta (uk 13).

**MS:** Meya: Ikiwa Mungu atatusaidia tukaondokana na balaa hili, nitamlazimisha kila mfanyabiashara atoe kilo kadhaa za nta ya kutengenezea shumaa hilo. (Uk 18).

Mfano wa 46 unabainisha kuwa, katika MMS na MS kipengele cha dhuluma kimejitokeza Mkuu wa Wilaya (Meya) alipoagiza kuhusu matayarisho kwa ajili ya mapokezi ya mgeni. Kwa mfano katika MMS, Mkuu wa Wilaya anatoa ombi kwa Mungu amwepushe na balaa kisha anamwahidi Mungu kwamba, atamwashia mshumaa kubwa kuliko zote. Mkuu wa Wilaya anadai kwamba atafanya hivi kwa kumlazimisha kila mshenzi mfanyabiashara kuchanga kilo hamsini za nta. Kwa upande mwingine, katika tafsiri ya MS, Meya anasema kuwa, iwapo Mungu atawasaidia waondokane na balaa hilo (kutembelewa na Mkaguzi Mkuu wa serikali) atawaamuru wafanyabiashara watoe kilo kadhaa za nta ili kutengenezea shumaa.

Vifungu vilivyopigiwa mistari vinadhihirisha tofauti za kimaana katika uhawilishaji wa ujumbe baina ya MMS na MS. Kwa mfano, katika MS (mfano 46), Meya hajataja kiasi cha nta ambacho atamtoza kila mfanyabiashara tofauti na ilivyo katika MMS (mfano 46) ambapo mkuu wa Wilaya anapanga kuwatoza wafanyabiashara kilo hamsini za nta. Katika MS (Mfano 46), Meya hajatumia neno mshenzi jinsi Mkuu wa Wilaya alivyotumia neno hilo katika MMS.

Katika utafiti huu, tulidahili kuwa, hoja ya kuwa Meya hakutumia neno mshenzi lakini neno hilo lilitumiwa na Mkuu wa Wilaya, haimaanishi kwamba watafsiri hao wawili hawakuelewa lugha iliyotumiwa katika matini chanzi. Tofauti katika uhawilishaji wa ujumbe unaashiria upekee wa kila mtafsiri wa kufasiri na kuteua msamiati katika mchakato wa tafsiri. Mfano 47 ufuatao pia unabainisha ujumbe wa dhuluma katika MMS na MS.

**Mfano 47**

**MMS:** Mkuu wa wilaya: Majuma mawili! ...! Na muda wote huo wafungwa hawajalishwa! (Uk 10).

**MS:** Meya:..! Wiki mbili nzima! ... Wafungwa walinyimwa chakula. (uk 14).

Katika mfano 47, ulionukuliwa kutoka katika tamthilia za MMS na MS, Mkuu wa Wilaya (Meya) kama kiongozi wa serikali anatumiwa kuendeleza ujumbe wa dhuluma au unyanyasaji dhidi ya wafungwa. Hata hivyo, tofauti inayotokea katika uteuzi wa msamiati katika muktadha huu wa mfano 47, inaathiri uwasilishaji wa ujumbe wenyewe. Kwa mfano, kifungu katika MMS, “majuma mawili na wafungwa hawajalishwa” hakibebi maana inayofanana na kifungu katika MS, “imechukua wiki mbili tangu wafungwa kunyimwa chakula”.

Ingawa ujumbe wa unyanyasaji unadokezwa katika sentensi zilizopigiwa mistari, neno ‘kunyima’ linaashiria ujumbe wa dhuluma kwa uwazi zaidi kwa maana linaonyesha ‘chakula kilikuwepo lakini wafungwa walikatazwa’. Kwa upande mwingine, neno “hawajalishwa” linaweza kuwa na maana ya kwamba labda kulikuwa na ukosefu wa vyakula ndiposa wafungwa wakakosa kulishwa hivi kwamba lawama ya dhuluma haitadhihirika sana.

Katika tamthilia za MS na MMS, muktadha ulionukuliwa kama (mfano 47), unaonyesha kuwa, uteuzi wa maneno unaweza kuathiri pakubwa uwasilishaji wa ujumbe. katika uchanganuzi wa tasnifu hii, tulihoji kuwa, katika mchakato wa tafsiri, watafsiri wana uhuru wa kuteua msamiati kulingana na namna walivyofasiri ujumbe wa matini chanzi kwa sababu hakuna kanuni ya kuwaongoza katika shughuli za tafsiri. Kwa mfano, katika mfano 47, watafsiri hawajashurutishwa kutumia ama kitenzi: kunyima au kikanushi: hawajalishwa. Tamthilia ya MMS ilitafsiriwa miaka

ishiri kabla ya tamthilia ya MS, kwa hivyo, huenda mabadiliko katika matumizi ya lugha iliibua tofauti inayobainika katika mfano 47. Unaofuata ni ujumbe wa matumizi mabaya ya mamlaka katika MMS na MS.

#### 4.2 Matumizi Mabaya ya Mamlaka

Watafsiri wa MMS na MS walifanikiwa kutafsiri kazi ya matini chanzi huku wakidumisha ujumbe wa matumizi mabaya ya mamlaka kupitia mifano kadhaa na tulianza kwa kuangazia mfano 48 ufuatao.

#### Mfano 48

**MMS:** Mkuu wa wilaya: ... Amosi Fyodorovich, mtumishi wako anafuga bata katika vyumba vya ndani pamoja na kuku, na wanazururazurura wakiokota miguuni pako.. lakini hawezi kufuga mahali pengine? Wanapafanya panuke mno. (uk 3).

**MS:** Meya: ...chumba chako cha mahakama kimejaa uchafu! Mwambie mlinzi wako awahamishe bata mzinga wake kutoka pale barazani. Wateja wanapokuwa pale bata-mzinga hao huwadonadona miguu yao kutwa nzima. (uk 4).

Katika mfano 48, ujumbe wa matumizi mabaya ya mamlaka unadhihirishwa katika MMS na MS Hakimu/Jaji alipomruhusu mtumishi wake kufuga ndege mahakamani. Hata hivyo, mfano 48 unabainisha kuwa tungo katika MMS na MS, hazifanani kimaana. Kwa mfano, katika MMS (mfano wa 48) kuna kifungu: mtumishi wako anafuga bata katika vyumba vya ndani pamoja na kuku ambacho ni tofauti kimaana na kimantiki na kifungu katika (MS) (mfano wa 48): chumba chako cha mahakama kimejaa uchafu! Mwambie mlinzi wako awahamishe bata mzinga wake kutoka pale barazani.

Msomaji yeyote wa tamthilia za MMS na MS atagundua ya kwamba vifungu vilivyopigiwa mistari havifanani kimaana na kimantiki kwa kuwa watafsiri wa MMS na MS waliteua misamiati tofauti katika kuhawilisha ujumbe kutoka matini chanzi

hadi matini pokezi. Mfano 48 pia, unonyesha kuwa sehemu ya sentensi katika tamthilia ya (MS) ni; 'bata mzinga wanadonadona miguu ya wateja kutwa nzima' ambayo haipo katika sentensi ya MMS (mfano 49). Hivyo, tulihoji kuwa Madumulla alinua kuhawilisha ujumbe wa matini chanzi huku akidumisha usanii au mvuto wa kazi ya sanaa. Pia, kutokana na tofauti za kimaana katika vifungu vilivyopigiwa mistari, tulidahili kwamba, katika mchakato wa tafsiri, uteuzi wa maneno yanayotumiwa na mtafsiri kuhawilisha ujumbe wa matini chanzi humtegemea mtafsiri mwenyewe.

Tulidahili pia kuwa, aghalabu mtafsiri hutaka kuendeleza mtindo wa kisanaa huku akiwasilisha ujumbe kutoka matini chanzi hadi matini pokezi kwa kutumia ama tafsiri ya neno kwa neno au tafsiri ya kimawasilisano. Aidha, mtafsiri huweza kuamua kuongeza sentensi zingine au maneno mengine ambayo hayakuwemo katika matini chanzi ili kuhakikisha kwamba ameshughulikia hadhira lengwa. Mfano 49 ufuatao pia unabainisha ujumbe wa matumizi mabaya ya mamlaka ulivyojitokeza katika tamthilia za MMS na MS.

#### **Mfano 49**

**MMS:** Mfanyabiashara 2: Hasa! Lakini ukidiriki kusema neno atakutumia kikosi kizima cha rungu. Ama la sivyo ataifunga biashara yako. (uk 55)

**MS:** Abdullin: Lakini hatuthubutu kulalamika, Mheshimiwa atakuletea kikosi kizima cha askari ukigundulika kuwa umefanya hivyo au hata kufunga biashara yako... (uk 81).

Mfano 49 unathibitisha kuwa, ujumbe wa matumizi mabaya ya mamlaka uliangaziwa katika MMS na MS, Mkuu wa Wilaya (Meya) alipowatisha wafanyabiashara. Kwa mfano, katika MMS ni Mfanyabiashara wa 2 anasema kuwa, 'Lakini ukidiriki kusema neno atakutumia kikosi kizima cha rungu, ama la sivyo ataifunga biashara yako', Katika MS ni Abdulin anasema kuwa: Lakini hatuthubutu kulalamika, Mheshimiwa

atakuletea kikosi kizima cha askari ukigundulika kuwa umefanya hivyo au hata kufunga biashara yako". Kutokana na tungo zilizopigiwa mistari katika mfano 49 tuligundua kuwa anayezungumza katika MMS (mfano 49) ni Mfanyibiashara wa 2 ilhali anayezungumza katika MS ni Abdulin. Aidha, kutokana na tungo hizo zilizopigiwa mistari katika (mfano 50), swali linaloibuka ni je, tungo hizi: Lakini ukidiriki kusema neno atakutumia kikosi kizima cha rungu ni sawa kimaana na kusema Mheshimiwa atakuletea kikosi kizima cha askari? .

Katika MMS na MS (Mfano 49), maneno yanayotofautiana kimaana na msomaji yeyote wa tamthilia za MMS na MS (mfano 49), atagundua kuwa rungu sio sinonimi ya askari. Maoni y Munday (2001) kwamba mawasiliano nimuhimu katika tafsiri wala sio tafsiri sisisi au ya neno kwa neno ndiposa Tumehoji kuwa, tofauti katika uhawilishaji wa ujumbe katika mfano 49 imetokana na uhuru walionao watafsiri wa kuweza kuteua msamiati na kuhawilisha ujumbe wa matini chanzi hadi matini pokezi. Hii ndiyo sababu katika mfano 49, maneno mawili: rungu na askari ambayo hayafanani kimaana yametumiwa kama kwamba ni sinonimi. Ujumbe wa matumizi mabaya ya mamlaka katika MMS na MS pia umeelezwa katika mfano 50 ufuatao.

### **Mfano 50**

**MMS:** Mkuu wa wilaya (kwa Abdulin): ...nilikusaidia beberu we! Na pia naweza kukupeleka jela. Unasemaje? (uk 67)

**MS:** Meya: Mnataka kulalamika, siyo? (akimwandama tena Abudlin) Nadhani ulisahau hilo? Ninaweza kunong'ona tu na ninyi nyote mkajikuta mko Siberia! Mnaonaje kuhusu hilo? (Uk 101).

Uhawilishaji wa ujumbe wa matumizi mabaya ya mamlaka katika MMS na MS umedhihirishwa katika mfano 50 Mkuu wa Wilaya (Meya) alipowakaripia wafanyabiashara kwa vitisho. Kwa mfano, katika MMS, Mkuu wa Wilaya anamwambia Abdullini: nilikusaidia beberu we! Na pia naweza kukupeleka jela.

Unasemaje? Lakini katika MS, Meya anasema: Mnataka kulalamika, siyo? (akimwandama tena Abudlin) ..Nadhani ulisahau hilo? Ninaweza kunong'ona tu na ninyi nyote mkajikuta mko Siberia! Mnaonaje kuhusu hilo?

Matokeo ya mchakato wa tafsiri yanayowasilishwa katika mfano 50 yanaonyesha kwamba, mbinu ya tafsiri huru ilidumishwa na Madumulla (katika MS) na Mwakasaka (katika MMS). Tafsiri huru ni hali ya mtafsiri kuteua msamiati kwa minajili ya kurithisha hadhira lengwa. Kwa mfano, tafsiri huru inabainika kupitia tungo zilizopigiwa mstari katika mfano 50, ambapo katika MMS, Abdulin peke yake anatishiwa bali katika MS, wafanyabiashara kwa jumla wanatishiwa. Isitoshe, maelezo kuhusu kupelekwa Siberia yapo katika MS lakini hayakujitokeza katika MMS.

Siberia na jela pia ni dhana mbili tofauti na haziwezi kuwakilisha maana moja. Siberia ni jina la nchi bali jela ni mahali wahalifu hufungiwa wanapotengwa ili wasitangamane na wanajamii wengine. Katika tasnifu hii tulihoji kuwa, mfano 50 unaonyesha kuwa, watafsiri wa MMS na MS walifasiri na kuwasilisha ujumbe unaotofautiana kimaana. Tulidahili pia kuwa, mbinu ya tafsiri huru haiwezi kudumisha sifa za matini chanzi, hivyo, ujumbe wa matini chanzi unaweza kupotoshwa katika matini pokezi. Aidha, ujumbe wa ufisadi umejitokeza katika MMS na MS na umeshughulikiwa katika sehemu ifuatayo.

### **4.3 Ufisadi**

Kwa mujibu wa Ndalau na wenzake (2013), ufisadi ni hali ya kutoa ama kupokea kitu kwa njia ambayo siyo ya haki, yaani tendo la kukosa uadilifu. Ufisadi ni mojawapo wa ujumbe katika tamthilia za MMS na MS ulioangaziwa katika mifano ifuatayo na tumeanza kwa kushughulikia mfano 51 ufuatao.



## Mfano 51

**MMS:** Mkuu wa wilaya: ... kile ambacho Chimihovu anakiita “chembe za udhaifu” Ni mapenzi ya Mungu..Hakimu:..Nakubali wazi kuwa napokea hongo, lakini aina gani ya hongo? Vimbwa vidogo na sio zaidi! (uk 4).

**MS:** Meya: ...Na hilo ambalo Chimikov analiita “upungufu wetu mdogo” Jaji: Mimi sijali kukiri wazi kuwa huwa ninapokea rushwa lakini ni kutoka kwa wale watu wenye uwezo tu; na hiyo huwezi kuita dhambi. (Uk 5).

Mfano 51, ulionukuliwa kutoka tamthilia za MMS na MS, unaashiria kwamba watafsiri, Mwakasaka na Madumulla walihawilisha ujumbe wa ufisadi. Kwa mfano, katika MMS, (Mfano 51), Hakimu anakubali waziwazi kuwa, yeye hupokea hongo kwa kiwango kidogo bali katika MS, (Mfano 51), Jaji mwenyewe anakiri kuwa, yeye hupokea rushwa kutoka kwa wale wanaojiweza tu. Tukichunguza sentensi zilizopigiwa mistari (mfano 51), kuna tungo zinazotofautiana kimaana navyo ni, kwa kiwango kidogo na kutoka kwa wale wanaojiweza tu.

Katika MMS (mfano 51), Mkuu wa Wilaya anakiri kuwa, yeye hupokea hongo lakini kidogo tu, hivyo, inamaanisha kwamba, anaweza kupokea hongo kutoka kwa yeyote (awe anajiweza au hajiwezi). Kwa upande mwingine, katika MS (mfano 51), Meya anaeleza kuwa yeye hupokea hongo lakini kutoka kwa watu wanaojiweza. Kutokana na tofauti hizo za kimaana, tulihoji kuwa, watafsiri wa MMS na MS walifasiri maana iliyobebwa katika matini chanzi, (mfano 51) kisha kila mmoja wao akaitafsiri akitumia maneno na sentensi alizoamua kwa kuwa kila mmoja aliathiriwa na hadhira lengwa.

Katika tasnifu hii tulidahili kuwa, tungo zilizionukuliwa kama mfano 51, zinabainisha kwamba watafsiri wa MMS na MS walitumia uhuru wao kama watafsiri kuzua ujumbe tofauti. Pia tulidahili kuwa, matumizi ya mbinu ya kimawasiliano iliweza

kuwasaidia Madumulla na Mwakasaka kupitisha ujumbe wa ufisadi kwa namna tofauti. Hii ni kwa vile, mbinu hiyo haiwalazimu kutafsiri matini chanzi kwa njia ya neno kwa neno hadi matini pokezi. Hata hivyo, Mwakasaka na Madumulla walifaulu kufasiri ujumbe wa ufisadi na kuiwasilisha katika tamthilia tafsiri za MMS na MS (Mfano 51). Sehemu ifuatayo ya mfano 52, pia inahusu ujumbe wa ufisadi ulivyowasilishwa katika tamthilia za MMS na MS.

### **Mfano 52**

**MMS:** Bw Huruma: Sijui unawaza nini Amosi Fyodorovichi, lakini naona afadhali tufanye chochote. Hakimu: una maana..? (akionyesha ishara ya kula, kama hongo). (uk 45)

**MS:** Kamishina: ... mpaka hapo umefanya vizuri sana, Amos Fyodorov lakini ninadhani kwamba inafaa tufanye kitu fulani zaidi...kitu fulani. Jaji: kitu gani?. Kamishina: unajua nina maana gani. Jaji: (akifikicha dole gumba na cha shahada) kitu kama...eh? Kamishina: Naam, ama siyo? (uk 63)

Watafsiri wa MMS na MS, walifaulu kuwasilisha ujumbe wa ufisadi kwa matumizi ya viziada lugha kama inavyojitokeza katika mfano 52. Yaani, imebainika kwamba, tafsiri iliyofanywa katika MMS na MS (mfano 52) imechangia kuendeleza ujumbe wa ufisadi licha ya kuwa kuna matumizi ya viziada lugha. Kwa mfano Katika MMS (mfano 52), kiziada lugha kilitafsiriwa kama “akionyesha ishara ya kula, kama hongo” lakini kiziada lugha hicho kilitafsiriwa katika MS kama “akifikicha dole gumba na cha shahada”. Swali muhimu linaloibuka ni je, kuna kiziada lugha kinachoweza kuwa kisawe cha kiziada lugha cha lugha nyingine? Yaani, kuna uwezekano wa kutafsiri kiziada lugha kutoka matini chanzi hadi matini pokezi?

Katika tasnifu hii tulihoji kuwa, viziada lugha hivyo vinavyojitokeza katika tafsiri za MMS na MS (Mfano 52): “akionyesha ishara ya kula, kama hongo” na “akifikicha dole gumba na cha shahada” vinadokeza changamoto zinazohusu uhawilishaji wa viziada lugha katika mchakato wa tafsiri. Kiini cha changamoto hii ni ukosefu wa

kanuni zinazowaongoza watafsiri katika shughuli za tafsiri. Hivyo, kwa kuwa kila mtafsiri ana namna yake ya kufasiri na kutafsiri viziada lugha. Sehemu ifuatayo ya 4.4 imeshughulikia ujumbe wa kutowajibika ulivyojitokeza katika tamthilia za MMS na MS.

#### **4.4 Kutowajibika**

Kwa mujibu wa Kamusi Elezi (2016), kuwajibika ni hali ya mtu kutenda jambo au kutimiza jukumu linalomhusu. Kwa upande mwingine, kutowajibika ni kinyume cha kuwajibika, hivyo ni kitendo cha mtu kufeli kutimiza jukumu lake. Mfano 53 ufuatao unaangazia ujumbe wa kutowajibika ulivyojitokeza katika tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (1979) na *Mkaguzi wa Serikali* (1999).

#### **Mfano 53**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ...(akimgeukia Bwana Huruma) Hasa wewe, Artemi Filipovich; ni dhahiri kuwa huyo mgeni atayakagua mashirika yako, na Tafuta mavazi na nguo za kutandika safi;...Na ingefaa wagonjwa wenyewe waonekane afadhali kidogo kuliko wakoka makaa. (uk 2)

**MS:** Meya .. Na hasa wewe Artemi Philipovich! (Kwa Kamishina). Huyu Mkaguzi kwa hakika ataitembelea sehemu yako, kwa hiyo ingefaa uhakikishe kuwa kila kitu ni safi. Wapatie wagonjwa wako mashuka safi na waogeshwe vizuri. Nilipowaona safari iliyopita walikuwa kama wamepakwa masizi! (Uk 4).

Katika mfano 53, ujumbe wa kutowajibika kwa viongozi wa serikali ulidhihirika katika MMS na MS, Mkuu wa Wilaya (Meya) alipowajulisha viongozi hao kuhusu mkaguzi wa serikali aliyetarajiwa kuzuru wilayani. Mkuu wa Wilaya (Meya) alishikwa na wasiwasi kwa sababu ya maajilio ya mkaguzi wa serikali ndiposa akaitisha mkutano wa viongozi wote wa idara mbalimbali za serikali, kisha aliwaamrisha viongozi hao washughulikie idara zao ili wajiweke katika nafasi nzuri ya kumpokea mgeni mtarajiwa.

Katika MMS (mfano 53), Mkuu wa Wilaya anasema, “ingefaa wagonjwa wenyewe waonekane afadhali kidogo kuliko wakoka makaa’ na katika tamthilia ya MS (mfano 54) Meya anasema kuwa: ‘Nilipowaona (wagonjwa) safari iliyopita walikuwa kama wamepakwa masizi’. Mtafsiri wa MMS (mfano 53) pia, alitumia hali ya masharti “nge” ‘Na ingefaa wagonjwa wenyewe’ ilhali mtafsiri wa MS, (mfano 53) alitumia kibainishi cha wakati uliopita ‘li’ ‘Nilipowaona safari iliyopita’? Shitemi (1990) na Omboga (1986), wanadai kwamba tafsiri haianywi katika ombwe tupu kwa kuwa mtafsiri huathiriwa na mila na utamaduni wa jamii yake. Ndiposa mfano 53 unabainisha tofauti ya uhawilishaji wa ujumbe. Kwa mfano tumehoji kuwa katika tungo hizo zilizopigiwa mistari, matumizi ya ‘nge’ yanaashiria kwamba mhusika alikuwa na uwezo wa kuwajibika lakini matumizi ya ‘li’ yanaondoa nafasi ya shaka linalohusu kule kukosa uwezo wa kutenda jambo. Mfano 54 ufuatao pia unadhihirisha ujumbe wa kutowajibika kwa viongozi katika tamthilia za MMS na MS.

#### **Mfano 54**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya (kwa Hakimu): na wewe unapaswa kufanya kitu kuhusu hali ya mahakama yako, Amosi Fyodorovich. Mtumishi wako anafuga bata katika vyumba vya ndani pamoja na kuku, na wanazururazurura wakiokota miguuni pako. Lakini hawezi kufugia mahali pengine? Wanapafanya panuke mno. (uk 3)

**MS:** Meya: Ehee, na wewe Amosi Fyodorovich, bora na wewe uanze kurekebisha mahakama yako. Mahakama yako ni kama shamba kabisa. Mwambie mlinzi wako awahamishe bata-mzinga wake kutoka pale barazani. Wateja wanapokuwa pale, bata-mzinga hao huwadonoadonoa miguu yao kutwa nzima, (uk 4).

Mfano 54 ulionukuliwa kutoka tamthilia za MMS na MS unadhihirisha kuwa, uchafu wilayani umetokana na kuzembea au kutowajibika kwa viongozi. Kwa mfano, uchafu unaosababishwa na ufugaji wa ndege mahakamani, unaashiria kudumishwa kwa ujumbe wa kutowajibika katika tafsiri za MMS na MS (mfano 54). Aidha, kifungu, ‘mahakama yako ni kama shamba kabisa’, kiko katika MS (mfano 54) bali hakipo katika MMS.

Mfano 54, unabainisha kwamba katika MMS, kuna matumizi ya utungo, Wanapafanya panuke mno ambao haupo katika MS. Aidha, mfano 54, unathibitisha kuwa watafsiri wa MMS na MS walitofautiana katika uhawilishaji wa ujumbe kwa kuwa kila mmoja ana namna yake ya kufasiri ujumbe wa matini chanzi. Katika tasnifu hii tulihoji kuwa, tofauti za kitafsiri katika uhawilishaji wa ujumbe baina ya matini pokezi mbili za matini chanzi moja ni sifa mojawapo inayoweza kujitokeza katika mchakato wa tafsiri unaohusu kazi za fasihi ambazo huenda isifae katika tafsiri ya sajili za sayansi au sheria. Shitemi (1990) na Omboga (1986), haiwezekani tafsiri kufanywa katika ombwe tupu Ufuatao ni mfano 55 ambao pia unashughulikia ujumbe wa kutowajibika katika MMS na MS.

#### **Mfano 55**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Halafu ofisi zako zimejaa kila aina ya takataka. Ngozi zilizotundikwa ili zikauke, mijeledi, na vifaa vingine vya kuwindia vikichanganyika na makaratasi...huyo karani wako! Anaweza kuwa mjuzi sana, lakini anatoa harufu kali mno ya vodka. (uk 3).

**MS:** Meya: (Akiupuuza mwaliko). Amosi Fyodorovich, chumba chako cha mahakama kimejaa uchafu! Zana zako za kuwindia zimezagaa ovyoovyo, hatamu na matandiko viko kwenye shubaka la stakabadhi muhimu,...Yaani ni mchafukoge mtupu. Na yule karani wako! Ni mwerevu sana yule, lakini kutwa kucha ananuka pombe! (uk 5)

Mfano 55 unasheheni ujumbe wa kutowajibika katika MMS na MS ingawa tungo zilizotumiwa na watafsiri zinatofautiana kimaana. Kwa mfano, utungo katika MMS (mfano 55) unataja ‘ofisi yako’ ilhali utungo katika MS (mfano 55) unataja ‘chumba chako cha mahakama’. Kimaana, maneno haya: ‘chumba chako’ hayawezi kuwa kisawe cha maneno: ‘afisi yako’. Mfano 55 pia, unathibitisha kuwa tamthilia ya MMS (mfano 55) inazungumzia Ngozi zilizotundikwa ili zikauke bali ngozi hizo hazijatajwa katika tamthilia ya MS (mfano 55). Isitoshe, katika MMS (mfano 55), Mkuu wa Wilaya anazungumzia mnuko wa pombe ya vodka lakini katika MS, Meya alieleza kunuka kwa pombe tu pasipo kutaja aina ya pombe yenyewe.

Katika tasnifu hii, tulidahili kwamba, katika uhawilishaji wa ujumbe wa kutowajibika, (mfano 55) mtafsiri wa MS ametumia zaidi tafsiri inayoegemea kwa hadhira lengwa kwa sababu ametumia maneno ya Kiswahili yanayoeleweka barabara. Kwa upande mwingine, katika MMS (mfano 55), matumizi ya msamiati kama vile ‘ofisi’ na ‘vodka’ yanaifanya kazi iliyotafsiriwa kuegemea zaidi kwenye utamaduni wa lugha chanzi (Kiingereza) kuliko ule wa lugha pokezi (Kiswahili). Mfano 56 ufuatao, pia unazungumzia hoja ya kutowajibika katika MMS na MS.

### **Mfano 56**

**MMS:** M/Wilaya: Majuma mawili! Mama yake Mungu! Na muda wote huo wafungwa hawajalishwa! Mke wa sajenti amechapwa! Mitaa haijafagiliwa! Mji wote ni kama zizi. Aibu! (Uk 10).

**MS:** Meya: Mungu, Yesu na Maria tulindeni! Wiki mbili nzima! Katika kipindi hicho mke wa sajenti alicharazwa bakora, wafungwa walinyimwa chakula, mitaa haikufagiliwa, mji mzima ulikuwa kama jaa la taka. Ooo, aibu gani hii! Ni kuvunjika gani kwa heshima! (Uk 14).

Diskosi zilizonukuliwa katika mfano 56 zinaendeleza ujumbe wa kutowajibika katika MS na MMS. Kwa mfano, katika MMS (mfano 56), Mkuu wa Wilaya anasema kuwa, Majuma mawili! Mama yake Mungu! Na muda wote huo wafungwa hawajalishwa! ...Mji wote ni kama zizi. Aibu. Kwa upande mwingine, katika MS (mfano 56) Meya anasema kuwa, Mungu, Yesu na Maria tulindeni! Wiki mbili nzima! Katika kipindi hicho... wafungwa walinyimwa chakula, .. mji mzima ulikuwa kama jaa la taka. Ooo, aibu gani hii! Ni kuvunjika gani kwa heshima.

Matini zilizonukuliwa zinatofautiana kutokana na namna watafsiri walivyohawilisha. Mathalani, maneno ‘mama yake Mungu’ yametumiwa katika MMS (mfano 56) lakini maneno ‘Mungu, Yesu na Maria’ yasiyotaja ‘mama wa Mungu’ yametumiwa katika MS (mfano 56). Miunganisho hiyo ya maneno iliyofanywa na watafsiri hawa wawili

katika MMS na MS inabeba fahiwa mbili zisizohusiana (mama yake Mungu na Mungu, Yesu na Maria) licha ya kutumiwa ili kuendeleza ujumbe wa matini chanzi.

Katika MMS (mfano 56), Mkuu wa Wilaya alipochukizwa na uchafu uliokithiri mji wao anasema neno moja: Aibu na kwa upande mwengine, Meya katika MS, anasema: aibu gani hii! Ni kuvunjika gani kwa heshima! Hivyo, mtafsiri wa MS alitumia maneno mengi kumliko Mwakasaka. Tofauti hizo za uwasilishaji (mfano 56) zinaashiria uhuru alionao mtafsiri wa kuweza kuteua msamiati anavyotaka ndiposa katika matini pokezi mbili za matini chanzi moja, usemi fulani unaweza kutokea katika kazi ya mtafsiri mmoja lakini usitokee katika kazi ya mtafsiri mwingine. Aidha, tofauti za kidini huenda ndio kichocheo. Kwa mfano Wakatoliki na Waprotestanti wana misimamo tofauti katika kuhusu nafasi ya Maria katika Biblia. Kwa mfano Wakatoliki wanamuenzi sana Maria. Ujumbe wa unafiki umeshughulikiwa katika sehemu ya 4.5 ifuatayo.

#### 4.5 Unafiki

Kulingana na Ndalu (2013), unafiki ni hali ya kutokuwa mkweli. Wahusika wengine katika tamthilia za MMS na MS walidhihirisha tabia ya unafiki inavyojitokeza katika mifano mbalimbali na tulianza kushughulikia mfano ufuatao wa 57.

#### Mfano 57

**MMS:** M/Wilaya: ...(Anaguna) sasa kama huyu Mkaguzi anamuuliza askari polisi yeyote, “Umeridhika?” lazima waseme, “Tumeridhika kabisa, Mheshimiwa.” Na kama yeyote hajaridhika kabisa nitawapa chochote cha kuridhisha. (Uk 13).

**MS:** Meya:...(Anapumua kwa nguvu)...kama Mkaguzi huyu akija kuwapeleleza watu wako kwa kuwauliza kama wanafurahia kazi yao, hawana budi kujibu haraka, “Ndiyo, Mheshimiwa, tuliifurahia mno.” Na kama kuna mtu atasema haifurahii kazi yake, basi mwambie huyo mtu kuwa nitamfanya asiifurahie kazi yake baadaye. (uk 18).

Mfano 57 unaashiria namna ujumbe wa unafiki ulivyohawilishwa katika tafsiri za MS na MMS. Kwa mfano, katika MMS, Mkuu wa Wilaya anasema: sasa kama huyu Mkaguzi anamuuliza askari polisi yeyote, “Umeridhika?” hawana budi kujibu haraka, “Tumeridhika kabisa, Mheshimiwa”. Na kama kuna mtu atasema haifurahii kazi yake basi, na kama yeyote hajaridhika kabisa nitawapa chochote cha kuridhisha. Kwa upande mwingine, katika tamthilia ya MS, Meya anasema, kama Mkaguzi huyu akija kuwapeleleza watu wako kwa kuwauliza kama wanafurahia kazi yao hawana budi kujibu haraka, “Ndiyo, Mheshimiwa, tuliifurahia mno.” Na kama kuna mtu atasema haifurahii kazi yake basi, basi mwambie huyo mtu kuwa nitamfanya asiifurahie kazi yake baadaye.

Tungo zilizopigiwa mistari katika (mfano 57) hazifanani kimaana na kiidadi. Kwa mfano neno ‘ridhika’ lililotumiwa katika MMS sio sinonimu ya neno ‘furahia’ lililotumiwa katika MS. Aidha, Mkuu wa Wilaya anasema kuwa, yule ambaye hajaridhika ataweza kuridhishwa baadaye bali katika MS Meya anaashiria kuwa, yule atakayesema kwamba hajafurahia kazi ya Meya atafanywa asiifurahie kazi yake baadaye. Ingawa maelezo hayo yanaendeleza ujumbe wa unafiki, lakini kuna tofauti katika uwasilishaji wa ujumbe. Kwa mfano, katika mfano 57, mtafsiri wa MMS anaambatanisha ujumbe wa unafiki na wema (ataweza kuridhishwa baadaye) huku mtafsiri wa MS akiuambatanisha ujumbe huo na kuhatarisha maisha (atafanywa asiifurahie kazi yake baadaye).

Katika utafiti huu tuliakisi kwamba, huenda hali hizo mbili (wema na uovu) zinazotofautiana zilisababishwa na uhuru wa watafsiri wa kuteua msamiati wanavyotaka katika mchakato wa tafsiri. Aidha, tulidahili kwamba, tofauti za hali hizo (wema na uovu) huweza kuwa ni kosa la mtafsiri mmoja la kutafsiri ujumbe



katika hali ya kukanusha badala ya hali yakinifu. Mfano 58 ufuatao pia unaangazia ujumbe wa unafiki ulivyowasilishwa katika tamthilia za MMS na MS.

### **Mfano 58**

**MS:** Meya: Sijawahi kushika karata tangu kuzaliwa na hata kama ningeishika singejua nifanye nini nayo! .. wakati mmoja nilitaka kuwafurahisha watoto kwa kuwajengea nyumba kwa kutumia karata. Niliota juu ya karata usiku mzima (uk 50)

Mkaguzi: (pembeni): huyu Bwana! Jana tu jioni amenichomoa laki mbili katika mchezo wa karata, (uk 50).

Mfano 58 ni dondoo iliyonukuliwa kutoka katika tamthilia ya MS na linabainisha tabia ya Meya ya kuwa mnafiki. Kwa mfano, katika MS (mfano 58), Meya alikejeliwa pembeni na Mkaguzi wa Elimu alipodai kwamba hajawahi kucheza karata. Mkaguzi (pembeni) anaeleza kuwa, huyu Bwana! Jana tu jioni amenichomoa laki mbili katika mchezo wa karata. Katika tasnifu hii tulihoji kuwa katika mfano 58, usemi uliotolewa kimyakimya (pembeni) na Mkaguzi unaonyesha unafiki wa Meya. Mathalani, Mkaguzi alieleza wazi kuhusu namna ambavyo Meya hupoteza wakati kwa kucheza karata ilhali Meya hujidai kwamba kila wakati akipata muda huwa anawazia kuhusu namna ya kutumikia nchi yake.

Dondoo hilo (mfano 58) halipo katika tamthilia ya MMS, hivyo, katika tasnifu hii tulihoji kuwa ukosefu wa sehemu hii (mfano 58) katika MMS, unaonyesha jinsi mtafsiri anaweza kutumia mbinu ya kimawasiliano kudondoa ama kuongeza sehemu ya matini chanzi. Tulidahili pia kuwa maana ya ujumbe uliotarajiwa katika kipashio kilichodondolewa hatimaye huweza kupotea kwa kutegemea iwapo mtafsiri amepunguza aya nzima, sehemu au sentensi nzima. Aidha, ujumbe wa unafiki unajitokeza katika mfano 59 ufuatao.

**Mfano 59**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Sawa sawa, hili ni kasha. Jamani! (akivaa kofia yake) sasa kumbuka, mtu yeyote akiuliza ni kwa nini kanisa la hospitali ambalo tulipata fungu lake miaka mitano iliyopita halijajengwa, jibu ni kuwa lilianzishwa lakini likaungua moto. (Uk 13).

**MS:** Meya: *(Akilivurumisha chini kasha)* Na jua, mjinga wee! Sikiliza. Nimepata wazo jingine. Kama Mkaguzi huyu atauliza juu ya kanisa kwa ajili ya hospitali – unajua ile ambayo tulipatiwa fedha tuijenge miaka mitano iliyopita- usisahau iliteketezwa na moto. (uk18).

Mfano 59 unathibitisha kuwa watafsiri wa MMS na MS walifaulu kuhawilisha ujumbe wa unafiki Mkuu wa Wilaya (Meya) anapojifanya kuwa mcha Mungu ilhali hajalijenga kanisa ambalo alipokea pesa za kulijenga miaka mitano iliyopita. Kwa mfano, katika MMS, Mkuu wa Wilaya anaeleza kuwa: mtu yeyote akiuliza ni kwa nini kanisa la hospitali ambalo tulipata fungu lake miaka mitano iliyopita halijajengwa, jibu ni kuwa lilianzishwa lakini likaungua moto. Katika MS, Meya anasema: Kama Mkaguzi huyu atauliza juu ya kanisa kwa ajili ya hospitali...usisahau iliteketezwa na moto.

Kutokana na mfano 59, tulihoji kuwa, katika MMS, usemi wa Mkuu wa Wilaya umetafsiriwa kijumla bila kumrejelea mtu yeyote mahususi. Kwa mfano, Mkuu wa Wilaya anasema kuwa, ‘mtu yeyote akiuliza kwa nini kanisa halijajengwa’ bali katika MS, usemi huo huo umetafsiriwa kwa kumhusisha mhusika maalum ambaye ni Mkaguzi wa Serikali aliyetarajiwa kuzuru eneo hilo. Kwa mfano, Meya anasema kuwa, Kama Mkaguzi huyu atauliza juu ya kanisa kwa ajili ya hospitali.

Tulihoji pia kuwa, urejelezi wa kijumla; ‘mtu yeyote’ (ilivyo katika MMS) unafaa katika kudhihirisha kwamba tabia ya unafiki ya Mkuu wa Wilaya haijulikani na yeyote. Kwa upande mwingine, matumizi ya urejelezi wa mhusika mahususi; Kama Mkaguzi huyu (ilivyo katika MS) unafaa kwa kuonyesha kwamba uovu (unafiki) huo

labda umekuwa bayana kwa wengine lakini ni muhimu kuuficha kwa Mkaguzi (mgeni mtarajiwa) pekee. Sehemu ifuatayo inaangazia ujumbe wa matumizi ya dawa za kulevya ulivyojitokeza katika MMS na MS.

#### **4.6 Matumizi ya Dawa za Kulevya**

Ujumbe wa matumizi ya dawa za kulevya katika matini pokezi za MMS na MS umejitokeza katika miktadha iliyonukuliwa kama mifano mbalimbali. Kwa mujibu wa tasnifu hii, dawa za kulevya ni tumbaku, sigara na pombe. Mfano 60 ufuatao umeangazia ujumbe wa matumizi ya dawa za kulevya katika MMS na MS.

#### **Mfano 60**

**MMS:** Ghlestakov: Karibu. Kaa chini. Karibu sigara. (uk 47).

**MS:** Hilestakov: Haya haya chukua! Si sigara mbaya huwezi kuilinganisha hata hivyo na zile za Petersburg. (uk 69).

Mfano 60, umebainisha ujumbe wa matumizi ya dawa za kulevya katika tamthilia za MS na MMS. Kwa mfano, katika MMS (mfano 60), Ghlestakov alimkaribisha M/Elimu kwa kumwambia: Karibu. Kaa chini. Karibu sigara bali katika MS, Hilestakov alimkaribisha Mkaguzi wa Mashule kwa kumwambia: Haya haya chukua! Si sigara mbaya huwezi kuilinganisha hata hivyo na zile za Petersburg. Katika tasnifu hii tulidahili kuwa, matamko katika MMS (mfano 59): ‘Karibu’ na ‘karibu sigara’ na katika MS (mfano 60): ‘Haya haya chukua! Si sigara mbaya’ yametokana na athari za lugha chanzi.

Tungo zilizopigiwa mistari katika MMS na MS (mfano 60) zinadhahirisha kuwa, watafsiri wa MMS na MS, waliathiriwa na utamaduni wa Kimagharibi. Tulihoji kuwa, katika utamaduni wa Kimagharibi, mtu anaweza kumwalika mwenzake kwa dawa za kulevya kama vile sigara kwa kusema ‘welcome’ na akajibiwa ‘Thank you’ au ‘No thank you’.

Tulidahili pia kuwa, watafsiri wa MMS na MS katika (mfano 59) wameathiriwa na utamaduni wa Kimagharibi kwa kuwa utamaduni wa kumwalika mtu kwa dawa za kulevya umepenya hadi matini zilizotafsiriwa za Kiswahili (*Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*). Mfano 61 ufuatao, pia unaangazia ujumbe wa matumizi ya dawa za kulevya katika MMS na MS.

### **Mfano 61**

**MMS:** Bob: ...Pita Ivanovichi alikuwa amepata habari zote kutoka kwa mtumishi wako Avdotya ambaye alikuwa ametumwa kwa Pochechuevu ..Dob: Kuchukuwa mtungi wa kuweka mvinyo wa kifaransa. (uk 8).

**MS:** Bob: ...Kumbe Peter Ivanovichi alikuwa amekwishaeleza kila kitu na mtumishi wako wa nyumbani (Kwa Meya), Avdotya ambaye alikuwa ametumwa kwa Philip Antonovichi Pochechuev ...Dob: Kuchukuwa kasiki la vodka. (uk. 11)

Mfano 61 ulionukuliwa kutoka katika MS na MMS unabainisha kwamba, watafsiri wa MMS na MS walifaulu kudumisha ujumbe wa matumizi ya pombe. Kwa mfano, katika MMS Dob anasema, kuchukuwa mtungi wa kuweka mvinyo wa kifaransa bali katika MS Dob anasema, Kuchukuwa kasiki la vodka. Tumegundua kuwa katika kifungu cha mfano 61, katika MMS mtafsiri aliteua kutumia ‘mvinyo wa Kifaransa.’ Kwa upande mwingine, katika MS, mtafsiri alitumia kifungu ‘kasiki ya vodka’ ambacho ni mseto wa utamaduni wa Kiswahili (kasiki) na wa kigeni (vodka) ili kuhawilisha ujumbe wa matumizi pombe.

Katika tasnifu hii tulidahili kuwa, watafsiri wa MMS na MS walikuwa na uhuru wa kurejelea mvinyo unaopatikana katika utamaduni wa Kiswahili au hata wa Kiafrika kama vile mnazi, chang’aa ama busaa. Aidha, watafsiri hao walikuwa na uhuru wa kupuuzia kifungu katika matini chanzi kilichohusiana na matumizi ya pombe lakini waliamua kudumisha ujumbe wa matumizi ya pombe kwa kuwa waliathiriwa na

mitindo ya maisha ya kimagharibi. Mfano 62 ufuatao, unashughulikia ujumbe wa matumizi ya dawa za kulevya ulivyojitokeza katika MMS na MS.

### **Mfano 62**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ..Yuko wapi askari mwingine? Nilimwambia Prohorovu kuwa hapa. Yuko wapi? Askari: Wamemleta asubuhi hii amelewa taabani. Amenyunyuziwa bakuli mbili za maji baridi lakini hata hivyo mpaka sasa hajapata fahamu. (uk 11)

**MS:** Meya: ..Hivi polisi wote wamekwenda wapi? Prohorov yuko wapi? Aliambiwa awepo hapa. Sivistunov: Yuko stesheni afande na hawezi kutumwa. Meya: Hawezi? Una maana gani kuwa hawezi? Sivistunov: Aliletwa akiwa amelewa chakari leo asubuhi Afande. (uk 15).

Mfano 62 ulinukuliwa kutoka katika tamthilia za MMS na MS, unahusu kisa ambacho Prohorovu/Prohorov alikunywa pombe kupita kiasi mpaka akashindwa kujimudu. Mfano huo wa 62, unabainisha namna ambavyo unywaji wa pombe kupita kiasi unaweza kutatiza utendaji kazi wa maafisa wa serikali. Licha ya kwamba watafsiri wa MMS na MS (mfano 62) walifaulu kuhawilisha ujumbe wa matumizi ya dawa za kulevya, matini hizi zimetofautiana pakubwa kwa misingi ya kimaana. Kwa mfano, Katika MMS (mfano 62) kifungu: ‘Yuko wapi askari mwingine?’ si kisawe cha kifungu katika MS: ‘polisi wote wamekwenda wapi?’ na kwa hivyo haziwezi kuwakilisha ujumbe au maana ile ile aliyokusudia mwandishi wa matini chanzi.

Katika MMS (mfano 62), kishazi: ‘amelewa taabani’ ni tofauti na kishazi: ‘amelewa chakari’ ilivyo katika MS. Tulihoji kuwa, mtafsiri wa MMS aliamua kuvuruga sarufi kwa kuwa mtu anaweza tu ‘kuingia taabani’ lakini si ‘kulewa taabani’. Isitoshe, sentensi “Amenyunyuziwa bakuli mbili za maji baridi lakini hata hivyo mpaka sasa hajapata fahamu” ipo katika MMS lakini sinonimu yake haipo katika MS katika (mfano 62).

Katika tasnifu hii tulihoji kuwa, tofauti katika uwasilishaji wa ujumbe katika MMS na MS, imesababishwa na uhuru wa mtafsiri katika mchakato wa tafsiri wa kuweza kuteua msamiati anavyotaka kutegemea jinsi amefasiri ujumbe wa matini chanzi. Yaani, mtafsiri ana uhuru wa kupunguza, kuongeza au kubadilidha msamiati wa matini chanzi na kuhawilisha ujumbe katika matini pokezi. Ujumbe wa hofu unaelezewa katika sehemu ifuatayo ya 4.7.

#### **4.7 Hofu**

Kwa mujibu wa TUKI (2013), hofu ni hali ya kutokuwa na ushujaa au ni jambo linaloleta uoga au tishio. Ujumbe unaohusu hofu ulihawilishwa na watafsiri wa MMS na MS kupitia matendo na usemi wa wahusika zilizounukuliwa kama mifano mbalimbali na tulianza na mfano 63 ufuatao.

#### **Mfano 63**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ...Na kuhusu mke wa Sajeni, habari kuwa niliamuru achapwe ni uongo mtupu. Uzushi! Ni kubuni kwa maadui zangu. Watu kama hao! Kila siku napita nikiwa na hofu ya kuuawa. (uk 22-23).

Mfano 63 ni diskosi iliyozalishwa na Mkuu wa Wilaya katika matini tafsiri ya MMS alipoeleza kwamba, Watu kama hao! Kila siku napita nikiwa na hofu ya kuuawa. Tulidahili kuwa, katika MMS (mfano 63) unabainisha ujumbe muhimu kwamba, Mkuu wa Wilaya ana hofu kwa kuwa maisha yake yamo hatarini. Diskosi hiyo ya (mfano 63) ya ujumbe unaohusu hofu haipo katika tamthilia ya MS.

Tulihoji kuwa, ukosefu wa mfano 63 katika MS bali upo katika MMS, unabainisha kuwa katika mchakato wa tafsiri, watafsiri wanaweza kupuuza ujumbe uliopo katika matini chanzi kwa sababu hakuna kanuni zinazo washurutisha kushirikisha kila neno, sentensi au usemi uliopo katika matini chanzi katika matini pokezi. Bistin na Bandia (2006) wanadahili kwamba watafsiri huweza kupuuza suala la kuwa mwaminifu kwa

matini asilia. Hivyo, tulidahili kuwa, uhuru wa mtafsiri ulimwezesha mtafsiri wa MMS kuwa na ujumbe katika kifungu hicho (mfano 63) na uhuru huo huo ukamwezesha mtafsiri wa MS kutokuwa na kifungu (mfano 63) ambacho kilikuwa na ujumbe kuhusu hofu. Mfano 64 ufuatao, pia umeangazia ujumbe wa hofu ulivyojitokeza katika MMS na MS.

#### **Mfano 64**

**MMS:** Bw Posta: ..Sijawahi kuwa na hofu hivyo maishani ...Na nilipokuwa naibandua gundi, moyo ulipita katika mishipa yangu nikajisikia mwili mzima ukiwa moto. (Uk 72).

**MS:** Mkuu wa Posta: Mimi mwenyewe sijui.. Mara nilipoiguza ile nta, damu yangu ilichemka kama vile imo ndani ya moto. Nafungua barua, si kutetemeka huko kama vile mwili wote ulikuwa ndani ya barafu. Nilikaribia kuzimia! (uk 108).

Katika mfano 64, watafsiri wa MMS na MS walifaulu kuwasilisha ujumbe wa hofu na uoga. Kwa mfano, katika MMS (mfano 64), Bw. Posta anasema, Sijawahi kuwa na hofu hivyo maishani...Na nilipokuwa naibandua gundi, moyo ulipita katika mishipa yangu nikajisikia mwili mzima ukiwa moto bali katika MS (mfano 64), Mkuu wa Posta anasema, Nafungua barua, si kutetemeka huko kama vile mwili wote ulikuwa ndani ya barafu. Nilikaribia kuzimia.

Katika tasnifu hii tumegundua kuwa ujumbe ulionukuliwa kama mfano 63, una upekee kuhusiana na uhawilishaji wa ujumbe wa woga kwa sababu watafsiri wa tamthilia za MMS na MS (mfano 64) walitumia vinyume au antonimu ambazo ni baridi na joto ilhali walifanikiwa kuwasilisha ujumbe unaohusu woga. Kwa mfano, katika MMS Bw. Posta anasema, hali ambapo ‘mwili mzima ulikuwa moto’ lakini katika MS Mkuu wa Posta anasema, ‘mwili mzima ulikuwa ndani ya barafu.’ Hata hivyo, ingawa vifungu hivi vinakinzana kimaana, vyote vinausimba ujumbe unaohusu

hofu katika MMS na MS. Katika sehemu ifuatayo, tumeshughulikia ujumbe unaohusu nafasi ya mwanamke katika jamii ulivyojitokeza katika MMS na MS.

#### 4.8 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii

Ujumbe unaohusu nafasi ya mwanamke katika jamii ulihawilishwa na watafsiri wa MMS na MS kupitia mifano mbalimbali. Katika sehemu hii, tulianza kwa kuangazia mfano 65 ufuatao.

##### Mfano 65

**MMS:** Anna: wamekwenda wapi? (akifungua mlango) Antoni! Baba? (kwa Marya). Kila wakati kupoteza muda ukipekuapekua kutafuta pini na vidani. (uk 13).

**MS:** Ann: (akisema nje)...wamekwenda wapi watu wote? (anaingia kupitia mlangoni) Antoni! Antoni kipenzi! Toni! Uko wapi jameni? (kwa Maria, haraka) “Hebu nisubiri nijifunge hiki...Hebu nijifanye vile...!” (Uk 20)

Mfano 65 unamchora mwanamke kama kiumbe anayependa urembo katika MMS na MS. Mathalani, katika MMS na MS, wanawake wameangaziwa kama viumbe wanaopenda urembo na kujirembesha kwa ajili ya kujishindia wanaume pasipo kudhihirisha heshima kwa jamii zao, Anna/Ann alipochukizwa na tabia ya Maria ya kuchukua muda mwingi kujirembesha. Kwa mfano, katika MMS, Anna anamweleza Maria; Kila wakati kupoteza muda ukipekuapekua kutafuta pini na vidani ilhali katika MS, Ann alimwambia Marya: Hebu nisubiri nijifunge hiki...Hebu nijifanye vile!”.

Kutokana na mfano 65, tumegundua kuwa, Marya alimchelewesha mamake kwa sababu ya shughuli za kujirembesha. Kwa hivyo, watafsiri wa MMS na MS walifanikiwa kumsawiri mwanamke kama mja anayeweza kumkosea heshima mzazi wake kwa nia ya kuyafikia malengo yake ya kibinafsi pasipo kujali muktadha, hali zilizopo au matokeo yanayoweza kutukia kama inavyojitokeza katika diskosi hizo.



Aidha, mfano 65 unabainisha tofauti za kimaana katika uwasilishaji wa ujumbe katika MMS na MS (mfano 65), na tofauti hizo zimeibuka kwa kuwa, kila mtafsiri ana upekee wake wa kuteua msamiati katika shughuli za tafsiri. Swali ni je, kifungu katika MMS (mfano 65), kutafuta pini na vidani ni kisawe cha kifungu katika MS (mfano 65), Hebu nisubiri nijifunge hiki...Hebu nijifanye vile? Mfano 65, pia unaendelea kubainisha nafasi ya mwanamke katika jamii inavyojitokeza katika MMS na MS.

### **Mfano 66**

**MMS:** Ghlestakovu: Umevaa mkufu maridadi sana. (uk 59).

**MS:** Hilestakov: Shela ulilovaa ni zuri kwelikweli! (uK 86)

Katika MMS na MS (mfano 66), ujumbe wa nafasi ya mwanamke katika jamii umejitokeza, mwanamke anaposawiriwa kama mpenda urembo. Tumegundua kuwa matini tafsiri za MMS na MS, zinamtenga mwanamke na maswala ya uongozi, ulevi, kutowajibikia kazi, uchafuzi wa mazingira na matumizi mabaya ya mamlaka na kumwangazia kama kiumbe anayependa kujipamba.

Katika MMS (mfano 66), kuna vifungu vinavyoanza kwa kitenzi kisha kifuatwe na nomino. Kwa mfano katika MS (mfano 66); ‘Umevaa mkufu maridadi sana’. kuna utungo ulioanza kwa nomino kisha kitenzi, kwa mfano, ‘Shela ulilovaa ni zuri kwelikweli’. Aidha, nomino mkufu na shela ni misamiati miwili ambayo haifanani kimaana ingawa watafsiri wa MMS na MS wametumia neno mkufu kama kwamba ni sinonimi ya neno shela. Kulingana na Kamusi Elezi (2016), mkufu ni pambo linalovaliwa shingoni lifananalo na mnyororo bali shela ni kitambaa chepesi kinachovaliwa kichwani na wanawake na aghalabu huvaliwa pamoja na veli wakati wa arusi.

Tulidahili kwamba, msomaji huenda akajiuliza je, Marya/Maria alivaa shela ama mkufu? Kwa misingi hiyo, tulidahili kuwa tofauti katika uwasilishaji wa ujumbe katika MMS na MS (mfano 66), umeibuka kwa sababu ya uhuru wa mtafsiri katika uteuzi wa maneno. Aidha, katika tasnifu hii tulihoji kwamba, watafsiri wa MMS na MS wana taasubi ya kiume kwa kuwa katika (mfano 66), walimsawiri mwanamke kama kiumbe anayependa kujirembesha ilhali watafsiri hao (Mwakasaka na Madumulla) walikuwa na uhuru wa ama kubadilisha au kupuuzwa ujumbe huo wa mwanamke kupenda kujirembesha. Ufuatao ni mfano 67 ambao pia unazungumzia nafasi ya mwanamke katika jamii ilivyojitokeza katika MMS na MS.

### **Mfano 67**

**MMS:** Mke wa Mhunzi: Alipaswa kumchukua mwana wa Fundi Cherehani yule mlevi kupindukia lakini wazazi wake walimshawishi (ishara ya hongo) amwache; halafu akamchukua mwana wa Mshona Urembo lakini mamaye alimpelekea doti tatu za hariri mkewe; kwa hiyo akaja kwetu. (uk 57).

**MS:** Mke wa Fundi: ...bora angemchukua mtoto wa fundi cherehani yule ambaye si lolote bali ni ulevi tu. Ni kwa sababu tu wazazi wake walikuwa na uwezo wa kuhonga ndio maana akamng'ang'ania mtoto wa mchuzi wa nguo. Lakini mama yake ambaye ni mjane alituma majola matatu ya kitambaa kizuri cha kitani kwa mke wa Meya. (uk 83).

Katika mfano 67, ujumbe wa kuwa mwanamke amesawiriwa kama mhusika fisadi umejitokeza katika tamthilia za MMS na MS. Kwa mfano, katika MMS (mfano 67), Mke wa mhunzi anasema, lakini mamaye alimpelekea doti tatu za hariri mkewe; kwa hiyo akaja kwetu bali katika MS (mfano 67), Mke wa Fundi anadai kuwa; Lakini mama yake ambaye ni mjane alituma majola matatu ya kitambaa kizuri cha kitani kwa mke wa Meya. Kutokana na vifungu vilivyopigiwa mistari, tulidahili kuwa, katika mchakato wa tafsiri, aghalabu watafsiri hawazingatii msamiati aliotumia

msanii wa matini asilia moja kwa moja, badala yake wao huongozwa na haja ya kuwasilisha ujumbe, yaani, mtafsiri huwa na lengo la kurithisha hadhira lengwa.

Tulihoji kwamba, watafsiri wa MMS na MS waliweza kudhihirisha uyakinifu badala ya ubinafsi katika mchakato wa tafsiri. Uyakinifu unadhihirika kwa sababu, watafsiri hao hawakuathiriwa na haja ya kumtetea mwanamke kwa kumpatia sifa ama chanya au hasi. Kwa mfano, kama inavyojitokeza katika MMS na MS (mfano 67), wanawake wanaangaziwa kama watu waliochangia katika kuenea kwa ufisadi.

Iwapo watafsiri hao, Mwakasaka na Madumulla wangukuwa wameathiriwa na misingi mikali ya kifeministi, wangebadiilisha sifa hiyo na kumsawiri mwanamke kama asiyeshiriki katika ufisadi. Kama watafsiri, Mwakasaka na Madumulla walikuwa na uhuru wa kubadilisha ujumbe uliopo katika matini chanzi na kuibuka na msimamo wao tofauti. Kwa hivyo, watafsiri hao wangeweza kunyumbuanyumbua hali ilivyokuwa katika matini chanzi ili kuibua hali mpya lakini walichagua kudumisha ujumbe wa mwandishi wa matini chanzi. Mfano 68 ufuatao pia unashughulikia ujumbe wa nafasi ya wanawake katika jamii ulivyojitokeza katika MMS na MS.

### **Mfano 68**

**MMS:** Ghlestakovu: Huelekei kuwa mpenzi wa sigara. Sigara ndio udhaifu wangu. Na kama kawaida mabibi pia. Siwezi kujizuia. (uk 48).

**MS:** Hilestakov: Hayo ni matatizo yangu pia. Na tatizo jingine (anainama mbele) ni wanawake! Ah! Siwezi kujizuia kwa mwanamke mzuri. (uk 69).

Katika mfano 68, wanawake wamesawiriwa kama vyombo vya kumfurahisha mwanaume inavyodhihirika katika maongezi ya Ghlestakov/Hilestakov. Katika MMS (mfano 68), Ghlestakovu anasema: Sigara ndio udhaifu wangu. Na kama kawaida mabibi pia. Siwezi kujizuia. Kwa upande mwingine, katika MS (mfano 68), Hilestakov

anasema; Na tatizo jingine (anainama mbele) ni wanawake! Ah! Siwezi kujizuia kwa mwanamke mzuri.

Katika tasnifu hii tulidahili kuwa, uteuzi wa msamiati uliofanywa na watafsiri wa MMS na MS unaweza kuzalisha tungo za aina mbili zisizowakilisha dhana sawa. Hili linabainika katika utungo wa MMS (mfano 68), ‘na kama kawaida mabibi pia. Siwezi kujizuia.’ na utungo katika MS (mfano 68), Ni wanawake! Ah! Siwezi kujizuia kwa mwanamke mzuri. Tungo zilizopigiwa mistari zinadhihirisha kuwa, maana za leksimu hizi mbili: ‘bibi’ na ‘mke’ haziwezi kuchukuliwa kama visawe.

Kutokana na mfano 68, tumegundua kwamba, watafsiri wawili wa matini chanzi moja, wakiteua maneno ambayo si visawe ili watumie kuhawilisha ujumbe katika muktadha mmoja, ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa matini chanzi unaweza kubadilika, yaani, matokeo yatakuwa tofauti kama ilivyo katika mfano 68. Licha ya tofauti za kimaana zilizoibuka katika (mfano 68), ujumbe kuhusu mwanamke kama chombo cha kumfurahisha mwanaumme bado unajitokeza katika tamthilia za MMS na MS.

Katika mfano 68, mbinu ya ‘tafsiri ya kijumla’ imetumiwa katika MMS ambapo Ghlestakov anasema, Siwezi kujizuia.’ Kwa upande mwingine, mbinu ya ‘tafsiri mahususi’ imetumiwa katika MS, Hilestakov anaporejelea nomino kitajwa mahususi ‘Ah! Siwezi kujizuia kwa mwanamke mzuri.’ Ujumbe wa nafasi ya mwanamke katika jamii pia umeelezewa katika mfano 69 ufuatao, ulionukuliwa kutoka katika MMS na MS.

### **Mfano 69**

**MMS:** Mke wa Mhunzi: ... “Mumeo ni mwizi,” anasema, “Lakini bado hajaiba chochote; lakini yote ni mamoja, ataiba siku moja,” “Na mimi nabaki hapa bila mume, mwanamke mnyonge na dhaifu,” nilimwambia. Mke wa Sajeni: Ni huyu Mkuu wa Wilaya, bwana mkubwa. Aliamuru nichapwe; mtu katili...! (uk 57)

**MS:** Mke wa Fundi, Alimpeleka mume wangu jeshini. Ndilo hilo heshimiwa. Yeye (mume wangu) ameo, hivyo ni kinyume cha sheria kupelekwa jeshini). Mjane: Aliagiza nicharazwe bakora msheshimiwa. (uk 83- 84).

Ujumbe wa kudhulumiwa kwa wanawake unajitokeza katika MMS na MS (mfano 69), mwanamke anapodhulumiwa huku anaonyeshwa akitetea haki zake. Kwa mfano, katika MMS (mfano 69), mke wa Mhunzi anasema, Mumeo ni mwizi,” anasema, “Lakini bado hajaiba chochote; lakini yote ni mamoja, ataiba siku moja,” “Na mimi nabaki hapa bila mume, mwanamke mnyonge na dhaifu,” bali katika MS (mfano 69), Mke wa Fundi anasema, Alimpeleka mume wangu jeshini. Ndilo hilo msheshimiwa. Yeye (mume wangu) ameo, hivyo ni kinyume cha sheria kupelekwa jeshini. Utungo Na mimi nabaki hapa bila mume, mwanamke mnyonge na dhaifu,” sio sawa kimaana na utungo Alimpeleka mume wangu jeshini. Ndilo hilo msheshimiwa.

Tulihoji kuwa, tungo zilizopigiwa mistari zinaonyesha kwamba, huenda watafsiri wa MMS na MS hawakuelewa ujumbe wa (mfano 69) katika matini chanzi barabara, au wangeeleweka vizuri iwapo wangetumia tungo sahili. Isitoshe, hali ya kutoeleweka vizuri kwa vifungu vinavyozalishwa na watafsiri kunaweza kuhusishwa na kosa la watafsiri la kutoelewa barabara ujumbe kabla ya kuuhawilisha kwa maneno yao au sentensi zao tofauti. Pia, mfano 70 ufuatao unaangazia nafasi ya mwanamke katika jamii ilivyojitokeza katika MMS na MS.

### **Mfano 70**

**MMS:** Anna: Utakuwa na marafiki tofauti. Hakutakuwa na mahakimu wa kawaida wanaonuka harufu ya mbwa ambayo ni sumu kwa sungura au yule Zemlyanika mchafu. Rafiki zako watakuwa watu wa hali ya juu sana mawaziri na watu wengine wa jiji. (uk 65).

**MS:** Ann: ...Marafiki zetu watakuwa si wale tena akina domo-kaya ambao hawafikirii lolote zaidi ya kuwinda sungura. Marafiki zetu sasa watakuwa ni watawala ambao wana tabia za kistaarabu. (uk 98).

Katika tamthilia za MMS na MS (mfano 70), wanawake wamesawiriwa kama washauri wabaya, watu ambao wana madharau na wangepurahia kujitenga na watu wa tabaka la chini. Kwa mfano, katika MMS (mfano 70), Anna anamwambia Mkuu wa Wilaya kuwa, Hakutakuwa na mahakimu wa kawaida wanaonuka harufu ya mbwa ambayo ni sumu kwa sungura au yule Zemlyanika mchafu. Katika MS (mfano 70), Ann anamwambia Meya kuwa, Marafiki zetu watakuwa si wale tena akina domo - kaya ambao hawafikiri lolote zaidi ya kuwinda sungura.

Tungo zilizopigiwa mistari katika (mfano 70), zinathibitisha kuwa watafsiri wa MMS na MS, walidumisha sifa ya wanawake ya kuwa washauri wabaya. Kwa mfano, kifungu katika MMS (mfano 70), Anna anaposema, mahakimu wa kawaida wanaonuka harufu ya mbwa haipo katika MS (mfano 70). Tumegundua kuwa, uhawilishaji wa ujumbe kuhusu nafasi ya mwanamke umeambatana na tofauti za kileksika, kisarufi na kimaana. Kwa mfano, uteuzi wa jina hili: 'Zemlyanika' lilitumika katika MMS ilhali jina hilo halipo katika MS.

Tulihoji kuwa, watafsiri wa MMS na MS katika (mfano 70), walitofautiana katika uhawilishaji wa kipengele cha nafsi. Mathalani, katika MMS (mfano 70), mtafsiri amerejelea nafsi ya pili - umoja (wewe) katika utungo huu: 'Utakuwa na marafiki tofauti' bali katika MS (mfano 70), mtafsiri amerejelea nafsi ya kwanza wingi (sisi) katika utungo huu: 'Marafiki wetu watakuwa'. Hivyo, katika MMS ujumbe unamrejelea mtu mmoja (anayezungumziwa pekee yake) lakini katika MS ujumbe unamrejelea mzungumzaji pamoja na wengine. Sehemu ifuatayo ya 4.9 inashughulikia hitimisho ya sura ya nne.

#### 4.9 Hitimisho

Katika sura hii ya nne, tuliangazia ujumbe mbalimbali ulivyojitokeza katika MMS na MS. Ujumbe tulioshughulikia ni dhuluma, matumizi mabaya ya mamlaka, ufisadi, uasherati, kutowajibika, unafiki, madawa ya kulevya na nafasi ya wanawake katika jamii.

Kutokana na uhakiki wa ujumbe mbalimbali katika tamthilia za MMS na MS, ilibainika kwamba, kuna uwezekano wa kuwa na ujumbe katika kitabu kimoja na ujumbe huo ukawa haujashughulikiwa katika kitabu kingine. Aidha, kuna ujumbe ambao upo katika matini pokezi mbili: MMS na MS lakini tofauti ipo katika uteuzi wa msamiati na uhawilishaji wa ujumbe huo. Katika utafiti huu tulidokeza kwamba tofauti katika uteuzi wa msamiati na uhawilishaji wa ujumbe umeibuka kwa kuwa, katika mchakato wa tafsiri, watafsiri wana uhuru wa kuteua msamiati wanavyotaka.

- a) Mtafsiri anaweza kudondoa, kubadilisha au kupuuza sehemu ya matini chanzi na jambo hili limepelekea kuwepo na tofauti katika uhawilishaji wa ujumbe ulivyodhihirika katika sura hii ya nne. Pia, katika sura hii, tulijadili kwamba kuna uwezekano wa mtafsiri kuibuka na wazo ambalo ni tofauti kabisa na wazo katika matini chanzi kwa sababu, hakuna kanuni zozote ambazo humshurutisha mtafsiri kutafsiri neno kwa neno ama sentensi kwa sentensi ili kuwa mwaminifu kwa matini chanzi.

Kwa mtazamo wa nadharia ya uamilifu katika tafsiri, muundo na maneno ya lugha asilia yanaweza kuachwa na maana asilia ikawasilishwa kwa msamiati tofauti wa lugha lengwa ili kuupitisha ujumbe. Katika sura ya 5 (tano) ifuatayo, tulichanganua kiulingaishi uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali (1979)* na *Mkaguzi wa Serikali (1999)*.

## SURA YA TANO

### UTEUZI WA MSAMIATI KATIKA USAWIRI WA WAHUSIKA KATIKA

#### *MKAGUZI MKUU WA SERIKALI NA MKAGUZI WA SERIKALI*

#### **5.0. Utangulizi**

Katika sura hii ya tano, tulichanganua kiulinganishi tabia na sifa za wahusika ili kushughulikia lengo la tatu la utafiti huu ambalo ni kuhakiki kiulinganishi uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Mwakasaka, 1979) na *Mkaguzi wa Serikali* (Madumulla, 1999). Kabla ya kuchunguza tabia na sifa za wahusika, tulishughulikia vipengele vifuatavyo: ulinganishaji wa majina ya wahusika katika MMS na MS, upangaji wa majina ya wahusika katika MMS na MS, na tafsiri za majina ya wahusika kulingana na nafasi zao katika MMS na MS. Sehemu ifuatayo ya 5.1 inaangazia dhana ya wahusika na ulinganishaji wa majina ya wahusika katika MMS na MS.

#### **5.1 Majina ya Wahusika katika Tamthilia za MMS na MS**

Katika sehemu hii tumeeleza dhana ya wahusika kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali. Kwa mfano, kulingana na Senkoro (1982), wahusika ni watu au viumbe walioumbwa na mwandishi na huwakilisha tabia za watu katika kazi ya fasihi. Ni watu au viumbe waliotumiwa na mwandishi katika kazi ya fasihi ili kuwasilisha ujumbe, dhamira na falsafa yake kwa wasomaji ama wasilikilizaji. Kilonzo na Masaku (2017) wanaeleza kwamba mhusika ni mtu ama kiumbe ambacho hutumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi katika kupitisha ujumbe wake kwa wasomaji au wasilikilizaji. Ni kiini cha vipengele vyote katika fasihi kama vile dhamira, ujumbe na mada za fasihi.



Majina ya wahusika yametofautiana katika matini mbili za MMS na MS. Kwa mfano, katika MS, mtafsiri aliwapatia wahusika majina matatu ilhali katika MMS, mtafsiri aliwapatia wahusika wake majina mawili. Watafsiri wa MMS na MS, pia walitumia mwendelezo usiokuwa wa Kibantu katika kuunda silabi za majina ya mhusika Ghlestakov/Hlestakov. Kwa mfano, katika MMS, anaitwa ‘Ghlestakovu’, na katika jina hilo, silabi ya kwanza imeundwa kwa mfuatano wa fonimu ambayo ni kipasuo, kitambaza na irabu. Tulihoji kuwa mfuatano huo sio wa kawaida katika uundaji wa majina ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine, katika MS, Madumulla alitumia jina la Hilestakov, hivyo, alifuata ruwaza ya silabi ambayo ni ya kimsingi katika sarufi ya Kiswahili. Hata hivyo, katika kuunda silabi za jina ‘Hilestakov’, mtafsiri wa MS alibadilisha utaratibu wa kimsingi wa uundaji wa majina ya Kiswahili katika silabi ya mwisho ya neno hilo. Hivyo, tofauti na Mwakasaka, Madumulla aliunda jina linaloishia kwa silabi funge inayotamatishwa kwa kikwaruzwa ‘v’. Imebainika kwamba, watafsiri Mwakasaka na Madumulla waliegemea zaidi kwenye ruwaza za jina la matini chanzi badala ya kutafuta jina lingine tofauti la Kiswahili.

Katika tasnifu hii tulihoji kwamba, Mwakasaka na Madumulla walitofautiana katika kuendeleza jina hilo; (Ghelestakov na Hilestakov) kwa kuwa katika mchakato wa tafsiri, watafsiri wana uhuru wa ama kuteua msamiati au kuibuka na majina ya wahusika wanavyotaka. Hali hii huchangia maingiliano ya tamaduni kwa kuwa, majina yanayotumiwa katika lugha mbalimbali yanafungamana na tamaduni za jamii husika. Aidha, mtafsiri wa MMS aliswahilisha baadhi ya majina ilhali mtafsiri wa MS, hakiswahilisha majina kama inavyoonekana katika Jedwali 5.1 lifuatalo:

**Jedwali 5.1: Ulinganishaji wa majina katika Tafiri za: MMS na MS**

<b>Mwakasaka (MMS)</b>	<b>Madumulla (MS)</b>
Antoni Antonovichi	Antoni Antonovichi skvoznik
Amosi fysdorovichi Lyapkini	Amos Fyodorovich –Tyapkin
Atemi filiporich Zemiyanka	Atemi Philipovich Zemlyanka
Luka Lukichi	Luka Lukichi Klopov
Irani koosmichi	Irani Kuzmich Shpyokin
Stepani Iyichi	Luteni stefan Ilyich Ukhoryortov
Pita Lvanovich Bobchinski	Peter Lvanovich Bobchinski
Pita Lvanovich Dobchinski	Peter Lvanovich Dobchinski
-Irani Alekzandrovichi Ahlestakov	Iran Alexandrovich Hilestakov
-Yosif	Osipu
-Anna Andreyevna	Ann Andrenovna
-Marya Antonovna	Maria Antonovna
Mke wa mhunzi	Mke wa fundi wa vitaja
Mke wa sajani	Mke wa sajenti
Mkewe Korobkin	Mke wa Korobkin
Abdulini	Abdullin
Irani Rastakorski	Irani Lazarevich Rastakoriski
Stepani Iranovichi	Stepan Lvanovich Korobin
Dyerizimada	Dyerizmarda.

**5.2 Upangaji wa Majina ya Wahusika**

Watafsiri wa MMS na MS walitofautiana katika kuorodhesha majina ya wahusika. Kwa mfano, katika MMS, Mwakasaka amewaorodhesha wahusika kulingana na daraja za kifamilia hivi kwamba ameanza na Mkuu wa Wilaya, halafu akafuatia na mkewe (Anna), kisha Binti yake (Marya). Wahusika wengine ambao wana familia pia waliorodheshwa vivyo hivyo. Katika tamthilia ya MS, Madumulla kwa upande wake

amewaorodhesha wahusika kuanzia wale wa ngazi za juu madarakani hadi za chini. Kwa mfano Meya, Jaji, Kamishna wa Msaada, Mkaguzi wa Mashule, nk.

### 5.2.1 Tofauti ya Idadi ya Wahusika katika MS na MMS

Katika tamthilia ya MMS, Mwakasaka hakumworodhesha mganga kama mmoja wa wahusika wake ila amemtumia kama daktari ilhali katika MS, Madumulla amemworodhesha mganga kama mmoja wa wahusika na pia amempa nafasi ya kuongea. Katika MMS, mtafsiri ana wahusika anaowaita Vistoonovu na Dyerizimoda ilhali katika MS, mtafsiri hajawataja wahusika hao. Aidha, katika MS, Madumulla ametoa maelezo kwa muhtasari kuwahusu baadhi ya wahusika ilhali katika MMS, Mwakasaka hajatoa maelezo yoyote kumhusu mhusika yeyote.

### 5.2.2 Nafasi ya Wahusika

Katika tamthilia za MMS na MS, watafsiri wametofautiana katika kuyatafsiri majina ya wahusika. Kwa mfano, mtafsiri wa MS, ameegemea tafsiri tohozi ambapo ameswahilisha majina kama vile ‘Meya’ na ‘Jaji’. Utohozi huo wa majina yanayohusiana na nafasi ya mhusika haujafanywa na mtafsiri wa MS inavyodhihirishwa katika jedwali lifuatalo la 5.2:5.

#### Jedwali 5.3:5 Tafsiri za Majina kulinganga na Nafasi za Wahusika

Cheo cha wahusika	Mwakasaka	Madumulla
-Kiongozi wa wilaya	-Mkuu wa Wilaya	-Meya
-Mkuu wa mahakama	-Hakimu	-Jaji
-Anayesimamia mashirika	-Bwana huruma	-Kamishina wa misaada
-Anayesimamia elimu	- Mratibu wa elimu	-Mkaguzi wa mashule
-Anayesimamia posta	- Bwana posta	-Mkuu wa posta
-Anayesimamia polisi	- Mkuu wa polisi	-Inspecta wa polisi
- Washika doria	- Askari walinzi	-Makonstebo

Reiss (1977) anadahili kuwa, kila lugha huwa na upekee wake katika ubunifu wa majina. Yaani, lugha hazitoi majina au msamiati tu kwa vitu au dhana zilizopo bali zina mfumo maalum wa kubuni. Hivyo, tumegundua kuwa katika taaluma ya tafsiri, hakuna kanuni zozote zinazowaongoza watafsiri wanapoteua msamiati kama inavyojitokeza katika Jedwali 5.2. Kwa mfano, hakuna kanuni inayoeleza iwapo kutumia ‘Askari walinzi’ katika harakati za kutafsiri ni heri kuliko kusema ‘Makonstebo’. Aidha, tumegundua pia kwamba tafsiri nzuri ni ile itakayoweza kudumisha ufasihi wa kazi ya fasihi inayotafsiriwa. Sehemu ifuatayo imeshughulikia sifa na tabia za wahusika walivyosawiriwa katika MMS na MS.

### **5.3. Sifa na Tabia za Wahusika**

Katika sehemu hii, tuliangazia sifa na tabia za wahusika sita ambao tuliwateua kimakusudi kutoka katika tamthilia za MMS na MS. Aidha, tumemtaja kila mhusika kwa jina na kubainisha kiulinganishi sifa zake. Katika sehemu ifuatayo ya 5.3.1 tulieleza sifa za Mkuu wa Wilaya (Meya) kama alivyosawiriwa na watafsiri wa tamthilia za MMS na MS.

#### **5.3.1 Mkuu wa Wilaya (Meya)**

Katika MMS, Mkuu wa Wilaya ndiye kiongozi wa ngazi ya juu kuliko wahusika wengine na ndiye mhusika mkuu bali katika MS, Meya ndiye kiongozi wa ngazi ya juu kuliko wahusika wengine na ndiye mhusika mkuu. Watafsiri wa MMS na MS walimsawiri Mkuu wa Wilaya (Meya) akiwa na sifa kadhaa na mwanzo, tumebainisha sifa yake ya ukatili ifuatavyo.

### 5.3.1.1 Katili

Kulingana na TUKI (2014), katili ni mtu ambaye ni mwovu na hana huruma, anayeweza kuwatendea binadamu wenzake vitendo vya kinyama bila kujali. Katika MMS na MS, Mkuu wa Wilaya (Meya) amesawiriwa kama katili inavyobainishwa katika mifano ifuatayo na tulianza na mfano 71.

#### Mfano 71

**MMS:** Mke wa Sajeni: Ni huyu Mkuu wa Wilaya, Bwana Mkubwa. Aliamuru nichapwe, mtu katili! (uk 57).

**MS:** Mjane: Aliagiza nicharazwe bakora mheshimiwa kiasi kwamba nisiweze kuketi. (uk 84).

Mfano 71 ulionukuliwa kutoka tamthilia za MMS na MS, unathibitisha kuwa, Mkuu wa Wilaya (Meya) alikuwa katili alipowaamrisha polisi wampige mke wa sajeni/sajenti. Kwa mfano, katika MMS, mke wa sajenti anasema: Ni huyu Mkuu wa Wilaya, Bwana Mkubwa. Aliamuru nichapwe, mtu katili bali katika MS, Mjane analalamika kwamba: Meya Aliagiza nicharazwe bakora mheshimiwa kiasi kwamba nisiweze kuketi.

Katika utafiti huu tulihoji kwamba, mtafsiri wa MMS, ni mcheshi kwa kuwa alitumia mbinu ya chuku, Mke wa Sajeni aliposema kwamba, Meya aliagiza nicharazwe bakora mheshimiwa kiasi kwamba nisiweze kuketi. Kifungu hiki; kiasi kwamba nisiweze kuketi hakipo katika MMS, Pia, anayezungumza katika tamthilia ya MMS (mfano 70) ni Mke wa Sajeni ilhali anayezungumza katika MS (mfano 71) ni Mjane. Yaani, wahusika katika tafsiri za MMS na MS (mfano 71), walipewa majina tofauti. Mfano 71 pia unabainisha sifa ya ukatili ya mhusika Mkuu wa Wilaya (Meya) inavyojitokeza katika MMS na MS.

**Mfano 72**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: mtapaswa ku... Hakikisha kuwa hakuna yeyote anayeingia akiwa na maombi au bila maombi, au hata yeyote anayeelekea kuleta maombi dhidi yangu, watupwe nje kichwa kikitangulia, mnaelewa? (akionyesha teke la nguvu) kama hivyo. Mnaskia? (uk 41).

**MS:** Meya: Mkimwona yeyote akija hapa na kitu chochote hasa kama ni malalamiko dhidi yangu, muondoeni kwa nguvu na kumtupa nje. Fanyeni hivi, mnaona? (anampiga teke mtu asiyekuwepo), (uk 62).

Katika MMS na MS, (mfano 72), Mkuu wa Wilaya (Meya) alidhihirisha sifa ya kuwa katili kwa kuwaamuru polisi kumpiga mateke na kumfukuza yeyote aliyetaka kumwona Ghlestakov/Hilestakov. Kwa mfano, katika MMS (mfano 72), Mkuu wa Wilaya anamweleza askari kuwa, Hakikisha kuwa hakuna yeyote anayeingia akiwa na maombi au bila maombi, au hata yeyote anayeelekea kuleta maombi dhidi yangu. Katika MS (mfano 72), Meya aliwaamuru polisi kwa kusema, Mkimwona yeyote akija hapa na kitu chochote hasa kama ni malalamiko dhidi yangu.

Kutokana na mfano 72, Mkuu wa Wilaya anamwamuru askari kumzuia yeyote ambaye yuko tayari kuleta maombi dhidi yake asimwone Ghelestakov. Kwa upande mwingine, Meya anawaamuru polisi kumzuia yeyote ambaye anataka kuleta malalamiko dhidi yangu asimwone Hilestakov. Watafsiri wa MMS na MS (mfano 72), walitofautiana kimaana katika uwasilishaji wa vifungu vilivyopigiwa mistari. Katika Kiswahili, neno maombi lina maana tofauti na neno malalamiko. Tulihoji kuwa, kifungu katika MS (mfano 72); anayeleta malalamiko dhidi yangu kinaeleweka barabara kuliko kifungu katika MMS (mfano 71); kuleta maombi dhidi yangu.

Katika MMS (mfano 72), Mkuu wa Wilaya anawaamuru askari wamzuie yeyote aliyetaka kumwona Ghlestakov kwa kutumia teke kuwatupa nje kichwa kikitangulia. Kwa upande mwingine, katika MS (mfano 72), Meya aliwaamuru askari wamuondoe

kwa nguvu na kumtupa nje mtu aliyetaka kumwona Hilestakov huku akiwaonyesha kwa ishara ya teke jinsi watakavyofanya. Kutokana na tungo zilizopigiwa mistari (mfano 72) tulihoji kuwa, maelezo katika MS yanaeleweka barabara kwa kuwa, Meya alionyesha kwa vitendo alivyotaka askari watekeleze, kinyume na maelezo katika MMS. Mfano 73 ufuatao, pia unashughulikia tabia ya Mkuu wa Wilaya (Meya) kama mtu katili.

### **Mfano 73**

**MMS:** Abdulini: Hajatokea Mkuu wa Wilaya kama yeye, anayetunyanyasa kwa kututumia askari wenye rungu...Anatuvuta ndevu na kutukemea: Mfanyi biashara 2: Hasa! Lakini ukidiriki kusema neno atakutumia kikosi kizima cha rungu.... (Uk 55)

**MS:** Abdulin: Mheshimiwa!Hapajawahi kutokea Meya Mkuu wa Wilaya mwovu kama huyu, Lakini hatuthubutu kulalamika, Mheshimiwa. Atakuletea kikosi kizima cha askari ukigundulika kuwa umefanya hivyo, au hata kufunga biashara yako, (uk 80-81).

Watafsiri wa MMS na MS katika mfano 73, wamemsawiri Mkuu wa Wilaya (Meya) kama mtu katili. Kwa mfano, katika MMS, Abdulini anamwambia Ghlestakov kuwa: hajatokea Mkuu wa Wilaya kama yeye, anayewanyanyasa kwa kuwatumia askari wenye rungu, huku akiwavuta ndevu na kuwakemea. Kwa upande mwengine, katika MS, (mfano 73), Abdulin anasema kuwa hapajawahi kutokea Meya mwovu kama huyu, na mtu hawezi kusema mambo anayowatendea wafanyibiashara maskini. Kimaana, sentensi zilizopigiwa mstari katika mfano 73, zinadhihirisha kuwa katika MMS, Abdulini na mfanyi biashara wa 2 ndio wanaotoa malalamishi yao kwa Ghlestakovu dhidi ya Mkuu wa Wilaya bali katika MS Abdulin kwa niaba ya wafanyi biashara wengine ndiye anayetoa malalmishi yao kwa Hilestakov.

Ingawa watafsiri wa MMS na MS walifaulu kumsawiri Mkuu wa Wilaya (Meya) kama katili lakini maelezo katika MMS (mfano 73) yanajitokeza kwa uwazi zaidi.

Kwa mfano, sentensi zilizopigiwa mstari katika mfano 73 zinadhihirisha kuwa uhuru wa kitafsiri humwezesha mtafsiri kufasiri na kuteua msamiati katika kazi ya fasihi bila masharti ama kanuni zozote. Hivyo, kupelekea kuwepo na tofauti katika uwasilishaji wa ujumbe katika makala pokezi mbili: *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*. Mfano 74 ufuatao pia unahusu sifa ya ukatili wa Mkuu wa Wilaya (Meya) inavyojitokeza katika tamthilia za MMS na MS.

#### **Mfano 74**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya:.. nitamlazimisha kila mshenzi mfanya biashara kuchanga kilo hamsini za nta. (uk 13).

**MS:** Meya:nitamwamuru kila mfanyi biashara atoe kilo kadhaa za nta ya kutengeneza shumaa hilo, (uk 18).

Katika tamthilia za MMS na MS (mfano 74), Mkuu wa Wilaya (Meya) amesawiriwa kama mtu katili aliposema kuwa atawaamuru wafanyabiashara kutoa nta iwapo atafanikiwa. Mathalani, katika MMS (mfano 74), Meya anaeleza kwamba: atamwamuru kila mfanya biashara atoe kilo kadhaa za kutengeneza shumaa ilhali katika MMS (mfano 74), Mkuu wa Wilaya anasema kuwa: atamlazimisha kila mshenzi mfanyabiashara kuchangia kilo hamsini za nta, bila kuelezea nta hiyo ni ya kufanyia nini.

Mfano 74, unadhihirisha kuwa, neno mshenzi lipo katika MMS lakini halipo katika MS. Hivyo, tulidahili kuwa katika mchakato wa tafsiri, watafsiri wana uhuru wa ama kupuuza au kuongeza msamiati katika tafsiri, hali hii inaweza kuathiri uchambuzi wa sifa za wahusika. Kwa mfano, mchanganuzi wa tamthilia za MMS na MS anaweza kutumia mfano 74, kudai kuwa, Mkuu wa Wilaya ni mpyaro kwa sababu aliwatusi wafanyabiashara kwa kutumia neno ‘mshenzi’ ilhali Meya sio mpyaro kwa sababu mtafsiri wa MS hakudhihirisha sifa hiyo. Hivyo, tulijadili kwamba, tofauti baina ya



MMS na MS katika uhawilishaji wa ujumbe inaishia kumwashiria mhusika mmoja ambaye ni: (Meya na Mkuu wa Wilaya) kuwa na sifa zinazotofautiana. Katika sehemu ifuatayo ya 5.3.1.2, Mkuu wa Wilaya (Meya) pia amesawiriwa kama nafiki inavyojitokeza katika MMS na MS.

### 5.3.1.2 Nafiki

Kulingana na TUKI (2013), mnafiki ni mtu anayejifanya kuwa anatenda yanayostahili katika jamii ilhali anafanya kinyume na matarajio ya wanajamii. Kwa mfano, Mkuu wa Wilaya katika MMS anadhihirisha sifa ya unafiki jinsi Meya anavyoidhihirisha sifa hiyo hiyo katika MS kama inavyonukuliwa katika mifano tofautitofauti na tulianza na mfano wa 75.

#### Mfano 75

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Sasa kama huyu Mkaguzi anamwuliza askari polisi yeyote, “umeridhika?” lazima waseme, “tumeridhika kabisa mheshimiwa.” (uk 12-13).

**MS:** Meya: Sasa jambo jingine, kama Mkaguzi huyu akija kuwapeleleza watu wako kwa kuwauliza kama wanaifurahia kazi yao, hawana budi kujibu haraka, “Ndiyo, Mheshimiwa, tuliifurahia mno.” (uk 18).

Watafsiri wa MMS na MS, katika mfano 75 walifanikiwa kuhawilisha sifa ya unafiki ya mhusika Mkuu wa Wilaya (Meya). Kwa mfano, katika MMS (mfano 75), Mkuu wa Wilaya anasema kuwa: Sasa kama huyu Mkaguzi anamwuliza askari polisi yeyote ilhali katika MS, Meya anasema kuwa: Sasa jambo jingine, kama Mkaguzi huyu akija kuwapeleleza watu wako. Katika tasnifu hii, tuliuliza iwapo kimaana maneno: askari polisi yeyote ni sinonimi ya maneno: watu wako?

Tofauti nyingine baina ya ujumbe katika MMS na MS (mfano 75) ni kwamba, Mkuu wa Wilaya alitumia neno ‘kuridhika’ ilhali katika MS, Meya alitumia neno ‘kufurahia’. Kwa mfano, katika MMS (mfano 75), Mkuu wa Wilaya anasema kuwa,

lazima waseme, “tumeridhika kabisa mheshimiwa ilhali katika MS (mfano 75), Meya anasema kuwa, hawana budi kujibu haraka, “Ndiyo, Mheshimiwa, tuliifurahia mno.”

Tungo zilizopigiwa mistari zinatofautiana kwa kuwa, maneno haya mawili: kuridhika na kufurahia yanabeba fahiwa tofauti kwa kuwa, katika uhalisia wa maisha, mtu anaweza kuridhika pasipo kufurahi au akafurahi hata kama hajaridhika. Kwa mtazamo wa tasnifu hii, wahasika watakaomjibu Mkaguzi wa Serikali kwamba wameridhika watakuwa wameficha sifa ya unafiki wa Mkuu wa Wilaya. Pia mfano 76 ufuatao unaelezea sifa ya unafiki ya Mkuu wa Wilaya (Meya) ilivyojitokeza katika MMS na MS.

### **Mfano 76**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ... hata ninapoingia kitandani kulala, daima nawaza, “Eee Bwana Mungu, kama ningepata asante ya wakubwa wangu kwa ajili ya juhudi yangu, hilo lingetosheleza. (uk 34-35).

**MS:** Meya... Kuna mameya wengi ambao hupenda kujifanyia mambo ya kunufaisha nafsi zao wenyewe; lakini mimi nilalapo kitandani huwa ninawaza jambo moja tu: “Mungu uliye Mkuu” huwa ninajiwazia “nisaidie ili niweze kuwafurahisha wakubwa zangu!” (uk 49-50).

Katika MMS na MS (mfano 76), Mkuu wa Wilaya (Meya) alisawiriwa kama mnafiki anapomwomba Mungu amsaidie ili aweze kutambuliwa na kupata shukrani kutoka kwa wakubwa wake. Maombi yake ni ya kinafiki kwa vile anamwomba Mungu amsaidie ili wakubwa wake waweze kumtambua na kumtuzia ilhali anaelewa kwamba hatekelezi wajibu wake ipasavyo. Katika MMS, sifa ya unafiki inajitokeza wakati Mkuu wa Wilaya anaeleza kwamba, Mkuu wa Wilaya daima huwa anawaza akimhusisha Mungu kuwa angetuzwa kwa sababu ya juhudi zake. Kiongozi huyo (Mkuu wa Wilaya), anadai kuwa iwapo angetuzwa alivyotarajia angetosheka.

Kwa upande mwingine (mfano 76), katika MS, Meya anasema kuwa, kuna mameya wengi ambao hupenda kujifanyia mambo ya kunufaisha nafsi zao wenyewe; lakini nilalapo kitandani huwa ninawaza jambo moja tu: “Mungu uliye Mkuu” nisaidie ili niweze kuwafurahisha wakubwa zangu! Hivyo, unafiki unajitokeza Meya anapowashutumu mameya wengine kwamba wao hufanya mambo ya kujinufaisha ilhali yeye mwenyewe hatekelezi majukumu yake ya umeya. Mfano 76 ulinukuliwa kutoka MMS na MS na unashughulikia vilevile sifa ya unafiki wa Mkuu wa Wilaya/Meya.

### **Mfano 77**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya ... (Kwa mfanyabiashara 2)... Na jinsi unavyofutua tumbo! (kwa mfanyabiashara 3). Nguruwe we!... Na kadri tumbo lako linavyovimba ndivyo kadri unavyojiongezea maringo. Dude we! (Kwa Abdulin) ...Nilikusaidia beberu we! (uk 66-67).

**MS:** Meya.. (kwa wenye maduka) .... Nyie wabugia chai, waruka makaunta,na wachuuzi wapunjaji, kwa nini mliamua kulalamika dhidi yangu? Enyi wahuni, enyi panya buku msiyo adabu mtambaao na nyuso mbili! Takataka! (uk 98-99).

Katika mfano 77, Mkuu wa Wilaya (Meya) amesawiriwa kama mnaafiki katika tamthilia za MMS na MS. Hata hivyo, kuna tofauti katika uteuzi wa msamiati, na uhawilishaji wa ujumbe huo. Kwa mfano, kimantiki kuna tofauti kati ya dhana za ‘kila’, ‘o-ote’ na ‘ote’. Katika MMS (mfano 77), Mkuu wa Wilaya alimtusi kila mfanyabiashara ilhali katika MS (mfano 77), Meya aliwatusi wenye maduka kijumla bila kutaja mtu binafsi. Katika MMS (mfano 76), neno ‘wafanyabiashara’ limetumika ilhali katika MS (mfano 77), neno ‘wenye maduka’ ndilo limetumiwa.

Katika MMS (mfano 77), Mkuu wa Wilaya alimtusi mfanyabiashara kwa kutumia maneno haya; jinsi unavyofutua tumbo, Nguruwe we!, Dude we!, beberu we! Katika MS (mfano 77), Meya aliwatusi wafanyabiashara kwa kutumia maneno yafuatayo;

nyie wabugia chai, waruka makaunta, wachuuzi wapunjaji, enyi wahuni, enyi panya-buku msio na adabu mtambao nyuso mbili!, Takataka! Kimaana, matusi hayo katika sentensi zilizopigiwa mistari (mfano 77) yanatofautiana. Kwa mfano, tulidahili kwamba, kimaana panya buku na nguruwe ni wanyama wawili ambao ni tofauti mno. Isitoshe, Dude na beberu sio sinonimi ya waruka makaunta, wachuuzi, wapunjaji na wahuni. Mfano 78 ufuatao pia unaangazia sifa ya unafiki wa Meya/Mkuu wa Wilaya ulivyojitokeza katika MMS na MS.

### **Mfano 78**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Ni wajibu wangu kama mkuu wa wilaya hii, kuona kuwa wasafiri na watu wengine wa maana hawapati tatizo. (Uk 21).

**MS:** Meya (kwa Hilestakov): Tumepita tu mara moja, mimi na Peter Ivanovich, Dobchiniski-huyu hapa, tumepita ili kuona jinsi wageni wanavyohudumiwa...hiyo ni sehemu ya majukumu yangu (Uk 36).

Katika tamthilia za MMS na MS, unafiki wa Mkuu wa Wilaya (Meya) unabainika katika mfano 78, Mkuu wa Wilaya (Meya) anapomdanganya Ghlestakovu/Hilestakov kuwa alizuru hoteli kwa matembezi ilhali hajakuwa akifanya hivyo. Kwa mfano, katika MMS (mfano 78), Mkuu wa Wilaya anasema: “Ni wajibu wangu kama Mkuu wa Wilaya hii, lakini katika tamthilia ya MS (mfano 78), mtafsiri ameweka mwisho maelezo hayo: hiyo ni sehemu ya majukumu yangu.

Katika MMS (mfano 78), Mkuu wa Wilaya hakuwataja wenzake aliyetembea nao kinyume na ilivyo katika MS ambapo Meya anasema kuwa ameandamana na Peter Ivanovich Dobchiniski. Pia katika MMS, Mkuu wa Wilaya anaeleza kwamba alitembea kule hotelini ili kuhakikisha kwamba wasafiri na watu wengine wa maana hawapati tatizo, lakini katika MS, Meya anasema kuwa wamepita ili kuona jinsi wageni wanavyohudumiwa. Tulidahili kwamba, mbinu iliyotumiwa katika MMS na MS (mfano 78) ambapo mhusika mmoja anatenda matendo ambayo hayajulikani kwa

wahusika wengine lakini tayari yanajulikana kwa wasomaji au hadhira ilitumiwa ili kuendeleza sifa ya unafiki wa wahusika.

Tulihoji pia kuwa, katika MMS na MS (mfano 78) unafiki unajitokeza, Meya/Mkuu wa Wilaya anapodai kwamba kule kutembelea hoteli ni sehemu ya majukumu yake ilhali hakuwajibika hivyo hapo. Kuna visa mbalimbali katika MMS na MS, vinavyomwangaza Mkuu wa Wilaya (Meya) kama fisadi na vinashughulikiwa katika sehemu ifuatayo ya 5.3.1.3.

### **5.3.1.3 Fiisadi**

Kamusi ya TUKI (2013) inaeleza kuwa, fisadi ni mtu anayetoa ama anayepokea rushwa. Dhana hii pia inamrejelea mtu anayepotosha haki, anayetumia mamlaka yake vibaya au anayetumia mali ya watu wengine vibaya. Mifano ifuatayo ilibainisha sifa ya ufiisadi ya Mkuu wa Wilaya (Meya) katika matini za MMS na MS. Tumeanza na mfano 79 ufuatao.

#### **Mfano 79**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya ... Kama nimepokea hongo ni zile ndogo ndogo tu chochote kwa chakula au kipande cha nguo. (uk 22)

**MS:** ...na kama nimepata kupokea rushwa ni kidogo mno kwa ajili ya chakula, kitambaa cha koti.vitu vidogovidogo namna hiyo. (uk 34)

Mkuu wa Wilaya (Meya) amesawiriwa katika tafsiri za MMS na MS (mfano 79) kama fisadi alipoungama kwamba, yeye hupokea rushwa. Ingawa nadharia ya tafsiri hupendekeza kwamba usawa wa ujumbe au maana baina ya matini chanzi na matini pokezi unafaa katika mchakato wa kutafsiri, watafsiri wana uhuru wa kufanya uteuzi wa msamiati utakaohawilisha ujumbe kutoka matini chanzi hadi matini pokezi. Kwa mfano, katika MMS, (mfano 79), Mkuu wa Wilaya anaeleza kuwa, Kama nimepokea hongo ni zile ndogo ndogo tu chochote kwa chakula au kipande cha nguo ilhali katika

MS (mfano 79), Meya anaeleza kwamba, na kama nimepata kupokea rushwa ni kidogo mno kwa ajili ya chakula, kitambaa cha koti...vitu vidogo vidogo namna hiyo.

Katika tasnifu hii tulidahili kuwa, mtafsiri ana uhuru wa kuteua msamiati inayoweza kufanana kama katika matumizi ya maneno kama ‘hongo’ linalobeba dhana inayokaribiana sana na ile ya ‘rushwa’ au ‘kipande cha nguo’ kwa maana inayokaribiana na ya ‘kitambaa cha koti’. Tulihoji pia kwamba, tafsiri nyingi za matini chanzi moja ya fasihi zinaweza kuzalishwa kwa kutegemea mahusiano ya kimaana yanayojulikana kama usawe au usinonimia na yalijitokeza katika maneno ya lugha lengwa na lugha chanzi. Ufanisi huu wa kuhawilisha sifa za mhusika kutoka matini chanzi hadi matini pokezi ni kiashiria kimoja kinachoonyesha kwamba maana inaweza kupitishwa na mawasiliano kuendelezwa kupitia tafsiri. Mfano 79 ulionukuliwa kutoka MMS na MS pia umemsawiri Mkuu wa Wilaya (Meya) kama fisadi.

### **Mfano 80**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya (Kwa Abdulini): Ni nani aliyekufunza jinsi ya kuchuma katika zabuni ile ya daraja ulipoandika bei ya mbao kuwa shilingi 20,000 wakati hazikuwa na thamani ya mia! Nilikusaidia beberu we! (uk 67).

**MS:** Meya (anamkabili abdulini): wewe ni mdhulumaji. Unapata malaki ya fedha kutokana na mkataba wa serikali ambapo wewe hutoa mali mbovu, nawe ukanihonga yadi ishirini za mali hiyo isiyofaa na kutarajia upate medali? (uk 99).

Mfano 80 unadhihirisha kuwa, katika MMS na MS, Mkuu wa Wilaya (Meya) pamoja na mfanyabiashara aliyeitwa Abdulin walikuwa fisadi. Tulidahili kuwa, kwa vile kila mtafsiri hujenga sentensi zake katika akili yake kabla ya kuandika, basi tofauti za kitafsiri katika uhawilishaji wa ujumbe katika (mfano 80) zina misingi yake katika akili za watafsiri. Katika tasnifu hii tulidokeza kwamba, akili ya kila mtafsiri huteua

maneno kwa kutegemea, mazingira ya kulelewa, masuala ya kiutamaduni, kiwango cha umilisi wa lugha na ubunifu wake. Hivyo, huenda watafsiri wawili kama Madumulla na Mwakasaka wasiweze kuunda sentensi zinazofanana kimaana katika mchakato wa tafsiri.

Katika utafiti huu tulihoji kuwa, uhuru wa mtafsiri katika mchakato wa tafsiri ndiyo motisha iliyochochea watafsiri wa MMS na MS katika (mfano 80), kuunda sentensi zinazotofautiana kimaana. Kwa mfano katika MMS (mfano 80), Mkuu wa Wilaya anasema: “Abdulini alichuma katika Zabuni ya ile daraja kwa kuandika bei ya mbao kuwa shilingi 20,000” huku katika tamthilia ya MS, Meya anasema: “Abdulini ni mdhulumaji anayepata malaki ya fedha kutokana na mkataba wa serikali ambapo yeye hutoa mali mbovu na akamhonga Meya yadi ishirini za mali hiyo isiyofaa”. Mkuu wa Wilaya (Meya) pia alikuwa mtu mwenye dharau na sifa hii imeangazwa katika sehemu ifuatayo ya 5.3.1.3.

#### **5.3.1.4 Mwenye Dharau**

Kwa mujibu wa Kamusi Elezi (2016), mtu mwenye dharau ana sifa ya kupuuza mambo na kuyaona kuwa hayana umuhimu. Madharau aghalabu huandamana na kiburi na wale wanaowadharau watu huwa ama ni watu wanaomiliki vyeo vya juu kazini au ni matajiri. Kwa mfano, katika MMS na MS Mkuu wa Wilaya (Meya) amesawiriwa akiwa na sifa ya madharau inavyojitokeza katika mfano 81 ufuatao.

#### **Mfano 81**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya:... Shiii, ninyi! Vistoonovu na Dyerizimoda! Panda huku mara moja! (hatua zinasikika na mara wanaingia askari wawili) Shiii! Shiii! Dubu nyie! (uk 41).

**MS:** Meya: Shhhh! Acheni kelele nyie kenge! Mnaingia hapa kama mkokoteni uliojaa magogo. Shetani awapelekeni wapi? (Uk 61).

Katika tamthilia ya MMS na MS (mfano 81), Mkuu wa Wilaya (Meya) aliwatusi askari kwa kuwa walimpigia makelele Ghlestakov/Hilestakov. Usemi unaojitokeza katika mfano 81, unabainisha namna ambavyo watafsiri wa MMS na MS walivyomsawiri Mkuu wa Wilaya (Meya) kama mtu aliyejawa na kiburi na madharau. Mfano 80, unahusu matumizi ya kihisishi “Shhh!” katika MMS au “Shiii!” katika MS. Tulihoji kuwa aghalabu yule anayedharauliwa hawezi kutumia kihisishi hiki ila yule anayedharau. Aidha, mfano 81 unabainisha kuwa, mtafsiri wa MS ameswahilisha kihisishi hiki kama “Shiii!” kwa kuongeza irabu mwishoni mwake. Kwa upande mwingine, mtafsiri wa MMS hakukitohoa (kukiswahilisha) kihisishi Shhhh! katika tafsiri yake ili kiweze kutamkwa sawa na maneno ya Kiswahili.

Katika tasnifu hii tulihoji kuwa, tofauti zinazorejelewa katika mfano 80 ni za kitafsiri kwa sababu watafsiri walisoma matini chanzi kwa ajili ya kuelewa (kupata ujumbe wake) kisha wakahawilisha ujumbe kwa kuteua msamiati kwa namna kila mmoja wao alivyotaka. Aidha, tabia ya Mkuu wa Wilaya (Meya) ya kuwadharau watu wengine inabainika katika tafsiri za MMS na MS, inavyojitokeza katika mfano 81. Kwa mfano, katika MS (mfano 81), Meya anawatusi polisi kwa kuwaita ‘kenge’ ilhali katika tamthilia ya MMS (mfano 81), Mkuu wa Wilaya aliwatusi askari kwa kuwaita dubu.

Kulingana na kamusi ya TUKI (2013), kenge ni mnyama kama mamba mdogo aishie nchi kavu bali dubu ni mnyama mkubwa wa mwituni mwenye manyoya mengi. Tafsiri zote mbili licha ya kutumia wanyama wa aina tofauti, zimefaulu kudumisha sifa ya mhusika ya kuwadharau wenzake. Tulidahili pia kuwa, tofauti baina ya wanyama waliotajwa katika MMS na MS (mfano 81), inahusiana na tofauti za kimazingira ya kulelewa ya watafsiri ambayo hupelekea watafsiri kuwa na upekee wa



ubunifu wa msamiati katika mchakato wa tafsiri. Isitoshe, Mkuu wa Wilaya (Meya) pia amesawiriwa katika MMS na MS kama mtu mwenye sifa ya kuchanganyikiwa na ndiyo imeelezwa katika sehemu ifuatayo.

### 5.3.1.5 Mwenye Kuchanganyikiwa

Kamusi ya TUKI (2003) inaelezea kwamba, kuchanganyikiwa ni hali ya kisaikolojia inayohusu kuvurugukiwa kwa muungano wa mawazo unaoweza kuathiri utendaji wa mzungumzaji katika diskosi. Tafsiri za MS na MMS zimedhihirisha sifa hii ya kuchanganyikiwa katika maisha ya Meya/Mkuu wa Wilaya katika mfano 82 ufuatao.

#### Mfano 82

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Nenda mitaani na ... hapana usiende. Nenda ukalete ...Yuko wapi askari mwingine? Nilimwambia Prohorovu kuwa hapa. Yuko wapi? ( uk 11)...Wambie walinzi kuleta mitaa na kusafisha fagio- oh, sasa nasema nini? ...Waambie wafagie mitaa..., (uk 12).

**MS:** Meya: Naam, nenda nje na..hapana, ngoja. Usiende. Subiri. Eee kaniitie..Hivi polisi wote wamekwenda wapi? Prohorov yuko wapi? Aliambiwa awepo hapa..(Akimgeukia Sivistunov tena) Nenda uwatafute polisi waliobaki na kuwatuma washike mtaa mmoja kila mmojawao...ah, hivi nasema nini! Wapatie fagio wafagie mitaa, (uk 15 -16).

Katika mfano 82, watafsiri wa MMS na MS walimsawiri Mkuu wa Wilaya (Meya) kama mtu aliyechanganyikiwa. Kwa mfano, katika MMS (mfano 82), Mkuu wa Wilaya anamwambia askari kuwa, Waambie walinzi kuleta mitaa na kusafisha fagio- oh, sasa nasema nini? Waambie wafagie mitaa ilhali katika MS, Meya anamwambia askari kuwa, Nenda uwatafute polisi waliobaki na kuwatuma washike mtaa mmoja kila mmoja wao...ah, hivi nasema nini! Wapatie fagio wafagie mitaa.

Tungo zilizopigiwa mistari zinatofautiana kwa kuwa, katika MMS, Mwakasaka alitafsiri usemi kwa namna ya kukanusha ambapo mhusika anasema ‘nenda’ halafu kwa ghafla anasema ‘usiende’ kisha anatoa agizo ‘nenda ukalete’ na kabla hajamaliza

kishazi kitegemezi hicho, anataka kujua alipo askari mwingine. Hata kabla hajajibiwa, anazalisha miundo mingine miwili isiyokuwa sahihi kimantiki ‘lete mitaa’ na ‘safisha fagio’. Pia, Tulidahili kuwa uteuzi wa vishazi au sentensi uliofanywa na watafsiri wa MMS na MS (mfano 82), ulichangia kuendeleza mnato wa kifasihi kwenye tafsiri husika. Ufanisi huu wa watafsiri unafaa katika kudumisha mvuto wa kazi ya sanaa inayotafsiriwa kimtindo huku sifa za wahusika zikidumishwa. Sehemu ifuatayo ya 5.3.2 inashughulikia sifa za Ghlestakovu/Hilestakov zinavyojitokeza katika MMS na MS.

### **5.3.2 Ghlestakovu/Hilestakov**

Ghlestakovu ni jina la mhusika katika MMS, na mhusika huyo ni Hilestakov katika MS. Katika tamthilia za MMS na MS, Ghlestakovu/Hilestakov amesawiriwa kama kijana mdogo na mfanyikazi wa serikali huko Petersbag. Ghlestakovu/Hilestakov alipangisha chumba katika hoteli fulani humo wilayani baada ya kufilisika akiwa safarini na alidhaniwa kuwa mgeni (Mkaguzi wa serikali) aliyetarajiwa wilayani. Sifa za Ghlestakovu/Hilestakov zimeelezwa katika sehemu inayofuata na tumeanza na sifa ya kuwa mpenda anasa.

#### **5.3.2.1 Mpenda Anasa**

Kulingana na Kamusi ya TUKI (2013), anasa ni mambo au hali ya kupenda starehe na raha nyingi. Katika MMS na MS, Ghlestakovu/Hilestakov amesawiriwa kuwa na sifa ya mtu anayependa anasa. Sifa hiyo imebainishwa katika mifano ifuatayo na tulianza na mfano 83.

#### **Mfano 83**

**MMS:** Ghlestakovu: (kwa Hakimu) Sikiliza, nitazichukuwa kama mkopo...Nitazituma kwako nifikapo nyumbani...(Kwa M/Elimu) ...Unajua jambo la kipumbavu limenitokea nikiwa safarini kuja huku...

Unadhani unaweza kunikopesha tuseme shilingi 400? Nitazirudisha mara tu nifikapo nyumbani. (Uk 47- 48).

**MS:** Hilestakov: (Kwa Jaji) Tazama Jaji, unaweza kuniazima fedha hii...kwa muda mfupi? ...Nitakurejeshea mara nifikapo nyumbani. (Kwa Mkuu wa Posta) ...Unajua jambo la ajabu sana lilinitokea jana. ... Je, unaweza kuniazima rubuli kama mia tatu hivi? (uk 66 -68-72).

Katika tamthilia za MMS na MS (mfano 83), Ghlestakovu/Hlestakov amesawiriwa kama mhusika anayependa anasa. Kwa mfano, katika MMS (mfano 83), Ghlestakov anamwambia Bw. Hakimu kwamba, Unajua jambo la kipumbavu limenitokea nikiwa safarini kuja huku ilhali katika MS, Hilestakov anamwambia Jaji kuwa, Unajua jambo la ajabu sana lilinitokea jana.

Kutokana na tungo zilizopigiwa mistari (mfano 83), tumegundua kwamba, Ghlestakovu/Hilestakov hakutaka kueleza waziwazi kwamba alizivuja pesa zake katika shughuli za anasa kwa kuwa alijuta kujiingiza katika anasa na baadaye akafilisika. Kwa hivyo, katika MMS (mfano 83), anakiita kitendo cha anasa jambo la kipumbavu na katika MS (mfano 83), anakiita kitendo hicho cha anasa jambo la ajabu sana. Kifungu: jambo la kipumbavu hakiifanani kimaana na kifungu: jambo la ajabu sana.

Katika tamthilia za MMS/MS, Ghlestakovu/Hilestakov aliwaomba pesa viongozi wa wilaya akidai kwamba atazirejesha atakapofika nyumbani kwao. Kwa mfano, katika MMS (mfano 83) Ghlestakovu alimwambia Hakimu, Unadhani unaweza kunikopesha tuseme shilingi 400? Nitazirudisha mara tu nifikapo nyumbani. Katika MS Hilestakov anamwambia Jaji, Je, unaweza kuniazima rubuli kama mia tatu hivi? Swali linaloibuka ni je, shilingi mia nne ni sawa kiidadi na rubuli mia tatu? Tulidahili kuwa, tofauti hiyo inayotokea katika idadi ya pesa alizoazimwa Ghlestakovu/Hilestakov inasababishwa na uhuru walio nao watafsiri katika mchakato wa tafsiri.

Tumegundua kuwa, mtafsiri wa MMS (mfano 83), alihawilisha sifa ya Ghlestakovu ya kupenda anasa huku akitumia msamiati wa Afrika Mashariki unaohusiana na pesa. Kwa mfano, badala ya kutumia neno rubuli akatumia neno ‘shilingi’. Kwa upande mwingine, mtafsiri wa MS (mfano 83), alitumia neno ‘rubuli’ ambalo ni neno lilitoholewa. Tulihoji kuwa, msomaji wa tafsiri ya MS (mfano 83), asiyejua kwamba neno hili rubuli lilitoholewa atakuwa na tatizo la kubainisha maana yake na hali kadhalika kusimbua sifa ya Hilestakov ya kupenda anasa inavyoangaziwa katika mfano 83. Kisa kingine katika MMS na MS kinachobainisha tabia ya Ghlestakovu/Hilestakov ya kupenda anasa kimejitokeza katika mfano 84 ufuatao.

#### **Mfano 84**

**MMS:** Ghlestakovu: Lakini niambieni, hamna njia zozote za kupotezea muda? Kiburudisho chochote? Hamkusanyiki kamwe na kucheza kamali? (uk 35).

**MS:** Hilestakov: Hebu niambie, hakuna burudani katika mji huu. Yaani, sehemu ambazo mtu anaweza akapigapiga karata hivi au kitu cha namna hiyo. (uk 50).

Katika MMS na MS (mfano 84), Glestakov/Hilestakov amethibitisha kuwa, alipenda starehe za kujiburidisha. Kwa mfano, katika MMS, Ghlestakovu anasema: hamna njia zozote za kupotezea muda? Kiburudisho chochote? Hamkusanyiki kamwe na kucheza kamali? ilhali katika MS, Hilestakov anasema hakuna burudani katika mji huu? na sehemu ambazo mtu anaweza akapigapiga karata hivi au kitu cha namna hiyo. Tungo zilizopigiwa mistari zinatofautiana kimaana kwa kuwa watafsiri wa MMS na MS (mfano 84), wametumia uhuru walio nao katika mchakato wa tafsiri kuibuka na maneno, vishazi na hata sentensi ambazo hazifanani.

Tulidahili kuwa mtafsiri wa MS (mfano 84), ametumia lugha inayoeleweka barabara kuliko mtafsiri wa MMS. Katika MS, (mfano 84), Hilestakov anauliza: hakuna

burudani huku katika mji huu? inaeleweka barabara. Katika MMS (mfano 84), Ghlestakovu anauliza: hamna njia zozote za kupotezea muda?. Tulihoji kuwa mtu yeyote asiyelewa sarufi na utamaduni wa Kiswahili atahitaji maelezo ya kina kuhusiana na maneno: kupoteza muda. Glestakov/Hilestakov pia amesawiriwa kama msomi katika MMS na MS na madai hayo yanajitokeza katika sehemu ifuatayo.

### 5.3.2.2 Msomi

Kwa mujibu wa utafiti huu, msomi ni mtu mwenye elimu ya kumwezesha kusoma na kuandika. Katika MMS na MS, Glestakov/Hilestakov amesawiriwa kama mtu ambaye hupenda kusoma na kuandika mashairi. Sifa ya Glestakov/Hilestakov ya kuwa msomi imedhihirika katika mfano 85 ufuatao.

### Mfano 85

**MMS:** Ghlestakovu: Ndiyo, kuna giza. Lakini tajiri anakataa kunipa mishumaa. Kila mara nitakapo kufanya lolote, kusoma kidogo au ninaposkia wito wa kuandika, siwezi; kuna giza mno, giza mno. (uk 25).

**MS:** Hilestakov: Huyu tajiri mlaanifu hanipi hata mshumaa wa kusomea. Kuna wakati ambapo mtu hujiskia ustaarabu-kusoma insha moja au mbili, kusanifu kijishairi, lakini hapa haiwezekani, ni giza mno. (uk 37).

Katika mfano 85, Ghlestakov/Hilestakov amesawiriwa katika tamthilia za MMS na MS, kama msomi. Kwa mfano, Ghlestakov analalamika akisema: Ndiyo, kuna giza. Lakini tajiri anakataa kunipa mishumaa ilhali katika MS, Hilestakov anasema, Huyu tajiri mlaanifu hanipi hata mshumaa wa kusomea. Tumegundua kwamba katika MMS (mfano 85), Ghlestakov hakutumia matusi, badala yake anasema kwamba tajiri amekataa kumpa mishumaa. Kwa upande mwingine, katika MS (mfano 85), Hilestakov anasema kwamba, tajiri mlaanifu amekataa kumpa mshumaa.

Katika tafsiri za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*, (mfano 85), Ghlestakovu/Hilestakov anapohitaji kusoma inakuwa vigumu kwa sababu ya giza lakini watafsiri hao walitofautiana kwa namna walivyohawilisha ujumbe huo. Kwa mfano, katika MMS (mfano 85), Ghlestakov anasema kuwa, Kila mara nitakapo kufanya lolote, kusoma kidogo au ninaposkia wito wa kuandika bali katika tamthilia ya MS (mfano 84), Hilestakov anasema kuwa, Kuna wakati ambapo mtu hujiskia ustaarabu-kusoma insha moja au mbili, kusanifu kijishairi. Watafsiri wa MMS na MS pia wamemsawiri Glestakov/Hilestakov kama asherati ilivyobainika katika sehemu ifuatayo ya 5.3.2.1.

### 5.3.2.3 Asherati

Kwa mujibu wa Kamusi Elezi (2016), asherati ni mtu mwenye tabia ya kupenda kuzini au uzinifu. Sifa ya uasherati ya Glestakov/Hilestakov inajitokeza katika mifano ifuatayo. Tumeanza kwa kuangazia mfano 86 ufuatao.

### Mfano 86

**MMS:** Ghlestakovu: (Kwa woga) ...Na kama atanifanya nipelekwe jela? na kwa kweli nimekuwa nikionyesha mitindo na kufanya mahaba na binti ya mfanya biashara hapo jirani. (uk 21).

**MS:** Hilestakov: (anaogopa) Nini? Haiwezekani!.. Hapana! Hapana! Siwezi kwenda jela. Nisije nikaonekana na maafisa, au yule binti mzuri wa mchuuzi wa mbegu, binti ambaye nimekuwa nikitembea naye. (Uk 32).

Watafsiri wa MMS na MS katika (mfano 86), walimsawiri Glestakov/Hilestakov kama asherati kwa kuwa alipenda kuwa na uhusiano wa mapenzi ya kiholela na wanawake pasi na kuhalalisha uhusiano huo katika ndoa. Kwa mfano, katika MMS (mfano 86), Hilestakov anakiri kuwa, amekuwa akifanya mahaba na binti wa mfanya biashara bali katika tamthilia ya MS (mfano 86), Ghlestakov anakiri kwamba, amekuwa akitembea na binti wa mchuuzi wa mbegu.

Katika tasnifu hii tulidahili kwamba, mtafsiri wa MS alitaka kuondoa makali kwa kusema: kutembea na binti wa mchuuzi wa mbegu badala ya kusema kufanya mahaba na binti wa mchuuzi wa mbegu kwa sababu za masuala ya kitamaduni. Kifungu: kutembea na binti wa mchuuzi hakieleweki wazi wazi kimaana kama ilivyo kifungu: kufanya mahaba na binti wa mfanyabiashara. Tulihoji pia kuwa, mchakato wa tafsiri huathiriwa na masuala ya kiutamaduni. Kwa hivyo itakuwa vigumu kwa mtu asiyelewa utamaduni wa Kiafrika, kuelewa maana ya kifungu, kutembea na binti wa mchuuzi wa mbegu. Mfano 87 ufuatao, unabainisha tabia ya uasherati ya Ghlestakov/Hilestakov ilivyojitokeza katika MMS na MS.

### **Mfano 87**

**MMS:** Ghlestakov: (kwa Yosif) ...Na binti anaonekana mzuri kabisa na nadhani mama mwenyewe yuko tayari kwa lolote. (uk 46).

**MS:** Hilestakov: ..Nipo hapa ...nikiwatongoza mke wake na binti yake, wote kwa wakati mmoja! Sijaamua nianze kwenda na yupi-huenda mke wake ni mzuri zaidi, anaelekea kuwa yuko tayari kwa lolote! (Uk 109).

Mfano 87 ni nukuu ambapo Ghlestakov/Hilestakov amesawiriwa kama asherati katika MMS na MS kwa kuwatongoza Anna na Marya ambao ni mama na bintiye mtawalia. Kwa mfano katika tamthilia ya MMS (mfano 87), Ghlestakov anasema kwamba: binti anaonekana mzuri kabisa na anadhani mama yuko tayari kwa lolote, bali katika tamthilia ya MS (mfano 87), Hilestakov anakiri kwamba; anawatongoza mke na binti wa Meya kwa pamoja, na hajaamua aende na yupi kwanza.

Katika tasnifu hii tulidahili kwamba, ujumbe katika MS (mfano 87) ambapo Hilestakov anasema kwamba: anamtongoza mama na bintiye, umejitokeza kwa uwazi na wa kueleweka barabara kuliko ule wa MMS (mfano 87), ambapo Ghlestakov anasema binti anaonekana mzuri kabisa na anadhani mama yuko tayari kwa lolote.

Maelezo ya kumsawiri Ghlestakovu/Hilestakov kama mpenda anasa katika MMS na MS yamejitokeza katika mfano 88 ufuatao.

### **Mfano 88**

**MMS:** Ghlestakovu (pembeni): Na yeye pia kidosho hasa; si mbaya hata kidogo! (kipiga goti) Bibie, unaona, penzi linanichoma moyo! (Uk 60).

**MS:** Hilestakov (pembeni): Na yeye anavutia si haba-mm, mm, si mbaya hata kidogo... (anaelekea kwake kwa maoni). Bibie, huoni ninavyokufa kwa mapenzi! (Uk 88).

Watafsiri wa MMS na MS, wamemsawiri Ghlestakov/Hilestakov kama asherati inavyojitokeza katika mfano 88, alipotaka kuwa na uhusiano wa kimapenzi ya kiholela na Anna/Ann bali alielewa kuwa alikuwa mke wa Mkuu wa Wilaya (Meya). Kwa mfano, katika MMS (mfano 88), Ghlestakov anasema kuwa, na yeye pia kidosho hasa, bali katika MS, Hilestakov anasema kuwa, na yeye anavutia si haba-mm.

Kishazi tegemezi katika MMS na MS (mfano 88): Na yeye inamrejelea mhusika mwingine na katika tasnifu hii, tuanaelewa kwamba huyo aliyerejelewa alikuwa ni Marya/Maria ambaye ni binti yake Anna/Ann. Yaani, anachomaanisha Ghlestakov/Hilestakov ni kwamba kwake yeye, Anna/Ann na Maria/Marya wote ni warembo na wanavutia sana. Pia, katika MMS (mfano 88), Ghlestakovu alimpigia magoti Maria na kumwambia, Bibie, unaona, penzi linanichoma moyo bali katika MS,

Hilestakov alimpigia magoti Marya na kumwambia: Bibie, huoni ninavyokufa kwa mapenzi. Kimaana, Vifungu hivi: Penzi linanichoma moyo na ninakufa kwa mapenzi zinatofautiana. Aidha, Ghlestakov/Hilestakov amesawiriwa katika tamthilia za MMS na MS kama msaliti inavyojitokeza katika sehemu ifuatayo ya 5.3.2.7.



### 5.3.2.4 Msaliti

Kulingana na TUKI (2013), usaliti ni hali ya mtu kutoa mipango ya siri ya wenzake kwa watu wengine ili wenzake wakamatwe. Watafsiri wa MMS na MS walimsawiri Glestakov/Hilestakov kama msaliti na sifa hiyo ya usaliti inajitokeza katika mifano ya 88 na 89 na tumeanza kwa kushughulikia mfano 89 ufuatao.

#### Mfano 89

**MMS:** Mkuu wa wilaya: (kwa wafanya biashara) Oh, acha kufanya ghasia sasa. Mnajua kuwa yule mkaguzi mliyemkimbilia mkiomboleza anatarajia kumwoa binti yangu? Mnasemaje sasa? (Uk 66).

**MS:** Meya: (ameudhika) Sijali kuhusu maneno sasa hivi! (Kwa wenye maduka) Mlijuwa kwamba yule Mkaguzi wa Serikali mliyempelekea malalamiko yenu atamwoa binti yangu? Mlijua hilo? (Uk 99).

Mfano 89 ulionukuliwa kutoka tamthilia za MMS na MS umethibitisha kuwa Glestakov/Hilestakov aliwasaliti watu waliotoa malalamishi yao dhidi ya Mkuu wa Wilaya (Meya). Kwa mfano, katika MMS (mfano 89), Mkuu wa Wilaya anasema kuwa, Mnajua kuwa yule mkaguzi mliyemkimbilia mkiomboleza anatarajia kumwoa binti yangu ilhali katika MS, Meya anasema kuwa, Mlijuwa kwamba yule Mkaguzi wa Serikali mliyempelekea malalamiko yenu atamwoa binti yangu? Sentensi zilizopigiwa mistari zinathibitisha kwamba Mkuu wa Wilaya (Meya) alikuwa amepata habari kutoka kwa Glestakov/Hilestakov ya kuwa kuna watu waliotoa malalamishi dhidi yake.

Viungu hivyo; mliyemkimbilia mkiomboleza na mliyempelekea malalamiko havifanani kwa sababu maana ya kitenzi: kuomboleza sio sawa na maana ya kitenzi: kulalamika. Katika tasnifu hii tulidahili kwamba, tofauti ya kimaana kati ya vifungu vilivyopigiwa mistari zinasababishwa na uhuru alio nao mtafsiri kwa kuwa kila mtafsiri ana upekee wake katika kufasiri na kuhawilisha ujumbe kutoka matini chanzi

hadi matini pokezi. Mfano 90 ufuatao pia unadhihirisha sifa ya Ghlestakovu/Hilestakov ya kuwa msaliti inavyoangaziwa katika tamthilia za MMS na MS.

### **Mfano 90**

**MMS:** Ghlestakovu: Hilo si kitu. Kuolewa tu ni nini ukilinganisha na penzi la milele? Tutakimbilia mbali kwenye bonde zuri lililo na kivuli tulivu, karibu na kijito safi. Naomba mkono wako. (Uk 60).

**MS:** Hilestakov: Ni kweli inawezekana, ewe bibie mpendwa! Tutaruka pamoja, mkono kwa mkono, hadi kwenye kijito kibubujikacho... mkono wako, tafadhali mkono wako! (uk 89).

Katika MMS na MS (mfano 90), Ghlestakov/Hilestakov amesawiriwa kama msaliti alipotaka kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mke wa Mkuu wa Wilaya (Meya). Ghlestakov/Hilestakov alipofilisika akiwa safarini, alipokelewa vizuri na Mkuu wa Wilaya (Meya), na badala ya kumshukuru kwa kumkaribisha alitaka kumnyemelea kimapenzi mke wake. Kwa mfano, katika tamthilia ya MMS (mfano 90), Ghlestakov anamtongoza Anna kwa kumwambia kuwa, tutakimbilia mbali kwenye bonde zuri lililo na kivuli tulivu, karibu na kijito safi.

Kwa upande mwingine, katika MS (mfano 90), Hilestakov anamtongoza Ann kwa kumwambia kuwa, Tutaruka pamoja, hadi kwenye kijito kibubujikacho. Tulihoji kuwa, hali ya Ghlestakov/Hilestakov ya kumtaka kimapenzi mke wa Mkuu wa Wilaya (Meya) ni usaliti. Aidha, utungo katika MMS (mfano 90), bonde lililo na kivuli tulivu sio sinonimi ya utungo katika MS (mfano 90), kijito kibubujikacho. Kwa hivyo, tulidahili kwamba, tofauti hizo katika matini tafsiri za MMS na MS (mfano 90), zimesababishwa na athari za mazingira ya kulelewa kwa watafsiri hao (Mwakasaka na Madumulla). Watafsiri wa MMS na MS pia wamemsawiri

Hilestakov/Ghlestakov kama mtovu wa nidhamu na tumeangaza sifa hiyo katika sehemu ifuatayo.

### 5.3.2.5 Mtovu wa Nidhamu

Katika MMS na MS, Hilestakov/Ghlestakov amesawiriwa kama mtu asiye na nidhamu, hasa anapomtusi babake inavyojitokeza katika mfano 91 ufuatao.

#### Mfano 91

**MMS:** Ghlestakov: Kwa kweli sijui. Unajua, baba yangu ni mpumbavu na mkaidi kama pande la gogo. Lakini nitamweleza ukweli, ...lakini mimi siwezi kuishi mbali na Pitasbag. (uk 24).

**MS:** Hilestakov: Kwa kweli sijui. Baba yangu ni mjinga kama punda, na ukaidi wake hali kadhalika. Anaweza kusema atakalo. Lakini siwezi kuishi mahali pengine isipokuwa Petersburg. (uk 36).

Watafsiri wa MMS na MS katika mfano 91, wamemsawiri Glestakov/Hilestakov kama mhusika asiye na nidhamu alipomtusi babake. Kwa mfano, katika MMS (mfano 91), Ghlestakov anasema kuwa, baba yangu ni mpumbavu na mkaidi kama pande la gogo lakini katika MS (mfano 91) Hilestakov anasema, baba yangu ni mjinga kama punda na ukaidi wake hali kadhalika. Katika tasnifu hii tulidahili kuwa, licha ya kwamba watafsiri wa MMS na MS walitumia tashbihi katika mfano 91, kuna tofauti za kimaana katika tungo zilizopigiwa mistari. Kwa mfano, kifungu katika MMS: mpumbavu kama pande la gogo sio kisawe cha kifungu katika MS: mjinga kama punda. Tulidahili pia kwamba, tofauti katika uhawilishaji wa ujumbe baina ya MMS na MS (mfano 91), imeibuka kwa kuwa watafsiri wana tajriba tofauti katika maisha.

Mwakasaka alitafsiri tamthilia ya MMS miaka ishirini kabla ya Madumulla kutafsiri tamthilia ya MS. Tulihoji kuwa, ingawa miaka ishirini ni muda mrefu sana ambapo kuna uwezekano wa mabadiliko katika matumizi ya lugha lakini kifungu: mpumbavu kama pande la gogo hakiwezi kuwa ksawe cha mjinga kama punda. Aidha, watafsiri

katika MMS na MS walimsawiri Ghlestakov/Hilestakov kama mhusika mwenye sifa ya afisa asiyewajibikia kazi yake na tabia hiyo inajitokeza katika sehemu ifuatayo ya 5.3.2.6.

### 5.3.2.6 Asiyewajibika

Watafsiri wa MMS na MS wamemsawiri Ghlestakovu/Hilestakov kama mtu mzembe asiyependa kuwajibikia majukumu yake ilivyojitokeza katika mfano 92 ufuatao.

#### Mfano 92

**MMS:** Ghlestakovu: Ahaa, shamba! ...Na mimi napita katika ofisi nyingine kuwaeleza wafanye nini. Kuna mtu mmoja ambaye hafanyi lingine ila tu kuandika barua zangu siku nzima. (Uk 36).

**MS:** Hilestakov: Na shambani nako kuna uzuri wake.... nakwenda ofisini dakika chache, natoa maelekezo na kumwacha karani mkongwe akiandika andika mezani pake. (Uk 52).

Katika tamthilia za MMS na MS (mfano 92), Ghlestakovu/Hilestakov amesawiriwa kama mtu asiyewajibika majukumu yake. Kwa mfano, katika MMS (mfano 92), Ghlestakov anamwambia Anna/Ann kuwa, Na mimi napita katika ofisi nyingine kuwaeleza wafanye nini, na katika MS (mfano 92), Hilestakov anasema kuwa, nakwenda ofisini dakika chache. Utungo; mimi napita katika ofisi nyingine kuwaeleza wafanye nini inaeleweka barabara kuliko utungo; nakwenda ofisini dakika chache, kwa kuwa, Hilestakov hajasema ameenda ofisini dakika chache kufanya nini.

Katika MMS, Ghlestakovu anasema kuwa, Kuna mtu mmoja ambaye hafanyi lingine ila tu kuandika barua zangu siku nzima na katika MS (mfano 92), Hilestakov anasema kuwa, natoa maelekezo na kumwacha karani mkongwe akiandika andika mezani pake. Tumegungua kuwa katika MMS, (mfano 92), maneno: mtu mmoja sio sinonimia ya maneno katika MS, (mfano 92): karani mkongwe. Maneno hayo: mtu mmoja yanawakilisha mtu wa rika la makamo au kijana tofauti na maneno: karani

mkongwe. Aidha, tungo katika tamthilia ya MMS (mfano 92): hafanyi lingine ila tu kuandika barua zangu siku nzima ni tofauti kimaana na tungo katika MS (mfano 92): akiandika andika mezani pake. Ghlestakovu/Hilestakov ni mhusika mwenye madharau na tabia hiyo imeelezwa katika sehemu ya 5.3.2.7 inavyojitokeza katika MMS na MS.

### 5.3.2.7 Mwenye Madharau

Ghlestakovu/Hilestakov amesawiriwa katika tamthilia za MMS na MS kama mhusika mwenye madharau kwa wenzake. Ifuatayo ni mifano inayodhibitisha ujumbe wa madharau na tumeanza na mfano 93.

#### Mfano 93

**MMS:** Ghlestakovu: ...Nasikitika Joakim hakutaka nikodeshe gari lake. Lakini wao ni washamba na hawangeelewa kitu. (uk 18-19).

**MS:** Hilestakov: ...Nasikitika kwamba Osipu alinizuia nisikodi gari lile, kwani ingekuwa ni fahari ilioje kuingia jijini kwangu .Je, familia za kichochole mpo?" (uk 27–28)

Katika mfano 93, watafsiri wa MMS na MS walifaulu kumsawiri Ghlestakovu/Hilestakov kama mtu mwenye madharau. Kwa mfano, katika MMS (mfano 93), Ghelestakov anasema; washamba wasioelewa kitu akiwalenga watu maskini wa huko kwao na katika MS (mfano 93) Hilestakov anasema: Je, familia za kichochole mpo?. Vifungu vilivyopigiwa mstari vinadhihirisha kuwa mzungumzaji ni mtu mwenye kiburi na madharau.

Kulingana na utafiti huu, tulihoji kuwa, watafsiri wa MMS na MS (mfano 93), waliteua maneno tofauti kwa kuwa wana uhuru wa kufanya hivyo katika mchakato wa tafsiri. Aidha, tulidahili kuwa, neno ‘utajiri’ halihusiani moja kwa moja na sifa ya kuwa na kiburi na dharau walakini, kisdafa, watu ambao ni matajiri, aghalabu huwa

na madharau, kiburi au majisifu kama alivyobainisha Ghlestakovu/Hilestakov katika MMS na MS (mfano 93). Mfano 94 ufuatao, pia ni nukuu kutoka MMS na MS ambayo inamwangaza Ghlestakovu/Hilestakov kama mhusika mwenye madharau.

#### **Mfano 94**

**MMS:** Ghlestakovu: Hayawani we! ...Hi ni supu ya aina gani? Umeweka tu maji machafu katika bakuli. Hakuna ladha; inanuka uvundo....Shetani tu ndiye ajuaye ni nini, lakini sio kuku. ...(uk 20).

**MS:** Hilestakovu: .... Unaiita hii supu? Walichofanya ni kutia tu maji ya moto katika sufuria chafu! Haina ladha hata kidogo! ...Ni Mungu tu anajua lakini hii si nyama. ... Labda wamepika kishoka cha kuchanjia nyama kwa bahati mbaya. (Uk 31).

Watafsiri wa MMS na MS katika mfano 94 walimsawiri Ghlestakov/Hilestakov kama mhusika mwenye madharau alipokidharau chakula alichopewa akiwa hotelini. Kwa mfano, katika MMS, Ghlestakov anamkemea mpishi kwa kusema kuwa, Umeweka tu maji machafu katika bakuli. Hakuna ladha; inanuka uvundo. Ghlestakov alikiita chakula (supu na kuku) ambacho alikuwa amepewa, akasema kuwa, supu ni kama maji machafu yaliyowekwa kwenye bakuli na nyama ni kama gome la mti mkavu.

Kwa upande mwingine katika tamthilia ya MS (mfano 94), Hilestakov alimkemea mhudumu wa hoteli kwa kusema kuwa, Umeweka maji ya moto katika sufuria chafu! Haina ladha hata kidogo! ya nyama na tena badala ya nyama ni pande la kishoka cha kuchinjia nyama. Kimaana, tungo zilizopigiwa mstari zinatofautiana kwa kuwa, katika MMS, Ghlestakovu anamkashifu mpishi kwamba aliyaweka maji chafu kwenye sufuria badala ya supu ya kuku na katika tamthilia ya MS (mfano 94), Hilestakov alimkashifu mhudumu wa hoteli kwamba aliweka maji moto katika sufuria chafu badala ya supu ya kuku.

Katika tasnifu hii tulidahili kuwa, tofauti kati ya uwasilishaji wa ujumbe katika MMS na MS (mfano 94) imeibuka kwa kuwa katika shughuli za tafsiri, kila mtafsiri ana upekee wake katika uteuzi wa msamiati na uhawilishaji wa ujumbe kutoka matini chanzi hadi matini pokezi. Watafsiri wa MMS na MS pia walimsawiri Ghlestakov/Hilestakov kama mhusika mwenye madharau inavyojitokeza katika mfano 95 ufuatao.

### **Mfano 95**

**MMS:** Ghlestakov (kwa mpishi): Hayawani! Hakuna haja ya yote hayo. Deni langu ni ngapi, jumla? (Uk 26).

**MS:** Hilestakov (kwa mhudumu): Mjinga we! sihitaji orodha ya vitu nilivyovitumia, ninataka kujua ninadaiwa kiasi gani! (Uk 38).

Mfano 95 unadhihirisha kwamba Ghlestakovu/Hilestakov ana madharau anapomtusi mpishi/mhudumu inavyojitokeza katika MMS na MS. Kwa mfano katika MMS (mfano 95), Ghlestakov anamwambia mpishi: Hayawani! Hakuna haja ya yote hayo ilhali katika tamthilia ya MS (mfano 95), Hilestakov anamwambia mhudumu: Mjinga we! sihitaji orodha ya vitu nilivyovitumia. Hivyo, tulihoji kuwa tungo zilizopigiwa mstari hazifanani kimaana kwa sababu, neno hayawani lilotumiwa katika tamthilia ya MMS (mfano wa 95), sio sinonimu ya neno mjinga lilotumiwa katika MS (mfano 95).

Katika MMS, kifungu: Hakuna haja ya yote hayo, ni tofauti kimaana na kifungu katika MS (mfano 95): sihitaji orodha ya vitu nilivyovitumia. Aidha, kutokana na vifungu vilivyopigiwa mistari, tulihoji kuwa maelezo ya mtafsiri wa MS yanaeleweka barabara kuliko maelezo ya mtafsiri wa MMS. Mfano 96 pia ni nukuu kutoka tamthilia za MMS na MS inayobainisha sifa ya Ghlestakovu/Hilestakov ya kuwa mhusika mwenye madharau.

**Mfano 96**

**MMS:** Ghlestakov: Utathubutuje, we nyamaume! (uk 17).

**MS:** Hilestakov: Nyamaza, mjinga we! Inatosha! Nenda ukawaambie waniletee chakula. (uk 25).

Katika MMS na MS (mfano 96), Ghlestakov/Hilestakov amesawiriwa kama mhusika mwenye madharau alipomtusi Yosif/Osipu. Tulihoji kuwa, kimaana, maneno nyamaume na mjinga yaliyopigiwa mistari katika mfano 96, hayafanani. Kwa mfano, neno hili: nyamaume lililotumika katika tamthilia ya MMS (mfano 96) lina maana ya mtu mwenye sifa ya kutokuwa na haya au aibu. Kwa upande mwengine, neno: mjinga lilivyotumiwa katika MS (mfano 96), lina maana ya mtu asiyejua jambo au kitu chochote.

Tulihoji pia, kuwa tofauti ya uhawilishaji wa ujumbe baina ya tafsiri za MMS na MS, (mfano 96) imeibuka kwa kuwa, katika shughuli za tafsiri, kila mtafsiri ana upekee wake wa kufasiri na kutafsiri ujumbe uliopo katika matini chanzi kulingana na tajriba yake katika maisha. Mfano 97 ufuatao pia unaangaza tabia ya Ghlestakov/Hilestakov ya kuwa mtu mwenye madharau ilivyobainishwa katika MMS na MS.

**Mfano 97**

**MMS:** Bw Posta: (akiisoma barua) ...Kwanza, kuna huyu Mkuu wa Wilaya: lakini ni mpumbavu kama punda kihongwe!” ..Korob: “Bwana Huruma, Zemlyanika, amefanana kabisa na nguruwe jike aliyevaa tunga.” “Mratibu wa elimu ananuka vitunguu sumu kila sehemu.”... (Uk 74).

**MS:** Mkuu wa Posta: (akiisoma barua)... Kwanza, kuna Meya. Jinsi anavyoonekana ni pumbavu kama fisi-si mwerevu sana...” Mkuu wa Posta ni nusu kipofu, ana akili nusu, ijapokuwa ni mwepesi wa kufungua fungua barua anapotaka kufanya hivyo...” Korobkin: “Kamishina wa misaada, Zemlyanika, yuko kama-nguruwe aliyevaa wigi.” (uk 109-112).



Mfano 97 ulionukuliwa kutoka katika tamthilia za MMS na MS, unathibitisha kwamba, Ghlestakov/Hilestakov aliwadharau viongozi waliompokea alipomwandikia rafiki yake barua ya kuwatusi viongozi hao. Kwa mfano, katika tamthilia ya MMS, (mfano 97), Ghlestakov anamtusi mkuu wa wilaya kuwa; ni mpumbavu kama punda kihongwe ilhali katika MS (mfano 97), Hilestakov anamtusi Meya kuwa; ni pumbavu kama fisi-si mwerevu sana. Ingawa watafsiri wa MMS na MS (mfano 97) walithibitisha kwamba Ghlestakov/Hilestakov aliwatusi viongozi wa Wilaya kwenye barua aliyomwandikia rafiki yake, lakini je, kifungu: mpumbavu kama punda kihongwe ni sawa kimaana na kifungu: pumbavu kama fisi-si?

Tulihoji pia kwamba, ingawa watafsiri wa MMS na MS (mfano 97) walitumia wanyama katika kuhawilisha ujumbe wa madharau lakini punda na fisi ni wanyama tofauti. Isitoshe, katika tamthilia ya MMS, (mfano 97), Ghlestakov anasema; Bw. Huruma amefanana kabisa na nguruwe jike aliyevaa tunga ilhali katika MS (mfano 96), Hilestakov anaeleza kuwa, Mkuu wa Posta yuko kama-nguruwe aliyevaa wigi.

Kutokana na mfano 97 tulihoji kwamba, kuna vifungu ambavyo vimetumiwa na mtafsiri wa MMS na havipo katika MS. Kwa mfano, katika MMS (mfano 97), Ghlestakov anasema kuwa; Mkuu wa Posta ni nusu kipofu, ana akili nusu, ijapokuwa ni mwepesi wa kufungua fungua barua anapotaka kufanya hivyo, kifungu hiki hakipo katika tamthilia ya MS (mfano 97). Pia, katika MMS, Ghlestakov anasema kuwa, Mratibu wa elimu ananuka vitunguu sumu kila sehemu, kifungu hiki hakijazungumziwa katika MS.

Tulidahili kuwa tofauti za kimaana huzuka kwa sababu ya uhuru wa mtafsiri ambaye katika mchakato wa tafsiri ana uwezo wa kuibuka na kazi tofauti kabisa na ya msanii wa matini chanzi kwa minajili ya kutaka kuwatosheleza wasomaji wa lugha lengwa.

Mfano 98 ufuatao unabainisha sifa ya Ghlestakov/Hilestakov ya kuwa mwenye madharau inavyojitokeza katika MMS na MS.

### **Mfano 98**

**MMS:** Ghlestakovu: ...Inaelekea kuwa wananichukulia kuwa mtu mkubwa sana Serikalini. Kwa kweli hawa watu wapumbavu sana! Bila shaka niliwadanganya vizuri sana jana. (uk 52).

**MS:** Hilestakov:.. Wote hawa inaelekea wanadhani kuwa mimi ni afisa fulani wa serikali. Nadhani niliwavuna sana jana. Ni kikosi cha majuha mno. (uk 76).

Mfano 98, ulionukuliwa kutoka tamthilia za MMS na MS, umethibitisha kuwa Ghlestakov/Hilestakov amesawiriwa kama mhusika mwenye madharau na asiye na shukurani. Kwa mfano, katika MMS (mfano 98), Ghlestakov anasema kuwa, Kwa kweli hawa watu wapumbavu sana! Bila shaka niliwadanganya vizuri sana jana bali katika MS, Hilestakov anasema kuwa, nadhani niliwavuna sana jana. Ni kikosi cha majuha mno. Kimaana, tungo zilizopigiwa mistari hazifanani kwa kuwa, kitenzi kuvuna sio sinonimu ya kitenzi kudanganya.

Katika tasnifu hii tulihoji kwamba, tofauti katika uhawilishaji wa tungo hizo zilizopigiwa mistari, (mfano 98), iliibuka kwa sababu tamthilia ya MMS (mfano 98), ilitafsiriwa miaka ishirini kabla ya tamthilia ya MS. Kipindi cha miaka ishirini ni muda mrefu sana ambapo kuna uwezekano wa kuwepo na mabadiliko katika matumizi ya lugha. Bwana Hakim/Jaji pia ni mhusika katika tamthilia za MMS na MS ambaye ameshughulikiwa katika sehemu ya 5.3.4 ifuatayo.

### **5.3.4 Bwana Hakim/Jaji**

Katika MMS, mhusika anayeitwa Bw. Hakim ndiye Jaji katika MS. Bw. Hakim/Jaji ni miongoni mwa maafisa wakuu serikalini na ana mtumishi na karani wake.

Zifuatazo ni sifa za Bw. Hakimu/Jaji zilivyojitokeza katika MMS na MS na tulianza na sifa ya kutowajibika.

#### 5.3.4.1 Asiyewajibika

Mifano ifuatayo inathibitisha sifa za kutowajibika kwa Hakimu/Jaji ilivyosawiriwa katika MMS na MS na tulianza kwa kuangazia mfano 99 ufuatao.

#### Mfano 99

MMS: Mkuu wa Wilaya (kwa Hakimu): ...Mtumishi wako anafuga bata katika vyumba vya ndani, pamoja na kuku na wanazururazurura wakiokota miguuni pako...wanapafanya panuke mno. (uk 3).

MS: Meya (kwa Jaji): Ehee, na wewe Amosi Fyodorovich, bora na wewe uanze kurekebisha mahakama yako. Mahakama yako ni kama shamba kabisa. Mwambie mlinzi wako awahamishe bata-mzinga wake kutoka pale barazani. (Uk 4).

Mfano 99 ulionukuliwa kutoka katika tamthilia za MMS na MS, unathibitisha sifa ya Bw. Hakimu/Jaji ya kutowajibika. Kwa mfano, katika MMS, Mkuu wa Wilaya anamwambia Bw. Hakimu kwamba, Mtumishi wako anafuga bata katika vyumba vya ndani, pamoja na kuku wanaozururazurura wakiokota miguuni pa wateja na wanapafanya mahakama panuke mno ilhali katika MS (mfano 99), Meya anamwambia jaji kuwa, itakuwa bora akianza kurekebisha mahakama yake na kwamba mahakama yake ni kama shamba kabisa.

Tungo katika MMS, (mfano 99): wanapafanya mahakama panuke mno ni tofauti kimaana na tungo katika MS (mfano 98): mahakama yako ni kama shamba kabisa. Aidha, tungo katika MMS (mfano 98), pamoja na kuku wanaozururazurura wakiokota miguuni pa wateja haipo katika tamthilia ya MS, (mfano 99). Kutokana na tofauti za kimaana katika tungo zilizopigiwa mstari, tulihoji kwamba, tofauti katika uhawilishaji wa jumbe katika mchakato wa tafsiri husababishwa na uhuru wa mtafsiri wa kuteua

msamiati anavyopenda. Mfano 100 ufuatao pia ni nukuu kutoka MMS na MS inayomwangazia Bw. Hakimu/Jaji kama afisa asiyewajibika.

### **Mfano 100**

**MMS:** Hakimu: Ni kwa sababu hiyo mimi sijali. Mahakama yangu inanuka kiasi kwamba hakuna atakayediriki kuingia na kuikagua. Lakini kama ungeona moja ya makaratasi basi maisha hayangekuwa tena mazuri kama yalivyo.... Solomoni mwenyewe hangejua vipi kutofautisha ukweli na uwongo! (uk 10-11).

**MS:** Jaji: Mungu amhurumie huyo atakayejaribu kuchunguza usahihi wa vitabu na stakabadhi zote zile, kwa sababu atajutia siku aliyozaliwa! Na sijapata kuona ripoti hata moja inayoeleweka. Hata yule Mfalme Suleiman anayesemekana kuwa alijaliwa hekima tele asingeweza kuchanganua mambo ya hapa. (uk 15).

Mfano 100 unathibitisha tabia ya kutowajibika ya Bw. Hakimu/Jaji ilivyojitokeza katika tamthilia za MMS na MS. Kwa mfano, katika MMS (mfano 100), Hakimu anaeleza kwamba: Mahakama yake inanuka kiasi kwamba hakuna atakayediriki kuingia na kuikagua na anaonya kwamba, iwapo mtu angeona moja ya makaratasi basi maisha yake hayangekuwa tena mazuri kama yalivyo. Kwa upande mwingine, katika MS (mfano 100), Jaji anaeleza kwamba: Mungu amhurumie huyo atakayejaribu kuchunguza usahihi wa vitabu na stakabadhi zote zile, kwa sababu atajutia siku aliyozaliwa.

Tungo zilizopigiwa mistari hazifanani kimaana kwa kuwa katika MMS, Bw. Hakimu anakiri kwamba, mahakama yake inanuka sana hivi kwamba hakuna mtu atakayeingia na kuikagua lakini katika MS (mfano 100), Jaji anaonya kuwa, yeyote atakayejaribu kuchunguza vitabu ofisini mwake, atajutia siku ya kuzaliwa.

Katika utafiti huu tulihoji kuwa maelezo katika MMS (mfano 100) yanaeleweka barabara kuliko yalivyo katika MS (mfano 100). Kwa mfano, katika tamthilia ya MMS (mfano 100), Bw. Hakimu anasema kuwa, hata Solomoni mwenyewe hangejua

vipi kutofautisha ukweli na uwongo bali katika MS (mfano 100), Jaji anasema kuwa, Hata yule Mfalme Suleiman anayesemekana kuwa alijaliwa hekima tele asingeweza kuchanganua mambo ya hapa. Sehemu ifuatayo ya 5.3.4.2 inashughulikia sifa ya Bw. Hakimu/Jaji kama fisadi inavyojitokeza katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*.

#### **5.3.4.2 Fisadi**

Watafsiri wa MMS na MS walihawilisha sifa ya Hakimu/Jaji kama fisadi inavyojitokeza katika mfano 101 ufuatao.

#### **Mfano 101**

**MMS:** Hakimu: Ndiyo, lakini kuna dhambi na dhambi. Nakubali wazi kuwa napokea hongo, lakini aina gani ya hongo? Vimba vidogo na siyo zaidi! (uk 4).

**MS:** Jaji: Mimi sijali kukiri wazi kuwa huwa ninapokea rushwa lakini ni kutoka kwa wale watu wenye uwezo tu; na hiyo huwezi kuita dhambi. (uk 5).

Katika tamthilia za MMS na MS (mfano 101), Bw. Hakimu/Jaji amesawiriwa kama afisa fisadi. Kwa mfano, katika MMS, (mfano 101), Bw. Hakimu anasema, nakubali wazi kuwa napokea hongo, lakini aina gani ya hongo? Vimba vidogo na siyo zaidi, bali katika MS (mfano 101), Jaji anasema kwamba, mimi sijali kukiri wazi kuwa huwa ninapokea rushwa- lakini ni kutoka kwa wale watu wenye uwezo tu; na hiyo huwezi kuita dhambi. Tulihoji kuwa, Katika kazi hii tulidahili kuwa, ukosefu wa kuwepo kwa mfumo rasmi au kanuni ya kuzingatiwa na watafsiri katika mchakato wa tafsiri, hupelekea mtafsiri kuteua msamiati anavyotaka. Kwa hivyo, mtafsiri huweza kuibuka na matini pokezi ambayo ni tofauti kabisa na matini chanzi.

Watafsiri wa MMS na MS (mfano 101), walihawilisha ujumbe wa kubainisha kuwa Hakimu/Jaji ni fisadi ingawa namna walivyoteua msamiati ulitofautiana. Kwa mfano,

katika MMS (mfano 101), Hakimu anaeleza kwamba yeye hupokea hongo ndogondogo ilhali katika MS (mfano 101), Jaji anasema kwamba yeye hupokea hongo kutoka kwa wale watu wanaojiweza tu. Bw. Hakimu/Jaji pia alisawiriwa kama asherati katika MMS na MS, ilivyoelezwa katika sehemu ifuatayo.

### 5.3.4.3 Asherati

Watafsiri wa MMS na MS wamemsawiri mhusika Hakimu/Jaji kama asherati inavyojitokeza katika mifano ifuatayo. Tulianza kwa kuangazia mfano 102 ufuatao.

#### Mfano 102

MMS: Bw. Huruma (kwa Ghlestakov):..sasa wakati wowote huyu Dobchiniski anapotoka nyumbani kwenda kokote, mara hakimu anamwingilia mkewe, na naweza kuapa...lakini waangalie watoto, Mheshimiwa! Hakuna anayefanana na Dobchinski, ila kila mmoja, hata yule binti mdogo, ni picha kamili ya hakimu! (Uk 49).

MS: Kamishina (Kwa Hilestakov):.. Maskini Dobchiniski akitoka tu nyumbani kwake, Jaji huingia kwa mlango wa nyuma ili kukutana na mke wa Dobchiniski! Na hii ni kweli tupu, Mheshimiwa! Hakuna hata mtoto mmoja wa Dobchiniski anayefanana na Dobchiniski. Hii unaweza kuhakikisha mwenyewe! Kila mmoja wao hata yule mtoto wa kike anafanana jaji! (Uk 71).

Mfano 102, ulionukuliwa kutoka katika MMS na MS, unathibitisha kuwa Bw. Hakimu/Jaji ni asherati kwa kuwa alimnyemelea kimapenzi mkewe Dobchiniski na katika uhusiano huo, wamepata watoto wanaofanana naye sana. Katika MMS, (mfano 102), Bw. Huruma anadai kwamba, Dobchiniski anapotoka nyumbani kwenda kokote, mara hakimu anamwingilia mkewe, kinyume na ilivyo katika MS (mfano 102), Kamishina anaeleza kwamba, Dobchiniski akitoka tu nyumbani kwake, Jaji huingia kwa mlango wa nyuma ili kukutana na mke wa Dobchiniski.

Kimaana, kifungu katika MMS (mfano 102); Kumwingilia mke wa Dobchiniski na kifungu katika MS (mfano 102), kukutana na mke wa Dobchiniski havifanani. Tulihoji kuwa vifungu hivyo vilivyopigiwa mistari havieleweki kwa uwazi kwa kuwa

watafsiri wa MMS na MS huenda waliamua kutumia tasfida kwa sababu ya kuathiriwa na masuala ya utamaduni wa Kiafrika. Mwakasaka na Madumulla katika (mfano 102), hawakutaka kusema wazi kuwa Hakimu/Jaji humwingilia kimapenzi mke wa Dobchiniski wakati Dobchiniski hayuko nyumbani kwake, badala yake wanatumia vijembe.

Tulihoji pia kuwa, msomaji yeyote asiyelewa utamaduni wa Kiafrika atakosa kuelewa wanachomaanisha watafsiri hao wanaposema: kumwingilia mke wa Dobchiniski na kukutana na mke wa Dobchiniski. Mfano 103 pia unaangazia tabia ya Bw. Hakimu/Jaji ya kuwa asherati ilivyoelezewa katika MMS na MS.

### **Mfano 103**

**MMS:** Hakimu (kwa M/Wilaya): ...Na umesikia juu ya Cheptovichi na Valinski? Hilo ni tuzo kubwa sana kwangu. Niko katikati kabisa ya unono. Naweza kwenda kuwinda katika bustani ya Cheptovichi siku moja na katika bustani ya Valanski siku ya pili! (Uk 7).

**MS:** Jaji: (kwa Meya)...Na kuhusu uwindaji mimi sasa ni mashuhuri. Je unajua kwamba Cheptovich amemshtaki Varhovinski? Kwa hiyo nimejipatia fursa ya kuwinda sungura bila malipo katika mashamba yao yote. Ninaweza kukuchukua tukaenda pamoja. (uk 10).

Katika mfano 103, watafsiri wa MMS na MS walifaulu kumsawiri Hakimu/Jaji kama asherati hata ingawa walitumia jazanda. Kwa mfano, katika MMS (mfano 103), Hakimu anadai kwamba, anaweza kwenda kuwinda katika bustani ya Cheptovichi siku moja na katika bustani ya Valanski siku ya pili. Katika MS (mfano 103), Jaji anasema kwamba amejipatia fursa ya kuwinda sungura bila malipo katika mashamba ya Cheptovich na Varhovinski. Katika tasnifu hii, tulidahili kuwa, watafsiri wa MMS na MS (mfano 103) walitumia jazanda katika tungo zilizopigiwa mstari kwa sababu ya masuala ya kitamaduni. Watafsiri hao (Mwakasaka na Madumulla), walitaka kuondoa makali kwa kutotaja moja kwa moja kuwa, Bw. Hakimu/Jaji alikuwa na

uhusiano wa kingono na wake wa Cheptovich na Varhovinski kwa kuwa bwana walipokuwa na kesi mahakani.

Katika MS (mfano wa 103), Jaji anasema kwamba: angeweza kumchukua mkuu wa wilaya wakaandamana naye kwenda kuwanyemelea wake wa Cheptovich na Varhovinski haupo katika tamthilia ya MMS (mfano 103). Hivyo, tulidahili kuwa tofauti ya kitafsiri katika MMS na MS (mfano 103) ni kwa sababu watafsiri hawafungwi na kanuni yoyote wanapoteua msamiati. Hivyo, wanaweza kubadili maneno na kuibuka na matini pokezi ambayo ina ujumbe tofauti na wa matini chanzi. Mratibu wa Elimu/ Mkaguzi wa Mashule ni mmoja wa wahusika wakuu katika MMS/MS na sifa zake zinajitokeza katika sehemu ifuatayo ya 5.3.4.4.

#### **5.3.4.4 Mratibu wa Elimu/Mkaguzi wa Mashule**

Katika tamthilia ya MMS, Mratibu wa Elimu ni mhusika ambaye anasimamia shughuli za elimu wilayani ilhali katika MMS, Mkaguzi wa Mashule ndiye anayesimamia shughuli za elimu. Kulingana na tamthilia za MMS na MS, Mratibu wa Elimu/Mkaguzi wa Mashule ni mmoja wa maafisa wakuu serikalini. Sifa zake zimeelezwa katika sehemu ifuatayo na tumeanza kwa kuangazia sifa ya kutowajibika.

#### **5.3.4.5 Asiyewajibika**

Katika tamthilia za MMS na MS, Mratibu wa Elimu/Mkaguzi wa Mashule amesawiriwa kama mtu asiyewajibika kutokana na hoja zinazobainika katika mifano ya 103 na 104 na tumeanza kwa kushughulikia mfano wa 104.



**Mfano 104**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Ni wajibu wako kusimamaia walimu...Mratibu wa Elimu: Nitafanya nini? Nilimzungumzia juu ya jambo hili mara moja, (uk 4).

**MS:** Meya: walimu wako! Wewe ndiye kinara wa mashule... Mkaguzi: Sasa nitafanyeje?, (uk 6).

Mfano 104 umethibitisha kuwa, katika MMS na MS, Mratibu wa Elimu/Mkaguzi wa Mashule ni mhusika asiyewajibikia majukumu yake kazini. Kwa mfano, katika MMS na MS (mfano 104), Mratibu wa Elimu/Mkaguzi wa Mashule ameshindwa kuliwajibikia swala la utovu wa nidhamu miongoni mwa walimu na anapoulizwa na Mkuu wa Wilaya (Meya) iwapo ameweza kufanya chochote kuhusu walimu, anasema kuwa, hana la kufanya. Kwa mfano, katika MMS (mfano 104), Mkuu wa Wilaya anamwambia Mratibu wa Elimu kuwa, Ni wajibu wako kusimamia walimu. Mratibu wa Elimu alimjibu kuwa Nitafanya nini? Nilimzungumzia juu ya jambo hili mara moja. Katika MS (mfano 104), Meya anamwambia Mratibu wa Elimu walimu wako! Wewe ndiye kinara wa mashule. Naye Mkaguzi wa Mashule anamjibu kuwa, Sasa nitafanyeje?

Kimaana, tungo hizo mbili: ni wajibu wako kusimamia walimu na wewe ndiye kinara wa mashule ni tofauti. Tulihoji kuwa, kinara wa mashule anaweza kuwa na jukumu la kila kitu shuleni, kama vile kuwasimamia walimu, wanafunzi, wazazi, vitabu na mijengo pale shuleni ilhali kusimamia walimu ina maana ya kuwa na jukumu la kushughulikia maswala ya walimu pekee. Mfano 105 ufuatao, pia unaangaza sifa ya kutowajibika ya Mratibu wa Elimu/ Mkaguzi wa Mashule inavyoelezewa katika MMS na MS.

**Mfano 105**

**MMS:** BW. Huruma: ...Mchukue Mratibu wa Elimu hapa...sijui ni kwa nini wakubwa wamwajiri mtu kama huyo! Ni mwovu zaidi kuliko mwasi! Anapanda mawazo maovu katika vichwa vya vijana. (uk 49).

**MS:** Kamishina: Na yule Mkaguzi wa Mashule.. jinsi alivyopewa kazi ile ni muujiza kabisa! Tazama, hayuko tofauti na nyapara, na ile shule yake ni chemchemi ya mapinduzi! (uk 71).

Katika mfano 105, Mratibu wa Elimu/Mkaguzi wa Mashule amesawiriwa kama mhusika asiyewajibika. Kwa mfano katika MMS (mfano 105), Bw. Huruma anasema: mchukue Mratibu wa Elimu hapa...Anapanda mawazo maovu katika vichwa vya vijana. Kwa upande mwingine, katika tamthilia ya MS (mfano 105), Kamishina anasema kuwa: Na yule Mkaguzi wa Mashule.. hayuko tofauti na nyapara, na ile shule yake ni chemchemi ya mapinduzi. Ingawa watafsiri wa MMS na MS walifanikiwa kuhawilisha ujumbe wa kutowajibika kwa Mratibu wa Elimu/Mkaguzi wa Mashule lakini kimaana, tungo zilizopigiwa mistari ni tofauti.

Katika tasnifu hii tulihoji kuwa, uhuru wa mtafsiri huchangia kuwepo na tofauti katika uteuzi wa maneno, hivyo kusababisha tofauti katika uhawilishaji wa ujumbe kutoka matini chanzi hadi matini pokezi. Kwa mfano, kutokana na tungo zilizopigiwa mistari (mfano 105), kifungu katika MMS: Anapanda mawazo maovu katika vichwa vya vijana ni tofauti kimaana na kifungu katika MS: shule yake ni chemchemi ya mapinduzi. Anna/Ann ni mhusika katika MMS na MS na sifa zake zimeshughulikiwa katika sehemu ifuatayo ya 5.3.4.6.

#### **5.3.4.6 Anna/Ann**

Katika tamthilia ya MMS, Anna ni mke wa mkuu wa wilaya ilhali katika MS, Ann ni mke wa Meya. Katika tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali* Anna/Ann ni mmoja wa wahusika wakuu. Zifuatazo ndizo sifa zake na tumeanza na sifa ya kuwa asherati.

### 5.3.4.7 Asherati

Mifano ifuatayo ni visa kutoka tamthilia za MMS na MS vinavyothibitisha tabia za Anna/Ann kama asherati. Mwanzo, tumeshughulikia mfano 106 ufuatao.

#### Mfano 106

**MMS:** Anna: Utaona kuwa yeye ni mwanamji wa Pitasbag. Si mikogo hiyo! Si maringo hayo! Nilimpenda mara moja na nilitambua kuwa alikuwa akinichungulia mara kwa mara. (uk 42).

**MS:** Ann: Ni mstaarabu kwelikweli. Unaweza kutambua mara moja kwamba ni mtu wa mtindo (fasheni)! Mungu wangu, vijana kama huyu ndio wanaonivutia! Alivyo na utu na mtindo! Tena mkakamavu. Niligundua kuwa macho yake yalikuwa hayamtoki kwangu. (uk 57).

Mfano 106 ni nukuu kutoka MMS na MS ambapo Anna/Ann amesawiriwa kama asherati alipomweleza Marya/Maria kwamba alivutiwa kimapenzi na Ghlestakov/Hilestakov. Kwa mfano, katika tamthilia ya MMS mfano (106), Anna anamwambia bintiye kuwa, Nilimpenda mara moja na nilitambua kuwa alikuwa akinichungulia mara kwa mara. Kwa upande mwingine, katika MS (mfano 106), Ann anamwambia bintiye kuwa, Mungu wangu, vijana kama huwa ndio wanaonivutia! Alivyo na utu na mtindo! Tena mkakamavu. Niligundua kuwa, macho yake yalikuwa hayatoki kwangu. Tamthilia za MMS na MS (mfano 106) ni thibitisho kuwa Anna/Ann ni asherati kwa sababu ana mme ambaye wake ilhali anakiri kwamba amevutiwa kimapenzi na Ghlestakov/Hilestakov.

Kifungu katika MMS (mfano 106): Mungu wangu, vijana kama huwa ndio wanaonivutia hakipo katika tamthilia ya MS (mfano 106). Aidha, tulihoji kuwa katika mchakato wa tafsiri, mtafsiri anaweza kudondoa au kubadilisha ujumbe wa matini chanzi na kuibuka na matini pokezi ambao una ujumbe tofauti na wa matini chanzi. Kwa mfano, katika MMS (mfano 106), mtafsiri ametumia idadi kubwa ya maneno

kuliko mtafsiri wa MS mfano 106. Pia, mfano 107 ufuatao ni nukuu kutoka MMS na MS inayoangaza sifa ya mhusika Anna/Ann kama asherati.

### **Mfano 107**

**MMS:** Ghlestakovu: ...watu hawa hawajapata kumwona mtu yeyote mashuhuri. Lakini kwa ujumla, ni wema wa moyo na wanajua wajibu wao. Na binti anaonekana mzuri kabisa na nadhani mama mwenyewe yuko tayari kwa lolote. (UK 46).

**MS:** Mkuu wa posta (akisoma barua): ...Nipo hapa sasa nikiishi maisha ya kifahari katika jumba la Meya, nikiwatongoza mke wake na binti yake, kwa wakati mmoja! Sijaamua nianze kwenda na yupi- huenda mke wake ni mzuri zaidi, anaelekea kuwa tayari kwa lolote! (Uk 109).

Watafsiri wa MMS na MS katika mfano 107 hapa juu, walifaulu kuhawilisha sifa ya Anna/Ann kama asherati kutoka matini chanzi hadi matini pokezi. Kwa mfano, katika MMS Ghlestakovu anasema kuwa, na binti anaonekana mzuri kabisa na nadhani mama mwenyewe yuko tayari kwa lolote. Katika MS, Hilestakov anasema; Nipo hapa sasa nikiishi maisha ya kifahari katika jumba la Meya, nikiwatongoza mke wake na binti yake, kwa wakati mmoja! Sijaamua nianze kwenda na yupi- huenda mke wake ni mzuri zaidi, anaelekea kuwa tayari kwa lolote. Tungo zilizopigiwa mistari zinathibitisha tofauti baina ya vifungu katika MMS na MS (mfano 106) katika uhawilishaji wa ujumbe. Kwa mfano kifungu katika MS (mfano 107: Nipo hapa sasa nikiishi maisha ya kifahari katika jumba la Meya hakipo katika MMS.

Katika tasnifu hii tulidahili kwamba, mtafsiri wa MS (mfano 107) anaelezea kwa uwazi kuwa Ghlestakov aliwatongoza mama na bintiye kwa wakati mmoja ilhali katika MMS, Ghlestakovu alitumia vijembe kwa kusema kuwa; Na binti anaonekana mzuri kabisa na nadhani mama mwenyewe yuko tayari kwa lolote. Huenda Mwakasaka alitaka kuficha ukali kwa sababu ya masuala ya kitamaduni ndiposa hakutaka kuzungumzia waziwazi hoja ya kutongozana. Sehemu ifuatayo

imemwangazia mhusika Anna/Ann kama mbishi alivyosawiriwa na watafsiri wa MMS na MS.

#### 5.3.4.8 Mbishi

Watafsiri Mwakasaka (1979) na Madumulla (1999) wamemsawiri Ann/ann kuwa ni mbishi. Sifa hiyo imebainika katika mifano ifuatayo na tulianzana mfano wa 108 ufuatao.

#### Mfano 108

**MMS:** Anna: (Kwa Marya)...Nilimpenda mara moja, na nilitambua kuwa alikuwa akinichungulia mara kwa mara. Marya (kwa mamake) Mama, unajuwa kuwa alikuwa akiniangalia mimi... Anna (kwa Marya) Sasa Mungu nipe nguvu! Haiwezekani kabisa! Yote yalieleweka jana. Kwa nini ajishughulishe nawe? Ukileta upuzi zaidi nitakupeleka chumbani kwako. (Uk 42).

**MS:** Anna: (kwa Maria) ...Niligundua kuwa macho yake yalikuwa hayamtoki kwangu... Maria (kwa mamake) Oh mama, mimi ndiye alikuwa akiniangalia! ... Anna (kwa Maria) Ati wewe? Acha ujuha wako...Maria: alikuwa akiniangalia mimi... Anna (kwa Maria) Mungu wangu, huyu mtoto hakomi kunisuta? Kwa nini akuangalie wewe? Unaweza kunipa sababu moja tu? (uk 57).

Mfano 108 ni nukuu kutoka kwa tamthilia za MMS na MS unaothibitisha kuwa, Anna/Ann alikuwa mbishi kwani alizua ubishi kati yake na bintiye kuhusiana na mapenzi kati ya Ann/Anna na Ghlestakovu/Hilestakov. Katika MMS, (mfano 108), Anna anamwambia Maria; Nilimpenda mara moja, na nilitambua kuwa alikuwa akinichungulia mara kwa mara na katika MS, Ann anamwambia Marya kwamba: Niligundua kuwa macho yake yalikuwa hayamtoki kwangu.

Watafsiri wa MMS na MS walifaulu kuhawilisha sifa ya Anna/Ann ya kuwa mbishi ingawa uteuzi wa msamiati ni tofauti. Katika MMS, Anna anamwambia Marya kuwa; Kwa nini ajishughulishe nawe? Ukileta upuzi zaidi nitakupeleka chumbani kwako. Katika MS, Ann alimwambia Marya Acha ujuha wako...Maria: Kwa nini akuangalie wewe? Unaweza kunipa sababu moja tu? Kutokana na mfano 108, tulihoji kuwa,

kifungu katika MMS (mfano 108): nilitambua kuwa alikuwa akinichungulia mara kwa mara sio sinonimu ya kifungu katika MS (mfano 108): Niligunduwa kuwa macho yake yalikuwa hayamtoki kwangu. Aidha, utungo katika MMS, (mfano 108): Ukileta upuzi zaidi nitakupeleka chumbani kwako na utungo katika MS (mfano 108); Unaweza kunipa sababu moja tu hazifanani kimaana. Mfano ufuatao wa 109, pia unaangazia sifa ya mhusika Anna/Ann alivyosawiriwa na watafsiri wa MMS na MS kama mbishi.

### **Mfano 109**

**MMS:** Marya: ni Dob mama. ...Anna (kwa Marya) Dobchniski kwa hakika! Njozi gani zinazokujia kichwani!! Ni dhahiri kuwa siye Dobchniski. ...Marya: Hakika mama ni Dobchniski. ..Anna: Unasema hivyo kusudi tu kunipinga. Nakwambia siye Dobchniski...Ndiyo. Sawa, sasa naona. Na wewe unabisha nini? (uk 29).

**MS:** Maria: Ni Dobchniski mama. ..Anna: Dobchniski! Usiwe mpuuzi, umeanza tena alinacha zako. Hawezi kuwa Dobchniski ila. ..Maria: Kweli ni Dobchniski mama. ..Anna: Usinipinge nitakwambia ni nani. ...Ndiyo ni Dobchniski na mimi nimemwona, sasa ubishi wa nini? (uk 42-43).

Katika mfano 109, Anna/Ann alizua ubishi kati yake na bintiye walipojaribu kumtambua mtu aliyekuwa akija inavyodhihirika katika MMS na MS. Kwa mfano, katika MMS (mfano 109), Anna anasema: Dobchniski kwa hakika! Njozi gani zinazokujia kichwani!! Ni dhahiri kuwa siye Dobchniski ilhali katika MS (mfano 109) Ann anasema: Usiwe mpuuzi, umeanza tena alinacha zako. Hawezi kuwa Dobchniski. Aidha, katika MMS (mfano 109), Anna anamwambia Maria kuwa; Unasema hivyo kusudi tu kunipinga. Nakwambia siye Dobchniski...Ndiyo. Sawa, sasa naona na katika MS (mfano 109), Ann anamwambia Marya kuwa; Usinipinge nitakwambia ni nani. .Ndiyo ni Dobchniski na mimi nimemwona. Kutokana na tungo zilizopigiwa mistari, tulihoji kuwa usemi katika MMS (mfano 109): Njozi gani zinazokujia kichwani,

haupo katika MMS. Pia usemi katika MS: umeanza tena alinacha zako, haupo katika MMS (mfano 109).

Katika utafiti huu tulihoji kuwa, watafsiri wa MMS na MS walifaulu katika kuhawilisha sifa ya Anna/Ann ya kuwa mbishi, hata ingawa kutokana na tungo zilizopigiwa mistari katika mfano 109, tumethibitisha kuwa namna walivyoteua msamiati ilitofautiana. Pia, tulidahili kuwa katika mchakato wa tafsiri, tofauti ya kimaana inaweza kutokea katika matini pokezi mbili ya matini chanzi moja kwa kuwa, mtafsiri anapoteua msamiati, huathiriwa na mazingira ya kulelewa pamoja na hali ya ubunifu ya mtu binafsi. Mhusika Maria/Marya ni kati ya wahusika wakuu katika tamthilia za MMS na MS na tumeshughulikia sifa zake katika sehemu ifuatayo.

### **5.3.5 Maria/Marya**

Katika MMS, mhusika Maria ni binti wa Mkuu wa Wilaya na Anna ilhali katika MS, mhusika huyo anaitwa Marya na ni binti wa Meya na Ann. Maria/Marya ana umri wa miaka kumi na minane. Watafsiri wa MMS na MS walimsawiri Maria/Marya kama mpenda urembo na tumeelezea kuhusu sifa hiyo ya urembo katika sehemu ifuatayo ya 5.3.5.1.

#### **5.3.5.1 Mpenda Urembo**

Kulingana na TUKI, (2013), urembo ni hali ya kupenda ama kutumia vitu vinvyotumika kama pambo, kama vile bangili, vipuli ushango, poda nk. Watafsiri wa MMS na MS wamemsawiri Maria/Marya kama mhusika anayependa urembo, inavyodhihirika katika mfano 110 ufuatao.

**Mfano 110**

**MMS:** Anna:..Kwa vile ulisikia Bwana Posta yuko hapa ukaona uanze kujirembesha mbele ya kioo! Unadhani atakutongoza na kila wakati yeye hukunja uso wake mara tu unapompa kisogo. ( uk 13-14).

**MS:** Ann:...Kwa sababu Mkuu wa Posta yupo hapa basi utajipuna na kujitazamatazama kwenye kioo kwa mwaka mzima. Unadhani anakupenda, kumbe mara tu unapompa mgongo yeye hukusahau kabisa kama upo hapa duniani! (uk 20).

Katika tamthilia za MMS na MS, (mfano 110), Maria/Marya amesawiriwa kama mhusika anayependa urembo kwa kuwa aliupoteza muda wake mwingi akijirembesha.

Kwa mfano, katika MMS (mfano 110), Anna anamwambia Maria kwamba, Kwa vile ulisikia Bwana Posta yuko hapa ukaona uanze kujirembesha mbele ya kioo ilhali katika MS, (mfano 110), Ann anamwambia Marya kwamba, Kwa sababu Mkuu wa Posta yupo hapa, basi utajipuna na kujitazamatazama kwenye kioo kwa mwaka mzima.

Tungo katika MMS (mfano 110): kujirembesha mbele ya kioo sio sinonimu ya tungo katika MS: kujitazamatazama kwenye kioo kwa mwaka mzima. Isitoshe, katika MMS (mfano 110), Anna anamwambia Marya: Unadhani atakutongoza na kila wakati yeye hukunja uso wake mara tu unapompa kisogo bali katika MS (mfano 110), Ann anamwambia Marya kuwa, Unadhani anakupenda, kumbe mara tu unapompa mgongo yeye hukusahau kabisa kama upo hapa duniani.

Utungo huu; unadhani anakupenda sio sawa kimaana na utungo; unadhani atakutongoza. Kumtongoza mtu ni hali ya kutaka kuwa na uhusiano wa mapenzi na mtu huyo na kumpenda mtu ni kumwonyesha upendo hasa kwa watu ambao wana uhusiano wa kimapenzi. Katika tasnifu hii tulidahili kwamba, kulingana na utamaduni wa Kiafrika, mzazi akiwa na uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa, hawezi kumwambia



mwanawe. Yaani, katika utamaduni wa Kiafrika, sio uungwana kwa mzazi na mwanawe kujadili maswala ya mapenzi na kutongozana.

Watafsiri wa MMS na MS (Mwakasaka na Madumulla) ni waafrika na kama watafsiri wangeweza kupuuzilia mbali (mfano 110) unaozungumzia masuala ya mapenzi na kutongozana lakini walihawilisha ujumbe huo unavyobainika katika (mfano 110). Tulihoji kuwa, watafsiri wa MMS na MS waliathiriwa na utamaduni wa Kizungu ndiposa hawakuona ubaya wowote katika mazungumzo yanayohusu masuala ya kutongozana baina ya mama na bintiye. Katika sehemu ifuatayo ya 5.4, tulihitimisha sura ya tano.

#### **5.4 Hitimisho**

Katika sura ya tano tulihakiki kiulinganishi jinsi wahusika walivyosawiriwa katika MMS na MS. Mwanzo, tulichunguza jinsi wahusika walivyopewa majina katika tamthilia zilizoteuliwa katika kazi hii. Imebainika kwamba, Mwakasaka na Madumulla walitofautiana katika kuwapa wahusika majina. Kwa mfano, Madumulla aliswahilisha majina ya wahusika kwa mfano, Meya badala ya ‘Mayor’. Mwakasaka kwa upande wake aliwapa wahusika wake majina kulingana na nafasi zao za kazi, kwa mfano, badala ya neno ‘Mayor’ akasema Mkuu wa Wilaya.

Katika sura hii, tulichunguza tofauti katika idadi ya wahusika na tulibaini kuwa watafsiri wa MMS na MS waliwasawiri wahusika kwa namna iliyotofautiana. Kwa mfano, katika tamthilia ya MMS, Mwakasaka alikuwa na wahusika ishirini na tisa ilhali katika MS, Madumulla alikuwa na wahusika ishirini na sita. Tulibaini pia kuwa, takriban wahusika wote katika MMS na MS walipewa sifa zinazofanana lakini tofauti ilijitokeza katika uteuzi wa msamiati na namna ya uwasilishaji wa sifa za wahusika.

Katika tasnifu hii tulidahili kwamba, tofauti za uteuzi wa msamiati na uwasilishaji wa sifa za wahusika zimeibuka kwa sababu, katika mchakato wa tafsiri, mtafsiri ana uhuru wa kuteua msamiati na kuhawilisha ujumbe wa matini chanzi anavyopenda. Hivyo, ilibainika kwamba, kulikuwa na tofauti ya uwasilishaji wa ujumbe katika matini pokezi mbili (MMS na MS) tulizozishughulikia katika tasnifu hii. Katika sura ya sita ifuatayo, tulishughulikia muhtasari, hitimisho, mchango na mapendekezo ya tasnifu hii.

## SURA YA SITA

### HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 6.0 Utangulizi

Katika utafiti huu, mtafiti alihakiki kiulinganishi mbinu za lugha, alichambua kiulinganishi uwasilishaji wa ujumbe na alichunguza kiulinganishi uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Mwakasaka, 1999) na *Mkaguzi wa Serikali* (Madumulla, 1979).

Katika sura hii ya sita nimeshughulikia masuala yafuatayo: muhtasari wa utafiti, kubainisha matokeo ya utafiti na kutoa hitimisho la tasnifu hii kwa jumla. Pia nimependekeza maoni yetu kutokana na matokeo ya utafiti huu. Yaani, nimeonyesha mapengo yaliyopo na kupendekeza kazi zinazoweza kushughulikiwa na watafiti wa baadaye ili kuyaziba mapengo hayo. Tulianza kwa kueleza muhtasari wa utafiti kama inavyojitokeza katika sehemu ifuatayo.

#### 6.1 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

- a) Mbinu za lugha katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali* zinafanana.
- b) Kuna tofauti kubwa katika uwasilishaji wa ujumbe katika tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*.
- c) Uteuzi wa msamiati kuhusu usawiri wa wahusika ulitekelezwa kwa namna inayofanana katika tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*.

Katika kukusanya data ya utafiti huu tulinakili kiulinganishi mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika MMS na MS. Madumulla (1999) alitafsiri tamthilia ya MS miaka ishirini baada ya Mwakasaka (1979) kutafsiri tamthilia ya MMS. Tulihoji kuwa miaka ishirini ni muda mrefu mno hivi kwamba mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na hata ya matumzi ya lugha katika kazi ya fasihi hayawezi kuepukika.

Sura ya tatu, ya nne na ya tano ndizo sura za uchanganuzi wa data katika utafiti huu. Kutokana na uchanganuzi wa sura hizo, kuna ushahidi wa kuwepo kwa tofauti katika, matumizi ya mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika tamthilia za MMS na MS. Hivyo, tuliibuka na matokeo ambayo tumeyaangaza katika sehemu ifuatayo ya 6.2.

## **6.2 Matokeo ya Utafiti**

Katika utafiti huu, malighafi ya data ilikuwa ni tamthilia za MMS na MS na nilinua kutimiza malengo yafuatayo: kuhakiki kiulinganishi mbinu za lugha katika MMS na MS, kuchambua kiulinganishi uwasilishaji wa ujumbe katika MMS na MS na kuchanganua kiulinganishi uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika MMS na MS. Tumehitimisha malengo hayo baada ya kuchanganua data katika sura ya tatu, nne na tano. Hivyo, tulichunguza kiulinganishi mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika na kuibuka na matokeo yaliyoangaziwa katika sehemu ya 6.2.1, 6.2.2 na 6.2.3. Tulianza kwa kushughulikia sehemu ifuatayo ya 6.2.1 inayoangaza matokeo ya utafiti kuhusu mbinu za lugha katika MMS na MS.

### **6.2.1 Mbinu za Lugha**

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kutambua kiulinganishi mbinu za lugha katika MMS na MS na tumelishughulikia katika sura ya tatu. tumechunguza mbinu zifuatazo: chuku, uzungumzi nafsia, kejeli, matumizi ya barua, kinaya, matumizi ya ndoto, kuchanganya ndimi, misemo na nahau. Imebainika kuwa, matumizi ya mbinu za lugha huchangia kukuza mawasiliano kati ya msanii na msomaji wa vitabu husika.

Tumegundua kuwa katika tamthilia za MMS na MS, mbinu za lugha kama vile chuku, jazanda, kinaya, matumizi ya ndoto na matumizi ya barua, uzungumzi nafsia, zilijitokeza katika mifano mbalimbali iliyonukuliwa. Hata hivyo, watafsiri wa MMS na MS walitofautiana kwa namna walivyohawilisha mbinu hizo za lugha kwa kuwa kila mtafsiri ana upekee wake wa kufasiri ujumbe wa matini chanzi. Kwa mfano katika MMS Ghlestakovu anasema kwamba alikuwa katika chumba duni kabisa ambapo kulikuwepo na aina ya kunguni ambao hajakata kuwaona. Kwa upande mwingine, Hilestakov anasema chumba alichokuwemo ni pito la uchafu ambapo kuna kunguniwanaouma kama mbwamwitu. Mwadumulla alitumia tashbihi ilhali Mwakasaka hakutumia. Katika sehemu ifuatayo ya 6.2.2, tumeshughulikia matokeo ya utafiti kuhusu uwasilishaji wa ujumbe.

### **6.2.2 Uwasilishaji wa Ujumbe**

Katika utafiti huu tumechambua kiulinganishi uwasilishaji wa ujumbe katika tamthilia za MMS na MS. Ujumbe ulioangaziwa na watafsiri wa MMS na MS ni: ukatili, uongozi mbaya, ufisadi, unafiki, usaliti, kutowajibika, matumizi ya madawa ya kulevya na nafasi ya mwanamke katika jamii. Tumegundua kuwa, katika MMS na MS, watafsiri waliwasilisha ujumbe kwa namna tofauti kwa kuwa kila mmoja alifasiri matini chanzi na kuteua msamiati kulingana mapenzi yake.

Tumegundua pia kwamba, katika matini pokezi mbili za matini chanzi moja, kuna uwezekano wa kuwa na ujumbe ambao umejitokeza katika tamthilia moja na haupo katika tamthilia nyingine. Kwa mfano, ujumbe wa ujinga umejitokeza katika tamthilia ya MS na haupo katika MMS. Hivyo, tunahoji kwamba kwa kuwa mtafsiri ana uhuru wa kufasiri na kutafsiri katika mchakato wa tafsiri, basi huweza kupuuza ujumbe uliopo katika matini chanzi.

Katika tamthilia ya MS, mtafsiri aliibua matukio mengi ambayo hayapo katika MMS. Kwa mfano, katika MS, Hilestakov anamwambia Meya kuwa, chumba hicho ni pito la uchafu na kwamba bado Meya hajawaona kunguni wanaouma kama mbwa mwitu (mfano 6). Tukio hili halijatokea katika MMS, kwa hivyo tunahoji kuwa huenda Madumulla alibuni matukio hayo kwa kutaka hayo kwa kutaka kuirithisha hadhira lengwa. Sehemu ifuatayo ilianguzia matokeo ya utafiti kuhusu uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika yalivyobainika katika uchanganuzi wa tasnifu hii.

### **6.2.3 Uteuzi wa Msamiati katika Usawiri wa Wahusika**

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kuhakiki kiulinganishi uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika tamthilia za MMS na MS. Mintarafu ya matokeo yaliyoibuka katika sura ya nne, ilibainika kwamba, majukumu ya wahusika katika MMS na MS yaliangazwa barabara. Hata hivyo, watafsiri wa MMS na MS waliwapa wahusika majina yanayotofautiana. Kwa mfano, mtafsiri wa MMS aliswahilisha majina ya wahusika, hivyo, jina Peter lilibadilishwa likawa Pita, Amos likawa Amosi, Abdulin likawa Abdulini lakini mtafsiri wa MS hakuyaswahilisha majina ya wahusika.

Tuligundua pia kwamba kulikuwa na tofauti ya idadi ya wahusika katika tamthilia za MMS na MS. Yaani, mtafsiri wa MMS alitumia wahusika ishirini na sita ilhali

mtafsiri wa MS alitumia wahusika ishirini na tisa. Ilibainika kwamba, matumizi ya lugha katika usawiri wa wahusika yalitofautiana katika MMS na MS. Yaani, watafsiri Mwakasaka na Madumulla wangeweza kumpatia mhusika sifa ya kuwa fisadi lakini kila mmoja alikuwa na upekee wake katika kuhawilisha ujumbe wa matini chanzi. Mchango wa utafiti ni kipengele muhimu pia katika utafiti huu na ndio imeangazwa katika sehemu ya 6.3 ifuatavyo.

### **6.3 Mchango wa Utafiti**

Katika tasnifu hii, tulihoji kuwa utafiti huu unatoa mchango wa kiakademia kuhusiana na taaluma ya tafsiri linganishi, hivyo utawanufaisha walimu, wataalamu na wapenzi wa tafsiri wenye hamu ya kujua kuhusu uhakiki wa kazi za tafsiri. Pia, katika tasnifu hii, wataalamu chipukizi ambao wangependa kuzamia katika kitengo cha tafsiri linganishi hasa kuhusiana na kazi zilizotafsiriwa watachochewa. Utafiti huu vilevile, utawafaidi wanafunzi wa ngazi mbalimbali hasa wale wa viwango vya uzamili na uzamifu ambao wanaweza kuzamia katika vipengele vingine vya lugha ambavyo havikushughulikiwa katika utafiti huu.

Katika utafiti huu, tulihakiki kiulinganishi mbinu za lugha, tukafafanua kiulinganishi uwasilishaji wa ujumbe na pia tukachunguza kiulinganishi uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*. Hivyo, utafiti huu utakuwa muhimu katika taaluma ya fasihi hususan katika nyanja ya tafsiri linganishi. Kulingana na uchunguzi wetu, utafiti wa kuhakiki kiulinganishi vipengele muhimu katika matini pokezi mbili za matini chanzi moja haujazingatiwa sana hususan katika fasihi ya Kiswahili, hivyo utafiti huu ulinua kuliziba pengo hilo.

Imebainika kuwa katika mchakato wa tafsiri, mtafsiri huweza kuibuka na matini pokezi ambayo ni tofauti na matini chanzi kwa sababu hakuna kanuni yoyote ambayo humshurutisha mtafsiri kutafsiri kila neno. Tulihoji pia kuwa matokeo ya uchunguzi huu yatawafaa watu ambao wana haja ya kusoma tafsiri linganishi na kuwapa watafsiri motisha ya kutafsiri vitabu ambavyo tayari vilishatafsiriwa ili viweze kuhakikiwa kiulinganishi. Katika sehemu ifuatayo tulishughulikia kipengele cha mapendekezo ya utafiti huu.

#### **6.4 Mapendekezo ya Utafiti**

Katika tasnifu hii nilihakiki kiulinganishi mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika tamthilia za MMS na MS. Matokeo yanayohusu mbinu za lugha yanaonyesha kuwa, kuna tofauti katika uhawilishaji wa ujumbe katika matini pokezi mbili kwa kuwa katika mchakato wa tafsiri, kila mtafsiri ana upekee wake wa kufasiri ujumbe wa matini chanzi.

Ninapendekeza kuwa, shule za upili na vyuo vikuu na vyuo vingine vya elimu nchini Kenya vishirikishe mafunzo ya tafsiri katika mitalaa yao. Isitoshe, ninapendekeza kwamba itakuwa ni jambo la muhimu iwapo wanaohusika na uundaji wa silabasi katika vyuo vikuu wataingiza vipengele vya nadharia ya uhakiki wa diskosi katika kozi ya tafsiri ili wanafunzi waweze kuwasilisha tafsiri zilizo mwafaka.

Tafsiri ni taaluma muhimu katika karne hii ya 21 kwa kuwa kupitia tafsiri watu kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu wanaweza kutagusana kwa urahisi kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo yamepiga hatua kubwa na kurahisisha mawasiliano. Pia, kupitia tafsiri, bidhaa kama vile madawa, mafuta ya kujipaka na ya kupikia, kemikali na vyakula kutoka nchi mbalimbali zitauzika kwa urahisi.



Hivyo, tunapendekeza kuwa utafiti unaoshughulikia vitabu vingine (tofauti na vya utafiti huu) Tulihakiki kiulinganishi utekelezwe ili kubainisha iwapo matokeo yatakuwa tofauti na yetu. Isitoshe, tasnifu hii imedhihirisha kwamba kuna haja ya kufanya utafiti katika Kiswahili ambao utachunguza suala la utamaduni katika matini pokezi mbili za matini chanzi moja. Kipengele cha utamaduni ni muhimu kwa kuwa, kama anavyodai Shitemi (1990) na Omboga (1986), haiwezekani tafsiri kufanywa katika ombwe tupu kwa kuwa mtafsiri kama msanii yeyote ni mzaliwa wa jamii fulani na katika kuhawilisha ujumbe wa matini chanzi ataathiriwa na mila na utamaduni wa jamii yake.

Mbinu za lugha, uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika tamthilia za MMS (1979) na MS (1999). Katika sura ya tatu, nne na ya tano ambazo ndizo sura za uchanganuzi katika utafiti huu, ilibainika kwamba watafsiri wa MMS na MS walitofautiana katika uteuzi wa msamiati na uwasilishaji wa ujumbe. Ndiposa tunapendekeza kwamba, watafiti wa baadaye wanaweza kutafitia nyanja zifuatazo:

- i. Wataalamu na wanafunzi wa tafsiri wanaweza kuhakiki kiulinganishi vitabu viwili au zaidi vilivyotafsiriwa na vinalenga matini chanzi moja tofauti na vitabu vilivyochunguzwa katika tasnifu hii (MMS na MS), huenda wakaibuka na matokeo tofauti.
- ii. Kuchunguza iwapo kuna tofauti katika tamthilia za MMS na MS, hasa kwa kuzingatia udondoshaji katika matumizi ya lugha.

## MAREJELEO

- Abdullaziz, M. (1979). *Muyaka. 19th Century Kiswahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Achebe, C. (1958). *Things Fall Apart*. London: Heinemann.
- Ba, M. (1994). *Barua Ndefu Kama Hii*. (Maganga, C. - Mtafsiri). Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.
- \_\_\_\_\_ (1979). *So Long a Letter*. (Modupe Bode- Thomas- Trans). London: Heinemann.
- Baker, M. (1992). *In other words: A course book on translation*. London: Routledge.
- Bassnett, S. (1993). *Comparative Literature: A Critical Introduction*. Oxford: Blackwell.
- \_\_\_\_\_ (2006). "Reflections on Comparative Literature in the Twenty-First Century". *Comparative Critical Studies* vol. 3, n° 1, *Comparative Literature at a Crossroads?* Robert Weninger (ed.), pp. 3-11.
- \_\_\_\_\_ (2010). *Introduction: What is Comparative Literature? How it came into being?* Paper no. – 10 E-E-205-A. 2010-11.
- Bistin, L. G. & Bandia, F. P. (2006). *Charting the Future of Translation History*. Canada: University of Ottawa Press.
- Bratoz, S. (2004). *A Stylistics Analysis of Four Translations of J.D Salinger's, The Catcher in The Rye*. London: Penguin.
- Bressler, C. E. (2007). *Literary Criticism: An Introduction to Theory and Practice* (4thEd.). New Jersey: Pearson.
- Brown, G., & Yule, G. (1983, 1984). *Discourse Analysis*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Cartford, J. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*. London: Oxford University Press.
- Chiduo, et al. (2016). *Kamusi Elezi ya Kiswahili*. The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi, Kenya.
- Coombes, P. (1969). *What is Educational Planning?* UNESCO, 11EP. Paris.
- Fadhil, E. (2014). *Dhima ya Mtindo katika Tamthilia za Kihistoria: Utafiti Linganishi wa Tamthilia ya Morani na Kinjeketile*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Farahzad, F. (2008). *Translation Criticism: A CDA Approach in Translation Studies Quarterly*, Vol.6. No. 24, pp 39-47.

- Farahzad, F. & MadaniGivi, F. (2009). *Ideology and Translation: A Case Study*. In *Translation Studies Quarterly*, Vol. 7, No. 26, pp. 11-30.
- Halliday, M. (1970). "Language structure and language function", in Lyons J. (ed.) *New Horizons in Linguistics*, Harmondsworth: Penguin, 140-164.
- Harries, L. 1952. 'Popular Verse of the Swahili Tradition', *Africa* 22: 158-164.
- Hatch, E. (1992). *Discourse and Language Education*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Hussein, E. (1969). *Kinjeketile*. Nairobi: Oxford University Press.
- \_\_\_\_\_ (1971). *Mashetani*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Imbuga, F. (1976). *Betrayal in the city*. Nairobi: East African publishing House.
- Jilala, H. (2014). Athari za Kiutamaduni katika Tafsiri: mfano katika matini za Kitalii katika makumbusho za Tanzania. (Haijachapishwa). Chuo kikuu cha Dar es Salaam.
- \_\_\_\_\_ (2014). *Matatizo ya Tafsiri katika matini za Kitalii Nchini Tanzania*. Kioo cha Lugha, Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Juz 12: 27-47. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kihore, M. Y. (2005). *Uzingatifu wa sarufi katika tafsiri*. *Swahili Forum* 12:109-120.
- Kilonzo, J na Masaku, M. (2017). *Mwongozo wa Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*. Globalink Publishers, Nairobi, Kenya.
- Knappert, J. 1979. *Four Centuries of Swahili Verse. A Literary History and Anthology*. London /Nairobi: Heinemann. (Reprint London: Darf, 1988).
- Mandana, E. F. (2012). A Discourse Analysis of the Novel "Things Fall apart" and Two of Its Persian Translations at Micro and Macro Level <http://dx.doi.org/10.5430/elr.v1n2p13>.
- Mwansoko, H. J. M na wenzake (2006). *Kitangulizi cha Tafsiri, Nadharia na Mbinu*. Toleo la pili. TUKI: Chuo kikuu cha Dar es salam.
- Madumulla, J. (1999). *Mkaguzi wa Serikali*. Benedictine Publications Ndanda-Peramiho. Tanzania.
- Massamba, D. P. B. na wenzake (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.
- Massamba, D. P (2002). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mbaabu, I. (1985a). *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

- \_\_\_\_\_ (1991). *Historia ya Usanifishaii wa Kiswahili*. Nairobi: Longman, Kenya.
- Mbogo, E. (1980). *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Dar es Salaam University Press. Dar es Salaam.
- \_\_\_\_\_ (1993). *Morani*. Nairobi: Oxford University Press.
- McCarthy, M. (2005). *Discourse Analysis for Language Teacher*. United Kingdom: Cambridge University Press.
- Mkuwili, O. (2004). *Fani na ujumbe katika Ngoma ya Ng'wanamalundi na Kivuli Kinaishi. Utafiti Linganishi*. Tasnifu ya shahada ya Uzamili katika *Kiswahili*. Dar-es-Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mningo, R. (2015). *Mwingiliano Matini katika Utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo*. Tasnifu ya shahada ya Uzamili katika *Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mosha, E. S. (2002). *The Uses of Metaphor in Chaga Folk Tales and Oral Poetry*, Tasnifu ya Umahiri. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.
- Mohammed, S. M. (1980). *Kivuli Kinaishi*. London: Oxford University Press.
- Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies: Theories and Applications*, London and New York: Routledge.
- Mvati, et al, (2017). *Mwongozo wa Tamthilia ya Kigogo*. The National Educational Services. Nairobi.
- Murasi, M. (2013). *Kidagaa Kimemwozea: Ufafanuo kwa wasomi*. Lurambi Publishers, Kakamega.
- Mwakasaka, C. (1979). *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*. Nairobi: Heinemann Educational Books.
- Mwansoko, H. J. M. (1996). *Kitangulizi Cha Tafisiri, Nadharia na Mbinu*: Dar es Salaam: TUKI.
- Newmark, P. (1982). *Approaches to Translation*: Cambridge: Cambridge University Press.
- \_\_\_\_\_ (1988a). *Approaches to Translation*. London: Prentice Hall.
- \_\_\_\_\_ (1988b). *A Textbook of Translation*. London: Prentice Hall.
- Neubert, A. & Shreve, G. (1992). *Translation as text*. Kent: The Kent State University Press.

- Nida, E. A. (1964). *Towards a Science of Translating. With Special Reference to Bibliography 337 Principles and Procedures Involved in Bible Translation*, Leiden: Brill.
- \_\_\_\_\_ (1964). Language and Ethnology in Translation Problems. katika E.A Nida, na A. Tabor (1969). *The Theory and Practice of Translation*: Leiden: Brill.
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nyerere, J. (1969). *Mabepari wa Venisi*. Nairobi: Oxford University Press
- Olgierda, F., na Achenbach, H. (2004). <http://irg.wfc.edu/Community>.
- Omboga, Z. J. (1986). Fasihi Tafsiri Katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili; Matatizo na Athari Zake. Tasnifu ya Uzamili. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Peck, A. (1988). *Language Teachers at Work*. Hemel Hempstead: Prentice Hall.
- P'Bitek, O. (1966). *Song of Lawino*. Nairobi: East Africa Publishers.
- Picken, C. (1993). (Mh.). *Translation: The Vital Link*. London: Institute of Translation and Interpreting.
- Ray, M. K. (2008). *Studies in Translation: Its Brief History and Theory*. Delhi: Nice Printing Press.
- Reiss, K. (1989) "Text types, translation types and translation assessment": *Readings in Translation Theory*. Helsinki: Finn Lectura. 306.
- \_\_\_\_\_ (2000). *Translation Criticism: Potential and Limitations*. Rhodes, Manchester: St Jerome and American Bible Society.
- \_\_\_\_\_ (2004). 'Type, kind and individuality of text: Decision Making in Translation', In L. Venuti (ed.): 168–79.
- Saleem, M. (2013). Ujumbe na Fani katika tamthiliya za Kiswahili: Utafiti linganishi wa Tamthiliya ya *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*. Tasnifu ya Uzamifu katika Kiswahili. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Tanzania.
- Serem, D. K. na wenzake (2013). *Understanding Research: A simplified Form*. Eldoret: Utafiti Foundation.
- Shitemi, N. L (1990). *Mawasiliano katika Tafsiri: Uteuzi wa Mtafsiri*. Tasnifu ya Uzamili. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1997). Uaminifu Katika Tafsiri za Ushairi wa Jadi wa Kiswahili: Utenzi wa Inkishafi, Utenzi wa Mwanakupona na Mashairi ya Muyaka. Tasnifu ya Uzamifu. Eldoret: Chuo Kikuu cha Moi.

- Shitemi, N. L. na Wenzake (2001). *Kiswahili: A Tool for Development, Multidisciplinary Approach*. Eldoret: Moi University Press.
- Scholes, R. (1972). *Semiotics and Interpretation*. Washington DC: The Vail-Ballou Press.
- TUKI (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la kwanza. Dar es Salam: Oxford University Press.
- \_\_\_\_\_ (2004). *Kamusi ya Kiwahili Sanifu*. Toleo la Pili. Nairobi: Oxford University Press.
- \_\_\_\_\_ (2014). *Kamusi ya Kiwahili Sanifu*. Toleo la Tatu. Nairobi: Oxford University Press.
- Van Dijk, T. A. (1983). Discourse Analysis: Its Development and Application to the Structure of News. *Journal of Communication*. 33, 2: 20-43.
- Venuti, L. (1998, 1992). *Rethinking Translation: Discourse, Subjectivity, Ideology*. New York: Routledge.
- Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- \_\_\_\_\_ (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.
- \_\_\_\_\_ (2003). *Kichocheo cha Fasihi*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Weisstein, U. (1973). *Comparative Literature and Literary Theory*. Bloomington & London: Indiana University Press.
- Wellek, R. (1988). *The Crisis in Comparative Literature in Concepts of Criticism*. Haven: Yale University Press. Pg: 282-295.
- Wellek, R. & Warren, A. (1996). *Theory of Literature*. New York: Brace and Company.
- Wills, S. (1992). *Mistranslation, Missed Translation in Rethinking Translation: Discourse Subjectivity Ideology*. New York: Routledge.

## KIAMBATISHO: (DATA)

### Mfano 1

**MMS:** Hakimu .... Lakini kama ungeona moja ya makaratasi basi maisha hayangekuwa tena mazuri kama yalivyo. ---Solomon mwenyewe hangejua vipi kutofautisha ukweli na uwongo! (uk 10-11).

**MS:** Jaji... Mungu amhurumie yule atakayejaribu kuchunguza usahihi wa vitabu na stakabadhi zote zile, kwa sababu atajutia siku aliyozaliwa!-- Hata yule Mfalme Suleiman anayesemekana kuwa alijaliwa hekima tele asingeweza kuchanganua mambo ya hapa (mahakamani). (uk 15)

### Mfano 2

**MMS:** Mkuu wa wilaya:... Lakini anafundisha kwa mori kiasi cha kuwa huwezi kumwelewa. ...lakini alipomfikia Aleksanda mkuu hungeweza kuamini kabisa, nilidhani kuwa mahali panaungua moto (uk 5).

**MS:** Meya: ... Mwalimu wa somo la historia ni mwerevu sana na hulimudu somo lake lakini mbona hupandwa na jazba kiasi kwamba anapofunza, mtu atadhani kwamba shule inaungua moto? (uk 6-7).

### Mfano 3

**MMS:** Ghlestakovu:. Mungu wangu! Aina gani hii ya supu? Sidhani kuna mwingine yeyote duniani anayeweza kumeza supu hii! Shetani tu ndiye ajuaye ni nini lakini si kuku. (Uk 20).

**MS:** Hilestakov: Mungu wangu, mchuzi umeoza kabisa! ... Siamini kama mtu yeyote anayeishi amepata kuonja kitu kibaya kushinda supu hii!. Ni Mungu tu anajua, lakini si nyama. Ni ngumu kabisa! (Uk 31).

### Mfano 4

**MMS:** Mkuu wa wilaya:... Nimewalaghai walaghai kwa maelfu. Majangili na majambazi ambao wangeweza kuiba dunia nzima, wote wamenaswa. (uk 76).

**MS:** Meya: Nimewahadaa magwiji wa kuhadaa ambao wangeweza kuwahadaa binadamu wote wakaangamia! (uk 113-114).

### Mfano 5

**MMS:** Mkuu wa wilaya: ... Mungu wangu! Nilisahau. Nyuma ya uzio huo kuna lundo la takataka ambazo hata mikokoteni arobaini haiwezi kuziondoa. (Uk 12).

**MS:** Meya: Hapana, ngoja! Mungu wangu! Nilisahau kabisa kuhusu rundo la takataka zilizooza lililopo nyuma ya ule ua. Hata mikokoteni arobaini haitaweza kulimaliza rundo hilo hata kama itafanya kazi hiyo kwa wiki nzima. (Uk 17-18).

### Mfano 6

**MMS:** Ghlestakovu: Ni chumba duni kabisa. Na kunguni waliomo, sijapata kuona aina yake. (uk 25).

**MS:** Hilestakov: Kina unyevunyevu? Mahali hapa ni pito la uchafu! Na bado hujawaona kunguni-wanaouma kama mbwamwitu. (uk 37).

**Mfano 7**

**MMS:** Yosif: Ngoja kidogo, ngoja nipumue. Tumbo wazi hukifanya kila kitu kizito. (uk 32).

**MS:** Osipu: Subiri kidogo nipumue. Whuu! Mzigo mzito huu! Hata mzigo wa nyoya ungekuwa mzito kwa mtu ambaye hajatia kitu tumboni. (uk 47).

**Mfano 8**

**MMS:** Ghlestakovu:...Na mnajua niliingia idara kama tufani, kama tufani kabisa! Kila kitu kilitetemeka na kutikisika kama jani! (uk 39).

**MS:** Hilestakov: ...Na mnajua? Nilipoizungukia idara, ungedhani kama kuna tetemeko la nchi kwa jinsi watu wote walivyotetemeka kwa hofu! (uk 55).

**Mfano 9**

**MMS:** Mkuu wa wilaya: Kuna nini ambacho hawakizungumzii! Kama ungekwenda ukawasikiliza, masikio yako yangevimba. (uk 44).

**MS:** Meya: ..Sema wee, sema wee-Wanawake watasema mpaka masikio yako yang'oke! (uk 61).

**Mfano 10**

**MMS:** Ghlestakov: Hali ya hewa ni nini kwangu ukilinganisha na hiyo midomo yako ya johari? (uk 59).

**MS:** Hilestakov: Na hiyo midomo yako, bibie, ni ya namna yake; na inavutia kuliko hali yote ya hewa! (uk 86).

**Mfano 11**

**MS:** Meya: ...Kukunjakunja uso mbele ya watoto darasani huenda ni sawa kwa sababu huenda ni mbinu ya ufundishaji. Lakini je, itakuwa vipi akifanya hivyo kwa mkaguzi? -- (uk 6)

**Mfano 12**

**MMS:** Yosif (akijisemeza): Ooou! Nina njaa mno na tumbo langu linanguruma kama ngoma..Nina njaa kiasi cha kuimeza dunia! (uk 15-16).

**MS:** Osipu (akijisemeza): Mungu wangu, ubao umenishika! Jinsi tumbo langu lilivyo tupu na linavyonguruma kwa njaa, utadhani ndani yake kuna kikosi kizima cha wapiga tarumbeta! (uk 22-24).

**Mfano 13**

**MMS:** Ghlestakov: Litakuwa janga iwapo hatanipa chochote cha kula... Nasikitika kuwa Joakimu hakutaka nikodishe gari lake... Ningewatembelea wakulima wengi, nikiendesha gari mpaka milangoni kwao; wenyewe wako nyumbani?? (Uk 18-19).

**MS:** Hilestakov: Sijui nitafanyeje iwapo ataendelea kukataa? Sijawahi kubanwa na njaa namna hii katika maisha yangu yote! ...kwani ingekuwa ni fahari iliyoje kuingia kijijini kwangu nikiwa ndani ya gari...Je, familia za kichochole mpo?? (Uk 27-28).



**Mfano 14**

**MMS:** M/Wilaya... (kwake mwenyewe, akitishia kujipinga ngumi) We nyama! We juha! We hayawani! We pua nene! ...(uk 76).

**MS:** Meya...(anajitishia mwenyewe kwa ngumi) Nilimchukua yule kidudu-mtu, kitita cha takataka, kuwa ni mtu mashuhuri! (uk 114).

**Mfano 15**

**MMS:** M/Wilaya (akijiwazia) Ni shughuli mbaya sana. ...Watu mashuhuri budi wawe kitu kinachovutia macho, lakini huyu ngedere anaweza kuwa chochote! (uk 42).

**MS:** Meya (kimya kidogo): Ah, hii ni dunia ya vichekesho. Unategemea kumwona mtu wa maana na hadhi yake, kumbe ni kijitu, takataka tu! (uk 59).

**Mfano 16**

**MMS:** M/Wilaya...(kwa sauti)... Wazo jema sana hilo. Japo katika safari kuna heri na shari... (Uk 24).

**MS:** Meya...(kwa nguvu) Vema sana. Ninakutakia safari njema. Wanasema atangaye na jua hujua.. (Uk 36).

**Mfano 17**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Siyo bahati tu! Yalikuwa malipo ya juhudi na kustahili. M/Elimu (pembeni):Mwamini nguruwe kunusa chakula kinono! (uk 70).

**MS: Meya :** Upuuzi, majaliwa hayana mikono. Upuuzi kabisa. Hiyo ni tuzo muafaka kwa sifa mustahiki. Hilo ndilo jambo lenyewe. Kamishina (pembeni)...Nguruwe mchafu zaidi ndiye huzipata njugu zilizojifukia chini ya udongo. (uk 105).

**Mfano 18**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Na wewe Luka Lukichi...Najua hao ni watu waliosoma sana, wamepita katika vyuo mbalimbali, lakini tabia yao ni ya ajabu kabisa. Kuna mmoja ambaye kila wakati anakunja uso wake. (uk 4).

**MS:** Meya: Na wewe Luka Lukich-walimu wako! ...ninajuwa kuwa walimu ni werevu, wasomi na ...lakini naona wanachekesha sana. Kuna yule kwa mfano... yule mwenye pua kubwa-hawezi kusimama mbele ya darasa bila kukunja uso kiajabu ajabu. (Uk 6).

**Mfano 19**

**MMS:** Ghlestakovu: Umeweka tu maji machafu katika bakuli. Hakuna ladha; inanuka uvundo. Sitakunywa supu hii... (akikinga supu isichukuliwe): Iache, iache hayawani! ..(anaendelea kunywa) (Uk 20).

**MS:** Hilestakov: Walichofanya ni kutia tu maji ya moto katika sufuria chafu!..Inanuka shombo la vyombo vichafu! Siwezi kula supu hii.. (Akikizua chakula kwa mikono yake). Acha, acha mjinga we! (ananywa supu kidogo), (uk 31).

**Mfano 20**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ..Ungeona jinsi mambo yanavyotekelezwa humu! Kila kitu kiko katika hali safi. (uk 26).

**MS:** Meya (pembeni): nitazame mimi kwa mfano ninaweza kukesha usiku kucha kwa kuitumikia nchi yangu kwa hali na mali. (uk 37).

**Mfano 21**

**MMS:** M/Elimu: ...Nilimzungumzia kuhusu jambo hili mara moja, ule wakati ambapo mwana wa mfalme alitutembelea. Huyu bwana alikunja uso sijapata kuona! Nilisutwa kwa kuwaacha vijana wafunzwe tabia ya kinyama na kishetani. (uk 4-5).

**MS:** M/Mashule: ..Nimemwonya mara kadha lakini hasikii. Siku moja Liwali alipoitembelea shule mwalimu huyo alikunja uso kiasi cha kutisha hata huyo mgeni rasmi akanishtaki kuwa tumemwajiri mwalimu mwenye fikra huria kufundisha watoto wetu. (uk 6).

**Mfano 22**

**MMS:** Yosif: Ooooo! Nina njaa mno na tumbo langu linanguruma kama ngoma. Na haielekei kuwa tutafika nyumbani kama mambo ndiyo hivi. Ni miezi miwili tangu tuondoke Pitasbag. (uk 15-16).

**MS:** Osipu: Mungu wangu, ubao umenishika! Jinsi tumbo langu lilivyo tupu na linavyonguruma kwa njaa, utadhani ndani yake kuna kikosi kizima cha wapiga tarumbeta! ...Huu ni karibu mwezi wa pili tangu tulipoondoka Petersburg. (uk 22-23).

**Mfano 23**

**MMS:** Ghlestakov: ...Na mnajua niliingia idara kama tufani, kama tufani kabisa! Kila kitu kilitetemeka na kutikisika kama jani! (Uk 39).

**MS:** Hilestakov: ..Na mnajua? Nilipoizungukia idara, ungedhani kama kuna tetemeko la nchi kwa jinsi watu wote walivyotetemeka kwa hofu! (uk 55).

**Mfano 24**

**MMS:** Ghlestakov: Rafiki mpendwa Ryapitikini ...Unakumbuka tulipokuwa sote tumefilisika na mwoka mikate akanitupa nje kwa kujaribu kumkopa katika jina la Mfalme wa Uingereza? (uk 73).

**MS:** Hilestakov: “Mpendwa Tryapichkin, ...Kumbuka siku ambazo tulikuwa tumebanwa tuliishi kwa akili zetu na siku ambayo yule mwandalizi wa tamutamu alitutupa nje kwa sababu nilimwambia “atupatie zile sambusa kwa bili ya Mfalme wa Uingereza”! (uk 109).

**Mfano 25**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Hapana, hapana ...Nimepata matatizo hapo awali, lakini nimepita katika yote. (uk 10).

**MS:** Meya: Potelea mbali na heshima. ...Tumewahi kuwa katika matatizo makubwa sana wakati mmoja hapo nyuma na wakati wote nilifaulu kuwatoeni salama. (uk 14).

**Mfano 26**

**MMS:** Yosif: Ni jenerali, kwa kweli, ndani na nje na kutoka nyuma hadi Mbele, (uk 33).

**MS:** Osipu: O, ni Jenerali kwa namna nyingine, (Uk 47).

**Mfano 27**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ... Si muda mrefu nitamwoza binti yangu lakini si kwa kabaila mdogo yeyote. Tayarisheni sawasawa hongera, mnaskia? (uk 67).

**MS:** Meya (kwa wenye maduka): ...Lakini chungeni sana kuanzia sasa! Binti yangu haolewi na mshamba kumbukeni hilo-hakikisheni kuwa hongera zenu ni zile zinazostahili-mnaelewa? (uk 101).

**Mfano 28**

**MMS:** Bw Posta: Si hiki wala kile. Ibilisi tu ndiye ajua yeye ni nani! (Uk 72).

**MS:** Mkuu wa Posta: Si chochote, si lolote! Sijui tumwiteje? (Uk 108).

**Mfano 29**

**MMS:** Bw Huruma (pembeni): Jinsi anavyoogopa! Mtu duni huyu! hakika yeye ni ibilisi aliyepewa ulimi mtamu na Mungu. (uk 35).

**MS:** Kamishina (pembeni): Msikilize anavyojjenga! Kipawa hicho ama anacho! (uk 50).

**Mfano 30**

**MMS:** Bw Huruma: ...Mchukue Mratibu wa Elimu hapa ...Sijui ni kwa nini miujiza kabisa! Tazama hayuko tofauti na nyapara na ile shule yake ni chemchemi ya mapinduzi, (uk 71).

**Mfano 31**

**MMS:** Mkuu wa wilaya: ... Najua kuwa walimu ni watu waliosoma sana, wamepita katika vyuo mbalimbali, lakini tabia yao ni ya ajabu kabisa. Labda hiyo ndiyo hali ya kawaida ya watu waliosoma sijui. Kuna mmoja ambaye kila wakati anakunja uso wake. (Uk 4).

**MS:** Meya: .ninajuwa kuwa walimu ni werevu, wasomi na ...lakini naona wanachekesha sana. Kuna yule kwa mfano... yule mwenye pua kubwa-hawezi kusimama mbele ya darasa bila kukunja uso kiajabu ajabu. Hufanya hivi (anaigiza namna ya kukunja uso). (Uk 6).

**Mfano 32**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ...Lakini nitawasomea barua ambayo nimeipata sasa hivi kutoka kwa Chimihovu. (Uk 1).

**MS:** Meya: .Na leo hii asubuhi imefika barua hii kutoka kwa Chimikov.(uk 1).

**Mfano 33**

**MMS:** Bw Posta: Hapana. Lakini kuna habari nyingi kuhusu walioko Kostroma na Saratovu. Ni jana tu Luteni mmoja alimwandikia rafiki yake kuhusu mpira katika lugha maridadi sana, fasaha kabisa. (Uk 6).

**MS:** Mkuu wa Posta: Hapana sijaona. Lakini kumekuwa na barua nyingi juu ya maafisa kutoka Saratov na Kostroma. Baadhi ya barua zao ni nzuri sana. ...Na kulikuwa na barua moja kutoka kwa Luteni kwenda kwa rafiki yake ikieleza juu ya ukumbi wa muziki alikopata kwenda. (Uk 9).

**Mfano 34**

**MMS:** M/Wilaya (kichinichini kwa Dob): Sikiliza. Nitaandika vikaratasi viwili vya ujumbe ambavyo lazima vipelekwe haraka unavyoweza. Kimoja kwa Zemlyanika huko hospitalini, na kingine kwa mke wangu. (uk 27).

**MS:** Meya (pembeni kwa Dob): Sikiliza, kimbia kama upepo uende nyumbani kwangu kutoa habari juu ya ugeni. (Uk 39).

**Mfano 35**

**MMS:** Ghlestakovu (kwa Tyapitkini kupitia barua): Rafiki mpendwa Tyapitkini: Lazima nikuandikie kukueleza visa vyangu vipya. (uk 73).

**MS:** Hilestakov (Kwa Tryapichkin kupitia barua): “Mpendwa Tryapichkin, mambo asiyo ya kawaida yamekuwa yakinitokea” (uk 109).

**Mfano 36**

**MMS:** Bw. Posta (akiisoma barua).....! Kwanza kuna huyu Mkuu wa Wilaya: ni mtu karimu, wema wake ni kama shoka la mchinja ng’ombe, lakini ni mpumbavu kama punda kihongwe!” (uk 73).

**Mfano 37**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ...Lakini nitawasomea barua ambayo nimeipata sasa hivi kutoka kwa Chimihovu. (Uk 1).

**MS:** Meya: ...Na leo hii asubuhi imefika barua hii kutoka kwa Chimikov. (Uk 1).

**Mfano 38**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Ndiyo ndiyo. Sasa mchukuwe mwalimu wa historia. Ni mtu mwenye uwezo mkubwa sana anayejua somo lake barabara, lakini anafundisha kwa mori kiasi cha kuwa huwezi kumwelewa. (uk 5).

**MS:** Meya: Hiyo ni mbaya! Mbaya sana. Je, na yule mwalimu wa historia? Ni mwerevu sana, mwenye akili mno, ambaye nina hakika analimudu somo lake barabara. Lakini kwa nini hupandwa na jazba? (uk 6-7).

**Mfano 39**

**MMS:** Mpishi: Sawa, vipo na tena havipo. (Uk 19).

**MS:** Mhudumu: Kiko, mzee, lakini vilevile hakiko. ( Uk 30).

**Mfano 40**

**MMS:** Bw Posta: Sauti ililia katika sikio moja: “Usiifungue!” na nyingine ilisema: ifungue! Ifungue!” (uk 72).

**MS:** Mkuu wa Posta :..Ndani ya sikio moja kulikuwa na sauti iliyoninong’oneza usiiguze hiyo lakiri, utajitia matatizoni ukifanya hivyo,” lakini ndani ya sikio jingine sauti nyingine yenye nguvu zaidi ilinong’ona, “ Hebu basi, vunja hiyo lakiri na kuifungua barua!”. (uk 108).

**Mfano 41**

**MMS:** Hakimu: Ndiyo, si muda mrefu kutakuwa na matatizo. Ehee Antoni Antonovichi, nilikuwa njiani kuja kukuonyesha mbwa wangu jike, mgeni, dada kabisa wa yule unayemwelewa. Na umeskia juu ya kesi ya Cheptovichi na Valinski? (Uk 7).

**MS:** Jaji: .. Antoni Antonovich, nilitaka kukupatia zawadi ndogo tangu zamani kidogo, lakini nimekuwa nikisahau. Kijibwa kizuri, ambacho ni mbegu ya lile jibwa kubwa la kwangu. Na kuhusu uwindaje, mimi sasa ni mashuhuri. Je, unajua kwamba Cheptovich amemshtaki Varhovinski? (Uk 10).

**Mfano 42**

**MMS -** Mkuu wa Wilaya: ...Jana nili...” Yafuatayo ni mambo ya kifamilia, “Binamu yangu Anna Kirilovna na mumewe wanaishi nasi. Mumewe amenenepa sana na kutwa anapiga zeze,” na kadhalika. (Uk 2).

**MS:** Meya: ...! Dada yangu Anna Krilovna na mumewe Ivan wanakaa pamoja nasi. Ivan Krilovich ameongezeka sana uzito, na haachi kupiga fidla...” Naam, yaliyobaki ni maswala ya kifamilia tu kama mnavyoonna. Hapo ndipo mwisho. (Uk 3).

**Mfano 43**

**MMS:** M/Wilaya: ...Lakini wewe... unapoanza kuzungumzia juu ya kuumbwa kwa ulimwengu, unazifanya nywele zangu zisimame. (Uk 4).

**MS:** Meya: Wewe je?...wewe unapoanza kuzungumza juu ya uumbaji wa dunia, unafanya nywele zangu zisisimke! (Uk 6)

**Mfano 44**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ...Usiku mzima uliopita nilikuwa nikiota juu ya panya wawili wakubwa sana. Hakika sijapata kuona madude makubwa kama yale, panya wakubwa sana weusi! Walifika, wakanusanusa na kuondoka wakatoweka. (uk 1).

**MS:** Meya: Jana usiku niliota ndoto juu ya mapanya-buku. Walikuwa ni mapanya-buku wawili weusi wakubwa mno ambao sijapata kuwaona maishani mwangu. ...Wakainua pua zao kubwa na kunusanusa kwa namna ya kutisha-kisha wakageuka, haooo, wakaenda zao. (uk 1).

**Mfano 45**

**MMS:** M/Wilaya: Wakati mmoja nililazimika kuwafurahisha watoto fulani na nikawajengea nyumba ya karata, lakini niliporudi kulala nilipatwa na jinamizi. (uk 35).

**MS:** Meya: Wakati mmoja nilitaka kuwafurahisha watoto kwa kuwajengea nyumba kwa kutumia karata. Unajua matokeo yake? Niliota juu ya karata usiku mzima. (uk 50).

**Mfano 46**

**MMS:** Mkuu wa wilaya: Eee Mungu! niepushe na mikono yao wakati huu na nitawasha mshumaa mkubwa kuliko yote uliyopata kuiona! Nitamlazimisha kila mshenzi mfanyabiashara kuchanga kilo hamsini za nta (uk 13).

**MS:** Meya: Ikiwa Mungu atatusaidia tukaondokana na balaa hili, nitamlazimisha kila fanyabiashara atoe kilo kadhaa za nta ya kutengenezea shumaa hilo. (Uk 18).

**Mfano 47**

**MMS:** Mkuu wa wilaya: Majuma mawili! ...! Na muda wote huo wafungwa hawajalishwa! (Uk 10).

**MS:** Meya:...! Wiki mbili nzima! ... Wafungwa walinyimwa chakula. (uk 14).

**Mfano 48**

**MMS:** Mkuu wa wilaya: ... Amosi Fyodorovichi, mtumishi wako anafuga bata katika vyumba vya ndani pamoja na kuku, na wanazururazurura wakiokota miguuni pako.. lakini hawezi kufuga mahali pengine? Wanapafanya panuke mno. (uk 3).

**MS:** Meya: ...chumba chako cha mahakama kimejaa uchafu! Mwambie mlinzi wako awahamishe bata mzinga wake kutoka pale barazani. Wateja wanapokuwa pale bata-mzinga hao huwadonadona miguu yao kutwa nzima. (uk 4).

**Mfano 49**

**MMS:** Mfanyabiashara 2: Hasa! Lakini ukidiriki kusema neno atakutumia kikosi kizima cha rungu. Ama la sivyo ataifunga biashara yako. (uk 55)

**MS:** Abdullin: Lakini hatuthubutu kulalamika, Mheshimiwa atakuletea kikosi kizima cha askari ukigundulika kuwa umefanya hivyo au hata kufunga biashara yako... (uk 81).

**Mfano 50**

**MMS:** Mkuu wa wilaya (kwa Abdulin): ...nilikusaidia beberu we! Na pia naweza kukupeleka jela. Unasemaje? (uk 67)

**MS:** Meya: Mnataka kulalamika, siyo? (akimwandama tena Abdulin) Nadhani ulisahau hilo? Ninaweza kunong'ona tu na ninyi nyote mkajikuta mko Siberia! Mnaonaje kuhusu hilo? (Uk 101).

**Mfano 51**

**MMS:** Mkuu wa wilaya: ... kile ambacho Chimihovu anakiita “chembe za udhaifu” Ni mapenzi ya Mungu..Hakimu: Nakubali wazi kuwa napokea hongo, lakini aina gani ya hongo? Vimbwa vidogo na sio zaidi! (uk 4).

**MS:** Meya: ...Na hilo ambalo Chimikov analiita “upungufu wetu mdogo” Jaji: Mimi sijali kukiri wazi kuwa huwa ninapokea rushwa lakini ni kutoka kwa wale watu wenye uwezo tu; na hiyo huwezi kuita dhambi. (Uk 5).

**Mfano 52**

**MMS:** Bw Huruma: Sijui unawaza nini Amosi Fyodorovichi, lakini naona afadhali tufanye chochote. Hakimu: una maana..? (akionyesha ishara ya kula, kama hongo). (uk 45)

**MS:** Kamishina: ... mpaka hapo umefanya vizuri sana, Amos Fyodorov lakini ninadhani kwamba inafaa tufanye kitu fulani zaidi...kitu fulani. Jaji: kitu gani?. Kamishina: unajua nina maana gani. Jaji: (akifikicha dole gumba na cha shahada) kitu kama...eh? Kamishina: Naam, ama siyo? (uk 63)

**Mfano 53**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ...(akimgeukia Bwana Huruma) Hasa wewe, Artemi Filipovich: ni dhahiri kuwa huyo mgeni atayakagua mashirika yako, na Tafuta mavazi na nguo za kutandika safi..Na ingefaa wagonjwa wenyewe waonekane afadhali kidogo kuliko wakoka makaa. (uk 2)

**MS:** Meya .. Na hasa wewe Artemi Philipovich! (Kwa Kamishina). Huyu Mkaguzi kwa hakika ataitembelea sehemu yako, kwa hiyo ingefaa uhakikishe kuwa kila kitu ni safi. Wapatie wagonjwa wako mashuka safi na waogeshwe vizuri. Nilipowaona safari iliyopita walikuwa kama wamepakwa masizi! (Uk 4).

**Mfano 54**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya (kwa Hakimu): na wewe unapaswa kufanya kitu kuhusu hali ya mahakama yako, Amosi Fyodorovich. Mtumishi wako anafuga bata katika vyumba vya ndani pamoja na kuku, na wanazururazurura wakiokota miguuni pako. Lakini hawezi kufugia mahali pengine? Wanapafanya panuke mno. (uk 3)

**MS:** Meya: Ehee, na wewe Amosi Fyodorovich, bora na wewe uanze kurekebisha mahakama yako. Mahakama yako ni kama shamba kabisa. Mwambie mlinzi wako awahamishe bata-mzinga wake kutoka pale barazani. Wateja wanapokuwa pale, bata-mzinga hao huwadonoadonoa miguu yao kutwa nzima, (uk 4).

**Mfano 55**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Halafu ofisi zako zimejaa kila aina ya takataka. Ngozi zilizotundikwa ili zikauke, mijeledi, na vifaa vingine vya kuwindia vikichanganyika na makaratasi...huyo karani wako! Anaweza kuwa mjuzi sana, lakini anatoa harufu kali mno ya vodka. (uk 3).

**MS:** Meya: (Akiupuza mwaliko). Amosi Fyodorovich, chumba chako cha mahakama kimejaa uchafu! Zana zako za kuwindia zimezagaa ovyoovyo, hatamu na matandiko viko kwenye shubaka la stakabadhi muhimu...Yaani ni mchafukoge mtupu. Na yule karani wako! Ni mwerevu sana yule, lakini kutwa kucha ananuka pombe! (uk 5)

**Mfano 56**

**MMS:** M/Wilaya: Majuma mawili! Mama yake Mungu! Na muda wote huo wafungwa hawajalishwa! Mke wa sajenti amechapwa! Mitaa haijafagiliwa! Mji wote ni kama zizi. Aibu! (Uk 10).

**MS:** Meya: Mungu, Yesu na Maria tulindeni! Wiki mbili nzima! Katika kipindi hicho mke wa sajenti alicharazwa bakora, wafungwa walinyimwa chakula, mitaa haikufagiliwa, mji mzima ulikuwa kama jaa la taka. Ooo, aibu gani hii! Ni kuvunjika gani kwa heshima! (Uk 14).

**Mfano 57**

**MMS:** M/Wilaya: ...(Anaguna) sasa kama huyu Mkaguzi anamuuliza askari polisi yeyote, “Umeridhika?” lazima waseme, “Tumeridhika kabisa, Mheshimiwa.” Na kama yeyote hajaridhika kabisa nitawapa chochote cha kuridhisha. (Uk 13).

**MS:** Meya:...(Anapumua kwa nguvu)...kama Mkaguzi huyu akija kuwapeleleza watu wako kwa kuwauliza kama wanafurahia kazi yao, hawana budi kujibu haraka, “Ndiyo, Mheshimiwa, tuliifurahia mno.” Na kama kuna mtu atasema haifurahii kazi yake, basi mwambie huyo mtu kuwa nitamfanya asiifurahie kazi yake baadaye. (uk 18).

**Mfano 58**

**MS:** Meya: Sijawahi kushika karata tangu kuzaliwa na hata kama ningeishika singejua nifanye nini nayo! .. wakati mmoja nilitaka kuwafurahisha watoto kwa kuwajengea nyumba kwa kutumia karata. Niliota juu ya karata usiku mzima (uk 50)

Mkaguzi: (pembeni): huyu Bwana! Jana tu jioni amenichomoa laki mbili katika mchezo wa karata, (uk 50).

**Mfano 59**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Sawa sawa, hili ni kasha. Jamani! (akivaa kofia yake) sasa kumbuka, mtu yeyote akiuliza ni kwa nini kanisa la hospitali ambalo tulipata fungu lake miaka mitano iliyopita halijajengwa, jibu ni kuwa lilianzishwa lakini likaungua moto. (Uk 13).

**MS:** Meya: (Akilivurumisha chini kasha) Na jua, mjinga wee! Sikiliza. Nimepata wazo jingine. Kama Mkaguzi huyu atauliza juu ya kanisa kwa ajili ya hospitali – unajua ile ambayo tulipatiwa fedha tuijenge miaka mitano iliyopita- usisahau iliteketezwa na moto.(uk18).

**Mfano 60**

**MMS:** Ghlestakovu: Karibu. Kaa chini. Karibu sigara. (uk 47).

**MS:** Hilestakov: Haya haya chukua! Si sigara mbaya huwezi kuilinganisha hata hivyo na zile za Petersburg. (uk 69).

**Mfano 61**

**MMS:** Bob: ...Pita Ivanovichi alikuwa amepata habari zote kutoka kwa mtumishi wako Avdotya ambaye alikuwa ametumwa kwa Pochechuevu ..Dob: Kuchukuwa mtungi wa kuweka mvinyo wa kifaransa. (uk 8).

**MS:** Bob: ...Kumbe Peter Ivanovichi alikuwa amekwishaelezwa kila kitu na mtumishi wako wa nyumbani (Kwa Meya), Avdotya ambaye alikuwa ametumwa kwa Philip Antonovichi Pochechuev ...Dob: Kuchukuwa kasiki la vodka. (uk. 11)

**Mfano 62**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ..Yuko wapi askari mwingine? Nilimwambia Prohorovu kuwa hapa. Yuko wapi? Askari: Wamemleta asubuhi hii amelewa taabani. Amenyunyuziwa bakuli mbili za maji baridi lakini hata hivyo mpaka sasa hajapata fahamu. (uk 11)

**MS:** Meya: ..Hivi polisi wote wamekwenda wapi? Prohorov yuko wapi? Aliambiwa awepo hapa. Sivistunov: Yuko stesheni afande na hawezi kutumwa. Meya: Hawezi? Una maana gani kuwa hawezi? Sivistunov: Aliletwa akiwa amelewa chakari leo asubuhi Afande. (uk 15).

**Mfano 63**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ...Na kuhusu mke wa Sajeni, habari kuwa niliamuru achapwe ni uongo mtupu. Uzushi! Ni kubuni kwa maadui zangu. Watu kama hao! Kila siku napita nikiwa na hofu ya kuuawa. (uk 22-23).

**Mfano 64**

**MMS:** Bw Posta: ..Sijawahi kuwa na hofu hivyo maishani ...Na nilipokuwa naibandua gundi, moyo ulipita katika mishipa yangu nikajisikia mwili mzima ukiwa moto. (Uk 72).

**MS:** Mkuu wa Posta: Mimi mwenyewe sijui.. Mara nilipoiguza ile nta, damu yangu ilichemka kama vile imo ndani ya moto. Nafungua barua, si kutetemeka huko kama vile mwili wote ulikuwa ndani ya barafu. Nilikaribia kuzimia! (uk 108).



**Mfano 65**

**MMS:** Anna: wamekwenda wapi? (akifungua mlango) Antoni! Baba? (kwa Marya). Kila wakati kupoteza muda ukipekuapekua kutafuta pini na vidani. (uk 13).

**MS:** Ann: (akisema nje)...wamekwenda wapi watu wote? (anaingia kupitia mlango) Antoni! Antoni kipenzi! Toni! Uko wapi jameni? (kwa Maria, haraka) “Hebu nisubiri nijifunge hiki...Hebu nijifanye vile...!” (Uk 20)

**Mfano 66**

**MMS:** Ghlestakovu: Umevaa mkufu maridadi sana. (uk 59).

**MS:** Hilestakov: Shela ulilovaa ni zuri kwelikweli! (uK 86)

**Mfano 67**

**MMS:** Mke wa Mhunzi: Alipaswa kumchukua mwana wa Fundi Cherehani yule mlevi kupindukia lakini wazazi wake walimshawishi (ishara ya hongo) amwache; halafu akamchukua mwana wa Mshona Urembo lakini mamaye alimpelekea doti tatu za hariri mkewe; kwa hiyo akaja kwetu. (uk 57).

**MS:** Mke wa Fundi: ...bora angemchukua mtoto wa fundi cherehani yule ambaye si lolote bali ni ulevi tu. Ni kwa sababu tu wazazi wake walikuwa na uwezo wa kuhonga ndio maana akamng’ang’ania mtoto wa mchuzi wa nguo. Lakini mama yake ambaye ni mjane alituma majola matatu ya kitambaa kizuri cha kitani kwa mke wa Meya. (uk 83).

**Mfano 68**

**MMS:** Ghlestakovu: Huelekei kuwa mpenzi wa sigara. Sigara ndio udhaifu wangu. Na kama kawaida mabibi pia. Siwezi kujizuia. (uk 48).

**MS:** Hilestakov: Hayo ni matatizo yangu pia. Na tatizo jingine (anainama mbele) ni wanawake! Ah! Siwezi kujizuia kwa mwanamke mzuri. (uk 69).

**Mfano 69**

**MMS:** Mke wa Mhunzi: ... “Mumeo ni mwizi,” anasema, “Lakini bado hajaiba chochote; lakini yote ni mamoja, ataiba siku moja.” “Na mimi nabaki hapa bila mume, mwanamke mnyonge na dhaifu,” nilimwambia. Mke wa Sajeni: Ni huyu Mkuu wa Wilaya, bwana mkubwa. Aliamuru nichapwe; mtu katili...! (uk 57)

**MS:** Mke wa Fundi, Alimpeleka mume wangu jeshini. Ndilo hilo heshimiwa. Yeye (mume wangu) ameo, hivyo ni kinyume cha sheria kupelekwa jeshini. Mjane: Aliagiza nicharazwe bakora mheshimiwa. (uk 83- 84).

**Mfano 70**

**MMS:** Anna: Utakuwa na marafiki tofauti. Hakutakuwa na mahakimu wa kawaida wanaonuka harufu ya mbwa ambayo ni sumu kwa sungura au yule Zemlyanika mchafu. Rafiki zako watakuwa watu wa hali ya juu sana mawaziri na watu wengine wa jiji. (uk 65).

**MS:** Ann: ...Marafiki zetu watakuwa si wale tena akina domo-kaya ambao hawafikirii lolote zaidi ya kuwinda sungura. Marafiki zetu sasa watakuwa ni watawala ambao wana tabia za kistaarabu. (uk 98).

**Mfano 71**

**MMS:** Mke wa Sajeni: Ni huyu Mkuu wa Wilaya, Bwana Mkubwa. Aliamuru nichapwe, mtu katili! (uk 57).

**MS:** Mjane: Aliagiza nicharazwe bakora mheshimiwa kiasi kwamba nisiweze kuketi. (uk 84).

**Mfano 72**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: mtapaswa ku... Hakikisha kuwa hakuna yeyote anayeingia akiwa na maombi au bila maombi, au hata yeyote anayeelekea kuleta maombi dhidi yangu, watupwe nje kichwa kikitangulia, mnaelewa? (akionyesha teke la nguvu) kama hivyo. Mnaskia? (uk 41).

**MS:** Meya: Mkimwona yeyote akija hapa na kitu chochote hasa kama ni malalamiko dhidi yangu, muondoeni kwa nguvu na kumtupa nje. Fanyeni hivi, mnaona? (anampiga teke mtu asiyekuwepo). (uk 62).

**Mfano 73**

**MMS:** Abdulini: Hajatokea Mkuu wa Wilaya kama yeye, anayetunyanyasa kwa kututumia askari wenye rungu...Anatuvuta ndevu na kutukemea:  
Mfanyi biashara 2: Hasa! Lakini ukidiriki kusema neno atakutumia kikosi kizima cha rungu... (Uk 55)

**MS:** Abdulin: Mheshimiwa!Hapajawahi kutokea Meya Mkuu wa Wilaya mwovu kama huyu, Lakini hatuthubutu kulalamika, Mheshimiwa. Atakuletea kikosi kizima cha askari ukigundulika kuwa umefanya hivyo, au hata kufunga biashara yako, (uk 80-81).

**Mfano 74**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya:.. nitamlazimisha kila mshenzi mfanya biashara kuchanga kilo hamsini za nta. (uk 13).

**MS:** Meya:nitamwamuru kila mfanyi biashara atoe kilo kadhaa za nta ya kutengeneza shumaa hilo, (uk 18).

**Mfano 75**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Sasa kama huyu Mkaguzi anamwuliza askari polisi yeyote, “umeridhika?” lazima waseme, “tumeridhika kabisa mheshimiwa.” (uk 12-13).

**MS:** Meya: Sasa jambo jingine, kama Mkaguzi huyu akija kuwapeleleza watu wako kwa kuwauliza kama wanaifurahia kazi yao, hawana budi kujibu haraka, “Ndiyo, Mheshimiwa, tuliifurahia mno.” (uk 18).

**Mfano 76**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: ... hata ninapoingia kitandani kulala, daima nawaza, “Eee Bwana Mungu, kama ningepata asante ya wakubwa wangu kwa ajili ya juhudi yangu, hilo lingetosheleza. (uk 34-35).

**MS:** Meya... Kuna mameya wengi ambao hupenda kujifanyia mambo ya kunufaisha nafsi zao wenyewe; lakini mimi nilalapo kitandani huwa ninawaza jambo moja tu: “Mungu uliye Mkuu” huwa ninajiwazia “nisaidie ili niweze kuwafurahisha wakubwa zangu!” (uk 49-50).

**Mfano 77**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya ... (Kwa mfanyabiashara 2)... Na jinsi unavyofutua tumbo! (kwa mfanyabiashara 3). Nguruwe we!... Na kadri tumbo lako linavyovimba ndivyo kadri unavyojiongezea maringo. Dude we! (Kwa Abdulin) ...Nilikusaidia beberu we! (uk 66-67).

**MS:** Meya.. (kwa wenye maduka) ... Nyie wabugia chai, waruka makaunta,na wachuuzi wapunjaji, kwa nini mliamua kulalamika dhidi yangu? Enyi wahuni, enyi panya buku msiyu adabu mtambao na nyuso mbili! Takataka! (uk 98-99).

**Mfano 78**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Ni wajibu wangu kama mkuu wa wilaya hii, kuona kuwa wasafiri na watu wengine wa maana hawapati tatizo. (Uk 21).

**MS:** Meya (kwa Hilestakov): Tumepita tu mara moja, mimi na Peter Ivanovich, Dobchiniski-huyu hapa, tumepita ili kuona jinsi wageni wanavyohudumiwa...hiyo ni sehemu ya majukumu yangu (Uk 36).

**Mfano 79**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya ... Kama nimepokea hongo ni zile ndogo ndogo tu chochote kwa chakula au kipande cha nguo. (uk 22)

**MS:** ...na kama nimepata kupokea rushwa ni kidogo mno kwa ajili ya chakula, kitambaa cha koti.vitu vidogovidogo namna hiyo. (uk 34)

**Mfano 80**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya (Kwa Abdulini): Ni nani aliyekufunza jinsi ya kuchuma katika zabuni ile ya daraja ulipoandika bei ya mbao kuwa shilingi 20,000 wakati hazikuwa na thamani ya mia! Nilikusaidia beberu we! (uk 67).

**MS:** Meya (anamkabili abdulini): wewe ni mdhulumaji. Unapata malaki ya fedha kutokana na mkataba wa serikali ambapo wewe hutoa mali mbovu, nawe ukanihonga yadi ishirini za mali hiyo isiyofaa na kutarajia upate medal? (uk 99).

**Mfano 81**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya:... Shiii, ninyi!Vistoonovu na Dyerizimoda! Panda huku mara moja! (hatua zinasikika na mara wanaingia askari wawili) Shiii! Shiii! Dubu nyie! (uk 41).

**MS:** Meya: Shhhh! Acheni kelele nyie kenge! Mnaingia hapa kama mkokoteni uliojaa magogo. Shetani awapelekeni wapi? (Uk 61).

**Mfano 82**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Nenda mitaani na ... hapana usiende. Nenda ukalete ...Yuko wapi askari mwingine? Nilimwambia Prohorovu kuwa hapa. Yuko wapi? ( uk 11)...Wambie walinzi kuleta mitaa na kusafisha fagio- oh, sasa nasema nini? ...Waambie wafagie mitaa.... (uk 12).

**MS:** Meya: Naam, nenda nje na..hapana, ngoja. Usiende. Subiri. Eee kaniitie..Hivi polisi wote wamekwenda wapi? Prohorov yuko wapi? Aliambiwa awepo hapa..(Akimgeukia Sivistunov tena) Nenda uwatafute polisi waliobaki na kuwatuma washike mtaa mmoja kila mmojawao...ah, hivi nasema nini! Wapatie fagio wafagie mitaa. (uk 15 -16).

**Mfano 83**

**MMS:** Ghlestakovu: (kwa Hakimu) Sikiliza, nitazichukuwa kama mkopo...Nitazituma kwako nifikapo nyumbani...(Kwa M/Elimu) ...Unajua jambo la kipumbavu limenitokea nikiwa safarini kuja huku... Unadhani unaweza kunikopesha tuseme shilingi 400? Nitazirudisha mara tu nifikapo nyumbani. (Uk 47- 48).

**MS:** Hilestakov: (Kwa Jaji) Tazama Jaji, unaweza kuniazima fedha hii...kwa muda mfupi? ...Nitakurejeshea mara nifikapo nyumbani. (Kwa Mkuu wa Posta) ...Unajua jambo la ajabu sana lilinitokea jana. ... Je, unaweza kuniazima rubuli kama mia tatu hivi? (uk 66 -68-72).

**Mfano 84**

**MMS:** Ghlestakovu: Lakini niambieni, hamna njia zozote za kupotezea muda? Kiburudisho chochote? Hamkusanyiki kamwe na kucheza kamali? (uk 35).

**MS:** Hilestakov: Hebu niambie, hakuna burudani katika mji huu. Yaani, sehemu ambazo mtu anaweza akapigapiga karata hivi au kitu cha namna hiyo. (uk 50).

**Mfano 85**

**MMS:** Ghlestakovu: Ndiyo, kuna giza. Lakini tajiri anakataa kunipa mishumaa. Kila mara nitakapo kufanya lolote, kusoma kidogo au ninaposkia wito wa kuandika, siwezi; kuna giza mno, giza mno. (uk 25).

**MS:** Hilestakov: Huyu tajiri mlaanifu hanipi hata mshumaa wa kusomea. Kuna wakati ambapo mtu hujiskia ustaarabu-kusoma insha moja au mbili, kusanifu kijishairi, lakini hapa haiwezekani, ni giza mno. (uk 37).

**Mfano 86**

**MMS:** Ghlestakovu: (Kwa woga) ...Na kama atanifanya nipelekwe jela? na kwa kweli nimekuwa nikionyesha mitindo na kufanya mahaba na binti ya mfanya biashara hapo jirani. (uk 21).

**MS:** Hilestakov: (anaogopa) Nini? Haiwezekani!.. Hapana! Hapana! Siwezi kwenda jela. Nisije nikaonekana na maafisa, au yule binti mzuri wa mchuuzi wa mbegu, binti ambaye nimekuwa nikitembea naye. (Uk 32).

**Mfano 87**

**MMS:** Ghlestakov: (kwa Yosif) ...Na binti anaonekana mzuri kabisa na nadhani mama mwenyewe yuko tayari kwa lolote. (uk 46).

**MS:** Hilestakov: ..Nipo hapa ....nikiwatongoza mke wake na binti yake, wote kwa wakati mmoja! Sijaamua nianze kwenda na yupi-huenda mke wake ni mzuri zaidi, anaelekea kuwa yuko tayari kwa lolote! (Uk 109).

**Mfano 88**

**MMS:** Ghlestakovu (pembeni): Na yeye pia kidosho hasa; si mbaya hata kidogo! (akipiga goti) Bibie, unaona, penzi linanichoma moyo! (Uk 60).

**MS:** Hilestakov (pembeni): Na yeye anavutia si haba-mm, mm, si mbaya hata kidogo... (anaelekea kwake kwa maoni). Bibie, huoni ninavyokufa kwa mapenzi! (Uk 88).

**Mfano 89**

**MMS:** Mkuu wa wilaya: (kwa wafanya biashara) Oh, acha kufanya ghasia sasa. Mnajua kuwa yule mkaguzi mliyemkimbilia mkiomboleza anatarajia kumwoa binti yangu? Mnasemaje sasa? (Uk 66).

**MS:** Meya: (ameudhika) Sijali kuhusu maneno sasa hivi! (Kwa wenye maduka) Mlijuwa kwamba yule Mkaguzi wa Serikali mliyempelekea malalamiko yenu atamwoa binti yangu? Mlijua hilo? (Uk 99).

**Mfano 90**

**MMS:** Ghlestakov: Hilo si kitu. Kuolewa tu ni nini ukilinganisha na penzi la milele? Tutakimbilia mbali kwenye bonde zuri lililo na kivuli tulivu, karibu na kijito safi. Naomba mkono wako. (Uk 60).

**MS:** Hilestakov: Ni kweli inawezekana, ewe bibie mpendwa! Tutaruka pamoja, mkono kwa mkono, hadi kwenye kijito kibubujikacho... mkono wako, tafadhali mkono wako! (uk 89).

**Mfano 91**

**MMS:** Ghlestakov: Kwa kweli sijui. Unajua, baba yangu ni mpumbavu na mkaidi kama pande la gogo. Lakini nitamweleza ukweli, ...lakini mimi siwezi kuishi mbali na Pitasbag. (uk 24).

**MS:** Hilestakov: Kwa kweli sijui. Baba yangu ni mjinga kama punda, na ukaidi wake hali kadhalika. Anaweza kusema atakalo. Lakini siwezi kuishi mahali pengine isipokuwa Petersburg. (uk 36).

**Mfano 92**

**MMS:** Ghlestakov: Ahaa, shamba! ...Na mimi napita katika ofisi nyingine kuwaeleza wafanye nini. Kuna mtu mmoja ambaye hafanyi lingine ila tu kuandika barua zangu siku nzima. (Uk 36).

**MS:** Hilestakov: Na shambani nako kuna uzuri wake.... nakwenda ofisini dakika chache, natoa maelekezo na kumwacha karani mkongwe akiandika andika mezani pake. (Uk 52).

**Mfano 93**

**MMS:** Ghlestakov: ...Nasikitika Joakim hakutaka nikodeshe gari lake. Lakini wao ni washamba na hawangeelewa kitu. (uk 18-19).

**MS:** Hilestakov: ...Nasikitika kwamba Osipu alinizuia nisikodi gari lile, kwani ingekuwa ni fahari ilioje kuingia jijini kwangu .Je, familia za kichochole mpo?" (uk 27–28)

**Mfano 94**

**MMS:** Ghlestakov: Hayawani we! ...Hi ni supu ya aina gani? Umeweka tu maji machafu katika bakuli. Hakuna ladha; inanuka uvundo....Shetani tu ndiye ajuaye ni nini, lakini sio kuku. ...(uk 20).

**MS:** Hilestakov: ... Unaiita hii supu? Walichofanya ni kutia tu maji ya moto katika sufuria chafu! Haina ladha hata kidogo! ...Ni Mungu tu anajua lakini hii si nyama. ... Labda wamepika kishoka cha kuchanja nyama kwa bahati mbaya. (Uk 31).

**Mfano 95**

**MMS:** Ghlestakov (kwa mpishi): Hayawani! Hakuna haja ya yote hayo. Deni langu ni ngapi, jumla? (Uk 26).

**MS:** Hilestakov (kwa mhudumu): Mjinga we! sihitaji orodha ya vitu nilivyovitumia, ninataka kujua ninadaiwa kiasi gani! (Uk 38).

**Mfano 96**

**MMS:** Ghlestakov: Utathubutuje, we nyamaume! (uk 17).

**MS:** Hilestakov: Nyamaza, mjinga we! Inatosha! Nenda ukawaambie waniletee chakula. (uk 25).

**Mfano 97**

**MMS:** Bw Posta: (akiisoma barua) ..Kwanza, kuna huyu Mkuu wa Wilaya: lakini ni mpumbavu kama punda kihongwe! ..Korob: “Bwana Huruma, Zemlyanika, amefanana kabisa na nguruwe jike aliyevaa tunga.” “Mratibu wa elimu ananuka vitunguu sumu kila sehemu.”... (Uk 74).

**MS:** Mkuu wa Posta: (akiisoma barua)... Kwanza, kuna Meya. Jinsi anavyoonekana ni pumbavu kama fisi-si mwerevu sana... Mkuu wa Posta ni nusu kipofu, ana akili nusu, ijapokuwa ni mwepesi wa kufungua fungua barua anapotaka kufanya hivyo...”  
Korobkin: “Kamishina wa misaada, Zemlyanika, yuko kama-nguruwe aliyevaa wigi.” (uk 109-112).

**Mfano 98**

**MMS:** Ghlestakov: ...Inaelekea kuwa wananichukulia kuwa mtu mkubwa sana Serikalini. Kwa kweli hawa watu wapumbavu sana! Bila shaka niliwadanganya vizuri sana jana. (uk 52).

**MS:** Hilestakov:.. Wote hawa inaelekea wanadhani kuwa mimi ni afisa fulani wa serikali. Nadhani niliwavuna sana jana. Ni kikosi cha majuha mno. (uk 76).

**Mfano 99**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya (kwa Hakimu): ....Mtumishi wako anafuga bata katika vyumba vya ndani, pamoja na kuku na wanazururazurura wakiokota miguuni pako....wanapafanya panuke mno. (uk 3).

**MS:** Meya (kwa Jaji): Ehee, na wewe Amosi Fyodorovich, bora na wewe uanze kurekebisha mahakama yako. Mahakama yako ni kama shamba kabisa. Mwambie mlinzi wako awahamishe bata-mzinga wake kutoka pale barazani. (Uk 4).

**Mfano 100**

**MMS:** Hakimu: Ni kwa sababu hiyo mimi sijali. Mahakama yangu inanuka kiasi kwamba hakuna atakayediriki kuingia na kuikagua. Lakini kama ungeona moja ya makaratasi basi maisha hayangekuwa tena mazuri kama yalivyo.... Solomoni mwenyewe hangejua vipi kutofautisha ukweli na uwongo! (uk 10-11).

**MS:** Jaji: Mungu amhurumie huyo atakayejaribu kuchunguza usahihi wa vitabu na stakabadhi zote zile, kwa sababu ataijutia siku aliyozaliwa! Na sijapata kuona ripoti hata moja inayoeleweka. Hata yule Mfalme Suleiman anayesemekana kuwa alijaliwa hekima tele asingeweza kuchanganua mambo ya hapa. (uk 15).

**Mfano 101**

**MMS:** Hakimu: Ndiyo, lakini kuna dhambi na dhambi. Nakubali wazi kuwa napokea hongo, lakini aina gani ya hongo? Vimba vidogo na siyo zaidi! (uk 4).

**MS:** Jaji: Mimi sijali kukiri wazi kuwa huwa ninapokea rushwa lakini ni kutoka kwa wale watu wenye uwezo tu; na hiyo huwezi kuita dhambi. (uk 5).

**Mfano 102**

**MMS:** Bw. Huruma (kwa Ghlestakov):..sasa wakati wowote huyu Dobchiniski anapotoka nyumbani kwenda kokote, mara hakimu anamwingilia mkewe, na naweza kuapa...lakini waangalie watoto, Mheshimiwa! Hakuna anayefanana na Dobchinski, ila kila mmoja, hata yule binti mdogo, ni picha kamili ya hakimu! (Uk 49).

**MS:** Kamishina (Kwa Hilestakov):.. Maskini Dobchiniski akitoka tu nyumbani kwake, Jaji huingia kwa mlango wa nyuma ili kukutana na mke wa Dobchiniski! Na hii ni kweli tupu, Mheshimiwa! Hakuna hata mtoto mmoja wa Dobchiniski anayefanana na Dobchinski. Hii unaweza kuhakikisha mwenyewe! Kila mmoja wao hata yule mtoto wa kike anafanana jaji! (Uk 71).

**Mfano 103**

**MMS:** Hakimu (kwa M/Wilaya): ...Na umesikia juu ya Cheptovichi na Valinski? Hilo ni tuzo kubwa sana kwangu. Niko katikati kabisa ya unono. Naweza kwenda kuwinda katika bustani ya Cheptovichi siku moja na katika bustani ya Valanski siku ya pili! (Uk 7).

**MS:** Jaji: (kwa Meya)...Na kuhusu uwindaji mimi sasa ni mashuhuri. Je unajua kwamba Cheptovich amemshtaki Varhovinski? Kwa hiyo nimejipatia fursa ya kuwinda sungura bila malipo katika mashamba yao yote. Ninaweza kukuchukua tukaenda pamoja. (uk 10).

**Mfano 104**

**MMS:** Mkuu wa Wilaya: Ni wajibu wako kusimamaia walimu...Mratibu wa Elimu: Nitafanya nini? Nilimzungumzia juu ya jambo hili mara moja. (uk 4).

**MS:** Meya: walimu wako! Wewe ndiye kinara wa mashule... Mkaguzi: Sasa nitafanyeje?. (uk 6).

**Mfano 105**

**MMS:** BW. Huruma: ...Mchukue Mratibu wa Elimu hapa...sijui ni kwa nini wakubwa wamwajiri mtu kama huyo! Ni mwovu zaidi kuliko mwasi! Anapanda mawazo maovu katika vichwa vya vijana. (uk 49).

**MS:** Kamishina: Na yule Mkaguzi wa Mashule.. jinsi alivyopewa kazi ile ni muujiza kabisa! Tazama, hayuko tofauti na nyapara, na ile shule yake ni chemchemi ya mapinduzi! (uk 71).

**Mfano 106**

**MMS:** Anna: Utaona kuwa yeye ni mwanamji wa Pitasbag. Si mikogo hiyo! Si maringo hayo! Nilimpenda mara moja na nilitambua kuwa alikuwa akinichungulia mara kwa mara. (uk 42).

**MS:** Ann: Ni mstaarabu kwelikweli. Unaweza kutambua mara moja kwamba ni mtu wa mtindo (fasheni)! Mungu wangu, vijana kama huyu ndio wanaonivutia! Alivyo na utu na mtindo! Tena mkakamavu. Niligundua kuwa macho yake yalikuwa hayamtoki kwangu. (uk 57).

**Mfano 107**

**MMS:** Ghlestakovu: ...watu hawa hawajapata kumwona mtu yeyote mashuhuri. Lakini kwa ujumla, ni wema wa moyo na wanajua wajibu wao. Na binti anaonekana mzuri kabisa na nadhani mama mwenyewe yuko tayari kwa lolote. (UK 46).

**MS:** Mkuu wa posta (akisoma barua): ...Nipo hapa sasa nikiishi maisha ya kifahari katika jumba la Meya, nikiwatongoza mke wake na binti yake, kwa wakati mmoja! Sijaamua nianze kwenda na yupi- huenda mke wake ni mzuri zaidi, anaelekea kuwa tayari kwa lolote! (Uk 109).

**Mfano 108**

**MMS:** Anna: (Kwa Marya)...Nilimpenda mara moja, na nilitambua kuwa alikuwa akinichungulia mara kwa mara. Marya (kwa mamake) Mama, unajuwa kuwa alikuwa akiniangalia mimi... Anna ( kwa Marya) Sasa Mungu nipe nguvu! Haiwezekani kabisa! Yote yalieleweka jana. Kwa nini ajishughulishhe nawe? Ukileta upuzi zaidi nitakupeleka chumbani kwako. (Uk 42).

**MS:** Anna: (kwa Maria) ...Niligundua kuwa macho yake yalikuwa hayamtoki kwangu... Maria (kwa mamake) Oh mama, mimi ndiye alikuwa akiniangalia! ... Anna (kwa Maria) Ati wewe? Acha ujuha wako...Maria: alikuwa akiniangalia mimi... Anna (kwa Maria) Mungu wangu, huyu mtoto hakomi kunisuta? Kwa nini akuangalie wewe? Unaweza kunipa sababu moja tu? (uk 57).

**Mfano 109**

**MMS:** Marya: ni Dob mama. ...Anna (kwa Marya) Dobchniski kwa hakika! Njozi gani zinazokujia kichwani!! Ni dhahiri kuwa siye Dobchniski. ...Marya: Hakika mama ni Dobchniski. ..Anna: Unasema hivyo kusudi tu kunipinga. Nakwambia siye Dobchniski...Ndiyo. Sawa, sasa naona. Na wewe unabisha nini? (uk 29).

**MS:** Maria: Ni Dobchniski mama. ..Anna: Dobchniski! Usiwe mpuuzi, umeanza tena alinacha zako. Hawezi kuwa Dobchniski ila. ..Maria: Kweli ni Dobchniski mama. ..Anna: Usinipinge nitakwambia ni nani. ...Ndiyo ni Dobchniski na mimi nimemwona, sasa ubishi wa nini? (uk 42-43).

**Mfano 110**

**MMS:** Anna: ..Kwa vile ulisikia Bwana Posta yuko hapa ukaona uanze kujirembesha mbele ya kioo! Unadhani atakutongoza na kila wakati yeye hukunja uso wake mara tu unapompa kisogo. ( uk 13-14).

**MS:** Ann: ...Kwa sababu Mkuu wa Posta yupo hapa basi utajipuna na kujitazamatazama kwenye kioo kwa mwaka mzima. Unadhani anakupenda, kumbe mara tu unapompa mgongo yeye hukusahau kabisa kama upo hapa duniani! (uk 20).